Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MKUTANO WA NANE

---

## Kikao cha Ishirini na Nane – Tarehe 16 Julai, 2012

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:-**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:-**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

**MHE. BETTY E. MACHANGU (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):-**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka 2011/2012 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:-**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaanza maswali Ofisi ya Waziri na Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh ndio atakayeuliza swali la kwanza.

Na. 196

### Uwekezaji Katika Sekta ya Uvuvi

**MHE RAMADHAN HAJI SALEH** aliuliza:-

Sekta ya Bahari ni chanzo cha pili cha Mapato katika nchi ukiacha Madini kama itatumika vizuri lakini bado Serikali haijawekeza katika sekta hiyo:-

Je, ni lini sasa Serikali itawekeza katika Sekta ya Bahari?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh, Mbunge wa Bumbwini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inakubali kwa Sekta ya Bahari na hususan uvuvi ni muhimu kwa mapato ya nchi yetu. Hivyo, Serikali imeendelea kuboresha mazingira kwenye Sekta ya Bahari na hasa uvuvi ili kuwezesha wadau wa sekta hiyo, ikiwemo sekta binafsi kuwekeza ipasavyo.

Baadhi ya mazingira hayo ni kuwepo kwa Sera ya Uwekezaji Nchini, Sera ya Taifa ya Uvuvi (1997), Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 na Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi kwenye Bahari Kuu Na. 17 ya mwaka 1998 na marekebisho yake ya mwaka 2007.

Aidha, Serikali imeandaa programu ya Kuendeleza Sekta ya Uvuvi ambayo tayari imeingizwa katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano

ambayo itatekelezwa na Taifa, Halmashauri zote nchini zenye maji. Sekta ya Bahari, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge inapewa umuhimu mkubwa.

Mheshimiwa Mbunge miundombinu mbalimbali imejengwa na kuboreshwa. Kwa mfano, Mialo 25 ya kupokelea samaki katika Ziwa Victoria imeboreshwa na Mialo mitatu (3) inajengwa katika ukanda wa Pwani.

Aidha, kwa kushirikiana na Mradi wa Uwiano wa Bonde la Ziwa Tanganyika, Serikali itajenga Mialo minne (4) katika ukanda wa Ziwa Tanganyika. Serikali pia imekamilisha ujenzi wa masoko makubwa ya kupokelea samaki ya *Ferry*, Dar es Salaam na Kirumba, Mwanza, pamoja na soko la Kasanga, Rukwa.

Vile vile, Serikali imehamasisha sekta binafsi kuongeza thamani ya mazao kwa kuanzisha viwanda vya kisasa 17 vya kuchakata samaki na mazao ya uvuvi, viwanda vidogo 17 na maghala 84.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi inaendelea kuhamasisha uwekezaji katika maeneo mbalimbali katika Sekta ya uvuvi. Aidha, Serikali imeondoa kodi ya ongezeko la thamani kwenye zana za uvuvi ikiwa ni pamoja na injini za kupachika, vifungashio, nyuzi za kutengeneza nyavu na kufuta kodi ya zuio kwa usafirishaji wa samaki nje ya nchi.

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nachukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri, lakini naomba nimwulize swali moja la nyongeza.

Kutokana na utafiti uliofanywa katika Bahari yetu ya Hindi kumegunduliwa samaki wengi sana na kutokana na meli nyingi kutoka nje kuja kuvua katika bahari yetu. Je, Serikali hili imeliona vipi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa na ni jambo la kufurahisha kwamba utafiti umeonyesha kwamba bahari yetu ina samaki wengi na wa kuvutia meli kufika kwenye eneo la bahari yetu kutaka kuvua ili na wao wanufaike. Serikali imeliona hilo itaongeza kwanza uwekezaji ili sisi wenyewe tunufaike na rasilimali samaki kwenye eneo letu la bahari.

Lakini vilevile kuongeza ulinzi ili meli kutoka nje zisiweze kuvua samaki wetu bali sisi wenyewe tunufaike nao. Pamoja na hivyo kama nilivyosema sera inaeleza kwamba lazima tushirikiane na sekta binafsi kuona kwamba uvuvi na teknolojia bora zaidi inatumika katika kuvua rasilimali kutoka bahari yetu.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Katika jibu la msingi Mheshimiwa Waziri amejaribu kuonyesha kwamba uwekezaji katika sekta ya Bahari ni suala la uvuvi tu. Lakini kuna suala hili la uzalishaji wa mabaharia hasa katika ngazi ya digrii na elimu zaidi ya hiyo.

Sasa Chuo chetu cha *DMI* ilikuwa kiingie ubia na Wachina na kujaribu kujenga chuo ambacho kitazalisha Mabaharia. Waziri anasema nini katika sekta hii ya Bahari katika uzalishaji wa mabaharia kuliko tu alichozungumzia uvuvi wakati swali zima linazungumzia sekta ya Bahari?

**SPIKA:** Sina uhakika kama ni uzalishaji wa mabaharia au ufundishaji wa mabaharia waliohusika.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lugola kama alirejea majibu yangu ya msingi, nilisema sekta ya Bahari nikasema hususan uvuvi.

Kwa hivyo sekta ya Bahari inahusisha na kuwafunza mabaharia au kuwanoa mabaharia kusudi basi tuwe na watu ambao wataendesha meli kwenda kuvua kwenye bahari yetu. Kwa hivyo na uvuvi nao unahitaji mabaharia hao wawe na uwezo, wawe na ujuzi na wawe ni majasiri kwenda kuvua hasa kwenye *deep sea* au bahari ya mbali.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ili niweze kumwuliza Waziri swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekubali kabisa kwamba bahari yetu ina samaki wengi sana. Je, ni jambo gani au ni sababu gani inayopelekea nchi yetu kuruhusu samaki kuingia nchini

kutoka nje ya nchi ikiwepo nchi ya Japan wakati ambapo tuna samaki wengi sana?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa mujibu wa utafiti kwamba tuna samaki wengi.

Lakini ni kweli vilevile kwamba katika enzi hizi za utandawazi huwezi ukazuia soko lako jambo lililo muhimu ni kwamba sisi Watanzania tupende vya kwetu zaidi hata pale ambapo watu wanakuwa na *choice* au wanaweza kuchagua kitu kutoka nje.

Lakini pamoja na uzalendo vilevile tuongeze uwezo wetu wa kuvua ili tuwe na samaki wa kutosha ili Watanzania waweze kuchagua samaki wa kwao badala ya wale wanaotoka nje wanaokaa kwenye barafu muda mrefu kwanza na usalama wake ukilinganisha na samaki wa kwetu watakuwa salama zaidi kwa sababu ni karibu na sisi.

Na. 197

**Gharama Kubwa za Kuendesha Chaguzi Ndogo**

**MHE. PINDI H. CHANA** aliuliza:-

Zoezi la kuendesha Chaguzi Ndogo nchini limekuwa ni gharama kubwa sana kwa vyama vya siasa na wananchi kwa ujumla:-

Je, Serikali haioni kuna haja ya kulitafakari upya jambo hili na kuja na mpango wa gharama ndogo ya kuendesha Chaguzi Ndogo ama kwa kutumia "*Proportional Representation*" au Uchaguzi kufanyika baada ya miaka miwili na nusu (2 ½ )?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE** alijibu:**-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba zoezi la kuendesha Chaguzi Ndogo limekuwa la gharama kubwa kwa Serikali, Vyama vya Siasa na Wananchi kwa ujumla. Katika hilo naomba nimpe mifano miwili inayothibitisha ukweli wa kauli hiyo Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo.

Baada ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2005 - 2010 zilifanyika Chaguzi Ndogo za Wabunge sita (6) katika Majimbo ya Wilaya ya Tunduru, Kiteto, Tarime, Mbeya Vijijini na Busanda. Wastani wa gharama zilizotumika katika Chaguzi Ndogo 2005-2010 kwa Ubunge peke yake ilikuwa ni shilingi 9,261,810,000/=. Lakini kwa Madiwani katika kipindi hicho zilifanyika Chaguzi

Ndogo 75 nazo ziligharimu shilingi bilioni 9,555,000,000/=.

Lakini kipindi hiki baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010 zimefanyika Chaguzi Ndogo mbili katika Majimbo ya Igunga na Arumeru Mashariki, fedha zilizotumika kuendeshea uchaguzi huu ni shs. 3,087,270,000/=. Lakini pia zimefanyika Chaguzi Ndogo 30 za Madiwani ambazo Serikali imetumia shs. 3,822,000,000/= na hizi fedha zote huwa kwa kweli ni za dharura.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mchakato wa mabadiliko ya Katiba umeshaanza, suala hili linaweza kujadiliwa kwa kina katika mchakato huo ikiwa ni pamoja na mapendekezo ya Mheshimiwa Mbunge.

Napenda kutumia fursa hii kutoa wito kwa wananchi wote, kujitokeza kwa wingi kutoa maoni yao kuhusu masuala mbalimbali, likiwemo hili la namna bora ya kujaza nafasi wazi za Ubunge na Udiwani wakati Tume ya Mabadiliko ya Katika itakapotembelea maeneo yao.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri wa Sera, Uratibu na Bunge.

Kwa kuwa fedha hizi tunazotumia kwenye Chaguzi Ndogo kwa kweli ni nyingi zingeweza kujenga madarasa, maji na kadhalika. Na kwa kuwa zoezi la Katiba linaloendelea ambalo ni matarajio yetu mwaka 2014 ndio liwe limekamilika haliathiri majukumu ya

Bunge la Jamhuri ya Muungano ambayo ni kutunga sheria na kurekebisha sheria.

Je, Serikali haioni ni wakati muafaka watuletee humu ndani Sheria ya Uchaguzi sisi Wabunge kwa pamoja tuijadili, tuitafakari ifanye kazi hadi Uchaguzi wa mwaka 2015 na baadaye maoni yatakapokuja kwenye Katiba basi maoni yale yatachukua nafasi yake?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika**,** ni kweli kama nilivyosema jambo hili lina gharama kubwa na imethibitisha hivyo. Lakini mapendekezo aliyotoa Mheshimiwa Mbunge ni mazuri sana ya kurekebisha sheria, lakini lazima uanzie kwenye Katiba.

Sasa namshauri tu kwamba kwa sababu yeye ndio Mwenyekiti wa Kamati ambayo inasimamia Wizara zote zinazoweza kufanya jambo hili, ikiwezekana labda angeitisha kikao kingine cha Kamati tuweze kulijadili vizuri zaidi badala ya kuahidi hapa tuone kama linawezekana au haliwezekani. Kwa sababu Mheshimiwa mwuliza swali ni mdau katika hili ni Mwenyekiti wa Kamati zetu ambazo zinahusika ambazo zingeweza zikafanya mambo haya. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kabisa gharama inayotumika kwenye Chaguzi Ndogo ni kubwa mno. Na kwa kuwa inapopatikana nafasi wazi kwa upande wa Viti Maalum, uchukuliwa yule aliyopo kwenye akiba kulingana na chama husika.

Je, Serikali haioni kwamba kuna haja sasa ya kuchukua wazo langu inapopatikana tatizo la jimbo kuondokewa na Mbunge basi matokeo ya Uchaguzi Mkuu aliyefuatiwa achukuliwe bila kujali chama alichokuwa nacho?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, miguno hii na minong'ono wameshakujibu hapo kwamba hilo haliwezekani. (*Makofi/Kicheko)*

Kwa sababu hilo linawezekana tu kwa Viti Maalum kwa sababu nyinyi mko kwenye *proportional representation style* na ndio maana nyie mnaenda kwa orodha. Sisi tunajua ninayosema hapa sio kwamba naomba Mungu afanye yaani likitokea la kutokea basi tunajua kabisa Tume ya Uchaguzi pale wana orodha kabisa kwamba anafuata fulani kwa sababu ya utaratibu wa Viti Maalum.

**WABUNGE FULANI:** Watauana hao!!!!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Lakini kwa Majimbo ni yule aliyechaguliwa siku ya Uchaguzi. Kwa hiyo haya ndiyo yale aliyosema Mheshimiwa Pindi Chana kwamba kama inawezekana twende kwenye sheria, twende kwenye Katiba turekebishe ili tuone ni utaratibu gani. Yako mengi ya kuzungumza katika eneo hili la Uchaguzi.

Mimi nafikiri utaratibu mzuri tusubiri marekebisho ya Katiba. Kwa sababu ni ukweli ulio wazi ni kwamba fedha hizi nyingi na mjue hata kwenye Bajeti hii hatuku-*vote* fedha za Uchaguzi Mdogo. Likitokea la kutokea tunakata zile za maji na barabara tunaweka humu. Ni fedha za dharura ambazo huwa hatubajeti. Kwa hiyo Chaguzi Ndogo kweli zina-*disturb* sana hata Bajeti za maendeleo katika nchi hii.

Na. 198

## Idara ya Uhamiaji Kununua Jengo la Benki ya Watu wa Zanzibar

**MHE. JADDY SIMAI JADDY** aliuliza:-

Idara ya Uhamiaji ilinunua jengo lililokuwa likimilikiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) lililopo Kunazini (Kivunge) Wilaya ya Kaskazini "A" – Unguja:-

(a) Je, ni nini lilikuwa kusudio la Idara ya Uhamiaji kununua jengo hilo?

(b) Je, ni mafanikio gani ambayo yamepatikana tangu kununuliwa kwa jengo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy, Mbunge wa Mkwajuni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kusudio la Idara ya Uhamiaji kununua jengo lililokuwa likimilikiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar lililopo Kinazini (Kivunge) Wllaya ya Kaskazini "A" ni kupata Ofisi za kutosha kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuhamiaji ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa mkakati wa kusogeza huduma za Uhamiaji karibu na wadau wake.

(b) Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana baada ya kununuliwa kwa jengo hilo ni kama ifuatayo:-

- Kurahisisha huduma mbalimbali za kiuhamiaji kwa wenyeji, wageni na wawekezaji katika Mkoa wa Kaskazini.

- Kupata Ofisi za kutosha katika kutoa huduma za Uhamiaji na kupata nyumba kwa ajili ya wafanyakazi.

**MHE. JADDY SIMAI JADDY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa lengo kuu lilikuwa ni kusogeza huduma za kihamiaji katika Mkoa wa Kaskazini Unguja na kwa kuwa si wengi wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja wenye kuelewa uwepo wa ofisi hiyo katika Mkoa wao.

Je, sasa Wizara ina mpango gani mahususi wa kutoa elimu kwa wananchi wa Mkoa wa Kaskazini

Unguja katika kuelewa uwepo wa Ofisi hiyo katika Mkoa wao ili waweze kuitumia ipasavyo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, Idara ya Uhamiaji inatumia njia mbili kuu katika kutoa elimu kuhusu shughuli zake. Moja inatoa vipindi vya radio *ZBC* kwa upande wa Zanzibar na pia *TBC* kwa Tanzania Bara kueleza mambo tofauti ambayo wanahisi wananchi wanatakiwa wayajue.

Radio kwa upande wa Zanzibar imekuwa inatumika kuwaeleza wananchi si wa Kaskazini peke yao lakini kwa kila Mkoa katika kujua huduma hizi zinapatikana wapi. Utaratibu wa pili ni kwenda kwenye maeneo tofauti kufanya vikao, mikutano mbalimbali na wadau ili wajue kwamba huduma hizi zinapatikana wapi na kwa namna gani.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Moja kati ya majukumu ya Idara ya Uhamiaji ni kutoa *Passport* ambayo ni haki ya kila Mtanzania. Je ni vituo vingapi ambavyo vinatoa *passport* ukiachilia mbali kituo kikuu cha Zanzibar kilichopo Unguja Mjini na cha Dar e Salaam?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba moja kati ya huduma za uhamiaji ni kutoa *passport* na *passport* inaanza kwa mwombaji kujaza fomu ambayo baada ya kujadiliwa na kuzingatiwa ndiyo ambayo inapelekea kupewa *passport.*

Kwa sasa maeneo yote ya Mikoa yanaweza kutoa fomu na mtu anaweza kwenda akajaza fomu na kuanza mchakato kwa ajili ya kupata *passport. Form* hizo baada ya kujazwa ndiyo zinapelekwa Makao Makuu kwa kufanyiwa utaratibu wa mwisho kutoa vitabu. *Otherwise* lengo ni kuhakikisha kwamba suala hili linapelekwa kwa wananchi zaidi hali ya fedha itakaporuhusu.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR**: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Je, Wilaya ngapi zina ofisi ya uhamiaji huko Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, Zanzibar ina Wilaya kumi na naamini Wilaya saba tayari zina ofisi za Wilaya za shughuli za Uhamiaji na Wilaya ambazo hazina nafikiri ni Wilaya ya Magharibi, Kusini na Kaskazini B.

**SPIKA:** Kwa hiyo huna uhakika, akipata jibu atakuja kuwaambieni kesho. *(Kicheko)*

Tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga taifa. Mheshimiwa Thuwaiba Idris Muhammed, atauliza swali hilo.

Na. 199

## Hitaji la Hospitali za Jeshi Nchini

**MHE. THUWAIBA IDRIS MUHAMMED** aliuliza:-

Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania linafanya kazi nzuri katika huduma ya afya kupitia hospitali ya Lugalo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga hospitali kama hiyo katika maeneo mengine ya nchi ili kuboresha huduma za afya?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Thuwaiba Idrisa, kwa kulisifu Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa kutoa huduma bora za afya kupitia hospitali yake ya Lugalo. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Thuwaiba Idrisa kuwa Jeshi letu lina hospitali nyingine katika maeneo mbalimbali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Jeshi limejenga hospitali za *TMA Arusha,* Nyumbu - Kibaha, Bububu - Zanzibar, hospitali za kanda katika Mikoa ya Tabora, Mwanza na Mbeya. Wizara yangu inaendelea kuzipatia hospitali hizi vifaa bora na wataalam ili niweze kutoa huduma nzuri kama zile zinazotolewa katika hospitali ya Lugalo.

**MHE. THUWAIBA IDRIS MUHAMMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante pia namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Hospitali za Kijeshi ni kimbilio la wengi na kwa kuwa Hospitali ya kijeshi iliyopo Morogoro ina matatizo ya fedha ya majengo ya wodi za wagonjwa. Je, Serikali mna mkakati gani wa kumaliza majengo hayo?

Swali la pili, kwa kuwa Hospitali ya Kijeshi ya Bububu iliyoko Zanzibar ina tatizo la vifaa tiba kwa maradhi au magonjwa ya wanawake na kwa kuwa Hospitali ya Mzinga iliyopo Morogoro ina tatizo la kifaa cha *X-ray* pamoja na *Ultrasound* hata inapelekea wagonjwa kukimbizwa kupelekwa kibaha.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapatia vifaa hivyo ili waweze kufanya kazi zao vizuri na bila kuwasumbua wagonjwa? Ahsante.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kupitia Jeshi la Wananchi wa Tanzania linayodhamira ya dhati ya kuimarisha huduma mbalimbali zinazopatikana katika Hospitali za kijeshi katika maeneo mbalimbali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa uzito huohuo tunayo nia ya dhati ya kuimarisha huduma za X-ray *Ultra Sound* na huduma zingine za kitiba katika Hospitali ya Mzinga Morogoro.

Lakini pia tunayo dhamira hiyohiyo ya kuongeza huduma zaidi za kitiba na wataalam katika hospitali ya Bububu. Ni vigumu sana mpaka sasa kumwambia ni lini masuala haya yatatekelezwa kwa sababu yanategemea sana upatikanaji wa fedha. Lakini ni matumaini yetu kwamba tutaendelea kujenga uwezo na *inshallah* Mwenyezi Mungu akipenda tutakusanya uwezo huo kwa kutekeleza azma hiyo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa Wizara hiyo inakuja mara tu baada ya maswali. Kwa hiyo, msimalize maneno ya kuchangia. Sasa tunaenda Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Mohamed Hamis Missanga, atauliza swali linalofuata.

Na. 200

**Nyongeza ya Pensheni Kwa Wastaafu**

**MHE. MOHAMED HAMIS MISSANGA** aliuliza:-

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameidhinisha nyongeza ya pensheni kwa wastaafu ambapo Waziri wa Fedha ameridhia nyongeza hiyo kupitia *Government Notice Na. 2006* iliyochapwa tarehe 29 Juni, 2009 na kwa mujibu wa kifungu Na. 30 cha *Public Service Retirement Act Cap. 371* aliwasilisha hoja ya nyongeza hiyo katika Bunge na kuidhinishwa na Bunge kwa kauli moja katika viwango tofauti kama inavyoonyeshwa kwa jedwali lililoambatanishwa nyuma.

(a) Je, ni kwanini wastaafu hawajaongezwa pensheni hiyo hadi leo hii kulingana na amri hiyo?

(b) Je, ni lini wastaafu hao wataongzewa pensheni zao kulingana na amri hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Hamis, Mbunge wa Singida Magharibi, lenye sehemu (a) na(b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali iliongeza kima cha chini cha pensheni kutoka shilingi 21,601/- kwa mwezi hadi shilingi 50,114/- kwa mwezi kuanzia Julai, 2009. Kufuatia nyongeza hiyo wastaafu walioko kwenye daftari la pensheni la Hazina, walirekebishiwa pensheni zao kuanzia Julai, 2009.

Wastaafu wa Serikali waliostaafu kuanzia Julai, 2004 wanaolipwa pensheni na mfuko wa pensheni wa watumishi wa Umma *(PSPF)* waliendelea kulipwa viwango vya zamani vya pensheni kutokana na utata wa Sheria. Kifungu cha 30(4) cha Sheria ya Mafao ya Hitimisho la Utumishi wa Umma Na.2 ya Mwaka 1999 inasema kuwa ongezeko lolote linalotokana na mabadiliko ya pensheni linapaswa kulipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya vikao vya pamoja kati ya Wizara kati ya Wizara ya Fedha na uongozi wa mfuko suluhu ilipatikana na Wizara imepeleka *PSPF* jumla ya Shilingi 62,192,330,296.99 ikiwa ni fedha za malimbikizo ya pensheni kuanzia Julai, 2009 hadi Juni, 2012, Kabla ya kulipa malimbikizo, Mfuko ulifanya uhakiki wa wastaafu wanaohusika ili kujiridhisha na madai yao.

Hadi kufikia Julai, 2012, wastaafu waliojihakiki wapatao 21,802 kati ya 29,574 wamelipwa malimbikizo ya pensheni zao za kuanzia Julai, 2009 hadi Juni, 2012.

Aidha kuanzia Julai, 2012, wastaafu wote wataendelea kulipwa viwango vipya vya pensheni kwa mujibu wa *Government Notice* Na. 2006 ya tarehe 29 Juni, 2009.

**MHE. MOHAMED HAMIS MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali kwa kutekeleza kilio cha siku nyingi cha wastaafu kama walivyoeleza. Sasa napenda kujua je, wale ambao hawajapata. Hawajapata kwa sababu hawajahakikiwa sasa Serikali itachukua utaratibu gani kuhakikisha kwamba na wale wachache ambao hawajapata marekebisho yao watapatiwa hayo marekebisho mapema iwezekanavyo?

Swali la pili; Mahakama Kuu chini ya Jaji Mihayo tarehe 9Julai, 2008 iliamuru kwamba watumishi 245 waliokuwa wa *TTCL* walipwe marekebisho yale ya

Pensheni na Katibu Mkuu wa Wizara wa Fedha mnamo tarehe 30 Januari, 2012 alikiri kupokea maelekezo hayo na kwamba walikuwa wanashughulikia ulipaji wa malipo hayo kulingana na amri ya Mahakama Kuu. Ningependa kujua kwanini mpaka sasa hazijalipwa na lini wafanyakazi 245 wa *TTCL* watalipwa stahili zao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Spika kwa wale ambao hawajalipwa malipo yao na ambayo tayari wameruhusiwa kulipwa tunaendelea kuhakiki na mara tunapohakiki tutaendelea kuwalipa fedha zao.

Kuhusiana na amri ya Mahakama iliyotolewa kwa ajili ya wafanyakazi wa *TTCL* ambayo tuliipokea mwanzoni mwa mwaka huu ni kweli tulipokea amri hiyo lakini ifahamike kuwa inabidi vilevile iwekwe kwenye Bajeti kwa ajili ya kuweza kuwalipa. Kwa hiyo, bado tunaendeleza na taratibu za kufanya mipango ya kuwalipa lakini amri hiyo tunayo na tutawalipa haraka iwezekanavyo fedha itakapokuwa tayari.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa kuna wafanyakazi 1200 waliokuwa wafanyakazi wa *Polytex* na mpaka leo hawajalipwa malipo yao na suala hili limepelekwa kwa Waziri Mkuu na *CHC l*akini mpaka leo wanapewa danadana kutoka Morogoro ni lini wafanyakazi hao watalipwa stahili zao?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)**: Mheshimiwa Spika, naomba nilichukue hili swali nikalifanyie kazi. Kwa sababu naamini Shirika hili litakuwa ni katika yale mashirika yaliyokuwa katika mchakato wa Ubinafsishwaji.

**MHE. RITTA E. KABATI**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa kuna baadhi ya wastaafu walilipwa pensheni zao kwa mkupuo.

Je, marekebisho haya yanawahusu na wao pia?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)**: Mheshimiwa Spika, wale waliokuwa wamelipwa pesa zao kwa mkupuo walikuwa wamelipwa hivyo kwa sababu umri wao wa kustaafu ulikuwa haujafika. Kwa wale ambao umri wa kustaafu umefika wanaanza kuingia katika utaratibu wa kulipwa kila mwezi kufuatana na taratibu ambazo zimewekwa.

**SPIKA:** Mmeona maswali yaliyovyoulizwa kifupi yamejibiwa kifupi, tumeweza kuwaweka watu watatu. Hivyo ndivyo inavyotakiwa. Tunaendelea na swali linalofuata Mheshimiwa Hamadi Rashid Mohamed.

Na. 201

**Matumizi ya Sarafu za Aina Mbili**

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR (K.n.y. MHE. HAMAD RASHID MOHAMED)** aliuliza:-

Je, kuna faida au hasara gani kwa nchi kutumia sarafu za aina mbili kwa wakati mmoja?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Wawi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, faida ya Sheria na Sera ya soko huria ya fedha za kigeni au ya kutumia sarafu za aina mbili kwa wakati mmoja ni kwamba inarahisisha upatikanaji wa fedha za kigeni na kuwahamisisha wale walikuwa nazo nje kuzirejesha nchini na kuzitumia bila woga.

Pia inahamasisha uzalishaji wa bidhaa na huduma kwa watalii au wawekezaji wa nje na wageni ambao wanahitaji kutumia kuagiza bidhaa kutoka nje kwa sababu wazalishaji wanakuwa na uhakika wa kumiliki mapato yao ya fedha za kigeni wanapopeleka bidhaa zao nje. Utaratibu huu ni kwa faida ya uchumi kwani ndiyo msingi wa uwezo wa kugharamia manunuzi yake ya bidhaa na huduma kutoka nje na huleta utulivu kwenye soko la fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, faida nyingine ni kuongezeka kwa fedha za kigeni inayotunzwa na Benki Kuu. Mfano akiba ya fedha za kigeni iliongezeka kutoka Dola za Kimarekani milioni 228.3 mwaka 1993 (Sawa na asilimia 6.3 ya pato la Taifa) hadi kufikia dola za kimarekani 4,053.8 (sawa na asilimia 16.9 ya pato la Taifa mwaka

2011). Hii ni baada ya Sheria kubadilishwa na kuruhusu matumizi ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, sarafu za kigeni hutumika katika uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa ajili ya uzalishaji na huduma za kijamii. Kwa mfano mwaka 2010 bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje zilikuwa ni asilimia 39 ya pato la Taifa. Manunuzi yote haya kutoka nje ya nchi yanagharamiwa kwa fedha za kigeni.

Kati ya bidhaa na huduma zote zilizoagizwa kutoka nje mwaka 2010, 22.4% ilikuwa mafuta, 30.1% mitambo na vifaa vya usafiri na ujenzi na 8% malighafi za viwanda na pembejeo za kilimo. Ili uchumi uweze kuendelea ni muhimu kuwa na mfumo utakao hakikisha kuwa kunakuwa na fedha za kutosha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo vilevile kuna hasara au changamoto zinazotokana na mfumo wa kuhodhi na kutumia sarafu moja ambayo huchochea utoroshaji wa fedha za kigeni na mitaji kwenda nje yaani *capital flight.*

Watu wengi wakipata fedha za kigeni kwa njia halali hushawishika kuzitunza katika mabenki ya nje ya nchi ili kukwepa ukiritimba na usumbufu wa kupata fedha za kigeni ukiritimba huu husababisha uhaba mkubwa wa fedha za kigeni hasa uwekezaji na uendeshaji wa shughuli mbalimbali. Mfumo hodhi wa sarafu moja husababisha pia kushamiri kwa soko lisilo rasmi la fedha za kigeni yaani *parallel black market*

mara nyingi wanaopata fedha za kigeni kwa njia halali kutoka Benki Kuu wanakwenda kuuza fedha wanazopata kwenye soko lisilo rasmi kwa bei ya juu zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano mwaka 1984 viwango vya soko lisilo rasmi lilikuwa zaidi ya mara 4 ya viwango vilivyopangwa na Benki Kuu watu walikuwa wakitumia njia zisizo halali kupata fedha za kigeni na hivyo kufungua mianya ya rushwa hasa kwa wale waliopewa dhamana ya kusimamia upatikanaji wa fedha za kigeni kwa bei rasmi.

Hasara nyingine ni kuongeza mfumuko wa bei pale ambapo huduma ambazo ni za matumizi ya ndani zinapolipiwa kwa kutumia fedha ya nje kwasababu ya kuzifanya ziwe aghali zaidi kuliko ambavyo ingepaswa kuwa, pamoja na kufungua mipaka ya soko huria la fedha za kigeni hapa nchini Sheria ya Benki Kuu ya 2006 sehemu ya 3 (26) inatamka kuwa shilingi ya Tanzania ndiyo fedha halali itakayotumika kwa malipo yote nchini hii ina maanisha kuwa sarafu ya Tanzania ndiyo sarafu pekee ambayo haiwezi kukataliwa na mtu yoyote kwa malipo halali hapa Tanzania.

Aidha ni kosa kwa mtu yoyote kukataa kupokea sarafu ya Tanzania kwa malipo halali hapa nchini mkazi yoyote wa Tanzania hapaswi kushurutishwa kufanya malipo yoyote kwa sarafu za kigeni. Huduma kama za mahoteli zina rasmishwa kutoa huduma za ubadilishaji wa fedha za kigeni kwa wateja wake walioko mahotelini na huu ni utaratibu wa kawaida Duniani

kote, matumizi ya kadi zenye sarafu za aina mbalimbali katika kulipia gharama za manunuzi ya bidhaa na huduma ndiyo njia mbadala wa kutumia sarafu mtu yeyote mwenye kadi ya *Yen, Euro, Dollar, Pound* na kadhalika hutumia kulipia gharama na huduma bila kubadilisha sarafu huu ndiyo utaratibu unaopaswa kutumika hata hapa Tanzania.

**SPIKA:** Jamani naomba utulivu ndani ya Bunge Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, swali la nyongeza.

**MHE. AMINA A. AMOUR:** Mheshimiwa Spika, Je, Uganda na Kenya kwa nini dola haitumiki Kama inavyotumika Tanzania na wao ndiyo walioimarika kiuchumi? Suala la pili. Je, huoni kuwa hii inawasaidia wafanyabiashara wachache wanufaike na wakati huo sarafu yetu inazidi kukosa thamani?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Spika, ninataka kumfahamisha Mheshimiwa Amina Amour pamoja na Wabunge wote kuwa Kenya, Uganda, Msumbiji, Malawi na nchi nyingine nyingi zinatumia fedha za kigeni lakini wanautaratibu wa kuhakikisha kuwa hazitumiki Sokoni. Uganda na Msumbiji ni nchi ambazo wao wamekuwa wakitumia fedha *paraley system* kama tunayotumia hapa ambayo ni *regulated* kwa sisi Tanzania hairuhusiwi isipokuwa imekuwa ikitumika.

Uganda wamekubali, Malawi walikuwa wamekubali kuwa hela yao na dola zitumike pamoja lakini sisi hatujakubali kuwa pesa ya nje itumike nchini

ingawa hutumika kwasababu ya mapungufu. Sasa ninachotaka kusema ni kuwa, hii ni kweli kuwa inadhoofisha hela yetu, inaweza kusababisha mfumuko wa bei.

Lakini vilevile ifahamike kuwa kutokana na utandawazi huwezi kuzuia moja kwa moja kila kitu ndiyo maana ni lazima kwa sasa tuje na utaratibu utakaoruhusu wale ambao inawabidi watumie fedha ya kigeni wawe na leseni au utaratibu utakaowaruhusu na wajulikane ili kuiwezesha Serikali kufuatilia matumizi ya fedha za kigeni na kujua ziko kiasi gani nchini na zinafanya shughuli gani. Kwa hiyo, ninakubali kuna mapungufu na tutakwenda kuyafanyiwa kazi na tutakapokuja kwenye Bajeti ijayo mtasikia kuwa kumetokea taraibu ambazo zitadhibiti zaidi utumiaji wa fedha za kigeni nchini kwa matumizi ambayo siyo ya lazima *(Makofi).*

**SPIKA:** Unyeti wa suala hili tumetumia muda mrefu dakika kumi swali moja kwa hiyo, tunaendelea na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Mheshimiwa Joseph Simkamba Kandege atauliza swali hilo.

Na. 202

## Uhaba wa Watumishi wa Afya- Rukwa

**MHE . DEUSDERIUS J. MIPATA ( K.n.y. JOSEPHAT S. KANDEGE)** aliuliza:-

Chuo cha Matabibu Wasaidizi Vijijini kilichopo Sumbwanga Mjini hutoa wastani wa wahitimu 45-50 kwa mwaka:-

(a) Je, ni wahitimu wangapi waliopangwa kufanya kazi Mkoani Rukwa kwa miaka mitatu ya hivi karibuni wapo katika vituo vya kazi?

(b) Je, Serikali haioni kuwa ni busara ikatenga nafasi za upendeleo kwa vijana wenye sifa kutoka Mkoa wa Rukwa na jirani ili kupunguza uhaba wa watumishi wa Afya hasa vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo;-

(a) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita kuanzia mwaka 2009/2010 hadi 2011/2012, Wizara ya Afya na ustawi wa Jamii iliwapangia kazi wahitimu wa kada za afya wapatao 238 katika Mkoa wa Rukwa. Zoezi la ufuatiliaji wa watumishi waliopangiwa kazi katika Mikoa mbali mbali kwa miaka miwili 2009/2010 na 2010/2011 inaonyesha kuwa Watumishi 102 waliopangiwa Mkoani Rukwa katika Halmashauri za Mkoa huo wanaendelea na kazi. *(Makofi)*

Tatizo la watumishi walio wengi wameshindwa kuripoti katika vituo walivyopangiwa kazi kutokana na hofu ya kukosa huduma za msingi kama nyumba katika maeneo mengi nchini. Serikali katika kutatua tatizo hili imeanza kujenga nyumba za watumishi, katika Mikoa iliyoko pembezoni ikiwemo Rukwa, ambapo jumla ya nyumba 40 zitajengwa katika ngazi za Vituo vya Afya na zahanati katika Wilaya ya Mpanda, Nkasi, Sumbawanga vijijini na Sumbawanga mjini.

(b) Utaratibu wa kuchagua wanafunzi kujiunga na vyuo vya Mafunzo ya Afya umefanyiwa mabadiliko katika mwaka 2011/2012. Lengo la mabadiliko hayo ni kutoa fursa kwa waombaji kuwasilisha maombi yao karibu na maeneo yao na pia kuongeza uwezekano wa waombaji kupata taarifa kwa urahisi. Sasa maombi yatakuwa yanapokelewa katika ofisi ya Kanda za mafunzo ambazo zina wastani wa Mikoa mitatu hadi minne. Maombi ya Mkoa wa Rukwa yatapelekwa Kanda ya Mafunzo iliyoko Mbeya.

**MHE . DEUSDERIUS J.MIPATA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumekuwa na wito kwa Serikali kutoa posho ya mazingira magumu katika maeneo ya pembezoni ambayo yanakimbiwa na watumishi ili kutoa morali kwa watumishi hao kuendelea kudumu katika maeneo hayo. Je, Serikali iko tayari kutoa posho hiyo sasa kwasababu maeneo kama Rukwa watumishi bado wanakimbia?

Swali la pili, Chuo cha Manesi cha *Saint Bakita* kilichopo Mjini Namanyere, hutumika kutoa manesi zaidi ya 80 kwa kila mwaka. Lakini Wilaya ya Nkasi na

Mkoa wa Rukwa kwa ujumla una uhaba mkubwa sana wa Wauguzi hawa. Je, Serikali iko tayari kuwaruhusu wahitimu hawa wanaomaliza zaidi ya 80 na wengine wanapenda kubaki katika Mkoa huo lakini wanakosa fursa hiyo kwa sababu hawaruhusiwi. Je, Serikali iko tayari kutoa fursa ya kuwaruhusu wale wanaotaka kubakia katika Mkoa unaohusika wafanye hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, suala la posho ya mazingira magumu ni suala ambalo limo katika mjadala lakini pia ni suala ambalo hata Halmashauri zinaweza zikaandaa namna na taratibu za kuwawezesha wale wanahitaji kwenda kuishi katika maeneo hayo yenye mazingira magumu ili waweze kuishi kule. Lakini taratibu rasmi za kuandaa posho ya mazingira magumu itafuata hapo baadaye baada ya kufanyiwa kazi na Wizara.

Kuhusu wanafunzi wahitimu kufanya kazi katika maeneo ambayo wamesoma kwanza tunapenda tutambue kuwa Vyuo hivi vyote ni kwa ajili ya kukamilisha kusudio la Serikali kuwapata watumishi kufanya kazi katika vituo vyote vya Serikali nchi nzima. Kwa tafsri hiyo ni vyema tukaona busara inatumika katika maeneo ya vyuo ambayo watumishi wameenda kusoma pale ili wanapomaliza waweze kufanya kazi katika maeneo hayo ya karibu

Lakini vilevile maeneo ya mbali kwa ujumla wake ili kuziba pengo la watumishi katika vituo vyote nchi nzima, lakini vilevile watumishi huwa wanapata fursa baada ya kukamilisha masomo yao kuchagua kwenda kufanya kazi katika baadhi ya Mikoa ambayo wao

wanatoa kipaumbele kama nafasi zitakuwepo ili waweze kupangiwa maeneo hayo. Sasa fursa hizo wanapozijaza huwa Serikali inajaribu mara nyingi kuweza kutimiza azma zao za maeneo ambayo wao wanapenda kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kama manesi hawa watakuwa wamependa kufanyia kazi katika Mkoa wa Rukwa au hapo Nkasi fursa hizo zikiwepo na nafasi zikiwepo wanaweza kupangiwa hapo. Lakini haina maana kuwa wote wanaweza kupangiwa hapo ila wengine wanaweza kupangiwa sehemu nyingine pia.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, tulikubaliana na aliyekuwa Waziri wa Afya na Naibu wake kuwa sisi tunaotoka Wilaya za pembezoni tulete majina ili wale waliohitimu mwaka huu waweze kupangiwa na majina hayo tulishayaleta. Sasa utaendeleza jambo hili na kuwapangia kule kwasababu kuna vyuo kule Kibondo na maeneo mengine ili na sisi tupate manesi kwa sababu hatuna manesi kabisa?

**SPIKA:** Majina hayo mliyaleta kwa barua gani? Mheshimiwa Naibu Waziri labda hujayakuta ofisini.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwa vile Mheshimiwa Mb unge anasema ameleta barua hiyo Wizarani na majina ya watu kwa ajili ya kuomba kupangiwa kazi maeneo fulani, Wizara itaangalia hilo na kuweza kulifanyia kazi ipasavyo. *(Makofi)*

Na. 203

## Ununuzi wa Vifaa vya Afya

**MHE. LETICIA M. NYERERE** aliuliza:-

Ukaguzi uliofanywa ulibaini kuwa Serikali ilifanya malipo ya vifaa mbalimbali vya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, bila vifaa hivyo kuwasilishwa:-

(a) Je, kwa nini Serikali ilitoa malipo kabla ya vifaa kuwasilishwa?

(b) Je, ni lini Serikali italeta Bungeni uthibitisho wa kuwasilishwa kwa vifaa hivyo?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara ilifanya malipo kabla ya vifaa havijawasilishwa kwa utaratibu wa aina mbili, kwanza kwa bidhaa zinazopatikana hapa nchini. Mfano magari yanayouzwa kupitia kampuni ya Toyota – Tanzania, Wizara ya Miundombinu ilikuwa inasimamia ununuzi huu na hivyo Wizara ilifanya malipo kwa kuzingatia utaratibu wa manunuzi ambao ilitakiwa kulipa fedha kabla ya magari hayajawasilishwa.

Aina ya pili ya malipo ni kwa bidhaa ambazo zinapatikana nje ya nchi. Mfano magari na utaratibu wa malipo ulifanyika kwa kufungua *letter of credit* kupitia Benki ya muuzaji ambayo inakuwa kama mdhamini kati ya mnunuaji na mwuzaji, baada ya taratibu kukamilika mnunuaji huagiza Benki imlipe

muuzaji baada ya taratibu za mapokezi ya vifaa kukamilika. Kwa ufafanuzu huu Wizara ilizingatia taratibu za manunuzi. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha wa 2009/2010 Wizara ilifanya ununuzi wa magari 7 kwa matumizi ya *mobile clinics* na magari 21 aina ya *Toyota Hard Top* ambayo yalipatikana kwa njia ya zabuni iliyofanyika kwa njia ya *Letter of Credit* ambapo malipo hulipwa kupitia benki ya mwuzaji. Magari haya yalipokelewa na kugawanywa katika vyuo mbalimbali vilivyo chini ya Wizara.

Vilevile, yapo malipo yaliyofanywa kwa watoa huduma na wazabuni mbalimbali yaliyofikia Tshs. 280,482,188/= vikiwemo vifaa vya ofisi, matairi ya magari, vifaa vya usafi, chakula na kuni kwa kituo chetu cha kulelea watoto Kurasini.

Vifaa vyote hivi vilipokelewa na kuingizwa katika *Ledger* ambazo zimehakikiwa na ofisi ya Mkaguzi wa Hesabu za Serikali na hoja hizi zimefungwa.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utaratibu wa kufanya malipo kabla ya bidhaa kukabidhiwa unaweza ukapelekea baadhi *suppliers* kuleta bidhaa ambazo hazina viwango. Serikali haioni kuwa kuna haja ya kubadilisha utaratibu huu ili *suppliers* waweze ku- *supply* bidhaa kwanza halafu walipwe?

Swali la pili, zahanati zetu vijijini hutumia vifaa mabvyo hulazimika kuvichemsha ili waendelee kuvitumia kwa mgonjwa mwingine. Kwa kuwa, vijiji vingi nchini havina umeme wala maji. Je, Serikali inachukua tahadhari gani kuhusu tatizo hili.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, katika kubadilisha utaratibu kinachozungumziwa hapa ni kufuata utaratibu na Wizara, Serikali kwa ujumla tutaendelea kufuata utaratibu wa manunuzi kama ilivyoainishwa kwa mujibu wa Sheria. *(Makofil)*

Kuhusu vifaa vinavyotumika kwa ajili ya kuchemshia vifaa ninafikiri ni *machines* hizi *autoclave* unazojaribu kuziizungumzia. Mheshimiwa Mbunge kama ndivyo hivyo basi maana yake ni kwamba vifaa hivyo viko katika vifaa tiba ambavyo vinaagizwa na vinaweza kupatikana kwa ajili ya matumizi ya kuchemshia vifaa vyetu vinavyotumika kuvifanya view safi na salama wakati wa matumizi.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kugharamia mabilioni ya fedha kununua vifaa vya uchunguzi katika hospitali za ubingwa maalum lakini vifaa hivyo vilivyo vingi vimeharibika na havifanyi kazi.

Kwa mfano kifaa cha *C.T. SCAN,* Kifaa cha *O.G.D* katika hospitali ya Taifa ya Muhimbili hivi sasa ni zaidi ya mwaka mmoja havifanyi kazi na wagonjwa kulazimika kwenda *private hospitals* kama *Regency, Agha Kahn na TMJ* ambapo gharama za hospitali hizo ni kati ya

laki mbili na themanini na nane mpaka laki nne na hamsini kwa kipimo, wakati katika hospili ya Taifa ilikuwa ni shilingi elfu hamsini tu. Je, Serikali inalifahamu suala hili?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kuna baadhi ya vifaa katika hospitali zetu hasa hospitali za Rufaa ambazo baadhi ya vifaa hivyo havifanyi kazi kwa sasa ikiwemo *C.T. SCAN.* Tatizo ambalo limejitokeza hapo ni kushindwa kwa hospitali hizi kulipia gharama za *service* ambazo zilikuwa zinatakiwa kulipwa kwa mujibu wa mkataba wa kuzifanyia *service* mara kwa mara kwa vifaa vyote hivyo kwa ujumla wake.

Kwa hiyo, Serikali imejipanga kwa mwaka huu baada ya Bajeti yetu kukamilika na kupitishwa na Waheshimiwa Wabunge tutakuwa tayari kuilipa kampuni ya *Phillips* ili iweze kukamilisha zoezi ambalo walikuwa wanatakiwa kulifanya kwa kufanya matengenezo na *service* mashine zote zilizomo katika hospitali zetu ikiwemo hiyo ya *C.T. SCAN* ili iweze kuendelea kufanya kazi kama kawaida. *(Makofi)*

Na. 204

**Ujenzi wa Soko la Kimataifa - Njia Panda Himo**

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA** aliuliza:-

Serikali imeamua kujenga soko la Kimataifa katika eneo la njia Panda- Himo:-

(a) Je, utekelezaji wa ujenzi wa soko hilo umefikia hatua gani?

(b) Je, wananchi wa Vunjo watanufaika vipi na soko hilo?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daktari Augustine Lyatonga Mrema Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa juhudi zake katika kufuatilia ukamilishaji wa soko hili muhimu katika eneo lililotengwa kwa ajili ya soko la nafaka la Lokolova. Serikali ya Mkoa wa Kilimanjaro kupitia kikao chake cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (*RCC*) kilichofanyika tarehe 11 Januari, 2012 kiliridhia mapendekezo ya kujengwa kwa soko la Lokolova kuwa la Kimataifa katika Kijiji cha Lotima. Hii ilitokana na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete alipotembelea soko la Njia Panda ya Himo (Mwezi Machi, 2012) na kutoa ushauri kuwa na masoko mawili (Soko la nafaka na soko la matunda na mbogamboga).

Mheshimiwa Spika, eneo la soko la Lokolova tayari limeshapimwa na kuidhinishwa na Mkurugenzi wa upimaji ramani na kupewa hati Na. 70/2. Aidha, mchoro wa soko hilo na andiko la mradi vimeshakamilika. Mazungumzo ya awali kati ya Serikali na Mkoa, Benki ya Rasilimali Tanzania (*TIB*) na Benki ya

Ushirika na Maendeleo Vijijini (*CRDB*) yamefanyika na wote wameonesha na wanayo nia ya kuwekeza katika soko la Lokolova lenye ekari 140.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa shughuli ambazo zimefanyika katika soko la mbogamboga na matunda lililoko njia panda ya Himo lenye ekari 9.9 ni pamoja na utengenezaji wa barabara ya kuingia sokoni, ujenzi wa ofisi za soko, choo na kuimarisha huduma za maji. Aidha, kiwanja hicho kimesafishwa na kusawazishwa kwa maandalizi na kuanza. Katika mwaka wa fedha 2012/2013, Halmashauri kupitia mradi wa *ASDP* imeomba jumla ya shilingi milioni 200 katika maombi ya awali na shilingi bilioni 2.5 kama maombi maalum kwa ajili ya ujenzi wa soko hili.

(b) Mheshimiwa Spika, kujengwa kwa masoko haya mawili kutakuwa na manufaa mengi kwa Mkoa, Wilaya ya Moshi Vijijini na wananchi wa Vunjo kwa ujumla. Baadhi ya manufaa na faida zitakazotokana na kuwepo kwa masoko hayo, ni ajira kwa vijana wa Wilaya ya Moshi Vijijini wakiwemo vijana wa Jimbo la Vunjo, usindikaji wa bidhaa za kilimo kwa kuongeza thamani, ongezeko la kipato kwa wakulima wanaozunguka eneo hilo, kukua kwa biashara nyingine kama maduka, hoteli, migahawa, nyumba za kulala wageni na hivyo kuchangia katika jitihada za Serikali kupunguza umaskini nchini na kuongezeka kwa pato la Taifa (*GDP*).

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru sana Waziri wa Viwanda na Biashara kwa maneno yake yenye matumaini kwa

wananchi wa Vunjo, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa soko hili litakuwa kubwa, ni soko la Kimataifa ambalo litaunganisha wakulima wa nafaka wa Rukwa, Songea, Mbeya, Iringa na pia litaunganisha wafanyabiashara mashuhuri kutoka Kenya, Somalia mpaka Sudan watakuwa pale Lokolova. Je, Serikali ina mpango gani wa kuingiza soko hili katika mpango wa *EPZ*?

Mheshimiwa Spika, ningeomba kujua Serikali itawashirikisha vipi wawekezaji na wadau ambao watafanya kazi katika soko hilo, watajenga soko hilo, wadau wanaotoka Vunjo Mkoa wa Kilimanjaro na Tanzania kwa ujumla?

**SPIKA:** Waziri naomba ujibu kwa kifupi kwa sababu jibu lake lilikuwa refu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, hivi sasa Wizara ipo katika mpango na mchakato wa kuingiza soko la Lokolova katika *EPZ* ili kuhakikisha kwamba mazao yanayopatikana pale yanasindikwa na kuongezwa thamani ya mazao hayo. Lakini vile vile tayari Serikali tupo katika utaratibu wa kujenga maghala ya kuhifadhi nafaka zile kabla na baada ya kusindikwa na tunao utaratibu sasa wa kushirikisha wadau wengine kupitia utaratibu wa *PPP*.

Mheshimiwa Spika, pili, tayari Mkoa wa Kilimanjaro umeshapanga kufanya kikao mwezi Agosti, 2012. Katika kikao hicho Mkoa unataraji kuitisha wawekezaji ili kuunga jitihada za Serikali za kuanzisha soko hili na

vile vile wao kuwa ndiyo wadau wa kwanza watakaoitishwa kuwekeza katika soko hili.

Na. 205

**Walimu Kucheleweshewa Madai yao**

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM** aliuliza:-

Kumejitokeza malalamiko ya mara kwa mara kwa Walimu kucheleweshewa madai yao ambayo wanadai Serikalini.

(a) Je, kwa nini mchakato wa kuhakiki madeni ya Walimu huchukua muda mrefu kiasi cha kuwaletea usumbufu katika kudai haki zao?

(b) Je, ni Walimu wangapi wameshalipwa na wangapi hawajalipwa madai yao kuanzia Juni, 2010 hadi Aprili, 2011 kwa mchanganuo wa kila Mkoa Tanzania Bara?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tatizo la Walimu kucheleweshewa kulipwa madai yao linatokana na sababu mbalimbali zikiwemo:-

(i) Walimu kuchelewa kutuma madai yao hivyo kulazimika kusubiri mwaka wa fedha unaofuata;

(ii) Baadhi ya Walimu kutowasilisha vielelezo muhimu kama vile fomu za madai, stakabadhi, tiketi, hati za kuzaliwa na hati za ndoa pamoja na barua ya kuripoti kituo kipya; na

(iii) Baadhi ya vielelezo kuwa na dosari za kiuhasibu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuharakisha ulipaji wa madai ya Walimu kwa kutoa maelekezo kwa walimu kupitia Wakuu wa Shule za Sekondari, kuhusu namna bora ya kuwasilisha madai na vielelezo muhimu ili yaweze kulipwa kwa wakati.

(b) Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Novemba 2011 jumla ya madai ya Walimu yenye thamani ya shilingi 52,053,314,239.41 yaliwasilishwa. Madai haya yanajumuisha madai ya walimu walio chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa shilingi 44,876,270,992.25, na walimu walio chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi shilingi 7,177,043,245.16.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2012, Wizara yangu ilishughulikia madai yasiyo ya malimbikizo ya mishahara ya Walimu 2,649 yenye thamani ya shilingi 3,453,111,980.00. Kati ya hayo

madai ya Walimu 1,653 yenye thamani ya shilingi 1,415,600,443.93 yalikubaliwa na kulipwa. Aidha, jumla ya madai ya walimu 996 yenye thamani ya shilingi 2,037,510,536.95 yalikataliwa kutokana na kutokuwepo kwa viambatisho na vielelezo vya kutosha ili kukidhi malipo.

Mheshimiwa Spika, walimu 23,167 walio chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa waliwasilisha madai yao yasiyo ya mishahara Serikalini. Kati yao walimu 18,344 walilipwa madai yao yenye thamani ya shilingi 16,567,655,437.34. Hivyo, jumla ya walimu 19,922 walio chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi wameshalipwa madai yao na walimu 5,819 bado hawajalipwa kutokana na sababu nilizozieleza.

Mheshimiwa Spika, orodha ya walimu waliolipwa na ambao hawajalipwa na ambao hawajalipwa kimkoa ni ndefu mno, hivyo nashauri Mheshimiwa Mbunge anione ili niweze kumpatia nakala.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, naomba muangalie muda niko *beyond* muda, nitamwita mwenye swali la msingi tu.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika nashukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza. Kabla ya swali la kwanza, swali langu la pili lilihusu ni wangapi, nilitaka idadi, sikuhitaji orodha, kwa hiyo Kiswahili kidogo kimeteleza, lakini kama ipo orodha nitaichukua.

Swali la kwanza; kwa kuwa imebainika fedha za mabadiliko ya mishahara ya Walimu wanaopandishwa madaraja yao huchukua muda wa miaka miwili hadi miaka mitatu ndiyo walimu hao huzipata kwa kurekebishiwa mishahara yao, baya zaidi hata pale wanapobadilishiwa mishahara yao, malimbikizo yao (*arrears*) huwa wanapunjwa. Je, tabia hii mbaya ya uwongo kwa Serikali ya kuwadanganya Walimu…

**SPIKA:** Hebu ondoa maneno yako ya uwongo kabla hujaendelea.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika nayaondoa.

**SPIKA:** Haya.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, tabia hii mbaya ya Serikali ya kuwapunja walimu fedha zao zinazostahili kwa wakati ni lini itakoma, hasa ukizingatia Waziri mwenyewe asingeweza kujibu maswali hapa vizuri kama si juhudi za Walimu? Kama si kweli kanusha.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, moja ya madai makubwa ya walimu ya muda mrefu ni posho ya kufundishia (*Teaching Allowance*). Je, Serikali ina mkakati gani wa ziada wa kuwapatia posho za kufundishia *teaching allowance* walimu, hasa ukizingatia mishahara yao ni midogo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimwambie Mbunge kwamba, Serikali haina nia mbaya na Walimu ya kuchelewesha malimbikizo ya fedha ya mishahara na yasiyo ya mishahara. Kama nilivyosema kuna sababu nyingi sana zinazofanya Serikali ichelewe hata kulipa madeni haya. Wakati najibu swali wiki iliyopita nilisema fedha zipo, Ofisi ya Waziri Mkuu, fedha zipo na zingine zimebaki, Wizara ya Elimu pia fedha zipo na zingine zimebaki. Sasa namna ya kulipa madeni hayo tunahitaji uhalali na viambatisho vilivyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, wote mtashuhudia kwamba zoezi la *CAG* mwaka huu limekwenda kwa uhakiki zaidi na Wahasibu wetu wanaogopa kulipa fedha ilimradi wanalipa tu, wanahitaji viambatanisho vilivyo sahihi. Napenda kuwaambia walimu wote nchini kwamba walete viambatanisho vilivyo sahihi, vyeti vya ndoa, vyeti vya kuzaliwa, lakini vile vile tiketi na kadhalika. Yote wanayodai, tunakosa kuwalipa hapa ni kwa shabby Walimu wetu hawaleti taarifa zilizo sahihi. Naomba siku moja kama naweza kupata nafasi nioneshe matatizo ya jinsi tunavyosumbuka kulipa madeni haya. Lakini fedha za Serikali zipo ila namna ya kuanza kulipa ni suala la kiuhasibu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la *Teaching Allowance*, hili limekaa katika mfumo wa *budgetary constraint*s kwamba tulishasema tuna fedha shilingi bilioni 22 za kuanza kulipa walimu kwenye ile *teaching hardship*. Lakini kule kwenye Halmashauri kuna Walimu, kuna watu wa Afya, kuna Wagani, tunaendelea kuangalia namna gani ya kuweza kuzilipa hizi fedha

kwa watumishi wote Serikalini, kwa sababu si Walimu tu wenye matatizo, hata watu wa afya wapo, Wagani na kadhalika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge leo tena nimepewa maswali kumi na moja badala ya kumi kinyume cha utaratibu na saa imefika mpaka na robo, siwezi ku-*entertain*. Nitamwomba Mheshimiwa Profesa Kahigi aulize swali linalofuata.

Na. 206

**Tatizo la Vijana Kutoendelea na Masomo**

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI** aliuliza:-

Katika Wilaya ya Bukombe kuna tatizo la vijana wengi wanaomaliza Darasa la Saba na Kidato cha Nne ambao hawaendelei na masomo:-

(a) Je, Serikali ina mipango gani ya kusaidia Wilaya kama Bukombe ambazo hazina Chuo cha Ufundi cha aina yeyote?

(b) Je, Serikali imeandaa miradi ipi ya kuwasaidia vijana hao wasio na matumaini ili waweze kumudu maisha?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Kulikoyela Kanalwanda Kahigi, Mbunge wa Bukombe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 na mwaka 2010 pamoja na mambo mengine iliahidi na kuagiza Serikali kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi katika kila Wilaya zisizo na Vyuo hivyo. Lengo ni kuwawezesha wahitimu wa Darasa VII na Kidato cha IV waliokosa nafasi ya kuendelea na masomo kupata stadi za kujiajiri au kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza agizo hilo, Wizara yangu imeandaa mpango wa ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi vya Wilaya zisizo na Vyuo vya Ufundi vya aina yoyote. Katika hatua ya kwanza mpango huu umefanya utambuzi wa mahitaji ya stadi zinazohitajika kufundishwa katika Wilaya 43 ikiwa ni pamoja na Wilaya ya Bukombe.

Wilaya hizo zimepangwa katika awamu mbili za utekelezaji wa ujenzi ambapo Wilaya ya Bukombe ipo katika awamu ya kwanza. Aidha, katika awamu hiyo mwaka 2011/2012 ujenzi umeanza kwenye Wilaya ya Makete na mwaka huu wa fedha ujenzi utaendelea katika Wilaya za Kilindi, Ukerewe, Chunya na Namtumbo katika mwaka 2012/2013, pale Wabunge mtakapopitisha bajeti yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wilaya ya Bukombe imeshafanyiwa utambuzi wa stadi na kwa kuwa ipo katika awamu ya kwanza, namwomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Wilaya hiyo kuendelea kuwa na subira wakati Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyuo hivyo ambapo Wilaya ya Bukombe inahusika. Aidha, wananchi na vijana wa Wilaya hiyo wanashauriwa kupata huduma ya Vyuo vya Ufundi Stadi katika vyuo jirani ambavyo ni pamoja na Chuo cha Ufundi Stadi Shinyanga Shinyanga (*VTC*) na Chuo cha Ufundi Mwanza, Mwanza (*RVTC*) wakati wakisubiri ujenzi wa Chuo cha Wilaya hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ushauri kwa vijana wote nchini wakiwemo wa Wilaya ya Bukombe ambao hawakupata fursa za kuendelea na masomo kujiunga katika vikundi vidogo vidogo *SACCOS* ili waweze kupata mikopo na hivyo kujiajiri katika fursa za kiuchumi zikiwemo kilimo cha tumbaku na pamba, ufugaji nyuki, uchimbaji mdogo wa dhahabu, ufugaji ng'ombe na biashara ndogo ndogo.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, kama awamu ya kwanza ilikuwa imeanza kwa ujenzi wa Chuo cha Ufundi Makete, awamu ya pili itaanza lini?

Swali la pili, Naibu Waziri anaweza kuniambia ni lini hasa Chuo cha Ufundi Bukombe kitajengwa kwa sababu wananchi wa Bukombe wamesubiri sana kwa muda mrefu na hawana Chuo cha aina yoyote, Chuo cha Ualimu wala Chuo cha Ufundi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza kama nilivyosema kwamba tumeanza na Wilaya ya Makete na Wabunge naomba mtambue kuwa Vyuo vya *VETA* gharama yake ni tofauti kabisa na hizi shule zetu za Kata. Chuo kimoja mpaka kikamilike na kuweka miundombinu na karakana zote inachukua takribani bilioni sita. Kwa hiyo, hatuwezi kwenda kwa mfumo wa vyuo vyote nchi nzima, tunakwenda kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mwaka wa fedha wa jana tumeanza na Wilaya ya Makete na mwaka huu kama nilivyosema kwamba tutaanza Wilaya nne na hii ni lazima niseme kwa Wabunge kwamba Serikali badala ya kutegemea fedha za nje, mwaka huu tumepanga bajeti ya ndani ili iweze kutekelezeka kwa Wilaya ya Namtumbo, Wilaya ya Chunya, Wilaya ya Ukerewe na Wilaya ya Kilindi. Tutaanza mwaka huu wa fedha baada ya kupitisha bajeti ya Wizara yetu. Kwa hiyo, hii ni furaha kwamba hatutategemea fedha za nje bali ni fedha za ndani zetu wenyewe.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tumechukua muda ambao siyo wa maswali kumalizia maswali na naomba ofisi yangu ikumbuke kwamba maswali ni kumi na siyo zaidi ya hapo, yanaleta matatizo.

Waheshimiwa Wabunge naomba niwatambulishe wageni tulionao asubuhi ya leo, kwanza kabisa tunao wageni wa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha ambaye kwanza ni mke wake, Bi Asha Shamsi Nahodha asimame mahali alipo, ahsante sana. *(Makofi)*

Tunao wageni kutoka Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwanza kabisa ni Ndugu Job D. Masima Katibu Mkuu wa Wizara, ahsante. Tunaye Injinia Musa I. Iyombe, Naibu Katibu Mkuu na Jenerali Davis Mwamunyange, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi nchini. Pia tunaye Luteni Jenerali Abdulraham Shimbo, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, tunaye *Major General* Samwel A. Ndomba, Mkuu wa JKT. Pia tunaye *Major General* Salum Kijuu, Mkuu wa Kambi ya Nchi Kavu. Ahsante na karibuni. (*Makofi*)

Tunaye vile vile *Major General* Omar, Mkuu wa Kamandi ya Wanamaji. Tunaye *Brigadier General* Kapwani, Mkuu wa Kamandi ya Anga. Tuna Bwana Hababilar Ngayonga, Kamishina wa Sera na Mipango. (*Makofi*)

Halafu naomba *Major Generals* wote wasimame walipo, tunao *Brigadier Generals,* wote wasimame walipo maana naona majina yao hayakutajwa. Tunao Makamishna na Makamishna Wasaidizi wote walipo wasimame kokote waliko. Ahsante sana. Ahsante sana kwa ujumla tunawakaribisha wote ambao mnahusika na Wizara yenu siku ya leo. Nadhani mtakuwa na siku nzima. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wako wageni wawili wa Mheshimiwa Daktari Festus Limbu hawa nafikiri Mr. Valentin Mehling na Mr. Micha

Podding ni wageni hawa, lakini hakueleza wanakuja kufanya nini.

Halafu ninao wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo, hawa niwa wageni wa Mheshimiwa *Brigadier General* Hassan Ngwilizi ambao ni Madiwani 21, Wenyeviti wa Kata 16 na wazee pamoja na Makada 11 kutoka Jimbo la Mlalo, Lushoto wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri, Mheshimiwa Lucas Shendolwa, Wageni wote hawa niliowataja wasimame pale walipo. Ahsante sana. Mheshimiwa Ngwilizi ana ugeni mzito tunawakaribisheni, poleni na safari. (*Makofi*)

Halafu tuna wana kikundi 10 kutoka Kikundi cha Shirika Maendeleo Endelevu sijui wapi huko? Wasimame hao washiriki maendeleo Endelevu sijui ni wapi huko. Mnakaribishwa labda watu watajifunza kujua hayo maendeleo endelevu ni kitu gani. Sijui hata wanatoka wapi. Ahsante sana na karibu. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 19 kutoka Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi ya Tiba, Bugando wanaofanya mazoezi hapa Dodoma. Hawa nao wako wapi? Ahsante karibuni sana tunategemea mtafanya kazi yenu kufuatana na wito ambao Mwenyezi Mungu amewapeni. Ahsante sana. *(Makofi)*

Tuna Doctor Fratelihe Kashanga, huyo ni Mhadhiri Mkuu, Chuo Kikuu cha Elimu Chang'ombe. Yuko wapi huyu, ahsante sana na karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mrema yeye hapeleki majina huko wanakoandika, kwa hiyo wakati mwingine tunashindwa kushindwa. Wako Ma-*sister* wanatoka Shirika la *Holly Spirit* huko Marangu – Vunjo naomba Ma-*sister* wasimame. Ni Sister Justa Mboya na mwenzake. Ahsante karibuni sana Ma-*sister* nashukuru sana.

Wageni wengine wote kwa kweli tunapenda kuwakaribisheni, hili Bunge ni la watu wote, kwa hiyo wanaotajwa ni wachache lakini wote mnakaribishwa. Tunaendelea na shughuli inayofuata.

Kabla ya hapo wale Wabunge wanaotoka maeneo yanayolima pamba wanaombwa wakutane Ukumbi wa Msekwa B, saa saba mchana. Hizi ni taarifa za vikaratasi.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliyenijalia afya njema na kuniwezesha kuwasilisha hotuba yangu ya bajeti kwa mwaka 2012/2013. Pili, namshukuru kwa dhati Mheshimiwa Daktari Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuniteua kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Nawathibitishia Waheshimiwa Wabunge wenzangu na wananchi wote wa Tanzania kwa ujumla kwamba nitatekeleza majukumu niliyokabidhiwa kwa umakini na uaminifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, tatu, napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Mawaziri na Manaibu Mawaziri walioteuliwa kushika nyadhifa hizi hivi karibuni. Vile vile nampongeza Mheshimiwa James Mbatia kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge. Nampongeza pia Mheshimiwa Mussa Azan Zungu kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge. Vile vile napenda kuwapongeza Watanzania waliochaguliwa na Bunge letu Tukufu kuwa Wabunge wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2011/2012, Wabunge wenzetu watatu waliiaga dunia. Wabunge hao ni Marehemu Jeremiah Sumari, Marehemu Mussa Silima na Marehemu Regia Mtema. Napenda kutoa pole za dhati kwako Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, ndugu, marafiki na Watanzania wote kwa ujumla kwa msiba huo mkubwa uliotupata. Namuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho zao Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika, napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Edward Lowassa, Mbunge wa Monduli kwa kutupa ushauri na mapendekezo mazuri sana wakati wakichambua mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu. Kamati hii imekuwa ikiishauri vyema Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu njia mbalimbali za kuimarisha utendaji wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Kujenga Taifa ili liweze kutekeleza majukumu yake ya Ulinzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa maelezo yangu kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2012/2013, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge kuwapongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, Waziri Mkuu; Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Daktari William Mgimwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Uhusiano na Uratibu), Mheshimiwa Steven Wasira kwa hotuba zao ambazo zimetoa mwelekeo katika masuala ya Mipango, Uchumi, Mapato na matumizi ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Dira ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni kuwa Taasisi iliyotukuka katika kudumisha amani na usalama wa Taifa. Aidha, Dhima ya Wizara hii ni kulinda eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania dhidi ya adui wa aina yoyote kutoka nje au ndani ya nchi na kuhakikisha uhuru na maslahi ya Taifa vinalindwa. Kutokana na Dira na Dhima hiyo, shabaha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni

kujenga na kuendeleza Jeshi la Wananchi wa Tanzania na vyombo vyake yaani Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) pamoja na Mashirika yake ya Mzinga, Nyumbu na SUMAJKT ili kuwa vya kisasa na imara katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imekabidhiwa majukumu ya kulinda uhuru na mipaka ya nchi yetu. Kwa mujibu wa Sheria ya Ulinzi wa Taifa ya mwaka 1966, majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni saba:-

(1) Wizara ina jukumu la kulinda mipaka ya nchi yetu;

(2) Wizara inasaidiana na Mamlaka za Kiraia katika kukabiliana na majanga ili kuwapatia wananchi waliofikwa na majanga misaada ya kibinadamu;

(3) Wizara inashiriki katika shughuli za Ulinzi wa Amani katika nchi zenye migogoro duniani;

(4) Wizara inaandaa umma wa Watanzania kushiriki katika shughuli za Ulinzi wa Taifa;

(5) Tano, Wizara inaimarisha moyo wa uzalendo na mshikamano wa Kitaifa miongoni mwa vijana wa Kitanzania na kuwaandaa kikamilifu katika shughuli za uzalishaji mali ili kukuza moyo wa kujitegemea;

(6) Sita, Wizara inafanya utafiti na kuendeleza teknolojia kwa ajili ya matumizi ya kijeshi na kiraia; na

(7) Saba, Wizara inasaidia kuimarisha amani na utengamano na nchi nyingine duniani hasa nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilikusudia kutekeleza malengo manane katika mwaka 2011/2012:-

(1) Wizara iliandikisha wanajeshi wapya na kuimarisha mafunzo na mazoezi ya kijeshi;

(2) Wizara iliimarisha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana wa kujitolea;

(3) Wizara iligharamia huduma muhimu ikiwemo umeme, maji, simu, mafuta na vilainisho kwa ajili ya uendeshaji wa majukumu ya msingi;

(4) Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliwapatia chakula, tiba na sare za wanajeshi, vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa na Watumishi raia;

(5) Wizara iliendeleza ushirikiano na nchi nyingine duniani katika nyanja za kijeshi;

(6) Wizara ilinunua zana na vifaa mbalimbali vya kijeshi;

(7) Wizara ilitekeleza mradi wa ujenzi wa maghala ya kuhifadhia silaha na milipuko; na

(8) Wizara pia ilijenga na kukarabati baadhi ya majengo na miundombinu katika Makambi ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, hali ya usalama wa mipaka katika mwaka 2011/2012, kwa kuwa jukumu kuu la Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni kulinda mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, uhuru na maslahi ya Taifa *(vital national interests),* naomba sasa nielezee hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi yetu katika mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki hali ya ulinzi na usalama wa mipaka yetu na nchi jirani ilikuwa shwari. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeendelea kudhibiti ipasavyo ulinzi wa mipaka yote ya Tanzania ili kuhakikisha kuwa nchi yetu inaendelea kuwa salama. Aidha, matukio ya uharamia katika eneo letu la Mwambao wa Bahari ya Hindi yalipungua. Kwa jumla kulikuwa na tukio moja tu la utekaji wa meli na majaribio matatu ya kutaka kuteka meli ukilinganisha na mwaka 2010/2011 ambapo meli nne zilitekwa na kulikuwa na majaribio 10 ya kutaka kuteka meli.

Mheshimiwa Spika, Jeshi liliwakamata maharamia hao na kuwakabidhi kwa vyombo vya dola kwa hatua za kisheria. Katika kipindi hiki vurugu katika baadhi ya nchi jirani zimesababisha ongezeko la wahalifu wanaoingia nchini wakiwa na silaha kwa lengo la kufanya vitendo vya ujambazi. Jeshi la Wananchi linaendelea kuimarisha ulinzi wa maeneo ya mipaka inayozunguka nchi yetu ili kudhibiti vitendo hivyo.

Mheshimiwa Spika, mpaka katika bahari ya Hindi una urefu wa kilomita 1,424. Katika mpaka huu

Tanzania inapakana na nchi za Kenya, Visiwa vya Ushelisheli, Komoro na Msumbiji. Hali ya usalama katika mpaka wa Bahari ya Hindi ilikuwa nzuri. Matukio ya vitendo vya uharamia yameanza kupungua kufuatia operesheni zinazofanywa na Jeshi letu la Wanamaji katika eneo la Bahari ya Hindi. Serikali pia inaendelea kuchukua hatua za kudhibiti vitendo vya uharamia katika mipaka yetu kwa kuimarisha uwezo wa Jeshi letu kiutendaji ili liweze kupambana na maharamia hao kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, katika mpaka wa Kaskazini, Tanzania imepakana na Kenya. Hali ya usalama wa mpaka wetu wa kaskazini kwa ujumla imekuwa shwari. Hata hivyo, kumejitokeza tatizo la ung'oaji wa alama za mipakani (*beacons*) unaofanywa na watu wanaoishi kwenye mpaka kwa lengo la kujipatia ardhi kwa ajili ya shughuli za kilimo, malisho ya mifugo na ujenzi wa makazi. Hapana shaka tatizo hili linatishia usalama wetu. Serikali inafanya mipango ya kurudisha alama hizo za mipakani.

Mheshimiwa Spika, vile vile Serikali inafanya uchambuzi wa gharama zinazohitajika katika ujenzi wa barabara za usalama mipakani *(Security roads).* Lakini kutokana na ukubwa wa kazi hii Serikali haitaweza kuitekeleza mara moja. Kazi ya ujenzi wa barabara za usalama mipakani itatekelezwa kwa awamu kwa kuanzia na maeneo ya mpakani yenye matishio mengi ya usalama ikiwemo mpaka wetu wa Magharibi.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali yetu ikiendelea kuchukua hatua kukabiliana na tatizo hili nawasihi

wananchi hasa wale wanaoishi katika maeneo ya mipakani kuheshimu na kuzitunza alama za mipakani kwa sababu alama hizi zina umuhimu mkubwa katika kudumisha ulinzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika mpaka wa Magharibi Tanzania inapakana na Burundi, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Hali ya usalama katika eneo la mpaka huu ni ya wastani. Hata hivyo, kumekuwepo na matukio ya ujambazi yanayofanywa na watu wenye silaha wanaodhaniwa wanatoka katika nchi jirani hasa Kongo na Burundi. Majambazi haya yamekuwa yakiwashambulia wavuvi na kuwanyang'anya vifaa vya uvuvi na wakati mwingine kuwaua. Mnamo mwezi Mei, 2012 majambazi yenye silaha za kivita kutoka nchi jirani waliwapora wavuvi wetu katika Ziwa Tanganyika, kufanya mauaji na kuwajeruhi askari.

Tukio hili ni mwendelezo wa matukio ya ujambazi yanayofanywa kwenye Ziwa Tanganyika. Jeshi la Wananchi wa Tanzania linaendelea kuchukua hatua madhubuti ya kukabiliana na vitendo hivyo vya ujambazi katika Ziwa Tanganyika. Katika kukabiliana na matukio hayo Serikali inafanya mipango ya kuipatia Kamandi ya Jeshi la Wanamaji meli na boti ziendazo kasi za kufanyia doria baharini na maziwa makubwa hasa Ziwa Tanganyika. Kwa nchi kavu jeshi katika eneo la Ziwa Tanganyika tayari limeanza utaratibu wa kuimarisha ulinzi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, katika mpaka wa Kusini Tanzania inapakana na Msumbiji, Malawi na Zambia.

Hali ya usalama katika mpaka huu imeendelea kuwa shwari. Hata hivyo, hivi karibuni zimejitokeza dalili za kuhatarisha usalama wa mpaka huo hasa kwenye eneo la Ziwa Nyasa. Serikali imeiagiza Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kutumia njia za kidiplomasia ili kulipatia suala hili ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa viashiria vya kuhatarisha usalama katika baadhi ya maeneo ya mipakani, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu na wananchi wote kwa jumla kwamba Jeshi letu limejiandaa vyema na lina uwezo mkubwa wa kukabiliana na tishio la aina yoyote dhidi ya uhuru na usalama wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapitio ya utekelezaji wa mpango na Bajeti ya Mwaka 2011/2012, naomba sasa nitoe taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2011/2012. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilikusudia kutekeleza malengo ya mpango mkakati wa kuimarisha utendaji na maslahi ya Wanajeshi kwa kipindi cha mwaka 2010/2011 hadi 2024/2025. Utekelezaji wa bajeti pia ulizingatia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 inayosisitiza umuhimu wa kujenga Jeshi dogo la kisasa, shupavu na lenye weledi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, ili kufikia azma hiyo bajeti ya mwaka 2011/2012, ililenga katika kununua zana na vifaa mbalimbali vya kijeshi, kujenga maghala ya kisasa ya kuhifadhia silaha na milipuko, kukarabati na kujenga nyumba za makazi katika makambi, shule,

vyuo na ofisi. Aidha, bajeti hiyo ilidhamiria kuimarisha malipo ya mishahara, posho, mavazi, usafiri na huduma za matibabu. Kwa ujumla utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka 2011/2012 ulikuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwisho wa mwezi Aprili, 2012, Mafungu ya Wizara hii yalikusanya mapato ya shilingi 47,123,636.00 ikilinganishwa na makadirio ya shilingi 28,355,000.00. Sehemu kubwa ya makusanyo haya ni maduhuli kutokana na mauzo ya nyaraka za zabuni na mapato kutokana na shughuli za mafunzo kwa vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliidhinishiwa jumla ya sh. 802,469,838,700.00 ambazo kati yake sh. 653,551,016,700.00 sawa na asilimia 81 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na sh. 148,918,822,000.00 sawa na asilimia 20 kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Juni, 2012, Wizara yangu ilipatiwa jumla ya sh. 797,251,016,700.00 sawa na asilimia 99 ya bajeti iliyoidhinishwa yaani sh. 802,469,838,700.00. Kati ya fedha hizo, sh. 653,551,016,700.00 zilitumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 100 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya shughuli hizo. Fedha zilizotolewa na kutumika kwa ajili ya shughuli za Maendeleo zilikuwa sh. 143,700,000,000.00 sawa na asilimia 96 ya sh. 148,918,822,000.00 zilizoidhinishwa kwa ajili ya shughuli hizo. Kwa hiyo, kiasi cha sh.

5,218,822,000.00 kilichoidhinishwa kwa shughuli za maendeleo hakikutolewa. Mchanganuo wa bajeti na matumizi hayo umeoneshwa kwenye mafungu matatu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, mafunzo na mazoezi ya Kijeshi kwa Wanajeshi, katika mwaka 2011/2012, Jeshi la Ulinzi limewapatia mafunzo maafisa na askari ili kuwawezesha kumudu vyema kuzitumia silaha, zana na vifaa vya kijeshi zinazotumika katika kutekeleza majukumu ya Ulinzi wa Taifa. Vile vile maafisa na askari walipatiwa kozi katika vyuo na vituo vya mafunzo ndani na nje ya nchi. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania lina jumla ya maafisa na askari 672 katika Vyuo Vikuu na Taasisi za elimu nchini na 113 wanaosoma kozi za kijeshi nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Ulinzi pia lilishiriki katika mazoezi ya pamoja na majeshi ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kutokana na makubaliano ya ushirikiano wa kiulinzi katika Jumuiya hiyo. Halikadhalika, Jeshi lilifanya mafunzo mawili. Kwanza, Jeshi liliandaa zoezi la *Natural Fire* -II lililofanyika mwezi Septemba, 2011 huko Zanzibar. Pili, Jeshi lilifanya zoezi la Ushirikiano Imara lililofanyika mwezi Oktoba, 2011 nchini Rwanda.

Mheshimiwa Spika, mafunzo kwa Jeshi la Akiba, Jeshi la Ulinzi limeendelea kuendesha mafunzo ya awali na uongozi mdogo kwa mgambo hapa nchini. Mafunzo ya mgambo yaliendeshwa katika mikoa 21 ya Tanzania Bara ambapo wananchi 12,825 walipata mafunzo hayo. Vile vile wanamgambo 40 walipewa

mafunzo ya uongozi mdogo ili kupata ujuzi wa kuwasimamia na kuwaongoza wanamgambo walio chini yao.

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa zana na vifaa vya Kijeshi, katika mwaka 2011/2012, Serikali imeendelea kuelekeza mkakati wa kuimarisha Jeshi la Wananchi kwa kulinunulia zana na vifaa vya kisasa. Miongoni mwa zana hizo zilizonunuliwa ni zile tulizozionesha kwenye uwanja wa Uhuru siku ya kilele cha Maadhimisho ya Miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara tarehe 9 Desemba, 2011. Aidha, kupitia mkakati huo, Kamandi ya Jeshi la Anga limepatiwa zana na vifaa muhimu ili kuimarisha utendaji kazi. Kamandi ya Jeshi la Nchi Kavu pia ilipatiwa zana na vifaa vipya.

Mheshimiwa Spika, matengenezo na ukarabati wa zana na vifaa kama mnavyoelewa gharama za ununuzi wa zana za kijeshi na ukarabati wake ni mkubwa sana ukilinganisha na uwezo wa kifedha tuliokuwa nao. Serikali imeweza kugharamia asilimia 20 ya mahitaji ya ukarabati na ununuzi wa zana mpya katika mwaka 2011/2012. Kwa kutambua umuhimu wa suala hili, Serikali inafanya juhudi ya kutafuta fedha kutekeleza mpango maalum wa matengenezo na ukarabati wa zana na vifaa vya jeshi letu kwa kutumia Taasisi yetu ya Nyumbu. Mpango huu ni muhimu hasa ukizingatia kwamba uwezo wetu wa kununua vifaa na zana mpya ni mdogo kama nilivyosema hapo awali.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano wa kiulinzi na kijeshi na nchi nyingine duniani ushirikiano kati ya nchi yetu na nchi nyingine katika nyanja za kijeshi ni suala muhimu

katika kudumisha usalama na amani duniani. Katika mwaka 2011/2012, ushirikiano huo ulitekelezwa kupitia ushirikiano baina ya nchi na nchi (*bilateral cooperation*), ushirikiano wa Kikanda (*regional cooperation)* na ushirikiano wa Kimataifa *(multilateral cooperation).*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali imeendelea kudumisha ushirikiano katika nyanja za kijeshi baina ya nchi yetu na nchi nyingine. Nchi tunazoshirikiana nazo ni pamoja na Canada, China, India, Jordan, Marekani, Uingereza, Ujerumani, Ufaransa, Uturuki na Umoja wa Falme za Kiarabu. Katika kuimarisha ushirikiano huo, Wizara inakusudia kufungua ofisi mpya za Waambata wa Jeshi katika nchi za Malawi, Ujerumani na Umoja wa Falme za Kiarabu. Ushirikiano baina ya nchi yetu na nchi nilizozitaja umejikita katika upatikanaji wa zana na vifaa, mafunzo na mazoezi ya kijeshi, misaada ya tiba, mafunzo ya ulinzi wa amani, mapambano dhidi ya uharamia, utafiti, uchunguzi wa milipuko katika makambi, teknolojia na michezo. Napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali na Majeshi ya nchi hizo kwa ushirikiano mzuri waliotupatia.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano wa kijeshi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika *(SADC)* ili kudumisha amani katika ukanda huu. Ushirikiano na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki unaendelea katika nyanja za mafunzo, mazoezi ya pamoja na michezo baina ya

majeshi ya nchi hizo. Majeshi yetu pia yamekuwa yakibadilishana taarifa za kiulinzi na usalama.

Mheshimiwa Spika, vile vile kupitia ushirikiano wa kiulinzi na kijeshi na Nchi za *SADC* tarehe 7 Februari, 2012, nchi yetu ilisaini makubaliano ya ulinzi wa pamoja kwenye Bahari ya Hindi na nchi za Afrika Kusini na Msumbiji ikiwa ni jitihada za kukabiliana na tatizo la uharamia.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inao wajibu mkubwa katika kushirikiana na nchi nyingine ili kudumisha amani duniani. Nchi yetu imekuwa ikishiriki katika operesheni mbalimbali za kulinda amani zinazoongozwa na Umoja wa Mataifa katika nchi zenye migogoro. Mpaka sasa Jeshi letu la Ulinzi limepeleka jumla ya wanajeshi 1,081 kushiriki operesheni za Ulinzi wa Amani katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Ivory Coast, Lebanon na Darfur – Sudan. Kutokana na utendaji mzuri wa vikundi vyetu vya Ulinzi wa Amani, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa limeiomba Serikali ya Tanzania kupeleka waangalizi wa amani kati ya 100 na 200 nchini Syria. Serikali imekubali ombi hilo.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Makao Makuu ya Jeshi yanafanya maandalizi ya kuwapeleka waangalizi hao Syria ili waweze kushiriki kwenye operesheni hiyo. Kutokana na uwezo mkubwa wa Makamanda wa Jeshi letu la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ninayo furaha kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa miongoni mwa Makamanda wa ngazi za juu wa Vikosi vya Umoja wa Mataifa vilivyopo huko Darfur-Sudan mmoja ni Mtanzania aliyekuwa Kamanda wa Kamandi ya

Jeshi la Nchi Kavu ya Jeshi letu la Ulinzi, Meja Jenerali Wynjones Kisamba. Meja Jenerali Kisamba ni Naibu Kamanda wa vikosi hivyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shughuli za Ulinzi wa Taifa Jeshi la Wananchi pia linatekeleza shughuli za viwanda. Shirika la Mzinga limekamilisha mradi wa ukarabati na uboreshaji wa kiwanda awamu ya kwanza. Shirika hili limeweka mitambo na kuwapatia mafunzo waendeshaji wa mitambo hiyo. Mradi huo ulizinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Daktari Jakaya Mrisho Kikwete tarehe 16 Januari, 2012.

Mheshimiwa Spika, Shirika linaendelea kufanya utafiti wa zana za kijeshi pamoja na kuzifanyia ukarabati ili zitumike katika hali ya usalama. Halikadhalika, Shirika la Mzinga limebuni vyanzo vya ziada vya kuliongezea mapato. Vyanzo hivyo ni pamoja na kuanzisha kampuni tanzu ya Mzinga *Holdings* itakayoshughulikia ujenzi na uendeshaji wa maduka yasiyotozwa ushuru *(duty free shops)* katika vikosi vya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Shirika la Nyumbu kwa upande wake limeendelea kutekeleza mpango wa muda mrefu (2010 - 2025) wenye malengo ya kufanya utafiti na uvumbuzi katika teknolojia za magari na mitambo, kuzalisha na kusambaza magari na mitambo ili kulifanya Shirika hili kuwa kituo kilichotukuka katika masuala ya teknolojia *(centre of excellence)* Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, shughuli zilizofanyika katika kutekeleza mpango huo ni pamoja na kuendeleza teknolojia za kilimo, kuimarisha uwezo wa kituo katika uzalishaji wa vipuri na kufanya upembuzi yakinifu wa mradi wa kujenga kituo maalum cha kuhakiki ubora wa vifaa vinavyotengenezwa. Hata hivyo, Shirika halikuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwa sababu halikutengewa fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Jeshi limetekeleza miradi kadhaa ya ujenzi wa majengo ya vyuo na shule za kijeshi hususan Chuo cha Unadhimu na Ukamanda (Tengeru, Arusha), Shule ya Kijeshi ya Ulinzi wa Anga (Tanga), shule ya Usalama na Utambuzi wa Kijeshi (Mbagala, Dar es Salaam), Chuo cha Ulinzi wa Taifa (Kunduchi, Dar es Salaam) na ujenzi wa Maktaba katika Chuo cha Kijeshi (Monduli, Arusha). Aidha, miradi ya ujenzi wa maghala bora ya kisasa ya kuhifadhia silaha na milipuko nayo imeanza.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma ya Serikali ya kuimarisha mafunzo ya maafisa wa juu wa Jeshi na Maafisa Waandamizi wa Serikali ninayo furaha kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ujenzi wa Chuo cha Ulinzi wa Taifa umekamilika na kinategemea kuanza kutoa mafunzo mwezi Septemba, 2012. Kozi ya kwanza itakuwa mahsusi kwa wanafunzi kutoka Tanzania pekee. Baada ya kupata uzoefu kutokana na uendeshaji wa kozi ya kwanza, Chuo kitaalika wanafunzi wenye sifa zinazolingana na hizo kutoka nchi jirani. Kozi zote zitaendeshwa kwa ushirikiano kati yetu na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Serikali imeendelea na utekelezaji wa mradi wa kuboresha Mtandao wa Mawasiliano Jeshini. Wizara inaendelea kuboresha mtandao huu kwa kuondoa mitambo ya zamani iliyochakaa na kuweka mitambo mipya na ya kisasa vikosini. Mradi huu umetekelezwa katika vikosi vilivyoko katika Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha maslahi ya wanajeshi ikiwa ni pamoja na stahili na huduma muhimu. Katika mwaka 2011/2012 mishahara ya askari ilipandishwa na posho ya chakula pia iliyopandishwa kutoka shilingi 5,000 hadi 7,500 kwa siku. Madeni ya wanajeshi yenye jumla ya sh. 43,201,205,416.00 pia yalilipwa. Halikadhalika, madeni ya wazabuni wanaotoa huduma mbalimbali jeshini yenye thamani ya sh. 24,248,160,000.00 (wakiwemo *TANESCO* na Mamlaka za Maji) yalilipwa. Aidha, katika mwaka 2011/2012, huduma ya mavazi iliboreshwa kwa wanajeshi kupatiwa sare mpya.

Mheshimiwa Spika, huduma ya tiba kwa wanajeshi na familia zao, vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa na Watumishi raia ndani ya Jeshi, imeendelea kutolewa kwa kutumia vituo visivyopungua 70 nchi nzima. Hospitali za Jeshi za Kanda na hospitali za Lugalo, Nyumbu (Kibaha), Mwanza na Tabora zimeimarishwa. Hospitali hizi zina wahudumia wanajeshi na raia wanaoishi karibu na maeneo ya kambi.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendeleza ujenzi wa nyumba za makazi ya maafisa na askari vikosini, pamoja na ujenzi mpya wa majengo mbalimbali.

Sambamba na uendelezaji wa ujenzi wa majengo hayo, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China imeridhia kutoa mkopo wa masharti nafuu wa Dola za Kimarekani 285,000,000 kwa ajili ya mpango wa ujenzi wa nyumba za kuishi maafisa na askari vikosini. Serikali imekamilisha taratibu za upatikanaji wa mkopo huo kupitia Benki ya *Exim* ya China. Mkataba wa mkopo umetiwa saini tarehe 20 Juni, 2012 na ujenzi unatarajiwa kuanza rasmi hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la wananchi lilishiriki katika kukabiliana na majanga, zikiwemo operesheni ya kuokoa watu na mali, kufuatia mafuriko makubwa yaliyotokea Mkoani Dar es Salaam mwezi, Desemba, 2011 na ajali ya kuzama kwa meli ya Spice Islander huko Nungwi, Unguja mwezi Septemba, 2011. Jeshi pia limetekeleza na kukamilisha zoezi la usombaji wa mahindi tani 5,000 kutoka Dar es Salaam kwenda Arusha, tani 10,000 kutoka Songea kwenda Makambako na tani 5,000 kutoka Makambako na Iringa kwenda Dar es Salaam. Jeshi pia limepewa kazi ya kusomba tani 30,000 za mahindi kutoka Sumbawanga kwenda Mpanda na Mbozi. Utekelezaji wa zoezi hili unasubiri upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafunzo ya Vijana wa JKT, umoja wa Kitaifa miongoni mwa wananchi ni jambo muhimu katika kuimarisha ulinzi wa Taifa letu. Kwa kutambua umuhimu wa suala hili, Serikali inaendelea kuwajengea vijana wa Kitanzania moyo wa Utaifa, ukakamavu na ujasiri kwa kuwapatia mafunzo ya uzalendo kupitia Jeshi la Kujenga Taifa.

Katika mwaka 2011/2012 vijana wa kujitolea 5,844 wamehitimu mafunzo ya awali ya JKT. Kati yao wavulana walikuwa 4,554 na wasichana 1,290. Mafunzo hayo yaliendeshwa katika makambi nane ya Msange, Kanembwa, Ruvu, Oljoro, Mgambo, Mafinga, Mlale na Bulombora.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuhitimu mafunzo hayo, vijana hao wameendelea na mafunzo ya stadi za kazi katika Vyuo vya Ufundi vilivyopo katika makambi ya Mgulani, Makutupora, Nachingwea, Mlale, Msange, Bulombora, Mafinga, Maramba, Kanembwa, Mgambo, Rwamkoma, Oljoro na Chita. Kati ya vijana 5,844 waliopatiwa mafunzo vijana 3,406 walifanikiwa kupata ajira katika vyombo vya Ulinzi na Usalama pamoja na mashirika mbalimbali. Wizara ya Ulinzi imeamua kutumia utaratibu wa kuajiri vijana wanaotaka kujiunga na vyombo vya ulinzi na usalama kutoka kwenye JKT na JKU ili kupata vijana wazalendo na wenye nidhamu.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa limefanya ukarabati wa majengo mbalimbali ili yaweze kutumiwa na vijana wa kujitolea. Ukarabati huo umefanyika katika makambi ya Bulombora na Kanembwa (Kigoma), Mafinga (Iringa), Makutopora (Dodoma), Mgambo (Tanga), Mlale (Ruvuma), Msange (Tabora), Oljoro (Arusha), Ruvu (Pwani) na Rwamkoma (Mara). Hivi sasa makambi haya yana uwezo wa kuchukua vijana 20,000 kwa wakati mmoja. Vile vile Jeshi la Kujenga Taifa limeyakarabati makambi ya Chita (Morogoro), Maramba (Tanga), Mbweni na Mgulani (Dar es Salaam), Itende (Mbeya) na Nachingwea

(Lindi) ili yaweze kutoa mafunzo ya stadi za kazi na maisha.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa limekarabati mahanga mapya ya vijana vikosini kwa ajili ya mafunzo ya awali na ukarabati wa nyumba za maafisa, askari na watumishi raia wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Aidha, ukarabati wa zahanati moja na ujenzi wa jengo la Utawala la Chuo cha Uongozi Kimbiji ulikamilika. Vile vile, miundombinu katika vikosi vya Kanembwa na Nachingwea iliimarishwa sambamba na upimaji wa eneo la vikosi hivyo.

Mheshimiwa Spika, Shughuli za Shirika la SUMAJKT. Katika mwaka 2011/2012, Shirika la SUMAJKT lilipata kazi mbalimbali zenye thamani ya sh. 10,615,667,122.00 na kupata faida ya sh. 1,232,726,924.00. Mapato yaliyopatikana katika kazi hizi yametumika kununulia vifaa kama vile magari na vifaa vya ofisini. Aidha, kutokana na utendaji wake mzuri shirika hili limeendelea kupata kazi mbalimbali. Shirika hili limetoa ajira kwa vijana zaidi ya mia tisa kwa ajili ya shughuli za viwanda, kilimo, ujenzi na ulinzi kupitia kampuni tanzu ya SUMA *Guard*.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, SUMAJKT ilitekeleza mradi wa uunganishaji na uuzaji wa matrekta 1,846 na zana zake 1,450. Matrekta na zana hizi zilinunuliwa kwa mkopo kutoka Serikali ya India. Hadi kufikia tarehe 9 Julai, 2012 SUMAJKT ilikuwa imeuza matrekta 786. Katika kusogeza matrekta karibu na wateja wake, *SUMAJKT* imefungua vituo vya kuuzia

matrekta hayo katika Mikoa ya Dodoma, Mbeya, Mwanza na Arusha.

Mheshimiwa Spika, nimemwagiza Wakala wa uuzaji wa matrekta kufanya mipango ya kuyahamishia matrekta yaliopo Mwenge Dar es Salaam na kuyapeleka Morogoro. Shirika la SUMAJKT linatarajia kufungua vituo zaidi vya mauzo ya matrekta kupitia kwa Wakuu wa Mikoa ili kurahisisha upatikanaji wa huduma mbalimbali kama vile ushauri na vipuri. Juhudi za kuyatangaza matrekta hayo zinaendeshwa kupitia vyombo mbalimbali vya habari vikiwemo vipindi maalum kwenye Televisheni.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa matrekta katika kuendeleza Kilimo Kwanza, Serikali imepunguza bei ya matrekta ambapo matrekta yenye *horse power* 50 yaliyokuwa yakiuzwa shilingi milioni 25.6 sasa yanauzwa shilingi milioni 16.5 na matrekta yenye *horse power* 70 yaliyokuwa yanauzwa shilingi milioni 45.8 sasa yanauzwa shilingi milioni 38.8. Hivi sasa Shirika linawapunguzia wateja malipo ya awali *(down payment)* kutoka asilimia 50 ya bei ya trekta moja hadi asilimia 30.

Mheshimiwa Spika, vile vile Shirika linafikiria kupunguza zaidi malipo ya awali hadi asilimia 15 kwa wateja watakaonunua matrekta kuanzia 50 na kuendelea. Halikadhalika, Halmashauri za Wilaya ambazo zitakuwa tayari kuwadhamini wakulima wadogo wadogo imependekezwa zilipe malipo ya awali ya asilimia 10.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza kauli mbiu ya Kilimo Kwanza, Jeshi la Kujenga Taifa limeendelea kutekeleza jukumu la uzalishaji wa mazao ya chakula, biashara na mazao ya mbegu bora za nafaka. Katika mwaka 2011/2012, JKT limezalisha tani 356 za mazao ya chakula na biashara na linakadiria kuvuna tani 1,511 za mbegu bora za mazao mbalimbali. Mbegu hizo zitauzwa kwa Wakala wa Mbegu *Agriculture Seed Agency* na kampuni binafsi ya *Southern Highland Seeds Growers*, Kampuni zenye mkataba na JKT katika uzalishaji mbegu.

Mheshimiwa Spika, aidha, ujenzi wa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji kwa awamu ya kwanza unaendelea katika kikosi cha Chita. Ujenzi huo utakapokamilika utasaidia kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kwa ekari 1,000 za zao la mpunga. Upanuzi wa kilimo hicho utaendelea hatua kwa hatua kadri fedha zitakavyopatikana. JKT ina lengo la kuendeleza ekari 30,000 za kilimo cha umwagiliaji katika kikosi hicho cha Chita.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha ufugaji wa kisasa, JKT limeanza kutekeleza uzalishaji wa ng'ombe wa kisasa kwa njia ya chupa *(artificial insermination)* ambapo wataalam wa fani hiyo wamepatiwa mafunzo katika Chuo cha Uhamilishaji Arusha *(National Artificial Insermination Centre)* huko *Usa River*, Arusha. JKT pia ina mpango wa kuanzisha kliniki ya mifugo na kituo cha ukusanyaji mbegu za madume bora ya ng'ombe wa maziwa na nyama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hifadhi ya mazingira. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya kuimarisha Mazingira. Katika mwaka 2011/2012, elimu ya utunzaji mazingira imeendelea kutolewa kwa vijana wa JKT, watumishi wa raia na wananchi wanaoishi jirani na makambi. Kazi ya upandaji miti katika makambi inaendelea.

Mheshimiwa Spika, aidha, baadhi ya vikosi vilishiriki katika kuwania tuzo ya Rais ya kuhifadhi vyanzo vya maji, kupanda na kutunza miti. Vikosi vya Kaboya (Kagera), Ruvu (Pwani) na Maramba (Tanga) vilipata ushindi Kimkoa. Pia vikosi vyetu vimeshiriki katika maadhimisho ya wiki ya Mazingira Duniani kwa kushiriki kwenye kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya usafi, kupanda miti na kutoa elimu ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto za utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2011/2012. Kama ilivyokuwa kwa miaka iliyopita, changamoto kubwa iliyoikabili Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika kutekeleza mpango na bajeti ya mwaka 2011/2012 ni kupatiwa kiwango kidogo cha ukomo wa bajeti ukilinganisha na mahitaji halisi ya Mafungu ya Wizara hii. Hali hii imeathiri sana utekelezaji wa mipango muhimu ya miradi ya maendeleo kama vile ununuzi wa zana na vifaa, ujenzi wa maghala ya kuhifadhia silaha na milipuko, ujenzi na ukarabati wa majengo ikiwemo nyumba za makazi katika makambi, uboreshaji wa viwanda vya utafiti na uzalishaji wa bidhaa za kijeshi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Matumizi ya Kawaida hali hiyo imeathiri shughuli nyingi muhimu ikiwemo ulipiaji wa huduma na mahitaji muhimu kwa ajili ya uendeshaji wa majukumu kama vile mafuta, maji, umeme na stahili za Wanajeshi na Watumishi raia. Shughuli nyingine zilizoathirika ni utoaji wa huduma ya tiba, ushiriki katika Jumuiya za Kikanda katika nyanja za kijeshi na uendeshaji wa ofisi zetu za Waambata Jeshi katika nchi za nje. Kwa jumla, hali hiyo inasababisha malimbikizo ya madeni licha ya Serikali kuchukua hatua za kupunguza madeni haya.

Mheshimiwa Spika, vile vile Wizara inakabiliwa na tatizo la kuchelewa kupokea fedha kutoka Hazina kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Hali hii imesababisha mipango kazi ya utekelezaji wa miradi kuvurugika na wakati mwingine kukiuka mikataba ya Kimataifa na hivyo kuzua manung'uniko kutoka kwa wadai na kutishia kutushtaki Mahakamani kwa kuvunja makubaliano ya mikataba hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu migogoro ya ardhi baina ya Jeshi na wananchi. Halikadhalika, Wizara yangu inakabiliwa na migogoro ya ardhi. Wakati wa kuhitimisha hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2011/2012, pamoja na mambo mengine, nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa nimeunda Kikosikazi cha kushughulikia migogoro hiyo katika maeneo yote nchini. Kufuatia hatua hiyo, tumeweza kubainisha matatizo yafuatayo:-

(a) Migogoro mingi ya ardhi kati ya jeshi na wananchi inatokana na maeneo kutopimwa na kupewa hati za umiliki;

(b) Baadhi ya wananchi wanavamia maeneo ya Jeshi hasa maeneo yenye vishawishi vya kimaendeleo kama vile kilimo, makazi na uwekezaji;

(c) Baadhi ya wananchi hawaheshimu alama za mipaka ya maeneo na hata kung'oa kwa makusudi alama hizo kwa nia ya kuvamia maeneo hayo; na

(d) Baadhi ya wananchi hawaelewi umuhimu wa jeshi kumiliki maeneo makubwa kwa matumizi ya kijeshi.

Mheshimiwa Spika, ili kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa suala hili, Wizara imeanza kuchukua hatua mbalimbali. Katika baadhi ya maeneo tutalazimika kuwaondoa wavamizi mara moja ili kupisha shughuli za jeshi. Aidha, kwa maeneo ambayo uingiaji wa watu umezidi kiwango kiasi cha kufanya eneo husika kutokufaa tena kwa shughuli za Jeshi, tutashauriana na mamlaka zinazohusika kuangalia uwezekano wa kupewa maeneo mbadala kama tulivyofanya katika eneo la Kikosi cha 977 *Tanganyika Packers* huko Arusha.

Mheshimiwa Spika, eneo hilo lenye ukubwa wa hekta 2495 lilitengwa kwa mafunzo ya mizinga na makombora. Hata hivyo, baada ya uvamizi mkubwa uliofanywa na wananchi, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete ameridhia

tupime na kurekebisha mipaka upya. Kwa msingi huo jeshi limepewa eneo mbadala la *Themi Holdings Grounds* huko Arusha.

Natoa wito kwa waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kuheshimu maeneo yanayomilikiwa na JWTZ. Jeshi lipo kwa sababu wananchi wa Tanzania wapo. Katika dunia ya leo ambayo inatawaliwa sana na tamaa ya kujipatia maslahi ya kiuchumi hatuwezi kuishi bila Jeshi. Wizara itaendelea kuchukua hatua ya kulinda maeneo hayo. Nawaomba Viongozi wote tushirikiane katika kutatua matatizo hayo ili kuepuka migororo isiyokuwa ya lazima.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria. Katika bajeti ya mwaka 2011/2012, Wizara yangu iliahidi kwamba itarejesha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria. Maandalizi ya kuanza zoezi hilo yamekamilika ambapo JKT wako tayari kuchukua vijana 20,000 kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, gharama za kuendeshea mafunzo hayo ni kubwa. Kwa hiyo, hatutaweza kuchukua vijana wote wanaostahili kupitia JKT kwa mujibu wa Sheria. Kutokana na hali hiyo Serikali inapanga kurejesha mafunzo hayo kwa majaribio ya vijana 5,000. Vijana hao ni miongoni mwa vijana 41,348 ambao watahitimu mafunzo ya Kidato cha Sita katika mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, kupata vijana 5,000 kati ya vijana 41,348 ni kazi kubwa. Kwa hivyo, Wizara imeweka vigezo maalum vya kuwapata vijana hao kwa kuzingatia makundi. Makundi ya vijana hao yatatangazwa mwezi Januari, 2013.

Mheshimiwa Spika, mafunzo hayo yanategemea kuanza mwezi Machi, 2013 na yatafanyika kwa miezi sita katika makambi ya Bulombora na Kanembwa (Kigoma), Mlale (Ruvuma), Mafinga (Iringa), Msange (Tabora) na Oljoro (Arusha). Mpango wa utekelezaji wa jukumu hili utakuwa kama ifuatavyo:-

(i) Kuandikisha vijana kutoka shuleni kuanzia mwezi Desemba, 2012 hadi Januari, 2013;

(ii) Kuwapokea vijana katika makambi kuanzia tarehe 7 hadi 16 Machi, 2013;

(iii) Kuanza Mafunzo ya awali tarehe 17 Machi, 2013; na

(iv) Mwisho wa Mafunzo tarehe 16 Agosti, 2013.

Mheshimiwa Spika, wakati wa mjadala wa Bajeti ya Wizara yangu ya mwaka 2011/2012, pamoja na mambo mengine tulipokea ombi la Wabunge vijana kuandaliwa mafunzo maalum ya Jeshi la Kujenga Taifa. Nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu imelifanyia kazi ombi hilo na kuandaa utaratibu wa mafunzo maalum ya wiki tatu kwa waheshimiwa Wabunge vijana. Mafunzo haya yataanza mwezi Machi, 2013 sanjari na kuanza rasmi kwa mafunzo ya vijana kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, Waheshimiwa Wabunge vijana wataungana na kundi la kwanza la vijana 5,000 niliowaeleza hapo juu. Ni imani yetu kuwa pamoja na Waheshimiwa Wabunge kunufaika na mafunzo hayo, watahamasisha zoezi la urejeshwaji wa mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria na kutoa taswira nzuri ya mafunzo haya kwa jamii. Naomba Waheshimiwa Wabunge mjiorodheshe kwa maandalizi ya mafunzo haya.

Mheshimiwa Spika, malengo ya mwaka 2012/2013, Mpango wa mwaka 2012/2013, umelenga kuendeleza juhudi zilizofanyika za kuliimarisha Jeshi pamoja na kutoa huduma mbalimbali kwa wanajeshi na Watumishi raia. Malengo ya mpango huo yatazingatia utekelezaji wa shughuli zifuatazo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Kawaida:-

(i) Kuandikisha wanajeshi wapya na kuimarisha mafunzo na mazoezi ya kijeshi ikiwa ni pamoja na kushiriki katika mazoezi ya pamoja na majeshi ya nchi nyingine na mafunzo ya Ulinzi wa mgambo;

(ii) Kuimarisha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana wa Kitanzania wa kujitolea;

(iii) Kugharamia upatikanaji wa mahitaji muhimu ikiwemo umeme, maji, simu, mafuta na vilainisho;

(iv) Kutengeneza na kukarabati magari, vifaa, mitambo na zana za kijeshi;

(v) Kutoa huduma muhimu kwa Wanajeshi na Vijana wa JKT ikiwemo chakula, tiba, sare na usafiri;

(vi) Kulipa stahili mbalimbali za Wanajeshi, Vijana wa JKT na Watumishi wa raia;

(vii) Kuendeleza shughuli za ushirikiano na nchi nyingine duniani katika nyanja za kijeshi na kiulinzi; na

(viii) Kurejesha utaratibu wa mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria.

(b) Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Maendeleo:-

(i) Kuimarisha Jeshi la Ulinzi kwa kulipatia zana na vifaa bora;

(ii) Kuendelea na ujenzi wa maghala ya kuhifadhia zana na vifaa vya Jeshi;

(iii) Kukarabati mitambo na miundombinu katika viwanda na vituo vya utafiti na uendelezaji wa teknolojia ya kijeshi; na

(iv) Kukarabati na kuendeleza ujenzi wa majengo na miundombinu katika makambi ya jeshi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru watu mbalimbali kwa michango waliyoitoa katika kutayarisha makadirio haya. Nawashukuru Katibu Mkuu Bwana Job D. Masima, Naibu Katibu Mkuu, Mhandisi Mussa I. Iyombe; Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Davis Mwamunyange; Mnadhimu Mkuu, Luteni Jenerali Abdulrahman Shimbo; Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jenerali Samuel A Ndomba; Meneja Mkuu Shirika la Mzinga, Brigedia Jenerali Dokta Charles Muzanila na Mkurugenzi Mkuu Shirika la Nyumbu Kanali Anselm Bahati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo (Makao Makuu ya Wizara), Wakuu wa Matawi (NGOME), Wakuu wa Idara (Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa), Makamanda wa Kamandi ya Jeshi la Nchi Kavu, Jeshi la Anga na Jeshi la Wanamaji, Maafisa, Askari na Watumishi wote raia wanaofanya kazi chini ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Vile vile namshukuru Mpigachapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapisha Hotuba hii kwa wakati. Mwisho nawashukuru wafanyakazi wote wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kunipa ushirikiano mkubwa katika kuongoza Wizara hii tangu tarehe 10 Mei, 2012 nilipofika rasmi Wizarani hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2012/2013 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imekadiria kukusanya mapato kiasi cha sh. 57,650,000.00 katika mchanganuo ufuatao:-

(a) Fungu 38 NGOME… … … … Sh. 2,650,000.00

(b) Fungu 39 – JKT… … … … … Sh. 30,000,000.00

(c) Fungu 57 – ULINZI… … … … Sh. 25,000,000.00

**Jumla... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 57,650,000.00**

Mheshimiwa Spika, ili Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iweze kutekeleza malengo yake iliyojiwekea kwa mwaka 2012/2013, naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha jumla ya sh. 1,086,550,058,000.00 ambazo kati yake sh. 678,363,492,000.00 zitatumika kwa ajili ya bajeti ya matumizi ya kawaida na sh. 408,186,566,000.00 ni bajeti ya matumizi ya maendeleo. Fedha hizi zimegawanyika katika mafungu matatu kama ifuatavyo:-

(a) Fungu 38 – Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania:-

(i) Bajeti ya Matumizi
ya Kawaida… ... ... ... Sh. 531,316,218,000.00

(ii) Bajeti ya Matumizi
ya Maendeleo... ... ... ... Sh. 14,000,000,000.00

(b) Fungu 39 – Jeshi la Kujenga Taifa:-

(i) Bajeti ya Matumizi
ya Kawaida… … … …Sh. 131,197,222,000.00

(ii) Bajeti ya Matumizi

ya Maendeleo… … … …Sh. 5,000,000,000.00

(c) Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

(i) Bajeti ya Matumizi
ya Kawaida… … … … Sh. 15,850,052,000.00

(ii) Bajeti ya Matumizi
ya Maendeleo… … … Sh. 389,186,566,000.00

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara yangu inawajibu wa kusimamia matumizi bora ya rasilimali za umma, nitajitahidi kufuatilia matumizi ya fedha zitakazoidhinishwa ili tuweze kutekeleza vyema malengo muhimu yafuatayo:-

(i) Kununua zana na vifaa vya kijeshi ili Jeshi liweze kulinda mipaka ya nchi yetu kwa ufanisi;

(ii) Kujenga maghala ya kuhifadhia silaha na milipuko;

(iii) Kujenga na kukarabati nyumba za kuishi maafisa na askari;

(iv) Kulipa madeni kwa kampuni zilizoliuzia zana na vifaa Jeshi la Wananchi wa Tanzania; na

(v) Kuwapatia mafunzo vijana 5,000 kwa Mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara *(www.modans.go.tz)*.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Jambo ambalo nimefurahishwa nalo hapa ni hawa Waheshimiwa Wabunge Vijana kwenda kupata mafunzo, labda watabadilika. *(Kicheko)*

Sasa nitamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, atoe maoni ya Kamati. Mheshimiwa Machangu kwa niaba ya Mwenyekiti!

**MHE. BETTY E. MACHANGU (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA):** Mheshimiwa Spika, kabla ya sijawasilisha taarifa, napenda kuwapongeza wanachama wa CCM popote walipo na hususan wanawake kwa kukamilisha chaguzi za chama na jumuiya zake ngazi za Matawi na Kata. Nawatakia kila la kheri katika chaguzi zinazoendelea za Wilaya, Mkoa na Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika**,** kwa niaba ya Wanawake wa Tanzania, tunalaami kwa nguvu zote mauaji ya Katibu wa UVCCM, Wilaya ya Iramba. Natoa pole kwa zile familia ambazo zimefiwa na ninaomba Jeshi la Polisi liwakamate wale wote waliohusika bila kujali nyadhifa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niwasilishe taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, Kanuni ya 99(7) na Kanuni ya 114(11), naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa kwa mwaka wa Fedha 2011/2012 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka 2012/2013 na kuliomba Bunge hili liyapokee maoni haya na hatimaye kuidhinisha bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inahusisha mafungu matatu: Fungu 38 – Ngome, Fungu 39- Jeshi la Kujenga Taifa na Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ilifuatilia utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2011/2012 kwa mafungu yote matatu. Mojawapo ya njia iliyotumika ni pamoja na kufuatilia kwa karibu hali ya ulinzi na usalama wa mipaka yetu na kutembelea vikosi muhimu vya ulinzi wa nchi yetu. Aidha, tarehe 05 Juni, 2012, Kamati ilikutana mjini Dar es Salaam na kupokea taarifa kuhusu utekelezaji wa jukumu la ulinzi wa mipaka yetu. Katika kikao hicho, taarifa zilionyesha kuwa hali ya mipaka yetu kwa ujumla ni shwari, vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vimejipanga kukabiliana na tukio lolote la uvamizi wa nchi yetu.

Kuhusu tatizo la mpaka wa Malawi na Tanzania katika Ziwa Nyasa, Serikali imeahidi kushughulikia mgogoro huo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kufuatilia utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha Julai – Desemba, 2012, tarehe 07 Juni, 2012, Kamati ilipitia na kujadili Taarifa ya Wizara hii kuhusu utekelezaji wa malengo ya bajeti kwa mwaka 2011/2012. Katika mapitio hayo, Kamati ilielezwa kuhusu utekelezaji wa malengo ya bajeti sanjari na taarifa kuhusu mtiririko wa bajeti. Vilevile taarifa iliyowasilishwa ilieleza kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati Bungeni wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012 yalikuwa sita yaliyotengewa bajeti ya matumizi ya kawaida ikiwemo kuajiri Wanajeshi wapya na kuimarisha mafunzo na mazoezi ya kijeshi pamoja na kutoa huduma muhimu. Kwa upande wa matumizi ya maendeleo Wizara ililenga kutekeleza majukumu matatu likiwemo jukumu la kununua vifaa na zana za kijeshi pamoja na kukarabati na kukamilisha ujenzi wa majengo na miundombinu katika kambi za Jeshi.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya utekelezaji imeonyesha kuwa Wizara imefanikiwa kutekeleza malengo hayo kwa kiasi kikubwa kulingana na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Kwa mfano, Wizara imeripoti kuwa fedha zilizopatikana kwa ajili ya matumizi ya kawaida zilitumika kulipa stahili za

Wanajeshi na huduma mbalimbali kwa Wanajeshi na vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na kugharamia mafunzo kwa Askari na Maafisa. Aidha, Jeshi liliwezeshwa kufanya mazoezi ya pamoja na majeshi ya nchi nyingine duniani, hususan zile za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Pamoja na hayo, Kamati ilijulishwa kuwa baadhi ya miradi ya maendeleo haikutekelezwa kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, ili kujiridhisha kuhusu dhamira ya Serikali katika miradi ya sekta hii, Kamati ilitaka kujua sababu za kutokamilika kwa miradi hiyo. Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, alieleza kuwa tatizo kubwa lilikuwa ni upatikanaji wa fedha ambapo baadhi ya miradi ilipata fedha chini ya viwango vya mahitaji halisi na mingine kutopata fedha kabisa. Mfano wa miradi hiyo ni pamoja na Ujenzi wa Maghala manne ya silaha, ukamilishaji wa Chuo cha Ulinzi wa Taifa (*The National Defence College*) na ukarabati wa majengo katika Makao Makuu ya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Jeshi la Kujenga Taifa, taarifa ilieleza kuwa Wizara imeweza kufanya ukarabati na ujenzi wa miundombinu na majengo katika kambi kumi ikiwemo Oljoro, Arusha na Makutupora, Dodoma. Hatua hiyo iliwezesha Jeshi la Kujenga Taifa kuimarisha utendaji na kuongeza uwezo wa kuchukua vijana zaidi wa kujitolea. Aidha, tarehe 09 Juni, 2012, Kamati ilipokutana tena na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ilielezwa kuwa katika mwaka huu wa fedha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa sheria yataanza kwa kuchukua vijana 5000.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya mapato na matumizi. Moja ya mambo ya msingi yaliyozingatiwa na Kamati wakati wa kuchambua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii ni mapitio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012 kama yalivyoripotiwa kwenye kikao cha Kamati. Taarifa zilionyesha kuwa Wizara ilipanga kukusanya mapato ya Shilingi 28,355,000 lakini ilikusanya jumla ya shilingi 103,716,459. Kamati ilipotaka ufafanuzi zaidi, ilijulishwa kuwa kwa sasa Hazina imetoa mwongozo wa utaratibu maalumu utakaobainisha picha halisi ya makusanyo.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa jumla wa matumizi na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina hadi mwisho wa mwezi Mei, 2012 ulionyesha kuwa Fungu 38 - Ngome walipokea asilimia 96.3 ya bajeti ya matumizi ya kawaida na asilimia 40 ya matumizi ya maendeleo. Aidha, Fungu 39 JKT walipokea asilimia 92.2 ya bajeti ya matumizi ya kawaida na asilimia 9.9 ya matumizi ya maendeleo. Kwa upande wa Fungu 57 - Makao Makuu ya Wizara, kiasi kilichopatikana ni asilimia 92.8 ya bajeti ya matumizi ya kawaida na asilimia 99.98 ya bajeti kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Mwenendo huu unadhihirisha kuwa upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo haukuwa mzuri kwa JKT na Ngome.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati. Wakati wa kupitia na kuchambua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Kamati ilitoa maoni na ushauri kuhusu mambo saba ya utekelezaji wa majukumu. Ili kujiridhisha na namna Serikali ilivyozingatia maoni na ushauri wake, Kamati ilitaka

kupata taarifa ya utekelezaji wa maoni na ushauri huo. Maelezo yaliyotolewa yalionyesha kuwa Serikali imezingatia ushauri ingawa sehemu kubwa ya ushauri huo inaendelea kufanyiwa kazi. Kwa mfano, Kamati ilishauri kuwa Serikali iandae mpango wa mafunzo kwa viongozi na Watendaji Waandamizi Serikalini na taarifa ya Waziri ilionyesha kuwa mpango wa mafunzo katika Chuo cha Ulinzi wa Taifa, unaonyesha kuwa kozi ya kwanza kwa viongozi na Watendaji Waandamizi wa Serikali itaanza kuendeshwa Mwezi Septemba, 2012 kwa muda wa wiki 48.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine wa ushauri ni kuhusu kupitia upya Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa, Sura ya 533 (*The National Services Act, CAP. 533).* Maelezo ya Mheshimiwa Waziri yalionyesha kuwa kwa kuzingatia ushauri huo, Wizara ya Ulinzi inaendelea na mchakato wa kuhuisha Sheria hii. Mapendekezo ya Wizara katika mchakato huo wa kuhuisha Sheria yanahusu lengo la kuwachukua vijana wanaotarajia kujiunga na Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwingine ulihusu Serikali kuendelea kuboresha uwezo wa Jeshi la Kujenga Taifa kuchukua vijana wengi zaidi. Taarifa iliyotolewa ilionyesha kuwa uwezo wa Jeshi hilo bado ni kuchukua vijana 20,000 kila awamu kwa awamu mbili kwa mwaka. Aidha, Kamati ilishauri kulipa madeni ya Askari na wazabuni kama inavyostahili. Maelezo ya Serikali yalionyesha kuwa ushauri huu ulizingatiwa lakini yamejitokeza madeni mengine yanayofikia takriban shilingi bilioni 36.5 na kwamba yamefikishwa Serikalini ili kuombewa fedha. Kamati

inasisitiza kuwa kuna umuhimu wa kuweka utaratibu mzuri zaidi wa kulipa madeni na kuepuka kuongezeka kwa madeni hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushauri wa Kamati unaopendekeza kuboresha Sheria ya Ulinzi wa Taifa, Sura ya 192 (*The National Defence Act, CAP. 192*), taarifa inaonyesha kuwa Serikali haijazingatia ushauri huu kwa zaidi ya miaka minne sasa tangu iliposhauriwa. Kamati inasisitiza tena kuwa ili kuimarisha taratibu na masharti sahihi katika eneo la ulinzi wa Taifa, umefika wakati kwa Serikali kudhamiria na kukamilisha maandalizi ya Muswada wa Sheria kwa ajili ya kuiboresha sheria hii.

Mheshimiwa Spika, malengo ya bajeti na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka 2012/2013. Katika kikao cha tarehe 07 Juni, 2012, kilichofanyika katika Ofisi Ndogo ya Bunge, Dar es Salaam, Kamati ilipokea maelezo ya Serikali kuhusu malengo ya bajeti na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2012/2013 na kuyachambua kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii, Kamati ilipokea taarifa kuhusu majukumu matano yanayopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Majukumu hayo ni pamoja na kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo ununuzi wa vifaa na zana mbalimbali za kijeshi. Malengo yanayowekwa katika mwaka huu wa fedha ni mwendelezo wa malengo yaliyopangwa katika mwaka wa fedha 2012/2013. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara

ilipanga kutekeleza mradi wa ujenzi wa maghala ya kuhifadhia silaha na milipuko lengo ambalo halilikukamilika na linapangwa kukamilishwa katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, kuhusu makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Kamati ilielezwa kuwa Wizara hii imekadiria kukusanya jumla ya mapato ya kiasi cha shilingi 57,655,000. Kiasi hiki kinatofautiana na lengo lililowekwa mwaka jana ambapo Wizara ilipanga kukusanya jumla ya shilingi 28,355,000. Tofauti hii ya lengo la mapato ni ongezeko la asilimia 103.33. Kwa upande wa makadirio ya matumizi, Kamati ilielezwa kuwa Wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 1,086,550,058,000/-. Kati ya fedha hizo sh.678,363,492,000/- ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 408,186,566,000/- zinaombwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kufanyia kazi makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii, Kamati ilizingatia pamoja na mambo mengine, maelezo ya kitaalamu katika uchambuzi wake ili kulishauri vema Bunge lako Tukufu. Kwa mfano, Kamati ilizingatia uhusiano mkubwa uliopo baina ya matumizi katika sekta ya ulinzi na kukua kwa uchumi wa nchi ambapo mawazo ya wataalamu katika makala iliyoandikwa na Adrian Kuah, Mtaalam na Mtafiti katika fani ya Uchumi na Ulinzi *(Defence Economics); An associate Research fellow specializing in Defence Economics)* na Bernard Loo, Profesa Msaidizi katika Fani ya Vita na Masomo ya Ulinzi *(An Assistant Professor specializing in war and strategic studies)* ambayo yalinukuliwa katika Makala

ya *Examining the Defence Industrialization – Economic growth Relationship: The case of Singapore* iliyochapishwa na *Institute of Development and Strategic Studies Singapore, July, 2004* yanasema kama ifuatavyo:-

*"A stable and secure polity (as a result of strong defence capabilities) is able to attract foreign direct investments (FDI) that provides for economic growth and development. In other words, there is a positive, linear progression between establishing a strong defence capability on the one hand, and experiencing economic growth and development on the other."*

Tafsiri isiyo rasmi ya maelezo hayo ni kuwa:-

*"Nchi yenye utulivu na usalama kutokana na uwezo madhubuti wa kiulinzi inaweza kuvutia uwekezaji kutoka nje ya nchi ambao utachangia kukua kwa uchumi na maendeleo. Kwa maneno mengine kuna uhusiano wa moja kwa moja baina ya kuimarisha uwezo wa kiulinzi kwa upande mmoja na kushuhudia kukua kwa uchumi na maendeleo kwa upande mwingine"*.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi ulionyesha kuwa ikilinganishwa na makadirio ya matumizi kwa mwaka jana, katika mwaka wa fedha wa 2012/2013, bajeti hii imeongezeka kwa asilimia 59.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati ilibaini kuwa asilimia 86.5 ya bajeti ya maendeleo si kwa ajili ya miradi mipya bali zitatumika kulipia mikataba mitatu ya

ujenzi wa nyumba za Wanajeshi pamoja na ununuzi wa vifaa na zana za kijeshi. Pamoja na hayo, Kamati inaamini kuwa bajeti hii ina mwelekeo unaokubaliana na dhana ya ulinzi na uchumi inayotafsiriwa na Michael D. Intriligator, Profesa wa Uchumi, Sayansi ya Siasa na Sera katika Chuo Kikuu cha California, Los Angeles (UCLA) katika Makala yake inayoitwa *On the Nature and Scope of Defence Economics, Defence Economics, page 3-11* ambaye anasema:-

*"Defence economics is concerned with that part of the overall economy involving defence-related issues, including the level of defence spending, both in total and as a fraction of the overall economy; the impacts of defence expenditure, both domestically for output and employment, and internationally for impacts on other nations; the reasons for the existence and size of the defence sector; the relation of defence spending to technical change; and the implications of defence spending and the defence sector for international stability or instability"*

Mheshimiwa Spika, kwa tafsiri ya maneno hayo tunaweza kusema kuwa dhana ya uchumi na ulinzi ni sehemu ya uchumi mkubwa ambao unahusika na masuala ya ulinzi ikiwemo kiasi cha matumizi kwa ajili ya ulinzi ama kwa ujumla wake au sehemu yake, athari ya matumizi katika uchumi ndani ya nchi na hata kimataifa, sababu za kuwa na ulinzi na ukubwa wake, uhusiano baina ya matumizi na mabadiliko ya teknolojia katika ulinzi na tafsiri yake katika utulivu na mashaka kimataifa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa makadirio ya matumizi ya kawaida, kuna ongezeko la asilimia 168. Kwa uchambuzi wa kina uliofanyika, Kamati inaafiki kwamba makadirio haya yamezingatia kwa kiasi umuhimu wa kukuza uwezo wa ulinzi wa mipaka yetu na kuongeza ujuzi, weledi na umahiri wa Askari na Maafisa wa Jeshi letu pamoja na kuboresha teknolojia inayotakiwa. Ni maoni ya Kamati kuwa nia ya Serikali kuendeleza juhudi katika kuimarisha zaidi ulinzi wa mipaka yetu ni jambo la kuungwa mkono na kuhimizwa kila wakati.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo, naomba kuwatanabaisha wataalamu wa bajeti na uchumi nchini kuwa zipo tafiti zilizofanyika kuhusu matumizi ya nchi zinazoendelea katika sekta ya ulinzi yanavyohusiana na ukuaji wa uchumi na maendeleo. Mfano wa tafiti hizo ni ule uliofanywa na Benoite Emil mwaka 1973 unaojulikana kama *Benoit's study on Growth and defence in Developing Countries, Economic Development and Cultural Change.* Utafiti huu ulionyesha kuwa nchi zinazoendelea ambazo kwa ujumla zina matumizi makubwa katika sekta ya ulinzi zilionekana kuwa na kasi nzuri ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ikilinganishwa na zile zinazotumia kiasi kidogo katika ulinzi wake.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka 2011/2012. Kabla ya kutoa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati inaunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

(i) Ili kuendelea kuboresha maslahi ya Wanajeshi wetu pamoja na mazingira yao ya kuishi na kufanyia kazi, uwekwe utaratibu wa kushughulikia madeni binafsi ya Wanajeshi na kuepuka kuongezeka kwa madeni yasiyolipwa.

Kwa mfano, kujitokeza kwa madeni ya Maafisa, Askari na watumishi wengine wa umma wa Wizara hii kwa mwaka 2010/2011 na 2011/2012, kusingekuwepo iwapo Wizara ingekuwa na utaratibu madhubuti wa kushughulikia madeni hayo na kulipa kwa wakati. Kamati inasisitiza kuwa deni la shilingi bilioni 36.5 katika mwaka wa fedha 2011/2012 na 2011/2012 lilipwe mapema inavyowezekana;

(ii) Kasi ya kukamilisha mapitio ya Sheria ya Ulinzi wa Taifa, Sura ya 192 (*The National Defence Act, CAP*. 192) na ile ya Jeshi la Kujenga Taifa, Sura ya 533 (*The National Services Act, CAP. 533*) hairidhishi. Kamati inaendelea kusisitiza kuwa suala hili lipewe msukumo mkubwa pamoja na kuharakisha maandalizi ya Sera ya Ulinzi wa Taifa;

(iii) Kwa kuwa Chuo cha Ulinzi wa Taifa kina umuhimu mkubwa katika mustakabali wa Taifa letu, Serikali iweke utaratibu wa kutenga fedha za kutosha kuendesha mafunzo kwa watu wanaokusudiwa na kuyatoa kwa wakati;

(iv) Pamoja na malengo mazuri ya Serikali kuanza mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria, ni maoni ya Kamati kuwa vijana 5000 ni idadi ndogo sana ikilinganishwa na mahitaji halisi. Ni vema Serikali ikajipanga kuongeza idadi hiyo kadiri inavyofaa; na

(v) Ili kudhibiti vema uwezekano wa kuzagaa na matumizi mabaya ya silaha, ni vema makampuni ya kigeni yasiruhusiwe kuweka walinzi wao na badala yake makampuni hayo yapewe ulinzi na vyombo vyetu vya dola.

Mheshimwa Spika, hitimisho. Napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii muhimu pamoja na maoni ya Kamati. Nachukua fursa hii pia kuitambua kazi nzuri inayofanywa na Serikali katika kuimarisha ulinzi wa nchi yetu. Namshukuru Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Mb, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa ufafanuzi alioutoa kwa Kamati wakati wa kuchambua bajeti hii. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga, Ndugu Job Masima na watumishi wengine wa Wizara hiyo kwa juhudi zao katika sekta ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, kipekee namshukuru Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Mb, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kwa Ushirikiano wake mkubwa katika kuiongoza Kamati hii. Aidha, nawashukuru sana Wajumbe wa Kamati hii kwa umakini wao wakati wa

kupitia na kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka 2012/2013 pamoja na kujadili kwa kina hali ya ulinzi wa mipaka ya nchi yetu. Kwa kuthamini michango yao, naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Makamu Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wajumbe ni Mheshimiwa Anna M. Abdallah, Mheshimiwa Kapt. Mst. John Z. Chiligati, Mheshimiwa Vita R. Kawawa, Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mheshimiwa Sadifa J. Khamis na Mheshimiwa Dkt. Mohamed S. Khatib. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Mussa H. Mussa, Mheshimiwa Eugen E. Mwaiposa, Mheshimiwa Mch. Israel Y. Natse, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mheshimiwa Brig. Jen. Mst. Hassan A. Ngwilizi, Mheshimiwa Rachel M. Robert, Mheshimiwa Masoud A. Salim, Mheshimiwa Muhamad I. Sanya, Mheshimiwa John M. Shibuda, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Annastazia J. Wambura na Mheshimiwa Betty E. Machangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, nawashukuru Ndugu Athuman Hussein na Ramadhani Issa, Makatibu wa Kamati hii kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kufanikisha taarifa hii kwa wakati. Nawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa

Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake.

Mheshmiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii na kuijadili pamoja na kuyakubali makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimwite Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Mch. Natse. *(Makofi)*

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, naomba kuwapongeza wananchi wa Vijiji vya Kiburumo, Kongwa, Nyarutanga waliofanya uchaguzi wao jana na kwa kauli moja kupitia sanduku la kura wameipatia CHADEMA ushindi mkubwa wa kuongoza Serikali katika vijiji hivyo chini ya Mwenyekiti Juma Hamza (Kiburumo), Juma Idi (Kibali - Kongwa) na Changanya Milenge (Nyarutanga). Hizo ni mvua za vuli, masika bado. Tunasema hivi; *the sun never set in* CHADEMA. CHADEMA hakuna kulala mpaka kieleweke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama hapa mbele ya Bunge hili, kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kambi ya Upinzani kuhusu

makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2012/2013 kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 99(7).

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za kipekee kwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, kwa imani yake kubwa kwangu na kuniteua kuwa Waziri Kivuli wa Wizara hii. Nami natoa ahadi kwake kuwa nitajitahidi kwa kadri ya uwezo wangu na kwa jinsi Mwenyezi Mungu atakavyonijalia, natumaini kwa uwezo wake nitatimiza matarajio yake kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Dkt. Willbrod Peter Slaa-Katibu Mkuu wa CHADEMA, Mbunge wa miaka 15 wa Jimbo la Karatu, kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuiongoza CHADEMA na kutupa miongozo ya namna ya kuwa Wabunge mahiri, sambamba na kuwa Mawaziri vivuli hasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru familia yangu kwa imani na uvumilivu waliouonesha wakati wote ambao ninakuwa mbali nao nikiwa katika shughuli za ujenzi wa Taifa. Maombi yenu ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sijatenda haki kwa wananchi wa Jimbo la Karatu kama sitawashukuru kwa imani kubwa waliyo nayo kwangu na kwa Chama changu cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA). Nami nawaahidi kuwa nitaitunza na kuiheshimu imani

yao kwangu, kuendelea kushirikiana nao kuleta maendeleo katika Jimbo na Wilaya yetu na mwisho kukifanya CHADEMA kuwa chama kiongozi kwa Wilaya na kwa nchi nzima katika uchaguzi wa mwaka 2015. Ahsanteni Sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wa Kambi Rasmi ya Upinzani pamoja na Kamati nzima ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa ushauri na ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika utendaji wangu kazi ndani na nje ya Bunge. Nasema ahsanteni sana!

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa ulinzi na usalama katika nchi yetu. Ni ukweli usiopingika kwamba nchi inapokuwa salama ndipo watu wake huweza kuishi kwa amani na utulivu. Amani na utulivu vinapotawala katika nchi, watu wake huwa na uhuru wa kufanya shughuli mbalimbali kwa ajili ya kujipatia mahitaji yao ya kila siku na kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa nchi yao.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imekuwa ikisifika duniani kwa kudumisha amani hadi kuitwa "Kisiwa cha Amani". Mwezi Agosti 2000, Rais Mstaafu wa Marekani Bill Clinton aliuita Mji wa Arusha kuwa ni "*Geneva of Africa*" kutokana na mji huo kuwa ni kitovu cha usuluhishi na upatanishi wa migogoro ya kimataifa. Hii ni sifa kubwa kwa Tanzania kwa kuaminiwa na mataifa mengine kuwa ni "Mlinzi wa Amani".

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka Serikali ielewe kwamba amani haipatikani kwa kutokuwa na vita katika nchi tu, ila amani huongezeka kama wananchi wanapata mahitaji yao ya msingi ambayo huwafanya waishi maisha ya staha. Amani huendelea kuimarika na kukomaa iwapo nchi itakuwa inatawaliwa kwa misingi ya haki, sheria na usawa katika mgawanyo wa rasilimali za nchi kwa faida ya wananchi wake wote.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatambua na inaheshimu vyombo vya ulinzi na usalama katika kulinda na kudumisha amani ya nchi yetu. Kambi inatambua vilevile kuwa ni kazi ngumu zaidi kuwalinda watu wasio na amani mioyoni mwao kutokana na kukosa haki zao za msingi. Hivyo ni dhahiri kuwa amani ya kweli ya nchi yetu itakuwepo na itaendelea kuwepo endapo Serikali iliyopo madarakani na Serikali itakayokuwa madarakani itatafuta kwanza amani ya nafsi za watu kwa kuwatimizia mahitaji yao ndipo kazi ya ulinzi wa amani katika nchi itakuwa rahisi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa Jeshi ni chombo huru ambacho hakitakiwi kuwa na itikadi ya chama chochote cha siasa au kuwa na mlengo wowote wa imani ya kidini. Lakini kwa masikitiko makubwa ni kwamba, sasa hivi wanasiasa wameanza kuingilia mchakato mzima wa uajiri wa wanaojiunga na jeshi hilo. Hili limekuwa linaharibu sifa kubwa ya jeshi letu, jambo linaloweza kugawa jeshi kwa misingi ya uchama. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuachia Jeshi lenyewe mchakato mzima wa uajiri kwa kulingana na matakwa ya jeshi lenyewe

kuliko shinikizo la wanasiasa kuingiza watoto wao, jamaa zao na watoto wa rafiki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa bajeti 2011/2012. Kwa ujumla, fedha iliyoidhinishwa kwa Wizara hii ilitolewa kwa kiwango cha kuridhisha isipokuwa fedha ya maendeleo ilikuwa ni asilimia 40% tu ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Hii haileti taswira nzuri, kwani maendeleo katika Wizara hii yako chini ya wastani.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Kamati ya Bunge ya tarehe 7 Juni, 2012 ni kwamba Fungu 57 - Ulinzi lilipokea shilingi bilioni 129**.** Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 30 ni fedha maalum *(ring fenced)* kwa ajili ya kununua meli za kivita, ambao mchakato wake umeanza na unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2012. Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali ihakikishe kuwa ahadi hii inatimia kwa maslahi ya ulinzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Waziri wa Ulinzi kwa Kamati ya Bunge, changamoto inayoathiri bajeti ya Wizara ya Ulinzi ni kuchelewa kutolewa kwa fedha kutoka Hazina kwa wakati, jambo ambalo limesababisha kushindwa kutekeleza baadhi ya majukumu yake kwa wakati. Tunapenda kusisitiza kwamba Serikali iepuke urasimu kwa mambo yanayohusu ulinzi na usalama wa nchi yetu. Kama bajeti imepitishwa na Bunge, jambo la kufanya ni kutoa fedha hizo kwa wakati ili kutekeleza majukumu yaliyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa zilizopo, gharama za kuondoa matrekta bandarini kwa mwaka 2011/2012 zilitumika jumla ya shilingi 4,048,325,331**.** Hakika fedha hizi ni nyingi sana kwa kazi ya kuondoa tu matrekta bandarini. Kambi ya Upinzani, inataka kupata majibu ni matrekta mangapi yaliyoondolewa na gharama ya kuondoa trekta moja ilikuwa kiasi gani? Je, gharama hizo zilikuwa ni kwa ajili ya shughuli gani haswa?

Mheshimiwa Spika, vyombo vya ulinzi na usalama na uajibu wake kwa wananchi. Madhumuni ya vyombo vya ulinzi na usalama ni kuwalinda raia wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ila kinyume na dhamira hiyo, uzoefu hapa kwetu Tanzania inaonekana kama vile vyombo hivi ni kwa ajili ya kuilinda Serikali. Ni kweli kwamba vyombo hivi vina jukumu pia la kuilinda Serikali, lakini kuna baadhi ya matukio ambayo inaonekana dhahiri vyombo hivi vikiacha jukumu la kuwalinda raia na badala yake kuwapiga na kuwanyanyasa raia.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya *"Tanzania Land Alliance" (TALA)* ya tarehe 30 Machi 2012, inasemekana kwamba mnamo tarehe 17 Machi, 2012, Askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) waliwaua kwa kuwapiga risasi watu watano na kuwajeruhi wengine watatu katika eneo la Maguba, Kitongoji cha Lupemenda, Kijiji cha Kiwale, Kata ya Igawa, Tarafa ya Malinyi, Wilayani Ulanga. Katika tukio hili, watu waliopoteza maisha ni Sanyiwa Ndahya (28), Lutala Ndahya (45), Kulwa Luhende (48), Ng'erebende

Nchambi Lukuresha (26) na Kashinje Msheshiwa (35). Waliojeruhiwa ni Zina Msheshiwa (29), Msheshiwa Ndahya (53), Khama Chisongelile Tiga (30).

Mheshimiwa Spika, taarifa ya uchunguzi wa *TALA,* inaonesha kuwa Wanajeshi waliohusika hawakuwa wakifanya doria kama ilivyodaiwa na Mkuu wa Wilaya ya Ulanga isipokuwa walivamia na kupora mifugo, fedha na mali ya wananchi na wakawa wanadai shilingi 10,000/= kwa kila kichwa cha mfugo ili wawaachie. Siku hiyohiyo walipora kiasi cha shilingi 205,000/= kutoka kwa watu wawili.

Mheshimiwa Spika, si nia ya Kambi ya Upinzani kuwasilisha Ripoti nzima ya tukio hili hapa, nia yetu ni kutaka kupeleka ujumbe kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kwamba vitendo kama hivi vinalivunjia Jeshi letu heshima kwa kiwango kikubwa sana mbele ya wananchi wa Tanzania na hata katika medani za kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasikitishwa sana na majibu ya kejeli yaliyokuwa yakitolewa na Mkuu wa Wilaya na Katibu Tawala wa Wilaya ya Ulanga kwa wachunguzi wa *TALA* kwamba mauaji ya wananchi hao ni jambo la kawaida kama ajali nyingine. Mkuu wa Wilaya alilinganisha mauaji hayo na ajali ya gari iliyowapata wanamuziki wa *Five Star Taarab* iliyotokea Mikumi mwaka 2011. Majibu kama hayo licha ya kuendelea kuwaumiza kisaikolojia ndugu wa marehemu na majeruhi, ni ishara mbaya kwa wananchi kwamba Serikali haiwajali wananchi

wake. Hii ni kwa mujibu wa *Report on TALA-Media Joint Mission on the Land Rights for Agro-pastoralists and Farmers in Ulanga District (Gathering facts in response to the killings of 5 people done by Tanzania Peoples Defense Forces in Muguba area, Malinyi Ulanga 17th March, 2012).* Taarifa hizi za tukio la Jeshi la Wananchi kuwanyanyasa na kuwaua raia hazijengi taswira nzuri kwa Jeshi letu na kwa Rais wa nchi ambaye pia ni Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inataka Serikali ielewe kwamba wananchi wameipa dhamana ya kumiliki nguvu za dola kwa madhumuni ya kuwalinda na kuwatetea. Kitendo cha nguvu hizi kutumika kuwaua na kuwanyanyasa wananchi, ni matumizi mabaya ya dola na kwa maana hiyo Serikali sasa imekosa sifa ya kumiliki nguvu za dola.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili kama ina taarifa za matukio ya Askari wa Jeshi la Wananchi kuwapiga, kuwanyanyasa na kuwaua raia wanyonge wasio na silaha. Pili, Serikali ieleze mbele ya Bunge hili hatua zilizochukuliwa kwa Askari waliohusika na mauaji ya Ulanga.

Mheshimiwa Spika, ahadi za Serikali na utekelezaji wake katika Wizara ya Ulinzi na JKT, kuimarisha Kamandi ya Jeshi la Wanamaji. Serikali iliahidi kuimarisha kamandi ya Jeshi la Wanamaji ili kukabiliana na vitendo vya uharamia. Aidha, Serikali iliahidi kununua meli za kivita kwa ajili ya ulinzi wa

*Exclusive Economic Zone.* Majibu ya Serikali kuhusu ahadi hii ni kwamba Wizara ipo katika hatua nzuri ya kuimarisha uwezo wa kulinda eneo la *Exclusive Economic Zone* bila kutaja mambo mahsusi iliyofanya. Pia kwenye ununuzi wa meli za kivita, Serikali inajibu kuwa upo mchakato ikiwa ni miaka miwili tangu ahadi hiyo itolewe.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kwamba katika mambo ambayo hayahitaji kabisa propaganda za kisiasa ni pamoja na ulinzi na usalama wa nchi yetu. Ni aibu kwa Serikali kuahidi jambo muhimu hivi kwa ulinzi wa nchi na kutolitekeleza kwa wakati. Ni aibu vilvile kwa Serikali kukiri kuwa na uwezo mdogo wa kufanya operesheni katika eneo la bahari kuu.

Mheshimiwa Spika, udhaifu katika kuimarisha kamandi hii, ni dhahiri kumelisababishia Taifa hasara kubwa kwani kumekuwa na wizi mkubwa wa rasilimali samaki. Meli iliyonaswa ikiiba samaki katika ukanda wetu wa bahari kuu, ni sehemu tu ya matukio ya kihalifu, ila matukio kama haya ya wizi wa rasilimali samaki yako mengi ila Serikali inashindwa kuyakabili kwa kukosa meli za kivita kwa ajili ya kufanya doria katika eneo la bahari kuu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kamandi yetu ya Wanamaji kutokuwa na vifaa vya kutosha na vya kisasa, makampuni yanayotafuta mafuta na gesi kwenye ukanda wa bahari kuu yameamua kuajiri makampuni binafsi ya ulinzi yenye silaha nzito kutoka nje ya nchi, jambo ambalo ni la hatari kwa usalama

wa taifa letu. Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kupiga marufuku mara moja makampuni ya nje kuingia na silaha nzito kwenye bahari yetu na tuimarishe kamandi ya Jeshi la Wanamaji mara moja ili itumike kufanya shughuli hiyo ya kutoa ulinzi kwenye makampuni haya na hiyo itasaidia kuifanya bahari yetu kuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuimarisha na kukarabati maghala ya silaha. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Serikali iliahidi kuimarisha na kukarabati maghala makubwa na madogo ya kuhifadhi risasi, milipuko, mabomu na vifaa vingine. Maelezo ya Serikali katika ahadi hii ni kwamba JWTZ linaendelea na jitihada za kukarabati maghala hayo ingawa tatizo ni kwamba fedha zinazopatikana hazitoshelezi kukarabati na kuboresha maghala yote kwa wakati unaostahili.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasikitishwa sana na majibu mepesi ya Serikali kwa mambo mazito ya kiusalama kama haya. Wote tunakumbuka madhara makubwa yaliyotokana na milipuko ya mabomu katika maghala ya silaha huko Mbagala na hatimaye Gongo la Mboto, Dar es Salaam. Raia walipoteza maisha, wengine walipoteza mali na nyumba zao kuharibiwa vibaya na wengine kubaki na ulemavu wa kudumu katika viungo vyao. Madhara haya yaliwapata Wanajeshi wetu vilevile. Katika mazingira ya hatari namna hii, ni aibu kwa Serikali kusema kuwa haina fedha za kukarabati maghala ya Silaha lakini fedha za kulipa posho zisizo na tija hazikosekani. Hii ni ishara kuwa Serikali haijali usalama wa Wanajeshi katika maghala hayo na raia

walio jirani na maghala hayo. Kambi ya Upinzani inasisitiza tena kwamba masuala yanayohusu ulinzi na usalama wa nchi yetu siyo ya mzaha hata kidogo. Serikali ihakikishe kwamba fedha za kutekeleza mikakati ya kiulinzi na usalama zinatolewa kwa wakati na mikakati hiyo itekelezwe kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, hali ya usalama wa mipaka ya Tanzania. Kwa mujibu wa hotuba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliyowasilishwa hapa Bungeni mwezi Julai, 2011, ni kwamba mipaka ya nchi yetu ni shwari isipokuwa katika mpaka wa kusini ambapo tatizo la mpaka katika Ziwa Nyasa halijapatiwa ufumbuzi wa kudumu. Kuendelea kuwa na tatizo katika mpaka wa Ziwa Nyasa si dalili nzuri kwa usalama wa nchi yetu. Aidha, kuendelea kwa tatizo hili bila ufumbuzi wa mapema, kutadumaza uhusiano wetu na nchi jirani ya Malawi. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa taarifa ya kiini cha mgogoro wa mpaka katika Ziwa Nyasa na hatua ambazo zimechukuliwa hadi sasa kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na malalamiko mengi toka kwa wananchi waishio maeneo ya mipakani mwa Mkoa wa Kagera na nchi jirani kuwa wanavamiwa na makundi yanayosadikiwa kuwa ni Askari wa Majeshi na kuwaibia mali zao na mahali pengine kuingiza makundi makubwa ya mifugo katika mashamba yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, taarifa kuhusu usalama na ustawi wa Mkoa wa Kagera unaonekana kuwa sio salama. Hili ni eneo ambalo Serikali

imeshindwa kulitawala kiasi kwamba Umoja wa Mataifa unatambua kwamba hili ni eneo hatari kiusalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika**,** suala hili la kuvamiwa kwa wananchi na kutishiwa, ni la muda mrefu na Kamati mbalimbali za Kudumu za Bunge zimekwenda na kujionea hali halisi lakini kwa masikitiko makubwa ni kwamba hali ya usalama wa wananchi bado iko mashakani. Aidha, kwa sasa inakadiriwa kuna wahamiaji haramu wapatao 35,000 na mifugo yao zaidi ya 200,000 katika misitu ya hifadhi na maeneo mengine katika Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasisitiza kuwa mbali ya wahamiaji hao haramu, kuna tatizo kubwa katika Ziwa Tanganyika ambapo kila mara wavuvi katika ziwa hilo wameporwa na Wanajeshi wenye silaha nzito kutoka nchi jirani. Hivi, kwa matukio haya yote, kama nchi tunapata wapi uthubutu wa kusema kuwa mipaka yetu na wananchi wetu ni salama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kupitia Jeshi letu kuweka ulinzi katika mipaka ya Mkoa wa Kagera hasa kwenye Ziwa Victoria pamoja na kutoa ulinzi wa uhakika kwenye ziwa Tanganyika. Aidha, tunaitaka Serikali ilieleze Bunge hili ina mkakati gani wa makusudi wa kuwalinda wananchi wa Mkoa wa Kagera dhidi ya matishio kutoka kwa wahamiaji hawa haramu ambao wameishawaua au kuwajeruhi rai kadha licha ya kuwapora maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa. Pamoja na umuhimu wa Jeshi la Kujenga Taifa katika kujenga ukakamavu, nidhamu na uzalendo miongoni mwa vijana wetu, jeshi hili pia limekuwa ni kiungo muhimu katika kukuza uchumi wa nchi kutokana na shughuli mbalimbali za uzalishaji mali. Hata hivyo, kufuatia kusitishwa kwa programu ya kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria mwaka 1994, nidhamu miongoni mwa vijana imeshuka sana, uzalendo pia umeshuka na ndio maana vijana wengi wanashabikia vitu vya nje kuliko vya nchi yetu; ukakamavu umeshuka na uvivu miongoni mwa vijana umeongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tayari hofu ya kuwa na Taifa la watu wazembe, wavivu, wasio wazalendo imeanza kujitokeza. Hata hivyo, hofu hii imeanza kutulizwa kidogo baada ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu mapitio na mwelekeo wa kazi za Serikali na makadirio ya matumizi ya fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2012/2013. Katika hotuba hiyo ukurasa wa 51, Waziri Mkuu alisema, ninanukuu:-

*“Jeshi la Kujenga Taifa limekamilisha ukarabati wa makambi 10 ya Jeshi la Kujenga Taifa yenye uwezo wa kuchukua vijana 20,000 kwa wakati mmoja. Kwa mwaka 2012/2013, jumla ya Vijana 5,000 wataanza tena kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria”.*Mwisho wa kunukuu*.*

Mheshimiwa Spika, ni jambo jema kuwa Serikali imetambua umuhimu wa vijana kujiunga na Jeshi la

Kujenga Taifa kwa mujibu wa sheria kwa vijana wetu waohitimu kidato cha sita. Kambi ya Upinzani inataka kufahamu kama zile sababu za kusitisha mafunzo ya JKT kwa vijana zimekwisha kabisa? Lengo la swali hili ni kuhakikisha kwamba utaratibu huu wa kujiunga na JKT unaoanza tena unakuwa ni endelevu na sio wa msimu. Pili, Kambi ya Upinzani inataka kujua vilevile kuwa Serikali ina mpango gani kwa wale vijana waliokosa mafunzo hayo tangu yalipositishwa?

Mheshimiwa Spika, viwanda, utafiti na uendelezaji wa teknolojia Jeshini. Teknolojia ni jambo la msingi na muhimu sana katika kujenga jeshi la kisasa. Kabla ya kuwa na teknolojia ya kisasa, suala la kwanza ni kuwa na rasilimali watu ambayo inao uwezo wa kubuni au kupokea na kuitumia teknolojia ya kisasa**.**

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2008/2009, ukurasa wa 20, alisema kuwa, ninanukuu:-

"...*ni kuendeleza utafiti na maendeleo ya teknolojia ya kijeshi katika viwanda vya kijeshi vya Mashirika ya Mzinga na Nyumbu***",** mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kwa nukuu hiyo inaonyesha kuwa utafiti ni kwa ajili ya vifaa vya jeshi tu. Hii ni kutolitumia vyema Jeshi kwa manufaa ya wananchi na nchi kwa ujumla kama wenzetu wa mataifa yaliyoendelea wanavyotumia majeshi yao.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Kambi ya Upinzani kwa mwaka wa fedha 2008/2009, aya ya 14,

iliongelea kuhusu umuhimu wa maendeleo ya sayansi na teknolojia; naomba kunukuu:-

"*Ili taasisi zetu za ulinzi zifanikiwe zinahitaji kuwa wazi, kuwa wavumbuzi na kukubali kubadilika na kuendana na maendeleo ya kisayansi na teknolojia. Mtaalamu wa fizikia Rutherford alinukuliwa akisema kwamba "we are short of money so we must think"***.** *Wanajeshi wetu wafahamu kuwa tuna tatizo la rasilimali fedha, hivyo inawalazimu kuwa wavumbuzi na wabunifu zaidi kukabiliana na changamoto zilizopo hivyo tunahitaji vipaji binafsi."* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, vipaji binafsi vya watendaji vinatafutwa toka ngazi za chini na kulelewa. Utaratibu huu ulikuwepo miaka ya nyuma, lakini kwa sasa nchi yetu imejikuta ikipoteza vijana wengi wenye vipaji kukimbilia nchi za nje na sasa wanafanya kazi huko. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge Jeshi letu lina mkakati gani wa kuibua vipaji na kuviendeleza ili kwa miaka ijayo tuwe na wanasayansi vijana wa kufanya tafiti sio tu kwenye nyanja za kijeshi bali pia kwenye nyanja za kilimo, madawa, mitambo, mifugo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia katika nyanja nzima za ulinzi na usalama, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutenga ardhi ya kutosha kwa ajili ya Jeshi kufungua Makambi yanayoweza kuhamishika kulingana na mahitaji ya wakati huo kuliko kugawa ardhi kiholela kwa wageni ambao hadi sasa hatujui watu hawa wana nia gani na Taifa huko mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jeshi na utekelezaji wa Kaulimbiu ya "Kilimo Kwanza." Ni jambo linalotia faraja kuona kwamba Jeshi letu la Kujenga Taifa linatekeleza kwa vitendo Kaulimbiu ya Kilimo Kwanza. Kwa mujibu wa Hotuba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika Bunge la Bajeti, Julai 2011 ni kwamba katika mwaka 2010/2011, Jeshi la Kujenga Taifa lililima ekari 1,625 za kilimo cha mbegu bora kwa matarajio ya kuvuna tani 1,039 za mbegu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pamoja mkakati huu mzuri, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuboresha mfumo huu usiwe wa kuzalisha mbegu peke yake bali pia kuwe na mikakati ya kujikita zaidi kwenye kilimo cha mazao ya chakula ili kuinusuru nchi na majanga ya njaa na pia kudhibiti mifumuko ya bei inayotokana na ukosefu wa chakula nchini. Kambi ya Upinzani inataka Serikali vilevile kutanua wigo wa shughuli za Jeshi la Kujenga Taifa kwa wananchi. Jeshi la Kujenga Taifa lishirikiane na wananchi kwa maana ya kuwaelimisha namna ya kuendesha shughuli za kiuchumi na kijamii, mfano kilimo na utunzaji wa mazingira kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza mkakati huu wa kuanzisha mahusiano ya Jeshi la Kujenga Taifa na wananchi katika shughuli za uzalishaji mali, Kambi ya Upinzani inapendekeza kwamba wale watakaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa, wawe wanafanya mafunzo ya vitendo *(internship)* kwa wananchi, katika maeneo yatakayokuwa yamechaguliwa ikiwa ni sehemu ya ukamilisho wa mafunzo yao.

Mheshimiwa Spika, utunzaji wa mazingira. Jeshi la Kujenga Taifa linashughulika pia na utunzaji wa mazingira ikiwa ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira. Hata hivyo, kwa mujibu wa Hotuba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa aliyoitoa mwezi Julai, 2011, utunzaji wa mazingira umefanyika tu katika makambi na maeneo ya Jeshi kwa kupanda miti na kuhifadhi misitu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatoa pendekezo kwa Jeshi la Kujenga Taifa kuendesha Operesheni Maalum ya Kupanda Miti Nchi nzima kwa awamu kwa kushirikiana na wananchi. Operesheni hii iendeshwe kwa utaratibu uleule kwa watakaojiunga na JKT kufanya mafunzo ya vitendo wakishirikiana na wananchi katika kutunza mazingira. Kwa kufanya hivyo, Taifa hili litaepushwa na unyemelezi wa jangwa na athari za tabia nchi zinazotokana na uharibifu wa mazingira. Kambi ya Upinzani inataka mabadiliko katika Jeshi la Kujenga Taifa ili kazi zake ziwe ni za Kujenga Taifa kweli na sio kujenga na kuendeleza makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, kashfa ya ufisadi kwa Maafisa wa JKT. Katika hotuba ya Kambi ya Upinzani mwaka 2011/2012 tulizungumzia suala la SUMA JKT kuingia mkataba wa ununuzi wa matrekta na mfanyabiashara ambaye alihusishwa na matukio ya ufisadi. Hata hivyo, kwa mujibu wa Taarifa Rasmi za Bunge za tarehe 13 Julai 2011 wakati Waziri wa Ulinzi anafanya majumuisho ya bajeti ya Wizara yake alikanusha habari hizi. Alisema, na nanukuu:-

*"….hakuna ukweli hata kidogo kwamba SUMA JKT imeingia mkataba na mfanyabiashara aliyemtaja Mheshimiwa Selasini". Mwisho wa kunukuu.*

Mheshimiwa Spika, magazeti ya Uhuru, Nipashe, Jambo Leo ya tarehe 3 Julai 2012 yana taarifa kuhusu Maafisa wa Jeshi la Kujenga Taifa ambao pia ni wajumbe wa bodi ya SUMA-JKT kushtakiwa Mahakamani kwa ufisadi wa matumizi mabaya ya madaraka na kuhamisha shilingi bilioni 3.8 kutoka katika akaunti ya Tanzania Korea Partnership (TAKOPA) kwenda kwenye akaunti ya SUMA-JKT. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa hizi zinaashiria kuwa uongozi wa Jeshi la Kujenga Taifa una matatizo ya uadilifu. Sasa kama Jeshi lenye jukumu la kujenga Taifa hili linaongozwa na viongozi wa namna hii, Watanzania wategemee nini kwa vijana wanaojiunga na JKT? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye ukaguzi maalum katika Jeshi la kujenga Taifa na hususan SUMA- JKT. Pili, Serikali itoe maelezo katika Bunge hili kuwa ina mpango gani wa dharura wa kusafisha taswira ya Jeshi la Kujenga Taifa ambayo imechafuka mbele ya jamii.

Mheshimiwa Spika, maslahi ya watumishi katika Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa. Ni uelewa wa kawaida kwamba ili mtu aweze kufanya kazi kwa ufanisi, ni lazima apate mahitaji yake ya msingi yatakayomwezesha kuishi maisha ya staha. Kwa

kuzingatia jambo hili na kwa kuzingatia umuhimu na unyeti wa kazi za majeshi yetu katika kulinda usalama na kujenga taifa letu, Kambi ya Upinzani inapendekeza maboresho ya maslahi ya watumishi katika jeshi yafanyike ili kuwapa motisha ili wafanye kazi kwa bidii zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali, kuandaa mazingira mazuri ambayo yatawasaidia wastaafu wa Jeshi kupata nafasi ya kufanya shughuli zitakazowapatia kipato cha ziada tofauti na mafao yao ya uzeeni. Kwa mfano Serikali iwakopeshe Wanajeshi Wastaafu fedha ili waanzishe vyuo vya mafunzo kwa vijana watakaotumika katika ulinzi shirikishi na ambao wataajiriwa katika makampuni binafsi ya ulinzi na kutoa huduma ya ushauri wa kitaalamu *(consultancy services)* kwa makampuni binafsi ya ulinzi.

Mheshimiwa Spika, Jeshi na migogoro ya ardhi na fidia kwa wananchi. Kwa muda mrefu sasa kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi baina ya Wanajeshi na wananchi kwenye maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Migogoro hii imepelekea kuwepo kwa mvutano baina ya wananchi na jeshi letu kwa upande mmoja na viongozi wa wananchi kwa upande wa pili.

Mheshimiwa Spika, mifano ya migogoro hiyo ni kama ile ya Ilemela, Tarime, Kunduchi na maeneo mengine mbalimbali ambayo yamekuwa yakilalamikiwa na Wabunge kwa muda mrefu. Mara zote Serikali imekuwa ikitoa majibu kuwa itawalipa fidia

wananchi ili waweze kuondoka na kuyapisha maeneo hayo kwa ajili ya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu wa fedha 2012/2013 zimeombwa kiasi cha shilingi bilioni moja kwa ajili ya kulipa fidia ya ardhi maeneo ya Mapinga, Shinyanga na Arusha. Kambi ya Upinzani inaona kuwa hakuna nia ya dhati ya kumaliza migogoro hii baina ya jeshi letu na wananchi kwani kiasi kilichotengwa ni kidogo mno kutosha kulipa fidia na hata maeneo yaliyotengewa fedha ni mawili tu. Tunaitaka Serikali iwe na nia ya dhati ya kuwalipa wananchi fidia ili kumaliza migogoro hii ambayo inawafanya wananchi walichukie jeshi lao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa tumemaliza kumsikiliza mwasilishaji wa maoni ya Kambi ya Upinzani.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mwongozo wa Spika!

**SPIKA:** Aah! Mheshimiwa, *what is a problem?* Tatizo gani?

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba Mwongozo wako kuhusiana na

hotuba ambayo imetolewa na Mheshimiwa Waziri kwa kutumia Kanuni ya 68(7) ambayo inafahamika.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 30, Mheshimiwa Waziri amesema, naomba ninukuu:-

*“Ninatoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kuheshimu maeneo yanayomilikiwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania.*

Mheshimiwa Spika, pia hapo juu alisema katika baadhi ya maeneo Wizara italazimika kuwaondoa wavamizi mara moja ili kupisha shughuli za Jeshi.

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako katika mazingira ambayo Waziri anajaribu kuwaaminisha Watanzania kwamba, Wabunge na wananchi ndiyo wamekuwa hawaheshimu maeneo yanayomilikiwa na Jeshi la Wananchi na katika mazingira ambayo hapa Bungeni tumekuwa tukilalamikia maeneo mengine Wanajeshi wenyewe ndiyo wanavamia maeneo ya Wananchi bila kuheshimu ardhi yao...

**SPIKA:** Sasa Mwongozo tafadhali! Mwongozo ni *specific* na siyo hotuba.

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Eeh, ndiyo nilikuwa naomba Mwongozo wako katika maeneo yale ambayo Jeshi na wao wamevamia na hapa wanasema wao watalazimika kuondoa wavamizi, wananchi wa kijiji cha Bunere pale Mwibara wao sasa watumie chombo gani pia kuwaondoa hawa?

**SPIKA:** Naomba usome Kanuni ya Mwongozo, sasa wewe unajadili, huombi Mwongozo wa mtu yeyote. Kwa hiyo, hakuna cha Mwongozo hapo, unajadili. *(Kicheko)*

Tunaendelea, Mheshimiwa Mchemba!

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU:** Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa kutumia Kanuni ya 47 inayosema:-

*"Baada ya muda wa Maswali kwisha, Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja kuwa shughuli za Bunge kama zilivyooneshwa kwenye Orodha ya Shughuli ziahirishwe ili Bunge lijadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa Umma. Hoja ya namna hii itakuwa maalum na inaweza kutolewa wakati wowote hata kama majadiliano yatakuwa yanaendelea."*

Mheshimiwa Spika, kufuatana na tukio la kinyama lililotokea Singida la kijana ambaye naweza nikasema ni msaidizi wangu, Katibu wa Umoja wa Vijana wa CCM wa Kata ya Ndago, kuuawa kinyama kwa kufukuzwa kama kuku akitokea kwenye mkutano uliokuwa unafanywa na CHADEMA na kukimbizwa hadi ndani ya nyumba na kuuawa, naomba kutoa hoja Bunge lako liahirishe shughuli zilizoko kwenye orodha ili kuweza kujadili hoja hii mahsusi; na hoja hii inaambatana pia na shughuli yoyote iliyofanywa kule ikionesha kwamba, ilikuwa imepangwa kwa sababu kabla ya tukio hilo kutokea, nimepokea *messages* za simu ambazo zimetumwa na baadhi ya Wabunge wa CHADEMA zikiwa zinanitishia baada ya mijadala iliyokuwa inaendelea hapa Bungeni na kuashiria kwamba, hata hilo lililofanyika kule lilikuwa na

uhusiano. Kwa ruhusa yako nitakuomba nizisome *messages* hizo ambazo Wabunge walinitumia, nilipeleka Polisi, wamejulikana na namba zao ninazo hapa...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, usijadili kwa sababu hoja sijaikubali, inatosha ukiieleza maana sasa utakuwa unajadili.

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU:** Natoa hoja Bunge lako lisitishe shughuli za leo kujadili hoja maalum, natoa hoja! *(Kicheko)*

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, msome vizuri Kanuni inayohusika. Bahati mbaya Kanuni ile inasema katika kifungu cha masharti, yako masharti mengi tu lakini la nne ambalo ni la mwisho linasema:-

*“Jambo lolote litahesabiwa kuwa ni lenye maslahi kwa umma iwapo utatuzi wake unategemea hatua zaidi kuliko zile za utekelezaji wa kawaida wa Sheria peke yake.”*

Sasa tunachokisema ni kwamba, mimi suala hili nimelisoma na nimesikia kwenye vyombo vya habari na bahati nzuri yule Msemaji wa Kamati amelaami kitu hicho, lakini tumeambiwa kwamba Polisi wanafanya uchunguzi wa kina. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa utaratibu huo ni kwamba, tukisema sisi tujadili tunataka tufikie wapi? Maana yake ni lazima iwe mahsusi. Kwa hiyo, tunaliomba Jeshi la Polisi na Waziri anayehusika hapa wafanye utafiti wa kutosha na wale wote ambao wataonekana wamehusika kwa namna yoyote wachukuliwe hatua bila kuonea mtu. *(Makofi)*

Lakini la pili, Waheshimiwa naona imeanzishwa tabia mbaya, sisi tunalindwa kwa mujibu wa Sheria ya Haki na *Privileges* za Wabunge, mtu akizungumza hapa yaishie hapa. Mnachukua maneno tena mnaanza kutishia wenzenu, wengine mnataka kuwaua, mnataka kufanya nini, jamani sasa Bunge lifanye kazi gani? Unaweza kumkubalia mtu maneno yake na mengine unaweza ukayaacha. Lakini mmeanzisha tabia ambayo ni ya kigaidi. Eeh, ni ya kigaidi na haina heshima kwenu. Kila mtu hapa atajadili na tunachooomba ajadili kwa heshima kwa sababu kwa mujibu wa Kanuni zetu hapa unatakiwa ujadili kwa heshima. Yale unayoyajadili kama ni hoja nzito, watu watakuunga mkono, lakini lugha za kihunihuni, kutishia wenzenu, mtamuua, mtafanya nini na mimi ninajua majina ya Wabunge wenyewe hao kwa sababu namba za simu zao zinaonekana zote. Jamani si heshima na hizo zote zinapelekwa Polisi kwa uchunguzi zaidi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, ninao wachangiaji, wapo wengi kidogo lakini nitaanza na Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis, atafuatia Mheshimiwa Deo Sanga, atafuatia Mheshimiwa Christowaja Mtinda, atafuatia Mheshimiwa Masoud

Salim nadhani mpaka sasa saba watakuwa wametosha hao. Mheshimiwa Sadifa Khamis!

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, *Subhanah Wataala***,** Muumba wa Mbingu na Ardhi na kila kilichomo ndani yake.

Mheshimiwa Spika, lakini pili nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii kuwa mchangiaji mwanzo katika Wizara ya Ulinzi. Tatu, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mkuu wa Majeshi, *Chief of staff* na watendaji wao kwa utendaji mzuri, mwanana na wenye kuvutia katika Wizara hii ya Ulinzi.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda mbali, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza wananchi wangu wa Jimbo la Donge kwa kutumia haki yao ya msingi ya kisheria kuniwezesha mimi kuwa Mbunge na kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kwa upande wa JKT. Ni ukweli usiopingika kusema kwamba mafunzo ya JKT ni mafunzo muhimu sana *regardless* kwamba huyu ni Mbunge au ni raia yeyote. Kwa maana ya kwamba mafunzo ya JKT huwa yanatoa uzalendo, ujasiri ndani yake. Mimi ninaunga mkono hoja hii kusema kwamba sisi Waheshimiwa Wabunge pia twende lakini pale Mheshimiwa Waziri alisema Waheshimiwa Wabunge vijana, mimi nasema isiwe Waheshimiwa Wabunge vijana pekee yako hata Waheshimiwa Wabunge wazee wanaopenda

waende. Mheshimiwa Samuel Sitta akipenda basi aende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema hivyo kwa sababu mafunzo haya ni mafunzo ambayo kama alivyosema Mheshimiwa Waziri yanamfanya raia yeyote kuwa na ujasiri, uhodari na uvumilivu ndani yake. Hata Waheshimiwa Wabunge humu tumekuwa, ndiyo haya yanayosemwa hapa sasa hivi mwenzako anasema wewe tena baadaye unaanza kumtumia *message* za kumuua, kumtishia. Kwa hiyo, kote huko kumekosekana haya ninayozungumza. Kwa hiyo, kufanya hivyo basi nasema itakuwa ni jambo nzuri.

Mheshimiwa Spika, labda nitoe ushauri wangu tu watakapopelekwa huko Waheshimiwa Wabunge kwenye hayo mafunzo ya JKT, mimi naona hayo mafunzo ya wiki tatu Mheshimiwa Waziri hayatoshi. Kwa sababu ninachokifahamu tu ndani ya mafunzo yale kuna *six week*s, zile tu pekee yake ni mwezi mmoja na nusu. Sasa sijui watakamilisha vipi mafunzo haya ili waweze kukomaa vizuri waonekane ni wanajeshi kweli. Mimi nasema hizi wiki tatu hazitoshi Mheshimiwa Waziri, ikiwezekana ninaomba ziongezwe *at least* wapate zile *six weeks* halafu baadaye wapate mwezi mmoja wa kupiga ile kwata ama ikiwezekana wasifanye mazoezi ya kwata, wafanye hizi kadebra maana kwata inawezekana isiwasaidie, lakini wafanye mazoezi ya kuruka kichurachura, wakipigwa fimbo basi hii itawasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumze kuhusiana na Jeshi. Kuna mambo ndani ya Jeshi sasa hivi

siyapendi. Wakati ule sisi tunafanya kozi *recruit* pale Kunduchi mwaka 2002, Mheshimiwa Waziri kulikuwa kuna fimbo kwa Wanajeshi, sasa hivi fimbo kwa Wanajeshi zimeondoka. Mimi nasema lazima Mwanajeshi akomae na awe Mwanajeshi kweli kweli, siyo Mwanajeshi unamkuta lelemama. Mheshimiwa Waziri sasa hivi Jeshi la sasa, mimi niombe radhi kwa lugha nitakayoisema, lina mwelekeo wa kidadadada.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Kwa nini ninazungumza hivyo, kwa sababu ya ubi-*show* fulani uliokuwepo.

**WABUNGE FULANI:** Tuombe radhi!

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Ndiyo maana nikaomba radhi, nimeomba radhi mapema.

**SPIKA:** Mheshimiwa, uondoe maneno ya kidadadada!

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Usharobaro... *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, uondoe maneno hayo unawaudhi wenzio.

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, hizi kauli ninazifuta, lakini nimeomba radhi mapema, yaani sijui nitamke namna gani? Lakini nasema hizi Haki za Binadamu ambazo zinakuwepo ndani ya Jeshi zinapelekea Jeshi letu kutokuwa imara.

Mheshimiwa Spika, mimi nawaambia mwaka 2003 wakati tunaenda Jeshini, Mwanajeshi anapigwa fimbo, sasa hivi hapigwi fimbo. Unakuta yule Mkufunzi sasa hivi anawekwa kitimoto kwa sababu amempiga eti mtoto wa mkubwa, kama mtoto wako unataka asipigwe fimbo usimpeleke Jeshini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo haya ambayo ameyasema Mheshimiwa Natse sasa hivi, unampeleka mtoto, lakini akipigwa fimbo mkubwa analalamika. Ninaamini kwamba Jeshi hili tulilokuwa nalo ni Jeshi imara lakini tunaomba sasa mwelekeo huu ambao unakwenda katika Jeshi letu basi ubadilike. Nashukuru, nadhani nimeeleweka vizuri.

Mheshimiwa Spika, nigusie suala la migogoro ya ardhi kati ya wananchi na Jeshi hili. Mimi Mheshimiwa Waziri ulipokuwa unasema hapa kutuomba sisi Waheshimiwa Wabunge, mimi nasema usituombe, chukua hatua, si kuna sheria, aliyevamia kama hakufuata sheria ina maana huyo amekwenda kinyume na sheria, hutakiwi tena kuja kuniambia Mheshimiwa Sadifa hapa hivi na hivi, hapana chukua hatua ambazo zinastahiki kwa mujibu wa sheria. Mimi nadhani hili nisilizungumzie sana.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna maeneo ambayo ni *very sensitive*, ni maeneo ambayo ni *potential* kwa Jeshi letu kwa mfano, kama kule Zanzibar maeneo ya Unguja Ukuu, ni mahali wanapopigia shabaha pale, ni eneo ambalo limevamiwa sasa hivi. Sasa sijui mtaliangalia namna gani ili kuweza kutatua suala hili. Mimi nasema shabaha kwa Jeshi letu ni muhimu, *we*

*have to solve this problem* ili jeshi letu liongezeke kuwa imara zaidi ya uimara huu ambao upo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine nizungumzie suala la ajira. Ajira tuliyokuwa nayo hii wanaoajiri Jeshi la Ulinzi, mimi nasema sasa hivi siipendi. Kwa nini nasema hivyo? Wao wana *system* ya kuchukua wananchi kupitia JKU na JKT lakini kule Zanzibar JKU namna ambavyo wanapatikana wale watu kuna uchakachuaji wa hali ya juu. Kuna ubinafsi wa hali ya juu. Mimi siridhiki na *system* ile. Lakini unakuta pia kule Zanzibar kuna kiongozi mmoja anatumia mamlaka na madaraka aliyokuwa nayo anachukua nafasi 40 pekee yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria na Katiba yetu, ajira au ujira ni haki ya kila Mtanzania. Sasa anapochukua mtu mmoja pekee yake ni kweli ametutendea haki Wazanzibar, ametutendea haki Watanzania? Mimi ninaomba sana, sikatai kiongozi asichukue nafasi, acha achukue, lakini basi angalau achukue nafasi 10 hizi zingine awaachie wengine. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Zote za nini?

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, haya ni mawazo yangu, ninaomba mniheshimu.

Mheshimiwa Spika, achukue nafasi 10 na nafasi 30 awaachie wananchi wapatiwe hizo nafasi, lakini alichukua nafasi 50, nina ushahidi, Jimbo moja tu anachukua mtu nafasi 50 pekee yake. Yule mtoto wa

mkulima akale wapi na afanye kazi gani? Mimi hilo nasema, hao viongozi wanajifahamu nisiwataje majina, ninaomba wajirekebishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie suala la maslahi kwa Wanajeshi. Ni ukweli usiopingika kila mwananchi anapiga debe kuhusiana na maslahi yake. Wanajeshi hawa hawawezi kuandamana. Niipongeze Serikali imejitahidi kwa namna ilivyoweza katika kuwasaidia Wanajeshi. Ni kweli imepandisha posho kutoka Sh.5,000 mpaka Sh.7500, niipongeze katika hili lakini naomba tuwasaidie na tuwafikirie kwamba *at least* itoke Sh.7500 ije mpaka Sh.10,000/=, hawana mahali pa kuandamana hawa, wakiandamana Wanajeshi hapa itakuwa ni balaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe na mimi tunalala usingizi mzuri hivi sasa kwa sababu hawa Wanajeshi wao ndiyo ambao wanatulinda lazima tuwafikirie, tuwaone na tuwajali kwa kiasi fulani na umuhimu wa kuwepo kwao. Ninasema hivi kwa sababu hata mimi nilikuwepo hukohuko. Hiyo kozi tu pekee yake ni balaa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. SADIFA JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nina *point* nyingi sana lakini muda hautoshi, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sanga atafuatiwa na Mheshimiwa Christowaja Mtinda.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi ili nami mchana huu niweze kuchangia. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri aliyowasilisha hapa inayohusiana na bajeti ya Ulinzi.

Mheshimiwa Spika, nijikite kuzungumzia habari ya mipaka kati ya wananchi na Jeshi. Kuna tatizo hili la mipaka ya wananchi na Jeshi hususan kule Makambako katika Kata ya Kitangirilo, Kata ya Mlowa na kijiji cha Kidofi. Wananchi hawa wanapata tabu sana juu ya mipaka yao na Jeshi. Nimewahi kwenda kwa Mheshimiwa Waziri nikimwomba kwamba ni vizuri aje atutembelee akalione tatizo hili ambalo lipo kati ya Jeshi na wananchi.

Mheshimiwa Spika, tatizo hili ni kubwa katika eneo langu la Njombe Kaskazini mpaka imefika mahali wananchi hawa wamenyang'anywa mpaka vitindi vyao vya ulanzi wanavyogema, ulanzi unawaletea pato kubwa sana wananchi hawa. Sasa hivi vitindi vile vinagemwa na Wanajeshi. Nakuomba Mheshimiwa Waziri kama ambavyo tulikuwa tumezungumza, ni vizuri ukatembelea eneo hilo ili tuongozane na mimi Mbunge na viongozi wenzangu wa eneo lile ili ukajionee mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, hivi Wanajeshi au Askari kwa ujumla, unamkuta wakati fulani amevaa *uniform* yake, *uniform* ile ina viraka au imechanika.

Sasa unashindwa kutofautisha huyu ni Askari au ni nani? Naomba kupitia Bajeti hii, ni vizuri Askari wetu wawe na nguo ambazo zinalingana na hadhi yao.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amezungumzia habari ya matrekta ya Kilimo Kwanza. Mheshimiwa Waziri katika ukanda wetu au kwenye Mkoa wetu wa Njombe na Iringa, sisi ni miongoni mwa wakulima wakubwa hususan Wilaya Njombe, Ludewa, Makete na Mufindi. Naomba angalau wafungue kituo cha matrekta katika eneo la Makambako ambalo litakuwa *centre* kwa Wilaya hizi ambazo nimezitaja, itatusaidia sanasana kuweza kupata haya matrekta.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amezungumzia habari ya vijana kujiunga na JKT kwa kipindi hiki kwamba watakuwa vijana zaidi ya 5000. Niungane na mwenzangu aliyechangia, idadi hii ni ndogo sana ukilinganisha na vijana ambao wanamaliza shule na katika vyuo mbalimbali. Naomba idadi hii iongezwe ili vijana wetu wakienda huko wawe wajasiriamali na wanapata mambo mazuri kupitia JKT.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo na mwenzangu amelichangia hapa kuhusu Waheshimiwa Wabunge kwenda kwenye mafunzo. Hata mimi nipo tayari kwenda kujiandikisha ili kuepusha haya ambayo alikuwa anazungumzia Mheshimiwa Mwigulu pale, tutakuwa na sisi tayari tuna nguvu, tuna uwezo wa kupambana na jambo lolote ambalo litakuwa mbele yetu.

**MBUNGE FULANI:** Unaweza?

**MHE. DEO K. SANGA:** Ndiyo ninaweza si unaona.

Mheshimiwa Spika, mwisho siyo kwa umuhimu, nimalizie tu kwa kumwomba Mheshimiwa Waziri kama ambavyo nilikuwa nimemwomba japo anajua kuna mambo ambayo tulikuwa tumeyazungumzia basi ahadi ambayo aliniahidi kwamba kabla Bunge halijamalizika tutaongozana siku za *weekend* ili tuweze kwenda huko Makambako ili aweze kwenda kuona maeneo ambayo yana matatizo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu kuhusu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwanza niwapongeze Wanajeshi wetu kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya pamoja na mazingira magumu wanayokabiliana nayo. Nawapongeza kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, mimi nianze moja kwa moja kwenye hoja kadhaa kama muda utaniruhusu. Nianze na huduma zinazotolewa kwa Wanajeshi wetu hususan maduka ya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa Wanajeshi iliweka utaratibu wa kuanzisha maduka ambayo yalitolewa msamaha wa kodi ya vifaa au bidhaa zinazoagizwa nje ili bidhaa hizo ziweze kuuzwa kwa bei nafuu na kuwafanya Wanajeshi

waweze kuzinunua. Lakini cha kusikitisha sana, maduka haya tangu mwaka jana katika hotuba ya Kambi ya Upinzani nadhani tulizungumzia sana suala hili, maduka haya badala ya kuuza bidhaa hizo kwa bei ambayo inatakiwa iuzwe maduka haya yamegeuzwa kuwa vitega uchumi vya wawekezaji. Niseme wazi naomba nisinukuliwe vibaya, siyo mbaguzi, maduka haya yanaendeshwa na wenzetu wenye asili ya Kiasia, Wahindi tena hawajui Kiswahili. Nisionekane ni mbaguzi hali halisi ndivyo ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa Wahindi wamekuwa wakiuza bidhaa kwa bei kubwa sana. Wakubwa wa Jeshi wapo hapa wanalifahamu suala hili, kwa sababu wao na familia zao wanakwenda kufanya *shopping* katika maduka haya.

Mheshimiwa Spika, nitoe mifano michache, maduka haya ni *duty free*, lakini sukari katika duka la Jeshi inauzwa kilo moja Sh.1800, maduka ya uraiani kilo moja inauzwa Sh.2000, *fridge* moja inaanzia Sh.500,000 mpaka Sh.700,0000 sawa na bei ya Kariakoo, *TV flat screen* moja inaweza ikauzwa kuanzia Sh.700,000 mpaka Sh.2,000,0000/= mpaka Sh.3,000,000/= sawa na maduka ya Kariakoo ambayo yanalipa kodi. Vilevile na mabati na vitu vingine kama *music system*.

Mheshimiwa Spika, *TRA* wanafahamu na wanalijua hili, viongozi wakubwa na Maafande mpo hapa mnalifahamu. Mimi nauliza kwa nini Serikali imetoa jukumu la kufuta kodi katika maduka haya lakini wenzetu wa Kiasia wanaendelea kuuza kwa bei kubwa na kujipatia faida? Naomba maelezo ya kina kwa

sababu mimi ni mdau wa maduka hayo na mimi ninafanya *shopping* pale, nina ushahidi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, kuna maneno yanazungumzwa kwamba maduka haya yana mkono wa wakubwa sijui wakubwa gani? Jeshi nzima lipo hapa, wakubwa wote mpo hapa kuanzia Mkuu wa Majeshi na wengine wote. Sasa sijui huo mkono ni wenu au ni wa nani, mtajichunguza au mtachunguza mtafahamu. Mimi nimetoa taarifa, nafikiri linafahamika. Mheshimiwa Waziri, naomba kupata maelezo katika hili.

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye nyumba za Wanajeshi. Pamoja na kwamba hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, imeonyesha kwamba kuna mkopo ambao utatolewa kujenga nyumba za Maafisa wa Jeshi na Askari wengine lakini kuna nyumba za Maafisa wa Jeshi ambazo wanakaa sasa hivi, hizo nyumba niseme wazi tangu zimejengwa hazijawahi kufanyiwa ukarabati, ni nyumba ambazo zinatia aibu Jeshi, zinatia aibu Maafisa wa Jeshi. Ukifungua mlango, mlango una mapengo, madirisha yamevunjika ni nyumba ambazo wanaishi Maafisa wa Jeshi. Matokeo yake wanatumia hela zao za mfukoni kukarabati nyumba hizo.

Mheshimiwa Spika, lakini Maafisa Jeshi wengine wanaokaa uraiani kwenye nyumba zao walizojenga wenyewe wanapewa *Ngome Allowance* kuanzia Sh.400,000 mpaka Sh.900,000 kutokana na vyeo vyao. Sasa hapa usawa uko wapi kwa Wanajeshi wetu hawa?

Mheshimiwa Spika, mimi nashauri jambo moja ili kuepukana na migogoro ya kuharibu nyumba hizi basi Maafisa wa Jeshi wanaoishi katika nyumba hizo wawe wanapewa *allowance* ya kukarabati nyumba hizo kama ambavyo wenzao wanapewa, wale wanaoishi uraiani. Nafikiri hilo ombi litachukuliwa kama ambavyo linatakiwa lichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine la madeni. Madeni yamezungumzwa sana. Niseme wazi kwamba katika Wizara zinazoongoza kuwa wadaiwa sugu wa Mamlaka za Maji na *TANESCO*, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma. Mamlaka zote za Maji zinazokuja kwenye Kamati yetu, Shirika la Umeme madai ni yale yale kwamba Jeshi halilipi madeni ya maji. Hiki kiwango kilichotolewa hapa cha Shilingi milioni 24 hakitoshelezi. Kila siku tunapitisha bajeti hapa tunapitisha bajeti ya Jeshi ambayo mojawapo ni kulipia maji na umeme. Hizi fedha zinakwenda wapi? Tunafahamu Wanajeshi na familia zao lazima walipiwe hizi huduma, sasa kama hawalipiwi, matokeo yake tunashuhudia; juzi juzi au miaka ya karibuni watumishi wa Mamlaka za Maji walivyokwenda kukata maji, walipigwa na Wanajeshi. Sasa wao wanakwenda kukata maji kwa mujibu wa taratibu zao, lakini wanapigwa. Sasa hii ni kudhalilisha Jeshi na Wanajeshi kwa ujumla. Tunahitaji maelezo, hizi fedha ambazo tunatenga kila siku na kuzipitisha, zinaliwa na nani au kwa sababu Wanajeshi hawaulizi, na kwa sababu ni

wapole hawawezi kugoma? Kwa kweli inatia aibu na inasikitisha sana. Madeni haya yalipwe!

Mheshimiwa Spika, kuna deni lingine tena, Suma JKT iliingia Mkataba wa ujenzi na Kampuni moja inayoitwa *Millenium Express Company Limited.* Hii Kampuni inaidai Suma JKT Sh. 194,718,000/=. Wamepelekana Mahakamani, hii Kampuni imeshinda, Mahakama imetoa kibali cha kwenda kuchukua mali zao. Wanapokwenda pale Suma JKT wanawaambia hili ni eneo la Jeshi, hawaruhusiwi mtu kuingia, kuna vifaa vya Jeshi, sijui kuna silaha; sasa kwa nini mliingia Mkataba na mkajengewa? Kwa kweli tunatishana. Hii ni haki ya watu, Suma JKT walipe hili deni kwa sababu ni aibu. Tunajua ndiyo, Makambi ya Jeshi yana silaha, lakini hii ni amri ya Mahakama na wanafahamu kwamba Jeshi ni mahali ambapo panahitaji ulinzi. Lakini siyo kwamba ni ruhusa ya kutokulipa deni. Deni hili ni kubwa kwa kweli linahitajiwa kulipwa.

Mheshimiwa Spika, nina suala lingine kuhusu Madaktari wa Jeshi hususan hospitali ya Lugalo. Madaktari hao wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu sana. Wanapogoma Madaktari wa Uraiani, Jeshi ndiyo linachukua nafasi ya kuhudumia wagonjwa wote wa Mkoa wa Dar es Salaam na Mikoa ya jirani, tunafahamu. Lakini angalia mishahara yao, kwa mfano hai kabisa, *specialist* wa Jeshi wa mifupa mwenye *Ph.D.* yaani yule analipwa mshahara wake Sh. 1,302,600/=. Lakini Daktari, raia mwenye *Masters,* yeye analipwa Sh. 2,162,000/= *basic salary.*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nahitaji maelezo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Wewe umesema ni Mjumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali au ya Mashirika ya Umma? Umesema Mjumbe wa Kamati gani?

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Kamati ya Mashirika ya Umma.

**SPIKA:** Lakini huku-*declare* pia *interest* nyingine kwamba mume wako pia ni Mwanajeshi. *(Makofi)*

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nahitaji maelezo kwa Mheshimiwa Waziri ya tatizo la mpaka, Wanajeshi kujiongezea eneo Unguja Ukuu. Eneo hili tangu mwaka 1964 lilionekana waziwazi kwamba lilikuwa linatumika kutoka Unguja Ukuu kuelekea Tindini na siyo kuelekea Kikungwi. Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anafanya majumuisho hapa, aniambie ni Mkakati gani, au ni mpango gani ambao anapanga wananchi hawa wa Unguja Ukuu waondokane na tatizo hili ambalo maeneo yao yamechukuliwa na Jeshi, sambamba na eneo la Chukwani lililokuwa la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, Kikosi cha 12 KJ Bavuwai kuna maeneo ambayo yameruhusiwa kulima, lakini kuna Kamanda ambaye ameharibu mazao ndio ana Kikosi cha 12JK kule Bavuwai. Ni kawaida kwamba mahali popote pale kuna maeneo yaliyoruhusiwa kulima mazao madogo madogo ya biashara. Sasa eneo hili kuna kiongozi, Kamanda wa 12 KJ Bavuwai ameharibu mazao. Naomba Mheshimiwa Waziri

utakapokuja hapa uniambie kiburi hicho na ubabe huo ameupata kwa nani?

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye suala la wastaafu. Imeelezwa wazi wazi, lakini tatizo la wastaafu la muda mrefu la kuwasahau kutowapatia chochote na ahadi za mara kwa mara kwa Serikali ni jambo baya ambalo halipendezi. Inakuwaje leo kunakuwa na Sherehe za Siku za Mashujaa ambayo inaadhimishwa kila tarehe 25 Julai, kwa kila mwaka watu ambao wamekwenda vitani Kagera au waliokwenda kule Msumbiji wanakumbukwa, lakini inasikitisha inatumiwa Sh. 582,000,000/= au Sh. 580,000,000/= lakini familia za wastaafu na ambao leo ni walemavu na familia zao hawatunzwi, wametupwa na wanaendelea kupata umaskini.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ana mkakati gani wa ziada kwa wastaafu hawa tangu baada ya vita, Mawaziri wenzake waliopita walikuwa wakilalamika. Naomba nikumbushe, mwaka 1980 – 1983 kulikuwa na Waziri aliyekuwa anaitwa Jenerali Abdallh Twalipo, mwaka 1983 – 1985, Brigedia Muhiddin Kimario, mwaka 1985 – 1989 Mheshimiwa Salim Ahmed Salim, mwaka 1989 – 1990 Mheshimiwa Jackson Makwetta, mwaka 1990 – 1995 Mheshimiwa Abdulrahman Kinana, mwaka 1995 – 2000 Mheshimiwa Edgar Maokola Majogo, mwaka 2001 – 2005 Mheshimiwa Philemon Sarungi, mwaka 2006 – 2008 Mheshimiwa Juma Kapuya, 2008 – mpaka Aprili, 2012 Mheshimiwa Hussein Mwinyi na wewe tarehe 10 Mei sasa ni Waziri, Wastaafu hawa wanalia machozi yao mpaka sasa hayajafutwa. Kuna mkakati gani

Mheshimiwa Waziri? Hawana miguu, hawana mikono, na viungo bandia hawa hawapati, vigari vyao waliokwenda vitani mpaka leo ndiyo vimemalizika na wao ndio hohehahe.

Mheshimiwa Waziri Shamsi Vuai Nahodha wakati ukifanya majumuisho utafuta vipi machozi ya watu hawa? Kila siku ikitokea, wakati mpaka wa vifo ndio mnakuja mnasoma risala, mnawathamini, lakini wenyewe wameshakufa. Wamefanya kazi nzuri, kazi nzito, hamwoni aibu! Hii siyo fedheha kwa Taifa? Angalieni nchi za wenzenu jirani ambao nao vilevile watu wao walikwenda vitani wanavyowatunza. Hilo lilikuwa dogo dogo.

Mheshimiwa Spika, la pili, katika jambo ambalo haliwapendezi wananchi hivi sasa ni suala zima ambalo Mheshimiwa Waziri amegusia, suala zima la maeneo ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Ukiangalia kitabu cha Serikali katika taarifa za utekelezaji wa ahadi za Serikali mwaka 2007, aliyoyasema Mheshimiwa Waziri yote hakuna jipya. Maeneo ambayo walichukua Wanajeshi kwenye kitabu hicho kwamba yatapimwa, yatatathminiwa na watapewa fidia. Leo imetengwa Shilingi bilioni moja kwa maeneo matatu; Arusha, Shinyanga na Mafinga, lakini yale maeneo ambayo watu wamechukuliwa maeneo yao hakuna fedha ambazo zinaandaliwa kutolewa. Nataka nimkumbushe Mheshimiwa Waziri, maeneo ambayo yamechukuliwa na Jeshi tangu mwaka 2007, Serikali imeahidi, lakini Serikali imesema uongo, tabia mbaya, hawajawalipa wafuatao: Wa kwanza Oldonyosambu Arusha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masoud maneno hayo katika kanuni zetu zinakataa, futa maneno "Serikali imesema uongo."

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naondoa.

Mheshimiwa Spika, Kunduchi *Referal Dar es Salaam* Serikali iliahidi mpaka leo bado. Bulombola JKT - Kigoma, Kyabakari 253 KJ - Mara, Buhemba JKT - Mara, Chita JKT - Morogoro, Makutopora JKT - Dodoma, Maramba JKT - Tanga, Mlale JKT - Ruvuma, Rwankoma JKT - Mara, Tunduru *TPDF* - Ruvuma, *Umoja Camp* - Mtwara, Mgambo JKT - Tanga, Kisanga *TPDF* - Rukwa yote yamo kwenye kitabu cha ahadi za Serikali, mpaka leo tangu mwaka 2007. Mheshimiwa Waziri Shamsi Vuai Nahodha lipi jipya wakati ukija hapa?

Mheshimiwa Spika, lingine naendelea. Katika jambo ambalo halifurahishi, ni kwa nini kama Serikali haijawa tayari na kwa sababu inatoa taarifa kuwaambia wananchi, kwa nini isitekeleze? Kusuasua huko ni kwa nini? Tatizo ni nini? Udhaifu uko wapi? Fedha hizi zinakwenda wapi? Tatizo hili kwa kweli limewachosha wananchi, hasa kwa hali hii, wananchi wanasema jamani, tusemeeni huko. Tunasema tunajitahidi, lakini Serikali hata ukisema haisikii, sio sikivu kweli, wana matatizo kweli! Wakali ukiwaambia, ukiwaambia wanakwambia wewe mbaya tu.

Mheshimiwa Spika, naendelea. Tatizo lingine ni tabia ambayo siipendi ya fedha za maendeleo kuchukuliwa kulipia madeni. Mwaka 2011/2012

kulikuwa na Shilingi bilioni 148 fedha za maendeleo na sasa umepewa Shilingi bilioni 400.8 ongezeko la Shilingi bilioni 300. Lakini maendeleo hayapatikani kwa sababu mara nyingi visasi na kama fedha za maendeleo zinachukuliwa, zinalipiwa madeni, tabia hii lini itakoma?

Mheshimiwa Spika, kwa haraka haraka niende katika suala zima la Tanzanisino Kiwanda cha Kutengeneza Madawa cha Binadamu. Kiwanda hicho kimepata faida kiasi gani kuanzia Juni, 2011 hadi Juni, 2012? Kiwanda cha Kushonea Nguo cha Kamisuma kimepata faida kiasi gani kuanzia Juni 2011 hadi Juni 2012? Wa Gongo la Mboto je, madai yao mmeshayamaliza au bado madeni yao au nao wamo kati ya hao? Wanadai baadhi ya askari mbalimbali fedha zao za likizo za safari madeni hayo na wao wamo, fedha zao nao bado zimo. Wanauliza mambo yamekuwa makubwa, madeni yanaendelea kuongezeka siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye uajiri. Uajiri ni tatizo kubwa, limekuwa na usiri mkubwa, ni kizungumkuti, kiini macho, hakuna kinachojulikana, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha utakapokuja hapa utuambie hasa utaratibu gani umeuandaa kuweka wazi bayana hadharani wa kuchukuliwa vijana hawa wakati wa uajiri. Mheshimiwa Sadifa hongera, umesema tatizo hili limekuwa na usumbufu kweli majimboni kwetu tunapata malalamiko makubwa, lakini tunayaleta hapa kila wakati tunaambiwa michakato inaendelea, vuta subira, mipango kabambe. Utakapokuja hapa wakati unafanya

majumuisho unasemaje Mheshimiwa Waziri Shamsi Vuai Nahodha?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JADDY SIMAI JADDY:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii niweze kuchangia machache katika Wizara hii. Kwanza nami pia napenda kumpongeza Waziri kwa kuwasilisha vizuri hotuba yake. Hotuba ambayo kwa kweli inatia matumaini.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mimi ninakoelekeza ni kuhusiana na Kambi za Maaskari. Waziri aliyepita kabla, ya aliyepo sasa niliwahi kumpa hoja ya uchakavu wa majengo ya kazi ya Kambi iliyopo Potoa ndani ya jimbo langu. Kwa kweli Kambi ile majengo yake yanatia aibu. Miundombinu ya Kambi ile kama utakwenda kutembelea wakati wa mvua, basi inabidi kwanza uende na mwamvuli, kwa sababu yanavuja. Maaskari wenyewe wakati wa mvua inabidi wawe ni watu wenye kuhamahama kwa sababu majengo yenyewe ni mabovu, hayafai kwa kweli kwa shughuli za kiaskari. Baada ya kulifikisha suala hilo kwa Mheshimiwa Waziri aliyekuwepo wakati ule, niliwasilisha hoja hili kwa njia ya swali na nilijibiwa kwamba tayari kumeshatengwa fedha kiasi cha Shilingi milioni 109 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya Kambi ile. Sasa ninachotaka kumwuliza Waziri, sijaona katika bajeti labda pengine kiko hicho kifungu sasa hivi cha kuweza kuendeleza hiyo miundombinu ya ile Kambi.

Mheshimiwa Spika, siyo tu miundombinu ya ile Kambi, lakini hata majengo ambayo wanaishi wenyewe maaskari, kama nyumba zao, ni majengo ya zamani sana, kwamba kwa sasa hivi milango ya kuingilia badala ya kutumia mbao sasa wanatumia vitambaa, imekuwa ni aibu! Kwa kweli, Ofisa wa Cheo cha juu anatoka nyumbani kuchafu, anakwenda kazini hakukaliki, ni matatizo! Ile Kambi pengine Mheshimiwa Waziri anaitambua kama ipo au haipo, siwezi kuelewa. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba siyo tu kuniambia kwamba hiyo bajeti inaendelea kuwepo au haipo, lakini pia ningemwomba Waziri afanye ziara makusudi ya kwenda katika ile Kambi kuona matatizo waliyonayo wale Maaskari. Kwa kweli ni hatari sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo, sasa nije katika suala la pili ambalo limezungumzwa na Wabunge wengi hapa kuhusiana na migogoro ya ardhi iliyopo baina ya Makambi na raia. Katika Kambi ile upo mgogoro wa zamani sana wa ardhi, mgogoro ambao maaskari au raia wanasema kwamba Maaskari wamejiongezea eneo la kiutawala wa ardhi, jambo ambalo askari wanasema kwamba toka hapo mwanzo ile ardhi ilikuwa ni sehemu yao. Wakati fulani nilipata bahati ya kutembelea ile sehemu na kweli nilikwenda kuona yale mabango yaliyowekwa kwa kutoka sehemu ambayo kulikuwa na hizo *beacons* za mwanzo walikuwa wameongeza eneo fulani na ndilo lilikuwa na mgogoro.

Mheshimiwa Waziri anatuambia sisi Wabunge tujitahidi kuelimisha raia wasivamie maeneo ya Kambi za Maaskari, Mheshimiwa Mbunge wa Mwibara hapa

alizungumzia suala hili, kwamba je, iwapo Maaskari wenyewe ndio wanatoka katika maeneo yao na kuingia uraiani, sasa Mbunge elimu gani atakwenda kutoa kwa Maaskari? Kwa raia, atasema, jamani msivamie Makambi. Sasa je Mbunge aende kwa Maaskari awaambie, jamani Majeshi msivamie raia! Inakuwa ni ngumu kidogo. Kwa hiyo, tungemwomba Mheshimiwa Waziri, hili suala la migogoro ya ardhi, nadhani limefika mahali sasa, ni vyema likaangaliwa kwa jicho pana zaidi kwa sababu unapotokea ugomvi kati ya raia na askari, kwa kweli ni hatari. Askari wanapoamua huwa wanavamia vijiji tu na wakifika eneo wanapiga mikanda tu wao. Sasa raia hawezi kwenda Kambini. Kwa hiyo, suala hili la utatuzi wa migogoro ya ardhi baina ya raia na Maaskari kwa kweli liko mikononi mwa Wizara husika na hususan Waziri mwenyewe. Kwa hiyo, suala la kumwambia Mbunge ndio *mediator* baina ya mgogoro wa pande mbili hizi itakuwa ni ngumu sana.

Kwa hiyo namwomba Waziri, atakapokuja hapa kufanya majumuisho ya bajeti yake aniambie kwa sababu tayari suala hili nimeshafikisha kwake, ni lini au ni hatua gani ambazo ameshazichukua au amekwishakusudia kuzichukua ili kuweza kutatua mgogoro ambao upo katika Kambi ile? Kwa sababu ni wimbo wa kila siku. Nikifika Jimboni, wananchi wananifuata, bwana tuna mgogoro na Kambi, unafanya nini katika kutatua tatizo hili? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nakuomba hili suala ulichukue na ulipe uzito mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa Wabunge, naona kwa asubuhi hii ndiyo hao waliweza kupata nafasi. Lakini tutakaporejea mchana atapatiwa Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mheshimiwa Dkt. Stephen Kebwe, Mheshimiwa Betty Machangu, halafu tutaendelea na wengine.

Nina tangazo moja tu kwa wale wanaolima Pamba, kutakuwa na kikao chao saa 7.00 hii Ukumbi wa Msekwa 'B'. Vinginevyo nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati naahirisha shughuli mchana, nilikuwa nimewataja wafuatao kwamba watachangia jioni hii. Ataanza Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Kebwe Stephen Kebwe.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia uzima na afya. Pili, Naomba nitoe mkono wangu wa pole kwa wananchi wa Iramba Magharibi kwa kifo cha kijana wao mpendwa, kifo hicho cha kikatili. Sisi sote tumesikitishwa na tunamwombea kijana wetu Mwenyenzi Mungu amjalie, amlaze mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Watanzania tutakuwa wezi wa fadhila tusipowashukuru wanajeshi wetu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Kwa kweli tumeona mengi wanayafanya katika kuhakikisha ulinzi na usalama wa nchi yetu. Hii imetuthibitishia hivi karibuni tulivyosikia wanajeshi wetu wameweza na wamethubutu kuwakamata maharamia wa kisomali ambao tayari walikuwa wameshaingia ndani ya bahari yetu. Lakini pamoja na hiyo, tumeona wanajeshi hawa katika Maziwa Makuu wanavyojitahidi katika kuilinda nchi yetu na mipaka yetu. Kwa kweli wanajeshi wetu wanastahili pongezi za hali ya juu na Mwenyezi Mungu awazidishie upendo na waendelee kuilinda nchi yetu na tuendelee kuipata amani na salama ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, napenda kuchangia kuhusu kuustaafu kwa hawa wanajeshi. Kwa upande wa matibabu, tunajua wanapokuwa wazima wanakuwa wanatumia zile fursa ambazo wapo jeshini, wanatibiwa katika hospitali za Jeshi na Hospitali hizi za Jeshi kwa kweli ni nzuri, hata sisi kule kwetu Zanzibar ipo Hospitali ya Bububu tunaitumia hata sisi raia. Lakini pia kuna hospitali ya Lugalo na nyingine nyingi Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Wanajeshi hawa wamekuwa katika mikataba yao, wana fursa kubwa ya kutibiwa kwenye hivi vyombo vyao vya kijeshi. Lakini tufikirie pale utumishi wao unapomalizika ndani ya jeshi, kwa kweli wanateseka na wanahangaika. Kwa sababu wanakuwa hawapati tena ile fursa ya kutibiwa ndani ya Jeshi. Hivyo, mimi nilikuwa nashauri Wizara hii wawaanzishie Mfuko wa Bima ya Afya. Hii Bima ya Afya

itaweza kuwasaidia hawa wanajeshi wakati ule wanapostaafu. Mfuko huu uwe wa hiari, isiwe lazima.

Mheshimiwa Spika, kila mwanajeshi ambaye anataka kujiunga, itolewe hiyo *order* aruhusiwe ajiunge, na hii itamsaidia pale atakapostaafu. Lakini pia itaweza kumsaidia hata akiwa hajastaafu kwa sababu anakuwa na familia, ataweza kuisaidia familia yake katika ule Mfuko wa Bima kama mama yake au watoto wake hawataki kwenda kutibiwa jeshini, wanataka kwenda kutibiwa *private, a*u wanataka kumwona *specialist* Muhimbili, pia itaweza kumsaidia ikiwa yule mwanajeshi amejiunda katika Bima ya Afya.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema pia kazi ngumu wanazozifanya wanajeshi wetu, tunawaona na sote ni mashahidi, lakini kwa kweli wanapostaafu pensheni yao pia ni ndogo sana. Kwanza, naishukuru Serikali ilikuwa inawalipa baada ya miezi sita, lakini sasa hivi imewarahisishia, *at least* miezi mitatu wanalipa. Lakini ukiangalia miezi mitatu, mwanajeshi analipwa Sh. 150,000/=, kwa kweli ni ndogo sana ndani ya miezi mitatu. Anakopa, anakuwa na matumizi makubwa, anakuja kupata hela miezi mitatu Sh. 150,000/=, kwa kweli inakuwa haimtoshi. Naiomba sana Serikali iangalie hii pensheni ya wastaafu wetu wa kijeshi waiongeze *at least* na wao wajione ni Watanzania ambao wameitumikia nchi yao.

Mheshimiwa Spika, naomba nije katika Jimbo langu la Kiembesamaki. Kule Kiembesamaki kuna kambi mbili za kijeshi, tunaita Yabuyu na Chukwani. Lakini hapo nyuma wanajeshi walipimiwa na

wakachukua maeneo ya wananchi. Maeneo yale wananchi hawajalipwa. Bado wana mgogoro na Jeshi na nimesikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeelezea tu baadhi ya sehemu ya Tanzania Bara ambazo zitalipwa, lakini haijataja hata sehemu moja ya Zanzibar ambazo zina migogoro ya mipaka na wanajeshi kulipwa kwake. Hivyo, naomwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo na ajue kuwa Zanzibar eneo la Jeshi na wananchi bado yana migogoro yakiwemo maeneo ya ndani ya Jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumjulisha Mheshimiwa Waziri kwamba kule Chukwani kuna kipande kimoja zamani kilikuwa kinatumika kwa ajili ya mafunzo ya mgambo. Sisi hatukatai kama wananchi wa Watanzania, wanajeshi kuwa na maeneo makubwa. Lakini lile eneo ni kubwa sana na kwa kweli tunajua linatumika. Lakini pale zipo Kambi mbili kwa pamoja. Sasa hivi Jimbo langu limekuwa karibu sana na Mji na hata eneo ninalolizungumzia tayari limeshaanza kuwa karibu na wananchi. Namwomba Mheshimiwa Waziri akae na Mkuu wa Majeshi, wakae na Mkuu wa Kambi ya Chukwani wafikirie lile eneo la zamani ambalo halikuwemo ndani ya Kambi ya Jeshi ambalo lilikuwa linatumiwa kwa mafunzo ya Mgambo lirudishwe kwa Serikali ya Kijiji. Hili litatusaidia, hata kuna wananchi ambao wanaondolewa kwa ajili ya upanuzi wa Uwanja wa Ndege katika Jimbo la Kiembesamaki waweze kugawiwa maeneo hayo kwa sababu maeneo ya ardhi ndani ya Jimbo langu yamekuwa madogo.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie kwenye Jeshi la Kujenga Taifa (JKT). Tumesikia hapa kuwa mwaka huu 2012, karibu vijana 5,000 watachukuliwa kwenda kuanza mafunzo. Ninachoshauri, jamani, tuangalie jinsia. Kati ya hawa vijana 5,000 tuangalie *at least* 2,000 wapelekwe vijana wetu wa kike kwa sababu ukiangalia hata *enrolments* za shule, wanafunzi wanaomaliza Shule katika madarasa ya *Form Four* na *Form Six* ni wanawake. Kwa hiyo, jamani tuangalie kabisa, kuwachukua vijana wetu wa kike wengi kuhudhuria katika hayo mafunzo wawe wengi. Hii itaondoa pia huu mfumo dume

Mheshimiwa Spika, hata leo asubuhi, inasikitisha ulivyokuwa unawatambulisha hapa Makamanda wote waliosimama walikuwa ni wanaume. Kwa hiyo, inaanza kutoka mwanzo kwa kuwa hatuwaajiri watoto wa kike wengi, ndiyo inafanya wanaume wanakuwa wengi. Kwa hiyo, naomba jeshi hili liangalie na lizingatie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu ilipata bahati ya kutembelea Bukoba. Kwa kweli Kamati yetu ya Kilimo, Maji na Uvuvi, tulikwenda kwenye mgogoro wa wafugaji na wakulima. Nilichokiona kule, kinasikitisha. Kwenye mpaka wetu pale Bukoba, wenzetu katika *border* wamewapa wastaafu wa kijeshi na kwa kweli tulipofika ilidhihirisha, kwa sababu walipoiona gari na walivyoona gari ya Polisi, wenzetu kule upande wa pili wote walikuwa wamesimama kutuangalie sisi.

Kama tunavyosema, wanajeshi hawastaafu. Kwa kweli ukija upande wetu, yaani ni kutupu, hakuna kitu, na inasikitisha, kiasi ambacho nahisi *movement* za

kutoka huku na huku kwa upande wa kwetu zinakuwa rahisi. Wenzetu kule wamejipanga kwa sababu katika *border* wamewapa wastaafu kwa ajili ya kujenga na mashamba. Kwa hiyo, naishauri Serikali, kwa sababu Serikali ya Mkoa wa Kagera ilituambia kuwa ilitoa maeneo kwa ajili ya uanzishwaji wa Kambi ya JKT, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri na Mkuu wa JKT analisikia hilo, kule Bukoba tayari Kagera lipo eneo kubwa, wafanye haraka kuianzisha Kambi hiyo, itaweza kutusaidia ulinzi na usalama katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye hoja hii ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Napenda nitoe pongezi za hali ya juu kwa jeshi letu kwa kazi kubwa inayofanya kwa kutuweka katika sura ya dunia kwa heshima kubwa ambayo tunayo hususan barani Afrika, nchi nyingi ambazo zimekombolewa katika Afrika kutokana na mkono, ushujaa na umahiri wa Jeshi letu la Ulinzi, hususan nchi ambazo zipo Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote na Watanzania wote ambao mnanisikiliza na ambao mnaangalia *TV* na mtakaosoma magazeti, naomba wote kwa mshikamano tushikamane kulaani kitendo cha mauaji cha huyu kijana wa Kata ya kule Singida. Kwa hali hii, Chama cha CHADEMA, hawana cha kukataa. Mkutano ulikuwa ni wa CHADEMA, viongozi wao

walikuwepo, Mkutano ule kuna uwezekano waliweka maneno mazito ya uchochezi na kusababisha mauaji haya. Hawana cha kukwepa na kutokana na hili, naomba Serikali, suala ambalo mara nyingi wanashika mkono Bunge wanaziba mdomo.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kebwe, endelea kuzungumza.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, mara nyingi tunaambiwa kwamba suala hili lipo Polisi, suala hili liko Mahakamani, Bunge hakuna kujadili. Suala hili lina uzito wa aina yake, la sivyo amani ya nchi hii inapotea kwa masuala ya kuachia vitu vingine vya namna hii. Mimi nina hakika Serikali ina uwezo, nafahamu ni nani waliochochea, wachukuliwe hatua na tupate taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la kuanzisha JKT, mimi naomba kabisa, suala la tahadhari kuhusu janga la UKIMWI lipewe kipaumbele. Historia wakati mwingine ni fundisho zuri. Kwa sababu katika mkusanyiko wa watu wengi, wanakutana watu wengi wa tabia tofauti. Idadi ya wanajeshi ambao tulikuwa nao zamani katika majeshi ya kujenga Taifa ni dhahiri imeongezeka. Naomba suala hili kuwe na maandalizi mazuri na kufuatilia ili kusudi kukinga janga la UKIMWI kwa hawa wanaokwenda Jeshini.

Mheshimiwa Spika, hawa Wabunge vijana ambao tumeambiwa na Waziri, waelezwe kwamba vijana hawa wanaandaliwa kwenda JKT, wiki tatu hazitoshi. Labda kama wanapelekwa *study visit,* basi ijulikane,

wanakwenda kuangalia yale Makambi ya Jeshi yakoje. Lakini wiki tatu katika kupita katika utaratibu mzima wa kumfundisha huyu Mtanzania aive, awe mahiri, haitasaidia, kwa sababu lengo kubwa la JKT, ni kumfundisha mtu uzalendo, ndiyo kipengele namba moja na ndivyo tulivyofanya enzi nzetu. Lakini inasaidia kuweka mshikamano, upendo na umoja ndani ya Taifa letu. Wiki tatu hizi hazitoshi.

Mheshimiwa Spika, *experience* ambayo sehemu nyingi inaonyesha, ni kweli Jeshi letu limezidi kupanuka na Miji imepanuka, lakini kwanini twende katika mazingira yale ya zamani? Hivi hata ukipita pale Dar es Salaam, ile Kambi ya Jeshi ya Lugalo hivi kweli utasema ni Kambi? Kwanza imechoka, hata *fence* hakuna, iko katikati ya Mji, halafu kwa aibu zaidi, ukipita kwenye mtandao, kuna kitu kinaitwa *Google Earth.* Hebu jaribu ku-*click* pale kwenye *Google Earth,* ile Kambi yetu iko wazi. Hivi sisi kama nchi, hatuna uwezo wa kufanya *shielding* kwenye yale maeneo ambayo ni nyeti? Maeneo yaliyo nyeti, basi yasiwe *pictured* katika *Google Earth* na ndivyo nchi nyingine zinavyofanya. Sisi Kambi zetu zimechoka, umaskini, halafu tunaziacha uchi. Haiwezekani!

Mheshimiwa Spika, pale Wilayani kwangu Serengeti, yalifanyika makubaliano huko nyuma, katika Kata ya Kisaka, kijiji cha Molenga kwenye Kitongoji cha Komung'we. Pale makubaliano yalikuwa kwamba wanajeshi wawe wanakwenda kufanya mazoezi kwa shabaha. Lakini unyemela huu ambao unaendelea, naomba Serikali iwe *serious* juu ya hili kwamba eneo hili lichukuliwe na Jeshi chini ya Kambi ya Makoko. Hilo sisi

Wanaserengeti hatutalikubali, kwa sababu suala hili la mafunzo kwa shabaha ni mazuri, makubaliano hayo yafanyike, wananchi wapande mazao ya muda mfupi, ikifika wakati wa mazoezi ya shabaha, waende, ruksa. Wananchi watakubali, Halmashauri watakubali na sisi wote Wanaserengeti tutalikubali hilo.  Ni kuimarisha Jeshi letu, lakini kulichukua eneo lile kinyemela, hiyo mimi na wananchi wangu tutapiga mguu mpaka Ikulu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine la msingi, ile Hospitali ya Jeshi ya Lugalo, bahati nzuri pale mimi nina *interest* kwa sababu hata kusoma Shule ya Msingi mimi nilikuwa Kambini pale Lugalo. Ile hospitali ilivyokuwa miaka ile ya 1980 mpaka leo iko vilevile. Wakijitahidi wanapakapaka rangi, ikajengwa na kupandikizwa hapa. Hakuna hata sura! Mimi nawapongeza sana, suala la usafi kwenye ile hospitali chini ya Kampuni ya *Sundown,* waendelee na hata hospitali na sehemu nyingine waende wakafanye ziara ya mafunzo.

Mheshimiwa Spika, historia inasema, Rais Kennedy wa Marekani alivyopigwa risasi, Wanajeshi ndiyo walifanya kazi kubwa ya kwanza kumhudumia. Leo inakuaje hospitali yetu ndiyo ya Jeshi na ndiyo kubwa, bado tunasema hospitali kubwa ya Jeshi; mimi natamka kimsingi tu, ile siyo hospitali. Hawa wanajeshi kwa mfano, Ujerumani, masuala ya mivunjiko na dharura, wanajeshi ndiyo wamepewa *first priority*. Ile *MOI* ndiyo ingekuwa Hospitali ya Jeshi ili kusudi kwa mazingira wanayofanya na kazi zao ndivyo inavyopaswa iwe. Mbona inavyotokea machafuko, hawa wanajeshi ndiyo tunawapeleka kufanya kazi?

Hospitali iwe nzuri, iweze kuangalia kusaidia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia katika bajeti iongezwe kwa sababu ile hospitali, asilimia 60 ya watu wanaotibiwa pale ni raia. Mheshimiwa Waziri anasema ni wale wanaotoka jirani siyo kweli. Wapo watu mimi nawafahamu wanatoka Mikoani kuja kwenye hospitali ile. Kwa hiyo, ni vizuri hospitali ile iangaliwe kwa jicho la huruma na upendo ili kusudi fedha ambayo imeongezeka, Shilingi milioni 300 katika bajeti isielekezwe tu katika kulipa madeni, hizo ndizo *development projects,* wajenge hospitali nzuri ya kisasa.

Sisi siyo lazima tupate *details* zake kwenye hotuba ya Waziri, lakini kimsingi, ni lazima hospitali ifanane kimazingira.

Mheshimiwa Spika, suala la kuchukua hawa vijana wa awali 5,000 ni kiasi kidogo. Nilikuwa napiga hesabu, ni kama asilimia 12.2 kati ya hao karibu 41,000. Hivi hawa 5,000 unawapeleka baada ya hapo na wengine hawa utakuja kuwamaliza lini? Kwa hiyo, bado nashauri, hata huku ndani Wabunge wamesema vijana, hata Wabunge wazee nao waende. Mbona zamani kule tulikuwa tunaona mtu amepigapiga chenga hajakwenda JKT, lakini wanamchukua kazini huko na kitambi chake, akifika getini anaambiwa bwana hayo mafuta wiki moja yarudi kwetu; wewe ulikula mafuta yetu. Hawa Wabunge watu wazima nao waende, kwa sababu ni kwa suala la uzalendo.

Mheshimiwa Spika, suala la madeni ambayo tumeona hizi Shilingi milioni 24, hiki ni kiini macho. Shilingi milioni 24 utaishia kulipa madeni na *suppliers* wengine ambao wana-*supply,* hivi utawalipa vipi? Shilingi milioni 24 hazitatosha, la sivyo ni kuendelea kulidhalilisha Jeshi letu, mwishowe watapelekwa Mahakamani, kesi ndiyo hizo unahukumiwa halafu ukiwakatia hawa umeme au maji, hivi itakuaje? Hivi pale Ikulu patakalika kweli! Hebu jaribu ukate umeme uone!

Mheshimiwa Spika, suala la SUMA JKT liangaliwe kwa mtazamo mzuri. Haiwezekani trekta zimeingizwa nchini 1,800 miaka miwili hadi mitatu hazijafanya kazi. Kama Tanzania tunazo hekta milioni 44, asilimia 29 tu ndiyo tunalima. Eneo hili ni tupu, liko wazi, hizi trekta zisambazwe katika JKT yafanye uzalishaji. Kama tutayapeleka kwa Wakuu wa Mkoa yatakwenda kukaa kule kama maonyesho tu, hayatafanya kazi. Yaende kwenye Kambi za JKT kwa sababu, sababu ambazo Waziri ametueleza mimi binafsi hainingii kichwani. Huwezi ukasema unachukuwa wanajeshi 5,000 unasema hawa ni kwa kuanzia.

Mheshimiwa Spika, mengine nitaweka kwenye maandishi, nashukuru kwa nafasi. Naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, mipaka ya nchi yetu haipo salama sana kila upande, kama vile Kagera, Kigoma, Katavi na Rukwa, pia mgogoro wa

muda mrefu wa mpaka wa Tanzania na Malawi hata ukanda wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, ukanda wa Pwani hatuna ulinzi wa kutosha kwa sasa kwa kukosekana nyenzo za kufanyia doria. Ilikuwepo ahadi ya Serikali kununua meli ya kivita kwa ajili ya doria, jambo ambalo hadi sasa Serikali imeshindwa kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, aidha, mpaka wa Magharibi bado una matukio ya uharamia, ujambazi na uporaji wa mali za wananchi zinajitokeza, pia wageni haramu kupitia Ziwa Tanganyika na uingizaji wa silaha katika eneo hilo, kwa sababu Jeshi letu linashindwa kutekeleza majukumu yake kwa ukosefu wa vifaa. Mpaka wa Kaskazini pia ni njia kuu ya wahamiaji haramu toka Somalia na Ethiopia. Hivyo basi, ni lazima sasa Serikali kutoa nyenzo za kutosha ili Jeshi litimize wajibu wake kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, makazi, maslahi na mafao kwa askari wetu ni lazima viangaliwe kwa umakini mkubwa. Makazi ya wanajeshi bado hayafurahisi sana. Maslahi yao yaboreshwe kukabiliana na hali ngumu ya maisha na mfumo wa bei. Lakini pia mafao baada ya kustaafu ni vyema yakaangaliwa na kuboreshwa. Askari walioumia na kupata ulemavu wakiwa kazini, wanaishi maisha magumu sana, ni vema tukaangalia njia bora za kuwasaidia askari hawa.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi kati ya Jeshi letu na wananchi, ni wajibu wetu sote kusaidia kupata ufumbuzi mapema. Serikali haiwezi kukwepa na

kuendelea kutokutoa maamuzi, na kero kuendelea na hatimaye kuleta mahusiano mabaya kati ya wanajeshi na raia. Ni vyema sasa Serikali ikatenga maeneo (ardhi) ya akiba kwa matumizi ya Jeshi letu.

Mheshimiwa Spika, majengo, maghala na vifaa vya kijeshi ni lazima tufufue utamaduni wa matengenezo ya mara kwa mara, jambo ambalo sasa siyo katika utamaduni wetu kama Watanzania, wa kufanya matengenezo hata kwa nyumba tunazoishi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, SUMA JKT ijipange upya kuweza kukabiliana na changamoto zilizopo, na kama Shirika, lifanye kazi zake kwa kuzingatia ubora wa huduma, kupunguza gharama na kuanzisha miradi yenye faida na wala SUMA JKT isitumike kama chombo cha kisiasa na kutekeleza maelekezo yasiyo na tija kwa SUMA JKT.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kuhimiza kuwepo na nidhamu kwa Askari na nidhamu ya matumizi mazuri ya fedha katika jeshi letu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba kulipongeza Jeshi la Ulinzi kwa kuwa na nidhamu nzuri katika Taifa letu. Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha bajeti ambayo inakidhi baadhi ya mambo muhimu katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara iweze kuimarisha ulinzi katika mipaka iliyoko katika maeneo hasa yaliyozungukwa na maji katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na Bahari ya Hindi kwa ujumla. Maeneo haya yamekuwa ni chanzo cha uhalifu wa kutoka kwa raia wa nje kuja nchini kufanya uhalifu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu Jeshi letu likaandaa mpango madhubuti wa kununua vifaa vya kisasa hasa vile ambavyo viko mipakani kwa ajili ya kukabiliana na wavamizi wanaoingia mipakani.

Mheshimiwa Spika, bila kuwa na vitendea kazi, hakuna tutakachokuwa tumeisaidia Wizara hii. Naiomba Wizara isaidie kikosi kidogo cha Jeshi kilichopo Mkoa wa Katavi eneo la Ikola kipewe kipaumbele cha vitendea kazi kama boti za kisasa kwa ajili ya kukabiliana na maharamia wanaoingia Ziwa Tanganyika na kuwanyang'anya wavuvi wa Tanzania zana za uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Jeshi linafanya kazi katika mazingira magumu na maeneo wanayoishi wanajeshi walioko hapo Iyola siyo salama, kwani wanajeshi hawana nyumba za kuishi, gari wanalotumia ni kuukuu sana kiasi kwamba mtumishi akipelekwa katika kituo hicho ni kama adhabu anayopewa. Naiomba Wizara iangalie suala hili na kufanya marekebisho ya haraka kama inavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine linalopaswa kuangaliwa ni ugomvi unaotokea kwa baadhi ya

Askari wa Jeshi na wananchi wa vijiji vinavyozunguka Kambi ndogo ya Ikola. Naiomba Serikali iimarishe nidhamu kwa Kambi hii ili migogoro kati ya raia na wanajeshi itoweke. Nidhamu ikiimarishwa, migogoro hiyo haitakuwepo.

Mheshimiwa Spika, pamoja a maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri, hasa kwa kurejesha Jeshi la Kujenga Taifa na kuwahusisha Wabunge Vijana, ninaunga mkono hoja hii.

**MHE. KAPT (MST) GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa natanguliza kusema naunga mkono hoja hii. Aidha, napenda kupongeza kazi nzuri inayofanywa na JWTZ na JKT katika kulinda Taifa letu na kuzalisha mali. Jeshi letu wakati wote limekuwa karibu sana na wananchi na limekuwa likitoa huduma kwa raia hasa matibabu kwa raia katika hospitali zake na vikosi vya Jeshi. Aidha, nawapongeza sana Madaktari wa Watumishi wa Sekta ya Afya Jeshini kwa kuwatumikia wananchi kwa bidii wakati wote. Nalipongeza Jeshi kwa kusaidiana na Serikali wakati wote wa maafa katika kuwahudumia waathirika.

Mheshimiwa Spika, kwa siku za nyuma, Tanzania iliwahi kuwika kimataifa kutokana na wanamichezo wanajeshi. Hii ni kwa sababu wanajeshi wetu wana afya nzuri, wanafanya mazoezi na wana lishe ya kutosha. Mashindano ya majeshi katika ngazi za vikosi, Brigedia na ya nchi nzima yaliweza kutupatia wanamichezo bora. Katika siku za karibuni hatujapata wanamichezo waliong'ara kimataifa. Nashauri mashindano ya majeshi yarejeshwe kama zamani

kama vile riadha, mpira wa wanawake, ngumi, netiboli na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Wananchi linatoa huduma nzuri katika hospitali zake hasa za Kanda. Kanda ya Kusini haina hospitali ya kanda kama ilivyo kwa kanda za Lugalo, Nyumbu (Kibaha), Mwanza na Tabora. Napenda kushauri na kuomba kuwa JWTZ sasa ipange na kutekeleza kuanzisha hospitali ya kanda kwa kanda ya Kusini ili wananchi wa kanda hiyo wanufaike, maana hata hospitali ya rufaa hawana.

Mheshimiwa Spika, hali ya ulinzi kando ya Ziwa Tanganyika kwa muda mrefu imekumbwa na uvamizi wa wavuvi wetu na majambazi toka nchi za jirani ambao huwanyang'anya nyavu na zana za uvuvi na kukimbilia kwao. Napongeza mpango wa Serikali kwa kuipatia Kamanda ya *Navy* boti na meli ziendazo kwa kasi ili kuimarisha ulinzi wa eneo hili. Serikali iharakishe mpango huu ili tatizo hili liishe mara moja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, Jeshi la Wananchi la Tanzania limejenga hospitali mbalimbali za kijeshi katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Hospitali hizi zinatoa huduma kwa wanajeshi wenyewe na kwa wananchi kwa ujumla. Wanajitahidi sana kutoa huduma iliyo nzuri licha kuwa hospitali hizo zinakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo vifaa tiba na madaktari.

Mheshimiwa Spika, nionavyo mimi, kwa Pemba hospitali zenye kulingana na hadhi ya Hospitali ya Bububu au Lugalo Haiko. Je, lini Jeshi la Wananchi la Tanzania litajenga hospitali hiyo Kisiwani Pemba ili wanajeshi wetu pamoja na wananchi waweze kupata huduma ya tiba kwenye hospitali hiyo hapo itakapojengwa?

Mheshimiwa Spika, nchi yetu mpaka sasa haijajitegemea kabisa katika suala zima la mbegu. Hii siyo hali nzuri hata kidogo. Kwanini angalau jukumu hili la kupata mbegu zinazotosheleza hapa nchini halikabidhiwi JKT ikawa ni mradi maalum? Ninavyoamini mimi ni kuwa, mradi huu utakuwa na pato kubwa la Jeshi letu, kwa sababu ya mtawanyiko wa maeneo mbalimbali kwa jeshi letu. Hali hiyo inaweza kuliwezesha Jeshi kuzalisha mbegu za aina mbalimbali kutoka sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Bahari ya Hindi hivi sasa inakabiliwa na maharamia na pia Serikali imeomba iongezwe eneo la bahari zaidi ya kilomita 200 na sasa ziwe kilomita 350. Iwapo maharamia na ongezeko la eneo la bahari (kama ombi letu litakubaliwa na Umoja wa Mataifa) suala la ulinzi wa bahari utaongezeka, kwa hiyo, ipo haja kwa Serikali kuwapatia vifaa vyote vinavyostahili kwa kikosi chetu cha wanamaji ili kikosi hicho kiweze kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa la mipaka baina ya Kambi za Kijeshi na maeneo wanayoishi wananchi. Matokeo yake, wananchi wanapata usumbufu mkubwa katika matumizi ya ardhi. Hali hii

huleta msuguano na malalamiko makubwa hasa kwa wananchi na husababisha kutokuwa na uhusiano mzuri baina ya Jeshi, na wananchi wakati haitakiwi iwe hivyo. Kwa hiyo basi, naomba Serikali iweke mkakati maalum wa upimaji wa maeneo ya kijeshi ili kila upande ujue haki inayostahiki.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, Wizara na Serikali kwa ujumla wanawapongeza kwa kurejesha vijana na wananchi kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa. Ni vyema sasa Wizara na JWTZ kuangalia na kuepuka mapungufu yaliyojitokeza wakati palipokuwepo shughuli za kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, pia nashauri uzalishaji katika mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa uzingatie sana kuelimisha vijana katika uzalishaji na ujasiriamali. Ni muhimu vijana wanapomaliza mafunzo wathamini kazi za mikono yao, na ujasiriamali ili waondokane na mawazo ya kazi za ukarani *(white color jobs).*

Mheshimiwa Spika, huduma kwa Askari wetu ni muhimu sana. Serikali ijitahidi kuendelea na juhudi za kujenga nyumba za Askari na kadhalika. Ni muhimu pia kuzingatia motisha kwa Askari ili wafanye kazi zao kwa ufanisi. Mafunzo pia ni muhimu sana kwa Askari. Ni vyema kulenga katika azma ya nchi kuwa na Jeshi

dogo la kisasa, shupavu na lenye weledi na kupigiwa mfano kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, ulinzi katika mipaka yetu ni muhimu uimarishwe hasa mpaka ya Magharibi ambayo hakuna utulivu wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nalipongeza Jeshi kwa utulivu na utunzaji wa amani yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninayapongeza majeshi haya kwa kazi nzuri ya kulinda nchi yetu na kutufanya tuheshimike Afrika na duniani kote. Jitihada za kudumisha amani nchini mwetu na nchi majirani. Nchi yetu ina amani.

Mheshimiwa Spika, sasa ni vyema majeshi yetu yakawa ni chachu ya kuanzisha na kuendeleza mapinduzi ya viwanda kwa kubuni na kutengeneza vifaa ambavyo vinatumia fedha za kigeni nyingi kwa vile vinaagizwa kutoka nje. Kwa mfano, mradi wa kujenga magari wa Nyumbu ungepewa msukumo upya ili magari, pikipiki, baiskeli na kadhalika vikawa vinaundwa hapo kwa soko la Tanzania na majirani zake.

Mheshimiwa Spika, ili kudumisha nidhamu kazini na uzalendo wa hali ya juu, napongeza jitihadi za Serikali kurejesha wajibu wa vijana kutumika kwenye Jeshi la Kujenga Taifa. Nashauri kuwa tusiishie hapo, bali pia wanasiasa wote ambao hawapitia JKT walazimishwe kufanya hivyo kwa mujibu wa sheria na sifa moja ya kugombea Ubunge na Udiwani iwe ni kutumikia JKT. Nashauri tena kuwe na utaratibu wa kuwawezesha wanasiasa wote waliokwisha tumikia JKT warejee tena huko kwa muda wa mwezi mmoja kila baada ya miaka mitatu. Hii ni kwa kuimarisha uzalendo na afya zao.

Mheshimiwa Spika, dhana na azma nzima ya Kilimo Kwanza ingetiliwa mkazo kuanzia jeshini, siyo tu kwa kuunda vitendea kazi kama matrekta, bali pia kwa kuwa na mashamba makubwa ya mfano katika kila Mkoa.

Mheshimiwa Spika, nashauri Jeshi letu liimarishwe kuweza kutoa huduma za jamii muhimu ili yatokeapo matatizo, basi Jeshi litumike kuokoa. Hali iwe hivyo kwa huduma za afya ambapo ni pendekezo langu kuwa, pamoja na wataalamu wa kutosha wa afya katika ngazi zote, pia Serikali ijenge Hospitali za Jeshi katika kila Mkoa na hospitali hizo ziwe na uwezo wa kutoa huduma angalau katika kiwango cha Hospitali za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, pia kuwe na akiba ya watalaamu kama hao katika nyanja nyingine za huduma kama waongozaji wa ndege *(Air Traffic controlers)* na nyingine Serikali itakazobaini.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko hasa Mikoani katika mchakato mzima wa kuwapata vijana wanaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa. Baadhi ya Maeneo yamekuwa yakipendelea watoto wa viongozi wa Jeshi hilo hata kama hawana sifa, wanapata nafasi na kuwaacha watoto au vijana wenye sifa ambao wamekosa watu wa kuwapigia debe.

Mheshimiwa Spika, ningependa kujua utaratibu gani unaotumika katika kuwachagua vijana wanaotaka kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa ili waitumikie nchi yao.

Mheshimiwa Spika, pia kumekuwa na malalamiko ya uchakavu wa miundombinu katika Kambi mbalimbali za Jeshi na kuwafanya waishi katika mazingira magumu, ikiwemo Kambi ya Jeshi Makongo, kwamba baadhi ya nyumba zimechakaa ikiwemo na vyoo kutofanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha wanafanya utaratibu kwenye nyumba katika Kambi za Jeshi ili wanajeshi hawa ambao ni muhimu katika Ulinzi wa Taifa letu wanaishi katika nyumba bora?

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Je, JKT itarudi lini? Nini mkakati wa Serikali? Kwani vijana wengi hawana kazi, JKT

itarudisha ari ya kazi/mashamba, uzalishaji/ufundi na kadhalika. Nini mkakati wa Serikali juu ya JKT?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga hoja kwa asilimia mia moja. Kwanza, nawapongeza wanajeshi wetu kwa juhudi zake za kusimamia shughuli za ulinzi wa wananchi na mali zao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zinazofanywa na jeshi letu, kuna changamoto zinazojitokeza ambazo zinahitaji kushugulikiwa haraka iwezekanavyo ili kuzuia madhara ambayo yanaweza kujitokeza. Kumekuwa na mwingiliano mkubwa wa wananchi na Jeshi. Kwa hiyo, migogoro ya ardhi ni mojawapo ya changamoto, ardhi ya jeshi iwe na alama maalumu, ipimwe na wavamizi waondolewe mara moja.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni *store* za silaha zikaguliwe mara moja. Silaha ambazo zimekwisha muda wake ziangamizwe mapema kabla hazijalipuka kama kule Gongo la Mboto na kwingineko.

Mheshimiwa Spika, nashauri mafunzo ya Jeshi kwa mujibu wa sheria yazingatie nidhamu kwa vijana ili waweze kutambua uzalendo na kuikomboa nchi yetu katika majanga ya madawa ya kulevya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama nchini, pamoja na wapiganaji wote nchini kwa kuendelea kufanya kazi kwa moyo thabiti, kuhakikisha wanasimamia amani na uhuru wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri Jeshi letu limekuwa likifanya kazi ya kusifika tangu Uhuru. Hata hivyo, kutokana na mabadiliko ya dunia ya sasa, na hali ya kiusalama duniani, ikiwa ni pamoja na tishio za kiusalama zinazotokana na vikundi vidogo vidogo vya kigaidi, au ujangili wa kimataifa, naomba kutoa mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iongeze *ceiling* ya Jeshi la Ulinzi na JKT. Vile vile Serikali iweke katika mpango wa muda, wa kati, na muda mrefu kulifanga Jeshi liwe la kisasa kwa vifaa *(military equipment)* ikiwa ni pamoja na ndege za kivita, *helkopter gunships* nazo za kivita za ardhini (vifaru) ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo wa *urban warfares* na kupambana na ugaidi.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliwezesha Jeshi kimafunzo *(military training and drills, military joint express and military intelligence gathering capabilities and counter interligence services).*

Mheshimiwa Spika, Jeshi liwe tayari (kiuwezo) kuweza kupigana vita *(convantinal warfare)* na nchi mbili zinazotuzunguka kwa pamoja na wakati moja. Hii ni tahadhari tu kuhakikisha hakuna nchi itakayothubutu

ama kutumiwa kuichokoza Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuongeza utayari *wa cyber warfares*, na kuelimisha *elite unit* kuwa tayari kulinda *vital installations* za nchi dhidi ya ujasusi na vita vya kimtandao.

Mheshimiwa Spika, jeshi lisaidiwe kuongeza ulinzi wa nchi majini na kwenye mipaka ya kimataifa *(international waters)* dhidi ya uharamia, *(pirates),* na kulinda nchi dhidi ya uhujumu uchumi unaofanywa na nchi, meli za uvuvi toka nchi nyingi zinazofanya uvuvi haramu ndani ya mipaka yetu. Inakadiriwa kuwa nchi inapoteza USD millioni 500 kila mwaka dhidi ya uvuvi haramu.

Mheshimiwa Spika, napendekeza jeshi liunde *(team)* ya washauri (niko tayari kuwa moja wa hao washauri) wa kuangalia ni jinsi gani Jeshi letu linaweza kujitegemea kiuchumi mithili ya Jeshi la China, na hivyo kuliwezesha kushiriki katika kuongeza kazi ya kukua kwa uchumi wa nchi kupitia Makampuni mahsusi ya Jeshi yatakayofanya kazi nchini, kiushindani, na katika baadhi ya mazingira maalum, kiupendeleo, pale ambapo suala husika lina maslahi ya zaidi kwa nchi. Kamati hii iwe na Maafisa Waandamizi Jeshini, Wabunge wenye uelewa, *passion*, na ujuzi juu ya mambo haya, na watalaam toka nje ya Serikali. Niko tayari kuwa Mjumbe.

Mheshimiwa Spika, jeshi liangalie kwa upya *strategic defence review, international cooperation on*

*defence,* na *regional secutry dynamics*, yote hayo yasaidie *preparedness* ya majeshi yetu kwa ulinzi thabiti wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja mia kwa mia na hongera kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa huduma nzuri inayofanywa na Jeshi katika maeneo mbalimbali na maafa kadhaa katika afya, mafuriko, na kadhalika. Pia nina haya ya kusema:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Lindi tuliahidiwa *Speed Boat* kwa ajili ya ulinzi katika Bahari ya Hindi ukanda wa Lindi na Mtwara. Je, mbona sasa mpaka leo bado hatujapewa tangu mwaka 1998 baada ya *operation* ya uvuvi haramu wa kutumia mabomu uliofanywa na Jeshi la Wananchi kwa jina na *PONO* ambapo zana mbalimbali za uvuvi haramu zilikamatwa ikiwemo tani 151 za mabomu watu 300 na vitu kadhaa. Inasemekana uvuvi huo sasa unarudia tena kwa sababu hakuna ulinzi tena. Tunaomba *Speed Boat* Lindi na Mtwara tupatiwe haraka.

Mheshimiwa Spika, ulinzi wa wananchi wenyewe ni mzuri pia. Namshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuanzisha ulinzi wa Kikosi Jamii kwa lengo la kusimamia usalama wa raia na mali zao, kwa tangazo la Serikali Na. 1 hapo Januari, 2006. Polisi Jamii inafanya kazi nzuri

sana. Hongera sana. Inabidi pia na jirani zetu katika nchi nyingine kama Kenya, Visiwa vya Shelisheli, Komoro na Msumbiji, pia Burundi, Kongo, Uganda, Malawi na Zambia mkae nao pamoja ili nao waweze kufundishwa na kushauriwa suala zima la mpango wa Polisi Jamii, kwani baadhi ya nchi hizo zina uchokozi wa makusudi kabisa kama nchi ya Malawi, Rwanda na Congo. Hawa wakijua na kutekeleza suala la Polisi Jamii, Ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao utaimarika mpakani.

Mheshimiwa Spika, mwisho, tunaiomba Serikali ifanye jitihada za makusudi ya kufuatilia ajira na mafunzo ya Askari JKT. Zinazopelekwa Mikoani kwamba kila Mkoa wanapata, kwani nafasi hizo za mafunzo hupewa kwa upendeleo na siyo kwa raia wa Mkoa ule ambao nafasi hizo zimepelekwa angalau basi 75% ya nafasi zile ziwe nafasi za raia wa Mkoa ule.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, baada ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri na kupongeza hotuba yake inayotoa mwanga katika Wizara hii na askari wa jeshi wa Tanzania, napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu majengo ya Ofisi kwa Jeshi katika Kikosi cha 151 KJ Wawi Pemba, ni dhahiri

kwamba majengo ya ofisi katika Kambi hii hayaridhishi, hasa tukitilia maanani kuwa eneo hilo lipo barabarani kwa barabara itokayo Chake Chake – Vitongoji; wananchi wanaopita katika barabara hiyo pamoja na wageni wanapopita katika eneo hilo wanajionea ofisi na majengo ambayo yamechakaa sana. Naishauri Serikali izifanyie ukarabati ofisi na majengo hayo ili isitoe picha mbaya kwa wanachi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Zanzibar pamoja na Serikali ya Marekani katika kisaidia Hospitali ya Jeshi, katika Kambi ya Jeshi Wawi, kwa kuifanyia ukarabati mkubwa wa majengo hospitali hiyo na kutoa picha nzuri kwa wapita njia na watumiaji wa hospitali hiyo. Hospitali hii inatoa huduma kwa wanajeshi na pia kwa wananchi wa Pemba kwa ujumla kitu ambacho kinaifanya hospitali hiyo kuhitaji madaktari wa kutosha pamoja na dawa za kutosha.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iipatie hospitali ya Jeshi 14 JK madaktari wa kutosha wa kada mbalimbali na dawa za kutosha ili iweze kuhudumia vyema zaidi wagonjwa wanaopata huduma katika hospitali hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nyumba za askari, pamoja na kuwajengea askari wake nyumba za kisasa katika maeneo mbalimbali, lakini bado askari wengi wanaishi uraiani. Naiomba Serikali iendelee kuwajengea nyumba za kuishi Askari wa Kikosi cha 14 JK na 151 KJ Wawi Pemba.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni Taasisi muhimu katika kudumisha amani na usalama wa Taifa, na kwa kulinda uhuru na maslahi ya Taifa. Hivyo, naomba kutoa mchango ufuatao kuhusu mapitio ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2011/2012 na Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, mosi, kuhusu hali ya usalama wa mpaka katika mwaka 2011/2012, kwa upande wa mipaka katika bahari ya Hindi Aya ya 11, ni muhimu hatua za kuimarisha uwezo wa Jeshi la Wanamaji zikachukuliwa kuwa kipaumbele kwa kiwango cha fedha kuongezwa kwa mwaka 2012/2013. Pamoja na vitendo vya uharamia, hatua hizo ni muhimu kadri Taifa linavyoongeza mikataba ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia katika bahari. Aidha, masuala ya ulinzi na usalama yazingatiwe katika majadiliano ya mikataba husika. Hivyo, Jeshi letu lijengewe uwezo wa kitaalamu katika masuala ya mafuta na gesi ili kuweza kufanya kazi vizuri na Taasisi nyingine za Serikali katika masuala ya ulinzi na usalama katika sekta husika.

Mheshimiwa Spika, ushushushu wa kijeshi *(military intelligence)* uhusishe pia masuala ya kiuchumi na rasilimali zenye taathira katika usalama. Kwa mipaka ya kaskazini (aya ya 12), ni muhimu Wizara ikatoa maelezo kuhusu kushamiri kwa biashara haramu ya usafirishaji watu *(human trafficking)* katika mpaka husika. Pia jeshi lishirikiane na vyombo vingine vya dola kudhibiti utoroshwaji wa vyakula toka Hifadhi ya Taifa

vinavyosambazwa kwa ajili ya kudhibiti mfumuko wa bei ya chakula, lakini vimekuwa vikitoroshwa nje ya nchi huku wananchi wakiwemo wa Jimbo la Ubungo wakinunua nafaka kwa bei ya juu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpaka wa Magharibi (aya ya 13) pamoja na Kigoma, nashauri Serikali iweke mkazo katika hali tete ya usalama iliyopo katika Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu ushirikiano wa kiulinzi na kijeshi na nchi nyingine duniani, naomba Wizara itoe majibu kuhusu hatua zilizochukua juu ya malalamiko ya wanajeshi wanaokwenda kushiriki operasheni mbalimbali zinazoongozwa na Umoja wa Mataifa katika nchi zenye migogoro kuwa, malipo yao huchelewa na wakati mwingine hutolewa pungufu.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuhusu Shirika la Nyumbu (aya 30), kazi za utafiti wa utambuzi katika teknolojia za magari na mitambo, naomba Shirika lijihusishe pia na masuala ya magari na mitambo kutumia gesi asili ili kuchangia katika kuliondoa Taifa juu ya matumizi ya gesi katika magari, mitambo ya viwandani na katika vifaa vya majumbani. Hatua hii itawezesha nchi kupunguza utegemezi wa mafuta kutoka nje, hali inayochangia katika ongezeko la gharama za maisha kwa wananchi na walishaji katika nchi.

Mheshimiwa Spika, nne, nashukuru kwamba ujenzi wa Chuo cha Ulinzi wa Taifa umekamilika, pamoja na kuwa Wabunge vijana tutahudhuria mafunzo maalum ya Jeshi la Kujenga Taifa (naomba jina langu liwekwe

kwenye orodha kwa mujibu wa mwito wa Waziri kwenye aya ya 55), nashauri Wabunge tupatiwe pia mafunzo ya ulinzi wa uongozi. Hii ni kwa kuzingatia kuwa kwa mujibu wa aya ya 32, mafunzo katika Chuo hicho yatatolewa kwa Maafisa wa juu wa Jeshi, na Serikali.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, napenda sana kutoa shukurani za dhati kwako na kwa Mwenyezi Mungu kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kutoa pongezi kwa Waziri Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha kwa kupewa dhamana ya kuongoza Wizara hii muhimu sana ya ulinzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mengi sana kutoka kwa wananchi wengi kuhusu migogoro ya ardhi kati ya Jeshi na wananchi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutambua kuwa katika dunia ya leo, teknolojia inayokua kwa haraka na kiasi kikubwa, kwa kasi ya ajabu ni teknolojia ya kijeshi.

Mheshimiwa Spika, pia ikumbukwe kuwa, mbali ya ofisi za majengo, Jeshi linahitaji eneo (ardhi) kubwa sana mbali na wananchi na yenye misitu minene na mikubwa.

Mheshimiwa Spika, kama tutaendelea na kukuza migogoro ya ardhi baina ya Jeshi letu na raia, basi kama tutasikilizwa kwa ajili ya azma zetu za kisiasa, hapo mbele tutakuwa na Jeshi lenye uwezo mdogo

sana kwa kulinyima Jeshi letu ardhi ya kufanyia mazoezi na kuweka Kambi za kijeshi ambazo zipo mbali na wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa sisi wanasiasa, bila kupata maelezo ya kina ya mahitaji ya ardhi kwa ajili ya ujenzi na kuweza kuelekeza na kuwafundisha wananchi wetu kuhusu hitaji kubwa la ardhi kwa majeshi yetu, basi huko mbele kuna shida kubwa.

Mheshimiwa Spika, napenda sana pia kuchukua fursa hii kuiomba Wizara kuwataka wakufunzi wa Jeshi watoe maelezo kwa Waheshimiwa Wabunge, ni jinsi gani hitaji la ardhi ni kubwa ili tupunguze kazi ya uvamizi wa maeneo ya Jeshi na kuepuka maafa kama ilivyotokea Mbagala na Gongolamboto.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe pia ni katika kipindi hiki ambacho majirani zetu wapo katika vita na migogoro ya wenyewe kwa wenyewe na inaweza kupelekea waasi wa nchi jirani, wanaweza kukimbilia kwetu na kusababisha uvunjifu wa amani na uporaji wa wazi toka nchi jirani. Kwa hiyo, tunahitaji sana kuwa na jeshi ambalo lipo tayari popote nchini na kwa muda wote tayari kukabili lolote.

Mheshimiwa Spika, wapo wastaafu wa jeshi wengi ambao ni mojawapo ya Watanzania wanaoishi kwa shida sana mbali na utumishi wao uliotukuka, tukumbuke kuwa hawa ni akiba kwa mbinu za utalaamu hasa pale wanapohitajika. Hatuoni sababu za kutosha kuacha wastaafu hawa kwa namna moja au nyingine ambapo Askari wastaafu

wanacheleweshwa kupata malipo au wanalipwa kidogo.

Mheshimiwa Spika, pia wapo Askari walipigana vita mbalimbali za ukombozi na wapo waliopigana Vita vya Uganda na kupoteza viungo vya mwili, lakini bado maisha yao ni duni sana na wapo wengine ambao bado wanadai wanachoamini kuwa ni fidia.

Mheshimiwa Spika, napenda sana kutoa pongezi kwa Waziri mpya wa Wizara hii. Hii ni Wizara yenye changamoto nyingi sana. Ushauri wangu wa mwisho ni kuwa sasa, tusiwape wageni ardhi ambapo hatujui wageni hao watakuwa na nia gani na nchi yetu huko mbele.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata wasaa huu wa kuchangia.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGINE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaji wengine wa Wizara hii kwa juhudi za kuratibu na kusimamia masuala ya ulinzi na usalama hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii, namwomba Mheshimiwa Waziri anijibu hoja zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, suala la migogoro ya ardhi baina ya Kambi za Jeshi na wananchi wanaozunguka maeneo hayo ya Kambi ni ya kutisha. Je, Waziri analifahamu hilo? Je, anajiandaje kukabiliana nalo?

Je, Waziri anafahamu juu ya mgogoro wa ardhi kati ya wananchi wa Tarime wa Ronsoti na wanajeshi wa Kambi ya Nyandoto? Je, Mheshimiwa Waziri amejiandaa vipi kutatua tatizo hili? Je, vipi kuhusu mipaka ya nchi yetu? Je, mipaka yetu ipo salama?

Mheshimiwa Spika, kuhusu JKT, naipongeza Serikali na kupitia Wizara hii kurejesha mafunzo ya JKT hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuuliza maswali yafuatayo: Je, ni lini mafunzo hayo yataanza? Je, Waheshimiwa Wabunge Vijana ambao hatukubahatika kupitia mafunzo hayo tutayapataje? Je, mafunzo hayo yatasaidiaje Serikali hasa katika Sekta ya uzalishaji mali?

Mheshimiwa Spika, baadhi ya makazi ya Maafisa wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) siyo ya kuridhisha. Je, Serikali kupitia Wizara hii ina mpango gani wa kuboresha makazi ya wanajeshi wetu nchi nzima?

Mheshimiwa Spika, kuna tetesi kuwa baadhi ya wanajeshi wetu wastaafu hawalipwi posho na mafao yao kama inavyostahili. Je, Serikali ina sera gani kuhusu hilo?

Mheshimiwa Spika, fidia kwa wanajeshi wetu waliopigana katika Vita ya Pili vya Dunia, Vita vya Uganda na kadhalika. Swali: Mheshimiwa Waziri nataka kufahamu kama kuna fidia toka nchi ya Uingereza kwa Askari Jeshi wetu walipigna Vita ya Pili

vya Dunia. Pia nataka kujua kama Serikali ya Uganda inatoa fidia kwa wanajeshi wetu walioshiriki ukombozi wa kumwondoa Nduli Idd Amin Dada?

Mheshimiwa Spika, *invoice* ya malipo kwa nchi tulizozisaidia kufanikisha ukombozi: Uganda, Msumbiji, Namibia, Angola, Zimbabwe na Afrika Kusini. Je, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa halioni kuwa kuna umuhimu wa kudai malipo halali kwa raslimali tulizopoteza kwa kupigania ukombozi katika nchi hizo?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu wa Majeshi na vyombo vyote vilivyo chini ya Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya kulinda na kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi nilizowapa, nawashauri waongeze mbinu na mikakati zaidi ili kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ugunduzi wa gesi nchini unaoendelea kufanywa na wawekezaji umeleta changamoto kubwa kuhusu uhakika wa usalama wa nchi yetu hasa kwa kuzingatia kwamba kampuni nyingi zinazofanya shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi zimekuwa zikitumia ulinzi unaotolewa na Makampuni ya nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba, pamoja na kuheshimu umuhimu wa kushirikiana na Makampuni ya nje ya nchi yetu, Serikali ijipange vizuri kuhakikisha kwamba jeshi letu ndiyo linalowezeshwa kuongoza ulinzi na usalama wa mali, watu na raslimali za nchi yetu. Wawekezaji walazimishwe kushirikiana na jeshi letu na washiriki kuliwezesha jeshi letu ili lichukue *lead role* kuhusu ulinzi na usalama kwenye nchi kavu na baharini pia.

Mheshimiwa Spika, aidha, naipongeza Serikali kukamilisha mchakato wa kuanza tena mafunzo ya JKT.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza kwa dhati Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Wasaidizi wake kwa kuwasilisha bajeti yenye matumaini makubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, napenda kutoa ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni kubwa sana na inazungukwa na nchi nane, hivyo kuwa na mipaka mikubwa na sehemu nyingine kuwepo kwa ugumu kwa ulinzi wa mipaka hiyo. Watu wamekuwa wakiingia nchini, wengine wakiwa wamebeba silaha nzito bila udhibiti wowote. Baadhi ya silaha hizi zimetumika katika vitendo vya uhalifu katika maeneo mengi ya nchi hii.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu katika hili ni kwamba Wizara ikishirikiana na Wizara nyingine za ulinzi na usalama, ziweke mikakati ya pamoja ili kulinda mipaka yetu kwa uhakika zaidi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa azma yake ya kuanzisha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), mafunzo ambayo pamoja na mambo mengine yataleta umoja wa kitaifa. Hata hivyo, kuchukua baadhi tu ya wahitumu wa Kidato cha Sita kujiunga na JKT hakutaleta tija inayohitajika. Natambua hili linatokana na ufinyu wa bajeti. Pamoja na ukweli huo, nashauri Serikali itafute kwa namna yoyote ile ili wahitimu wote wa Kidato cha Sita wajiunge na JKT kwa wakati mmoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa - Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Ndugu yetu Devisa Mwamunyange pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri ambayo imeandaliwa kwa umakini wa juu ikiwa imeainishwa vipaumbele kwa lengo la kuboresha Jeshi letu la Ulinzi pamoja na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, nina matumaini makubwa kuwa utendaji utaongeza nguvu ya majeshi yetu pamoja na kudumisha amani katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kuwa kazi za Wanajeshi wetu ni ngumu sana na za hatari kwa

maisha yao ukizingatia kufanya kazi zao za kila siku na za dharura kwa kulala huku wakisikiliza filimbi, ving'ora na kadhalika. Kila dharura inapotokea huwa tayari wakati wowote bila kujali kazi hizo zina hatari kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Spika, Naishauri Serikali kuhakikisha inawapa Askari hawa mishahara inayokidhi haja ya mahitaji yao ya kila siku na baadaye. Vilevile kuwapa marupurupu yote wanayostahili ili kuwatia moyo wa kufanya kazi kwa moyo mmoja pamoja na kuwaondolea vishawishi vya kuvunja sheria za nchi ikiwepo wizi au kudhulumu wananchi. Ninahitaji maelekezo ya Serikali ili Wanajeshi wasikie.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la Wanajeshi kukosa nyumba za kuishi, hivyo kulazimika kupanga nyumba Uraiani, mfano wanajeshi wa Kambi ya Ihumwa Dodoma wanaishi Dodoma Mjini au Ihumwa Kijijini. Hii ni hatari sana kwa wanajeshi hawa kutunza siri za Jeshi na hata kupata ushawishi wa kufanya vitendo vya uhalifu au kuhusishwa kwenye uhalifu hata kama hawakushiriki, kwani wanakula na kunywa na raia wengine.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kutenga fedha za kujenga nyumba nyingi za kuishi Wanajeshi wetu kama ambavyo imeanza kujenga. Nasubiri maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa siyo rahisi Wanajeshi wetu kujenga nyumba zao za kuishi na kusababisha Askari wengi wanapostaafu kukosa makazi, naiomba

Serikali kuweka utaratibu wa kuwakopesha nyumba za kuishi na kulipa kupitia mishahara yao ili iwasaidie kuondokana na tatizo la kukosa mahali pa kuishi pale wanapofikia umri wa kustaafu. Ikumbukwe kwamba wanajeshi hawana muda wa ziada wa kufanya shughuli za kifamilia.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa Uongozi mzuri wa Jeshi la Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa usimaizi na utoaji taaluma mzuri wa Shule za Sekondari za Jeshi. Hata hivyo, nashauri Serikali kuiwezesha Wizara hii fedha ili iweze kuongeza Shule nyingine za Sekondari kwenye Kambi za Jeshi ili shule hizo ziweze kutoa nafasi kwa raia wa kawaida kusoma katika Shule hizo ambazo kiwango cha taaluma kimekuwa juu sana pamoja na watoto wa Wanajeshi wengi kupata nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa mpango wake mzuri wa kupeleka vijana wengi kupata mafunzo ya Jeshi kila mara kwa Wilaya zote na Mikoa yote:

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali kuongeza idadi ya vijana wa kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa kuondoa wimbi la vijana wazururaji, watumiaji wa madawa ya kulevya pamoja na kujihusisha na vitendo vya ujambazi mijini na vijijini.  Vilevile naishauri Serikali kuajiri vijana wote pale wanapomaliza mafunzo kwa kushirikiana na Wizara nyingine ili kuondoa tatizo la kuwarudisha vijijini, kwani kuwarudisha huko ni kufanya watumie vibaya taaluma waliyoipata kwa kuanza

ujambazi, kwani watakuwa wataalam wa kutumia silaha. Nitashukuru kupata maelezo ya Waziri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuiomba Serikali kupunguza masharti ya kujiunga na mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa, mfano kijana mfupi kuachwa, anachukuliwa mrefu tu.

Mheshimiwa Spika, kumbukumbu zangu zinanipa kuwa Mwanajeshi anaruhusiwa kuoa au kuolewa baada ya kutumikia Jeshi hilo kwa muda wa miaka sita. Naiomba Serikali kama ndivyo, muda huu upunguzwe kuepusha maambukizi ya Ukimwi pamoja na wanawake kuwaepushia ugumu wa kujifungua wanapochelewa kuzaa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kumalizia mchango wangu kwa kuunga mkono hoja nikitegemea kuwa mchango wangu utafanyiwa kazi na Waziri atatoa ufafanuzi wakati wa majumuisho.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Taifa lolote duniani hutegemea sana amani katika Taifa lake, chombo muhimu katika kulinda amani ya nchi ni Jeshi. Kwa hiyo jukumu kubwa la ulinzi wa nchi hutegemea Jeshi lake. Jeshi hulinda mipaka ya nchi yake.

Mheshimiwa Spika, ili jeshi lifanye kazi yake vizuri, linahitaji kupewa vifaa sahihi ikiwa ni pamoja na ardhi, wapewe maeneo ambayo ni makubwa bila kubughudhiwa na raia kwa sababu mafunzo ya Kijeshi

yanahitaji kufanya mazoezi kwa vitendo ambavyo yanahitaji ardhi ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, suala la elimu kwa vijana wanapokuwa Jeshini ni muhimu kupata *course* ya Kijeshi kila mwaka ili kuwajenga vijana wetu kuwa imara Kijeshi. Kadhalika, suala la ajira kwa vijana katika Jeshi nafasi ziongezwe ili kupata jeshi la vijana.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba Wanajeshi waandaliwe vizuri maisha yao baada ya kustaafu, watengewe maeneo ya kujenga nyumba zao za kuishi.

Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mkuu wa Majeshi na Makamanda wote kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuilinda nchi yetu na mipaka yake.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri kuwa, katika mpango wa makazi ya Makamanda wetu Mkoa wa Mtwara usisahauliwe, kwani nyumba zilizopo ni chache na zimechakaa sana.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Jeshi iliyopo karibu na bandari Mkoani Mtwara, kwa sababu lile eneo lipo Mjini sana na kutokana na kukua kwa shughuli za bandari, nashauri Kambi hiyo sasa ihamishiwe sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SYLVESTER M. MABUMBA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha kwa kuteuliwa kwake na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Nampongeza Mkuu wa Majeshi General Davis Mwamnyange, Makamanda na wapiganaji wote kwa kazi nzuri ya ulinzi wa nchi yetu. Pamoja na pongezi hizi, nina maoni machache kuhusu Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa vile miaka ya hivi karibuni nchi yetu imeshuhudia baadhi ya Makambi yakikumbwa na milipuko ambayo imesababisha madhara kwa wananchi na Jeshi letu: Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuwa na Jeshi dogo la kisasa ambalo halitahitaji kuwa limejitanua maeneo hata yanayokaliwa na Raia? Nashauri Jeshi letu liwe na Wanajeshi kidogo wanaoweza kuhudumiwa kwa uzuri zaidi, wapewe zana za kisasa, wawe na nyumba nzuri za kuishi na wapewe mafunzo ya kivita, wawe tayari kukabili hali yoyote ile.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri wa Ulinzi asimamie ipasavyo stahiki mbalimbali za Wanajeshi wetu hasa wapiganaji wa ngazi za chini. Mimi nikiwa ni mmojawapo wa Wawakilishi wa wananchi, kuna taarifa ambazo tunapewa na Askari Jeshi Wastaafu kuhusu mafao yao ya kustaafu, naomba wapewe haki zao hizo ili kuwapunguzia ugumu wa maisha.

Mheshimiwa Spika, naomba pia Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi kwa kupitia kwake, Jeshi lifuatilie mwenendo wa kikundi cha Uamsho huko Zanzibar, kwani kinatishia uhai wa Serikali ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kazi ya Jeshi ni kulinda mipaka ya nchi yetu. Hata hivyo, kikundi cha Uamsho kimeendelea kupandikiza chuki dhidi ya kuwepo kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano: Je, Jeshi limejipanga vipi kuhakikisha kwamba viongozi na kikundi chote cha Uamsho hakifanikishi azma yake ya kuvunja Muungano wetu?

Mheshimiwa Spika, naomba pia nizungumzie eneo walikozikwa mashujaa waliopigania ukombozi wa Msumbiji pale Nalyendere Mtwara. Wizara ina mpango gani wa kulitangaza kuwa eneo la utalii na hivyo kuwa mojawapo ya maeneo ya kuliingizia Jeshi na Wizara mapato?

Mheshimiwa Spika, eneo la Nalyendere Mtwara linayo maeneo ambayo yapo chini ya Jeshi na yanafaa kwa uwekezaji mkubwa. Je, Serikali kupitia Wizara hii ina mpango upi kuhakikisha kwamba wanapatikana wawekezaji wazuri na hivyo eneo hilo kuwa chachu ya maendeleo huko Mtwara na Tanzania kwa ujumla?

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika,nampongeza Waziri na wataalamu wake kwa hotuba iliyowasilishwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, nitachangia katika maeneo kadha wa kadha. La kwanza, linahusiana na Taasisi ya Nyumba iliyo chini ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Taasisi hii ilianzishwa takribani miaka 40 iliyopita ikiwa na lengo kuu la kuwa Kituo cha Uhawilishaji wa Teknolojia. Taasisi ilianzishwa kwa msukumo wa Baba wa Taifa, Marehemu Julius Nyerere ikiwa na madhumuni mawili: Kwanza, Utafiti na kuendeleza teknolojia kusaidia Jeshi kutengeneza zana na vifaa vyake; pili, kuleta mapinduzi ya kiteknolojia nchini kwa kuzalisha mitambo ya magari na bidhaa nyingine kwa ajili ya viwanda na kilimo (Wavuti www.tatcnyumbu.org).

Mheshimiwa Spika, madhumuni haya ya toka Nyumbu ilipoanzishwa, yametajwa pia katika hotuba ya Waziri ukurasa wa 18. Maana yake ni kwamba Nyumbu bado ina malengo yale yale.

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi zimelitumia Jeshi kuleta mapinduzi katika baadhi ya teknolojia na hasa utafiti wa kiteknolojia katika zana za Kisasa. Marekani, Urusi, China na nyinginezo zimeendelea Kisayansi katika teknolojia za kijeshi (Jeshi la maji, anga, nchi kavu na kadhalika) kwa sababu majeshi yao yalichukua jukumu la kufanya utafiti wa kikweli kweli.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa ni takribani miaka 40 toka Nyumbu ianzishwe: Je, utafiti gani umefanyika hadi sasa? Je, hadi sasa ni mapinduzi gani ya kiteknolojia ambayo yamefanyika? Mitambo na magari mangapi yamezalishwa? Mitambo au zana gani ya kusaidia viwanda na kilimo? Kama hakuna

lolote lililofanyika kati ya hayo, kwa nini Nyumbu isifutwe? Naishauri Serikali itenge fedha ya kutosha kwa ajili ya kutekeleza madhumuni ya Nyumbu.

Mheshimiwa Spika, nitaongelea dhana ya "Jeshi dogo". Hakuna shaka Jeshi letu limejiandaa vizuri kutimiza majukumu yake, lakini ni ukweli usiopingika kamba jeshi letu ni dogo kulinganisha na majeshi ya nchi nyingine kwa udogo wake. Jeshi letu linahitaji jeshi kubwa sana la akiba.

Mheshimiwa Spika, zamani sera ya ulinzi wa nchi ilijikita kwenye fikra kwamba japo Jeshi la Wananchi ndilo lenye jukumu la ulinzi kikazi, lakini wananchi wote walikuwa na jukumu la ulinzi pia. Ndiyo maana mafunzo ya mgambo yalifanyika nchini kote, na ndiyo maana JKT ilitiliwa mkazo. Kwa hiyo, uamuzi wa Serikali kurejesha mafunzo ya lazima ya JKT ni mzuri, unaturejesha tulikotoka. Ni vyema sasa Serikali ikajipanga vizuri ili mafunzo ya Mgambo yarejeshwe kwa mkazo ule ule uliokuwepo zamani. Kila mwananchi mwenye afya na umri unaofaa anapaswa kupata mafunzo ya kijeshi ili Keshi la Akiba lilingane na ukubwa wa nchi hii kwa eneo na idadi ya watu.

Mheshimiwa Spika, la mwisho nitakalochangia ni swali. Je, Jeshi letu limejiandaaje kuhusiana na teknolojia ya habari na mawasiliano *(TEHAMA)?* Hili ni eneo la teknolojia ambalo maendeleo yake yanakwenda kwa kasi sana. Hapa ndipo Taasisi ya Nyumbu, kama ingekuwa imetekeleza majukumu yake, ingetoa mchango mkubwa wenye msaada. Kwa vyovyote vile, Jeshi la wananchi lazima lijipange vizuri

katika eneo hili kama linavyotakiwa kujipanga katika maeneo mengine pia. Ulinzi wa kisasa ni tofauti na wa zamani na kwa kiasi fulani unategemea *TEHAMA*. Serikali iliangalie hili na kuchukua hatua za dhati na thabiti.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, Jeshi ni chombo muhimu cha ulazima kwa nchi yoyote duniani, na kwa hapa kwetu tuna kila sababu ya kushukuru kwamba hadi sasa bado chombo hiki kinafanya kazi vizuri na kwa utaalamu na umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya matatizo ambayo yanaonekana bado yapo na yanaendelea kwa ujumla mpaka sasa, ni pamoja na dalili zinazoonyesha kutokuwepo kwa mahusiano mema kwa baadhi ya Makambi ya Jeshi yaliyo ndani ya Mitaa ya makazi ya raia, kutokana na wanajeshi wetu kufanya vitendo vya kikatili kwa wananchi kama vile: kuwapiga wananchi bure, kuvamia maeneo ya makazi ya watu na kufanya vitisho na uharibifu kwa raia, Askari kufanya vitendo vya fujo hata katika magari ya kiraia pale wanapodaiwa nauli katika magari hayo.

Mheshimiwa Spika, hadi leo hii bado kuna wananchi ambao walivamiwa na kupigwa na Wanajeshi wa Kambi ya Migombani na kuwasababishia maumivu na athari za kiafya ambazo hadi leo bado wananchi hao wanasumbuka na

matatizo waliyoyapata toka kwa Wanajeshi hao (eneo la Jang'ombe kwa Maharuki).

Mheshimiwa Spika, pamoja na mpango wa kupima afya kwa eneo la mipaka katika maeneo ya Makambi ya Majeshi yetu, naomba Mheshimiwa Waziri aangalie vyema maeneo hayo kwa upande wa Zanzibar hasa ukizingatia kwamba eneo la Zanzibar ni dogo sana, hivyo Kambi kama vile ya Misaili iliyopo Welezo ndani ya Jimbo langu la Magogoni katika Wilaya ya Magharibi Unguja, imeingia sana katika eneo la makazi ya raia takribani katika pande tatu za Kambi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kambi hii ipo ndani ya makazi ya watu kwa asilimia kubwa ya eneo lake, namwomba Mheshimwa Waziri aje katika Kambi hii na tutembee pamoja ili nimwoneshe eneo ambalo limo ndani ya makazi ya raia ili tuweze kufikiria namna ya kutumia mipaka ya asili ilipo kama vile barabara kuwa kama mipaka baina ya Kambi na makazi ya raia.

Mheshimiwa Spika, uhamisho kwa askari ni mfumuko wa kiutendaji kwa Askari wote, lakini inasikitisha kwamba uhamisho sasa unatumika kama adhabu kwa Askari wetu, kwani Askari anahamishwa na anapelekwa sehemu moja mpaka anasahauliwa, naye ana sahau kwao. Lakini jambo hili linasababishwa na viongozi, baadhi yao wanatumia nafasi walizonazo kuwaadhibu wapiganaji walio chini yao. Kwa kweli jambo hili linapelekea chuki baina ya Askari kwa Askari. Ni vyema kuwe na kipindi kinachoeleweka kwamba

Askari hatakaa katika Kambi moja kwa muda fulani mfululizo ili kila askari ajue hivyo.

Mheshimiwa Spika, pia kwa Askari wa Jeshi la kujenga uchumi, kuna tatizo la fursa kwa Askari wanaotaka kwenda kujiendeleza, aidha, kupata masomo katika Sekta za Afya na hata Kilimo. Naomba jambo hili nalo lizingatiwe kwa usawa unaostahiki.

Mheshimiwa Spika, kama Waziri alivyoeleza hapa kwamba wanategemea kuchukua vijana 500 katika Makambi ya JKT, nami namwomba tu kwamba na kwa Zanzibar JKU nao wachukuliwe, nao wapewe nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, nami nachukua fursa hii kuchangia hotuba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Zanzibar majengo ya Kambi za Jeshi ni machakavu hususan Kambi ya Jeshi ya Migombani, majengo yake ni chakavu sana, hayana hadhi ya kuishi Majeshi. Maafisa wa Jeshi ambao wanaishi kwenye nyumba za Jeshi na familia zao, milango wanayoitumia ni mibovu, madirisha ni madogo, vyumba vyenyewe ni vidogo na wanatumia mapazia kutenganisha familia baina ya baba, mama na watoto. Hamwoni kama huku ni kudhalilisha Wanajeshi wetu? Wanavunjika moyo kutumikia Serikali yao kwa uadilifu na kujiingiza katika vitendo viovu. Je, ni lini Waziri atafanya ziara ya Kambi zote za Unguja na Pemba ajionee mazingira

wanayoishi Wanajeshi wetu na ni lini hizi nyumba za Askari wetu wa Jeshi kwa upande wa Zanzibar zitakarabatiwa?

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Zanzibar Kambi za Jeshi ambazo zimepakana na wananchi kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi, wanasema wemechukuliwa maeneo kwa muda mrefu. Kwa mfano, kambi ya Jeshi Bavuai, Chukwani, kumekuwa na malalamiko siku nyingi, wananchi wamechukuliwa maeneo yao na majeshi bila kupata fidia yoyote na mpaka leo hii wananchi wanadai maeneo yao. Ni lini wananchi hawa watapata haki zao?

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya wananchi ambao sio waadilifu, wanatumia sare za Majeshi kufanya uhalifu na kuyachafua Majeshi yetu. Je, ni wahalifu wangapi ambao wameshakamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya Sheria kwa kutumia vibaya sare za Jeshi? Kuna baadhi ya Wanajeshi wanatumia sare za jeshi kwa kufanyia uhalifu. Je, ni Wanajeshi wangapi wamechukuliwa hatua kwa kudhalilisha Jeshi kwa kutumia sare za jeshi kufanyia uhalifu?

Mheshimiwa Spika, nafasi za ajira kwa upande wa Zanzibar zimekuwa zikilalamikiwa sana. Ni vegezo gani ambavyo vinatumika kuwachukua vijana wetu katika nafasi hii ya Jeshi? Vijana wengi wanaopitia JKU na JKT wamekuwa wakiachwa na kuchukuliwa vijana ambao hawajajiunga na JKU wala JKT na wanavyopelekwa kwenda kufanyiwa *enterview* na vipimo mbalimbali na

wanakuwa hawana sifa ya kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwa upande wa Zanzibar, zile nafasi za Wazanzibar zinapotea na kuchukuliwa na Tanzania Bara kutokana na kupeleka vijana ambao hawana sifa ya kujiunga na Jeshi.

Mheshimiwa Spika, ni kwa nini viongozi wetu wa Zanzibar wanakuwa sio waadilifu zinapoletwa nafasi za Jeshi, anachukua kiongozi wa juu na kupeleka Jimboni kwake bila kuzigawa kwa makundi ya vijana wa Zanzibar na Pemba waliokuwa na sifa ya kujiunga na Jeshi la kujenga Taifa bila kubagua watoto hawa ni wa viongozi au sio wa viongozi?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na wastaafu wa Jeshi, mpaka leo hii hawajalipwa mafao yao, wanahangaika kufuatilia mafao yao bila mafanikio yoyote na wengine ambao wapo Zanzibar Mikoani wanaingia madeni kwa kukopa pesa za kwenda kufuata mafao yao bila ya mafanikio yoyote. Serikali haioni kama hivi ni kuwadhalilisha Wanajeshi ambao ni waadilifu na wengine walipigana vita kwa ajili ya kuitetea nchi yetu? Ni lini Serikali itawalipa wastaafu hawa mafao yao kwa wakati muafaka kama nchi za wenzetu wanavyowaenzi Askari wao wastaafu kwa kuwapa huduma za jamii bila kuwasumbua? Serikali isingoje mpaka siku ya kufa wastaafu ndio waje watoe sifa kemkem na wadhifa wao Serikalini. Naiomba Serikali iwaenzi wastaafu kabla hawajafa, wawape mafao yao kwa wakati muafaka.

**MHE. PEREIRA AME SILIMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi ili nami nichangie kwenye Hotuba hii. Napenda nimpongeze Waziri na Watendaji wa Wizara hii, kwa Hotuba yao iliyoandaliwa na kuwasilishwa vyema. Pamoja na hayo, naomba nichangie kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo ya Jeshi yapo katikati ya makazi na ni hatari sasa kuweka miripuko ya kivita. Nchi yetu imewahi kupata maafa ya Mbagala na Gongo la Mboto ambapo maisha na mali zilipotea. Pamoja na uamuzi wa kujenga maghala lakini maeneo kama Mtoni hayajaweza kuendelea kuwa Kambi ya Jeshi kwa sababu ya kuzungukwa na makazi ya watu kila upande.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na jitihada nyingi za kuiimarisha JKT na hasa kutaka izalishe na kujitegemea. Nia hii ni nzuri lakini bado kuna safari ndefu ya kuitimiza. Hadi sasa JKT pamoja na kuwa na nguvu kazi ya kutosha, bado haijaweza kujitosheleza kwa chakula mbalimbali na tamaa ya kuzalisha ziada kwa ajili ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, uhusu huduma za maafa na mahitaji maalum; naomba nilipongeze Jeshi la Wananchi kwa kuwa tayari kutoa huduma za kusaidia wahanga wa maafa. Aidha, naomba niwapongeze kwa utayari wao wa kutoa huduma, kwa mfano, kusafirisha mazao kupeleka kwenye maeneo yenye shida au uhaba wa chakula.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FAKI HAJI MAKAME:** Mheshimiwa Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia afya njema, napenda niishukuru Ofisi yako kwa kuruhusu pia uchangiaji kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimwa Waziri anayehusika kwa kuitayarisha vizuri Hotuba hii. Hotuba inataja kuzingatia mafao ya askari wetu, jambo hilo ni muhimu kwa sababu hivi sasa wana mafao hafifu. Wanajeshi wetu wanaambulia kuwa walinzi wa ofisi za watu binafsi kwa sababu hivi sasa wana mafao hafifu, kiinua mgongo na pensheni ni nyepesi.

Mheshimiwa Spika, katika ajira ya Jeshi kwa sasa haipo kwa uwiano mzuri, ingefaa uwiano ukawa kwa asilimia 60 Tanganyika na asilimia 40 watoke Zanzibar. Baya zaidi, hata hao wanaopatikana (kidogo) kutoka Zanzibar, wengi ni watu kutoka Tanzania Bara! Jambo hili lizingatiwe vyema la sivyo tutafika mahala tuwe na Jeshi la watu wa upande mmoja tu, Tanzania Bara!

Mheshimiwa Spika, wengine tunawakumbuka kama Marehemu Mzee Yusufu Himid (Zanzibar) na Sarakikya (Bara) ndiyo waliotakiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waunganishe Jeshi letu. Nchi hizi mbili Zanzibar na Tanganyika zilikuwa huru! Kwa nini uwiano wa ajira haulingani na haki za nchi hizo zilizoasisi Tanzania?

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono suala la kuwapeleka vijana 5000 mwaka 2013 katika Makambi ya Vijana ya JKT. Jambo hili litajenga uzalendo, maadili na nidhamu kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ni kuwa idadi hii ni ndogo sana kwa ukubwa wa nchi yetu ulivyo, kulingana na wingi wa vijana wanaostahili na mmomonyoko mkubwa wa maadii katika Taifa letu. Nashauri idadi iongezeke angalu mara mbili yake kwa kila *intake*.

Mheshimiwa Spika, Kambi za Jeshi mfano Gongo la Mboto, Mbagala na hata Mtoni Zanzibar, Kikosi cha JWTZ kipo mitaani kabisa. Tunayo ardhi ya kutosha nchini Tanzania, kwa nini hatuwahamasishi Wanajeshi wakaenda maeneo mengine. Kama mabomu yameua Gongo la Mboto na Mbagala, yataua Chukwani, Mtoni na kwingineko.

Mheshimiwa Spika, Wastaafu wa Vita vya Uganda wananung'unika, wengine ni walemavu na tunajua kuwa tulipomaliza vita hatukuwapa ahsante.

Mheshimiwa Spika, utaratibu ufanyike, manung'uniko yaondoke.

Mheshimiwa Spika, katika suala la KILIMO KWANZA, ninaipongeza Serikali kwa kukabidhi SUMA JKT, wanafanya vizuri katika mauzo ya matrekta kwa bei nafuu. Ninashauri Wanajeshi hawa waendeshe ubia katika kilimo kati yao na Wananchi. Wananchi watoe ardhi yenye rutuba, Wanajeshi watoe vifaa na Serikali

itoe fedha. Kwa mtindo huo, tutaweza kuzalisha chakula na fedha tutapata na Wananchi wataneemeka.

Mheshimiwa Spika, nashauri katika bajeti iliyopangiwa Wizara hii na kuainishwa ukurasa wa 36 - 38 wa Kitabu cha Hotuba hii ni lazima wapewe. Bila ya kukamilishwa fedha hiyo, hatutaweza kuwapima na kuwahoji katika kipindi cha bajeti ijayo ya 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja.

**MHE. SALUM KHALFAN BARWANY:** Mheshimiwa Spika, Tanzania imekuwa ikijihusisha na harakati mbalimbali za ulinzi ndani na nje ya nchi. Tanzania ilikuwa mbele katika Ukombozi wa Bara la Afrika na sasa kusimamia amani katika nchi mbalimbali. Serikali inasemaje kuhusu mchango uliotolewa na Mikoa ya Kusini kwa kuwa ndiko kulikokuwa na Makambi ya Wakimbizi na Vituo vya Mafunzo kwa askari hao?

Mheshimiwa Spika, Serikali inasemaje kuhusu miundombinu ambayo ilishindikana kuwekwa kutokana na sababu hizo huko Kusini, kwa maana ya fidia kutokana na athari zilizojitokeza maeneo hayo na Wizara haioyeshi ni kiasi gani cha fedha ambazo hulipwa Serikali kwa ushiriki wake katika harakati hizo na ni malipo gani wanapatiwa askari wetu wanapokwenda kushiriki kulinda amani katika nchi hizo?

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara yako itoe maelekezo ya kina kuhusiana na vijana walioamua kujitolea wa Kikundi cha Jakaya Mrisho Kikwete cha hapa Dodoma, ambao waliandika barua kuomba kujitolea kwa kipindi cha miezi sita katika uhifadhi na upambanaji wa ujangiri ndani ya Hifadhi za Taifa kwa Waziri Mkuu, nakala kwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Waheshimiwa Wabunge, kwa lengo la kuipunguzia gharama Serikali. Idadi ya vijana hao ambao wamehitimu Mafunzo ya JKT ni 68 na ambao wamejitolea tokea mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika, Serikali inasemaje kuhusiana na gharama za kuingia Mikataba ya Kununua Askari kutoka JKT ambapo inakadiriwa Wizara ya Maliasili huwa inalipa takriban Shilingi 2,875,000 kwa ajili ya kumpata Askari wa Uhifadhi mmoja. Je, Serikali haioni kwa kuwa huo ni mzigo mkubwa wakati kuna vijana wapo tayari kujitolea kwa kazi hiyo? Serikali ieleze fedha hizi zinaingia Mfuko gani na zinafanya kazi gani?

Mheshimiwa Spika, Serikali inatoa tamko gani kwa vitendo vya unyanyasaji wanaofanyiwa wasichana wanapokuwa mafunzoni?

Serikali haioni kuwa vitendo vya kulazimisha ngono vinachangia kukua kwa kasi ya maambukizi ya Ukimwi na ni Rushwa ya ngono?

Mheshimiwa Spika, Serikali inasemaje kuhusu kucheleweshwa malipo au fidia kwa askari wanaoumia wakiwa katika mafunzo? Taarifa zinaonesha wapo vijana waliopata majeraha na athari mbalimbali,

ambao hawajalipwa hadi leo; mfano ni kijana Ac 8542 V/L John Godfrey, ambaye alimwandikia barua Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, tokea tarehe 25 Februari, 2008 lakini mpaka leo hajapatiwa ufumbuzi wowote.

Mheshimiwa Spika, Serikali inasemaje kuhusu kipindi kinachotolewa cha mafunzo cha miezi sita wakati mafunzo kwa vijana hao kama fani za ujenzi, uashi, umeme na kadhalika huhitaji kufanyika kwa muda usiopungua miaka mitatu?

Mheshimiwa Spika, Wizara itoe ufafanuzi juu ya vijana wanaoingia JKT kwa fani zao kama wachezaji wa mpira, wasanii na kadhalika, lakini wanapomaliza kozi zao hutelekezwa na kuonekana hawana nafasi ya kupata ajira ndani ya JKT.

Kadhalika, naiomba Wizara itoe ufafanuzi juu ya watoto na wajane wa askari wanaofariki wakiwa kazini, wengi huchelewa kupata mafao yao na au kupoteza kabisa.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi yake, kwa mwaka 2012/2013, kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumpongeza Waziri, kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye weledi uliotukuka.

Katika Hotuba ya Waziri ameonesha dhahiri kuwa Serikali ipo makini kuhakikisha kuwa ulinzi wa mipaka yetu unaimarika na nchi inabaki kuwa salama. Lipo tatizo kubwa katika eneo la ulinzi wa mipaka kwa maana kuwa hivi sasa yapo makampuni mengi ya utafiti wa matufa na gesi hapa nchini. Ninaloliona sasa ni kuwa, makampuni haya ya kigeni huajiri kampuni nyingine za kigeni kwa ajili ya kujihami na maharamia. Hii ni hatari kubwa kwa maana makampuni haya yanabeba silaha nzito sana, Serikali itoe fungu ili kujenga uwezo kwa jeshi letu kufanya kazi hizi. Ni imani yangu kuwa Jeshi letu lina uwezo mkubwa lakini wanakosa nyenzo.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Waziri, amezungumzia suala la Jeshi la Kujenga Taifa. Licha ya kurejesha Jeshi kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu, naishauri Serikali itumie Jeshi hili ili kutatua tatizo la ajira kwa vijana kwa kuanzisha Kambi Maalum, kwa kuwajengea vijana uwezo wa kujituma, kujiamini na uadilifu. Serikali iharakishe kutatua tatizo hili maana sasa limekuwa kama ni la kisiasa.

Mheshimiwa Spika, katika mishahara na maslahi, Serikali iangaliwe jinsi gani ambavyo maslahi ya Wanajeshi wetu yanaboreshwa kulingana na kazi nzito ambazo wanafanya kulinda mipaka yetu. Pia Serikali ihakikishe nidhamu katika Jeshi inasimamiwa vyema kwa maana inaonekana inashuka kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, juhudi za makusudi zifanyike kuhakikisha kuwa, mishahara hewa kwa watumishi inakoma na Serikali itumie pesa hizo kwa ajili ya

shughuli nyingine za maendeleo. Tatizo la usiri wa taarifa za Jeshi na Wanajeshi zisimamiwe vizuri kwa maana wanastahiki zao ambazo si vyema zikawa zinatolewa ovyo bila ya kuzingatia umuhimu wa Taasisi hii nyeti. Hapa nchini kumezuka tabia ya ajabu sana kwa baadhi ya watu, vyombo vya habari na hata wanasiasa kuzua taarifa za uongo na kulihusisha na Jeshi. Pia wamekuwa wanatumia muda mwingi sana katika kuchambua utendaji wa Taasisi hii nyeti kwa Taifa letu. Huu ni ukiukwaji mkubwa sana wa maadili na utawala bora nchini kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, jambo hili litafutiwe suluhisho la kudumu. Pia kwa kuangalia vyema huu uhuru uliovuka mipaka utatufikisha wapi? Haiwezekani kila mtu akaamua kufanya analotaka kwa wakati wowote. Hakuna nchi hata moja ambayo inaweza kuwa mfano unaowiana na hapa nchini. Nyaraka za siri imekuwa ni jambo la kawaida sana kuonekana, lakini pia siri za Serikali zinavuja kirahisi sana. Lazima ikumbukwe nchi hii ni huru, haipo kwenye mateka wala haijaingia vitani. Jeshi lifanye kazi kwa mujibu wa Sheria na lirejeshe imani kwa Wananchi na Jumuiya za Kimataifa ambapo zimekuwa zikiamini ni moja ya Majeshi makini Duniani.

Mheshimiwa Spika, Jeshi liendelee kutoa mafunzo ya kutosha kwa Watumishi na Maafisa wake ili liweze kujenga uwezo mzuri kukabiliana na changamoto zilizopo. Kwa kipindi kirefu tumeomba kuanzishwa kwa Kambi ya JKT katika eneo la Kilwa Kaskazini. Naamini uwepo wa Kambi hii utasaidia sana kuimarisha uchumi. Naiomba Serikali isikie kilio hiki cha muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RAJAB M. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri. Ni jambo la fedheha sana kusikia eti Jeshi letu lipo katika kashfa ya ughushaji wa vyeti. Kwa akili ya kawaida tu, mtu atapata mshtuko mkubwa anaposikia kitendo hiki cha aibu cha watu kughushi vyeti. Kigezo kimojawapo cha kujiunga na JWTZ ni kuwa na Elimu ya Kidato cha Nne na kuendelea na awe amefaulu.

Mheshimiwa Spika, nafikiri sababu mojawapo inayosababisha watu wengi kughushi vyeti kwani wengi wao huwa wanapata daraja la sifuri *(zero),* ambalo haliwaruhusu kujiunga na Jeshi. Ni jambo lisilopingika kuwa siyo vyema mtu ambae hajafaulu kujiunga na Jeshi kwani Sekta hii inahitaji watu wanaojitoa hasa, lakini pia wenye elimu ya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kuwa Jeshi letu likiwa na watu walioghushi vyeti, Taifa linakuwa katika hatari kubwa sana kwa sababu zifuatazo:-

(a) Ukosefu wa uadilifu; mtu yeyote aliyeghushi cheti, atajenga tabia mbaya na mwishowe kukosekana uadilifu Jeshini.

(b) Utendaji kazi kuzorota; huwezi kutarajia mtu goigoi aliyepita bila vigezo kuchapa kazi kwa kujituma.

(c) Hata akiwa ndani ya Jeshi, bado tabia ya kughushi itaendelea kuwepo kadiri mwanya utakavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, inaonekana Jeshi limelegea sana katika mchakato wa kuwapata watu wapya kuingia Jeshini. Ikumbukwe kuwa, Jeshi ndiyo kituvu cha ulinzi na usalama wa Taifa hili. Naomba kuhitimisha kwa kulishauri Jeshi letu, kufikiri upya namna ya kumaanisha katika michakato hii ya ajira. Chondechonde, Jeshi letu lisilegee katika masuala muhimu ya Taifa (ulinzi), kwa kuwaruhusu watu wasio waadilifu kuingia na kuliharibu Jeshi letu.

Mheshimiwa Spika, katika *intake* iliyopita, Tanzania Zanzibar ilipangiwa nafasi laki tano za ajira Jeshini. Ajira hizi zilitakiwa zipitie JKU, bali mgawanyo ambao ulifanyika haukutenda haki kwani kati ya nafasi hizo ni nafasi 100 tu ndizo ziligawiwa kwa Mikoa mitano ya Zanzibar, ambapo kila Mkoa ulipata nafasi 20 tu, nafasi 300 zilipelekwa JKT kwa kisingizio cha Wazanzibari walioko JKT ambao kwa imani yangu idadi hiyo haipo. Isitoshe, nafasi 100 zilichukuliwa na Ikulu Zanzibar, ambazo hatukujua kapewa nani. Kwa hakika hii siyo haki na wala siyo misingi ya Utawala Bora kwani vijana ambao walifanyiwa *interview* katika kila Mkoa walizidi 100. Ni vyema Waziri akalisimamia hili na kuona umuhimu wa vijana wetu hususan wale walioko katika Makambi yetu ya JKU. Binafsi nalaani ubaguzi na unyanyasaji huu uliotendeka kwa Vijana wetu wa JKU.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, napenda kufahamu Wizara ina mpango gani wa kuwapandisha vyeo Wahandisi na Wataalamu wa *IT* ambao wamelipa Jeshi sifa kubwa lakini hawapandishwi vyeo na badala yake wanaongezewa muda wa Utumishi wao kustaafu wakiwa na umri

mdogo, tofauti na madaktari na wanasheria. Jeshi linahitaji *IT* sana na hasa walio na weledi wa kutosha. Naomba jibu wakati wa kuhitimisha hoja ya Waziri.

Mheshimiwa Spika, kumezuka tabia ya ajabu sana ya Wanajeshi kujiongezea mipaka ya maeneo kwa mabavu. Lini Jeshi litarudisha maeneo ya Kyaka na Bunezi ambayo Wanajeshi wamechukua kwa wananchi kwa ubabe?

Mheshimiwa Spika, kuna suala la Vita ya Kagera ambapo Tanzania ilipokuwa ina Vita na Uganda, uwanja wa mapambano ulikuwa Mkoani Kagera, Wilaya ya Missenyi, mali za watu ziliharibiwa, majumba ya watu na hata wengine kushindwa kujenga tena.

Nauliza ni lini Jeshi litawalipa wahanga hao fidia ya mali zao?

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimwa Shamsi Vuai Nahodha (MB), pamoja na Uongozi mzima wa Wizara ya Ulinzi, kwa kuwasilisha Bungeni Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa linalotarajiwa kufufuliwa lijikite katika kufundisha vijana zaidi kwenye uzalendo, nidhamu na stadi za uzalishaji mali na masoko, hususan masoko ya nje, viwanda vidogo vidogo, usindikaji na mafunzo ya teknolojia zitakazorahisisha uzalishaji na kuongeza tija, thamani na

ubunifu. Vijana ni wabunifu, wapewe fursa za kutumia ubunifu huu vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, vijana wafundishwe teknolojia rahisi kwenye kilimo, umwagiliaji, viwanda, maji, ujenzi, utengenezaji wa miundombinu ya vijijini na vifaa vya ujenzi. Vijana watumiwe kwenye Miradi mbalimbali nchini na kwa hiyo kuwapa uzoefu, lakini vilevile kupunguza gharama na kuwapa ajira pamoja na kuwajegea imani kwa Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, masuala ya kuwalinda vijana wa kike katika Makambi yazingatiwe ili unyanyasaji wa jinsia usiwepo. Hii itawapa imani vijana wa kike kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa na kwa hiyo nao pia kunufaika. Mafunzo ya masuala ya kijinsia na Sheria za Unyanyasaji wa Kijinsia yazingatiwe ili ufahamu wa vijana uwe mpana katika jambo hili ili kuzuia athari kubwa zitakazoweza kutokea.

Mheshimiwa Spika, Vijana wa JKT watakapomaliza mafunzo wawekwe kwenye vikosi vya uzalishaji wa nyanja mbalimbali na kutumiwa kama vikosi kazi vya kuaminika kwa nidhamu na taaluma zao. Kwa kuwa watalipwa, hii italifanya Jeshi hilo kujitosheleza kimapato na vile vile kuwapa ajira vijana wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Vijana wa JKT wapewe mafunzo maalum ya ulinzi wa mazingira na kuchukuliwa kwenye vikosi vya kulinda misitu, wanyamapori na vyanzo vya maji ili kurudisha nidhamu kwa wananchi katika ulinzi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, suala la uwiano wa mapato na matumizi: Jeshi bado linaweza kuongeza bajeti/mapato zaidi kutokana na shughuli zinazofanywa na SUMA JKT. Ni vyema Serikali isimamie mapato halisi yanayotokana na SUMA JKT ili iweze kuongeza pato la Jeshi kuliko kutegemea tu mapato toka Serikalini. Hata hivyo, SUMA JKT inapaswa kuongeza vituo zaidi vya mauzo ya trekta ili iwafikie wakulima wengi walio vijijini. Ikumbukwe kuwa, mkulima wa kijijini anapata usumbufu na gharama kubwa ya kufuata matrekta na zana zake kwa umbali mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nashauri kazi zinazofanywa na SUMA JKT ni bora iratibiwe kwa karibu zaidi ili kujua mapato halisi yatakayolenga kuboresha mapato ya Jeshi. Matrekta na zana zake zinazouzwa na JUMA JKT zisogezwe karibu zaidi na wakulima.

Mheshimiwa Spika, nafasi ambazo zipo kwa ajili ya vijana wanaopenda kujiunga na Jeshi imekuwa ikifanyika kwa siri bila jamii na vijana husika kupata taarifa. Hali hii hupelekea vijana wanaochukuliwa kuonekana ni ndugu za Wanajeshi waliopo au wakubwa fulani; ni vyema utaratibu wa kuwapata vijana hawa uwe wa wazi ili kuondoa manung'uniko na dhana iliyojengeka.

Mheshimiwa Spika, usalama wa mipaka ni jambo linalohitaji kutazamwa na kuangaliwa kwa umakini

zaidi kwa kuwa bado kuna matatizo machache ya mipaka. Ni vyema Jeshi likaongeza nguvu ili kuimarisha usalama katika mipaka yetu.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ambayo Jeshi limewekeza kuna migogoro mikubwa ya ardhi kati ya Wananchi na Jeshi. Hata hivyo, katika Hotuba ya Waziri ametuarifu kuwa, aliunda kikosi kazi kufuatilia migogoro hiyo husababishwa na nini zaidi. Matatizo yaliyobainika yameainishwa katika Kitabu cha Bajeti, ukurasa wa 29. Nashauri mambo yafuatayo ili kupunguza na au kukomesha kabisa migogoro hiyo:-

Moja, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi ihakikishe maeneo yote ya Jeshi yanapimwa na kupatiwa hati miliki.

Pili, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI na Viongozi wengine wa Kisiasa waendelee kutoa elimu zaidi kwa wananchi ili wafahamu umuhimu wa Jeshi kuwa na umiliki wa maeneo makubwa, ikiwa ni pamoja na kufahamu athari ya Jeshi kuwa na maeneo madogo.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kurejesha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa. Hata hivyo, ni vyema mafunzo haya yasiathiri udahili wa wanafunzi au vijana kujiunga na Vyuo Vikuu. Jambo hili ni vyema litazamwe upya ili kuondoa athari inayoweza kujitokeza.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Spika, naomba sana suala zima la mipaka ya Kambi za Jeshi kwa pande zote mbili; Tanzania Bara na upande wa Zanzibar. Ni kweli kwamba, kutokana na kukosa elimu, baadhi ya raia wanajaribu kuvamia maeneo ya Kambi zote za pande hizo. Hivyo, kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi kwa pande zote mbili za nchi yetu, waone ni njia gani wanazoweza kuyapima maeneo haya na kupata hati miliki. Ieleweke kwamba, hata Kambi hizo zimeendelea kuchukua maeneo ambayo siyo yao, suala hili limeibuka huko eneo la Unguja-Ukuu na kuongeza eneo hadi Kikungwi.

Mheshimiwa Spika, eneo hili siyo lao na suala hili analielewa vyema Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi aliyepita na alisema hatua za kuondosha tatizo hili zitatafutwa lakini hadi leo ni kimya. Tunamwomba Waziri alitolee kauli leo; Wizara hii itashirikiana vipi na Wizara ya Ardhi ili limalizwe.

**MHE. DKT. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, Timu ya JKT Handeni (Mgambo JKT), imefaulu kuingia kwenye *Super Primier League Tanzania* na hivyo itabidi ishindikane kwenye Mechi za Taifa. Timu hii inahitaji uwezeshaji mkubwa na vile vile moja ya sharti la kutimizwa ni ukarabati wa Uwanja wa Mpira wa pale Chanika Handeni, ambapo watakuwa wakicheza na Timu nyingine ngazi ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mbunge wa Handeni na Mdau wa Mgambo JKT, Serikali ni vyema ikai-*support* Timu hii ya JKT ili iendelee na ushiriki wake katika *Super League (Primier)* ijayo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na Timu ya Mgambo JKT isaidiwe.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Suala la ulinzi kwenye utafiti wa *gas* na mafuta usifanywe na wageni. Uwezo wa Kamandi ya Navy unaboreka kwa kupata au kuagizwa boti za vita mbili. *Issue* ya Bima isiwe tija kwa wageni hawa, pesa zinazolipwa na Serikali kwenye Mkataba inajumuisha pesa za Bima. Jeshi letu siyo chini ya Dola za Kimarekani milioni tatu kwa mwezi kwa kutoa huduma ya ulinzi. Athari nyingine walinzi hawa wa kigeni wanatumia silaha kubwa na hii siyo sahihi.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kuunga mkono hoja hii na ninampongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa Hotuba nzuri waliyoiandaa.

Mheshimiwa Spika, nimebatahatika kutembelea Makambi mawili ya Jeshi na hapa nina maoni yafuatayo:-

Pale Kambi ya Mzinga kuna Hospitali ambayo ni ya Jeshi lakini inahudumia watu wengi wa Morogoro na Mikoa ya Jirani. Kuna majengo pale Hospitalini hayajaisha na ni ya kwa muda mrefu, ninaomba Serikali iwapatie fedha waweze kumalizia majengo hayo kwa faida ya Wanajeshi na Wananchi kwa ujumla. Pia naomba Serikali iwapatie fedha za kutosha kwa ajili ya dawa na huduma zingine iweze kukabiliana

na wingi wa watu wanaokwenda kupata huduma pale.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Ihumwa ni muhimu sana kwa ulinzi wa nchi yetu, lakini kuna baadhi ya silaha zipo peupe tu, hazina *shed* kiasi kwamba jua na mvua ni la kila siku; hivyo, kuathiri usalama na umadhubuti wa silaha hizo. Silaha zinaharibika kwa kukosa vivuli *(sheds)* za kuhifadhi silaha hizi. Kambi hii ipewe fedha za kutosha kwa ajili ya matufa hasa ya magari na vifaru kwa ajili ya kukarabati baadhi ya silaha na vifaa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Ihumwa haina eneo la kufanyia mazoezi, ninaomba Serikali iwapatie eneo kubwa la kuwawezesha kufanya mazoezi yake kwani askari bila ya mazoezi watadumaa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MATHIAS M. CHIKAWE:** Mheshimiwa Spika, kwanza, natamka kuwa naunga mkono hoja. Pili, napenda kuomba ushirikiano wa Waziri wa Ulinzi katika kutatua migogoro ya ardhi baina ya Wananchi na Jeshi letu la Ulinzi.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Jimbo langu wametoa ardhi kubwa kwa Jeshi letu, Kikosi cha Maji Maji, 41KJ, Faru 17. Awali Wananchi waliruhusiwa kulima hata mazao ya kudumu kama vile mikorosho.

Mheshimiwa Spika, Jeshi baada ya miaka zaidi ya kumi, linawafukuza wakulima hawa bila fidia yoyote

kwa mazao yao ya kudumu. Nashauri Jeshi ni muhimu wapate ardhi wanayodai, lakini Serikali ilipe fidia kwa mazao ya kudumua ambayo Jeshi waliruhusu Wananchi hawa wayapande.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri anipe ushirikiano mkubwa ili kwa pamoja tutatue tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Mnadhimu Mkuu na Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, kwa kudumisha amani na usalama wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii imekuwa ikisimamia mashirika yake kwa utendaji kazi wa kisasa (Nyumbu, Mzinga na SUMA JKT). Hapa suala kubwa ni kuhakikisha Mashirika haya yanatengewa fedha za kutosha ili kuweza kuzalisha zana bora na za kisasa zaidi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ina mpango gani wa kuwaendeleza au kuwaenzi wale ambao ni wabunifu kwenye Mashirika hayo? Kumekuwa na migogoro mingi sana ya mipaka katika maeneo ya Kambi za Jeshi na Makazi au Mashamba ya Wananchi; je, ni vipi Wizara imejipanga katika kutekeleza au kutatua migogoro hiyo?

Je, Wizara imetenga fedha kiasi gani ili kuweza kupima na kuhakisha mipaka ya Jeshi inajulikana na pia kuweza kutoa hati za kumiliki maeneo hayo?

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo kutaepusha migogoro na hata ile ya Wastaafu wa Jeshi (baadhi), kwa kuona hawajapata viwanja huamua kuvamia hayo maeneo.

Mheshimiwa Spika, nimeeleza hayo kwani Kamati yangu ya *PAC* tulitembelea baadhi ya Kambi za Jeshi na kubaini yafuatayo ambayo ninataka nipatiwe majibu vipi Wizara imejipanga kuyatatua:-

(i) Kambi ya Jeshi Kikosi 977, tatizo la uvamizi wa eneo hilo lilifikishwa kwa Waziri Mkuu ambapo yalitolewa maamuzi kwamba wapewe eneo ili wajenge Kikosi. Zinahitajika shilingi bilioni 52 kujenga Ofisi na fidia; je, zimetengwa?

(ii) Chuo cha Taaluma ya Kijeshi Tanzania (TMA), ni kizuri sana kwa Jeshi ambacho huchukua wanafunzi wanaotoka sehemu mbalimbali nchini, lakini Chuo bila maktaba kwa kweli hakijakamilika. Je, Wizara imejipanga vipi kwani zinahitajika shilingi milioni 592.4. Pia ni vyema tukajua nini mkakati wa kujenga bweni la wanawake. Vilevile napenda kujua Wizara imeshafanya tathmini ya uharibifu wa mazingira uliopelekea uharibifu wa bomba la maji na kujua gharama zake na kama tayari kazi hiyo itaanza lini?

(iii) Je, Wizara imejipangaje ili kujenga Chuo cha Ukamanda na Unadhimu kwani haipendezi kikazi

(kinidhamu) kwa wao kutumia Majengo ya TMA ambayo pia hayatoshi?

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuuunga mkono hoja, naomba nipatiwe majibu ambayo yataleta mafanikio kwa Jeshi letu.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ili kuwarahisishia Wanajeshi na familia zao upatikanaji wa bidhaa muhimu kwa bei nafuu, Serikali iliamua kuridhia uanzishwaji wa maduka ya Jeshi na hivyo kuyaondolea maduka hayo kodi ya uagizaji bidhaa. Pamoja na nia hii njema ya Serikali, wawekezaji hawa ambao wote ni wenye asili ya Kiasia, wamegeuza maduka hayo kama vitega uchumi vya kuwaletea faida kubwa. Hii ni kwa sababu, maduka haya badala ya kuuza bidhaa kwa bei nafuu, ukizingatia hayatozwi kodi, wao wamekuwa wakiuza kwa bei kubwa sana, sawa kabisa na bei za uraiani na hata wakati mwingine zaidi kumekuwa na malalamiko ya chini chini kwa Wanajeshi kwamba, maduka haya yapo mikononi mwa wakubwa, Makao Makuu ya Jeshi, ambao hushirikiana na wawekezaji hawa na hivyo kuficha uovu unaofanywa.

Mheshimiwa Spika, kama hili ni kweli ni kwa nini uchunguzi usifanywe kuwabaini hao ambao wanahujumu hadhi ya Wanajeshi wadogo na kulipotezea Taifa fedha nyingi kwa kutoa msamaha wa kodi?

Kama siyo kweli ni kwa nini Jeshi halifanyi uchunguzi kuona ukweli huu au ni kwa nini linakaa kimya wakati wakubwa wote nao hufanya *shopping* kwenye maduka hayo na hujionea bei hizi zilivyo kubwa?

Mheshimiwa Spika, JWTZ na JKT wanaongoza kuwa wadaiwa sugu wa Mamlaka za Maji nchini kote na kwa Shirika la Umeme *(TANESCO)*. Kwa nini wamekuwa na malimbikizo makubwa kama haya wakati kila mwaka tunapitisha bajeti katika Wizara hii na moja ya kazi ya fedha hizi ni kulipia maji na umeme; nani anatafuna fedha hizo?

Mheshimiwa Spika, SUMA JKT inadiwa jumla ya shilingi 194,718,000 na Kampuni ya ujenzi inayoitwa *Millenium Express Co. Ltd*. Baada ya kupelekana Mahakamani, Kampuni hii ilishinda na kupewa kibali na Mahakama kufuatilia mali zake ili kufidia deni, lakini SUMA JKT wamekuwa wakiwazuia kuingia kwamba ni eneo la Jeshi na kuna silaha, hivyo hawana ruhusa ya kuingia. Sasa kama mtu anadai haki yake ni kwa nini asilipwe na badala yake atishwe? Nataka maelezo ya kina kuhusu deni hili ni lini litalipwa na Kampuni hii iache kutishiwa?

Mheshimiwa Spika, Madaktari Wanajeshi wanafanya kazi kubwa hasa wakati wa migomo ya Madaktari wa uraiani, lakini mishahara yao ni midogo kulinganisha na wale wa uraiani. Kwa mfano, mshahara wa *Specialist* wa Jeshi wa Mifupa mwenye *Ph.D.* Cheo cha Meja analipwa shilingi 1,302,600 na Daktari wa uraiani mwenye *Masters* analipwa shilingi

2,162,000 *basic salary*. Hawa Madaktari wanasoma miaka ile ile sawa na wenzao wa uraiani na katika vyuo vile vile. Pia wale wa Kijeshi wanakwenda kwenye mazoezi ya kijeshi tena magumu kwa mwaka mmoja ili wawe Wanajeshi; kwa nini sasa mishahara yao inakuwa midogo kwani natambua kwamba mishahara ya Wanajeshi inategemea *ranks* za Wanajeshi lakini katika suala la utaalamu ni kwa nini hili lisiangaliwe kwa makini ili nao waweze kuwa na moyo wa kufanya kazi kwa ufanisi zaidi?

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Wanajeshi wanalipwa *ratio allowance* shilingi 225,000 kwa mwezi au shilingi 7,500 kwa siku. Pesa hii haitoshelezi, ni vyema wakaongezwa mpaka ifikie shilingi 15,000 kwa mwezi ili angalau waweze kukabiliana na ugumu wa maisha na gharama za bei zinapanda kila kukicha.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. AMINA N. MAKILAGI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na Timu yake, kwa kuandaa Hotuba yenye maelezo yanayojitosheleza. Pamoja na pongezi kwa Waziri, pia navishukuru Vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama, kwa kazi nzuri iliyotukuka katika kudumisha amani na usalama wa Taifa dhidi ya adui wa aina yoyote kutoka nje au ndani ya nchi na kuhakikisha uhuru na maslahi ya Taifa vinalindwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi, naomba kushauri masuala machache kama ifuatavyo:-

Serikali ijitahidi kutenga fedha za kutosha katika Sekta hii muhimu ili iweze kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:-

(a) Kulipa madeni ya maji na umeme, yaliyotokana na matumizi ya Vyombo vya Ulinzi na Usalama ili kulinda heshima ya Vyombo hivi. Siyo vema vyombo hivi ikiwa ni sehemu ya wadaiwa sugu wa madeni katika Taasisi za Umma na Binafsi, itapoteza heshima ya Vyombo hivi ambavyo vinaheshimika katika Jamii ya Watanzania.

(b) Kugharamia Mafunzo ya JKT kwa vijana wetu ili idadi ya vijana wanaokwenda JKT iongezeke zaidi kuliko ilivyo sasa. Nashauri vijana wachukuliwe moja kwa moja mashuleni kwa wale waliomaliza Kidato cha Sita na uwiano uwe sawa kati ya Wanawake na Wanaume.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nizungumzie kuhusu posho za askari (*Ration Allowance).* Nashauri posho hiyo iongezwe hadi shilingi 10,000 badala ya shilingi 7,500 iliyosukudiwa kuongezwa. Maisha ni magumu kulingana na *inflation* nchini. Tutafakari kwa dhati kama shilingi 7,500 inakidhi matatizo yetu? Wafikirie askari hao na uone kuwa mahitaji yao ni sawa na ya binadamu wengine pia.

Mheshimiwa Spika, askari waliostaafu wanalalamika Serikali kutokuwajali, mafao yao hayapatikani kwa wakati, chonde chonde Serikali

iangalie namna bora ya kuboresha mafao ya wastaafu wa Majeshi yetu ya Ulinzi na JKT. Malalamiko yao siyo jambo jema, hawa ni askari, wanaweza kufanya mambo mabaya wakichoka.

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi kikubwa nidhamu Jeshini, inaelekea kushuka siku hadi siku, ndiyo maana vitendo kama uvamizi wa maeneo (ardhi) ya watu vinafanyika. Huu ni utovu wa nidhamu, baadhi ya askari kuwa wababe mitaani na baadhi kujihusisha na uuzaji wa madawa ya kulevya kama bangi. Wizara na Serikali muimarishe nidhamu Jeshini.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali izindue duka la matrekta ya Kilimo Mkoani Kigoma kwa kuwa asilimia kubwa ya Wakazi wa Kigoma ni Wakulima. Zipo dalili za uhitaji mkubwa wa matrekta Kigoma. Hivyo, Kituo cha Kuuzia Matrekta Kigoma kianzishwe kama hiki cha Dodoma (SUMA JKT Kigoma).

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kumpongeza Mheshimwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii muhimu sana katika ulinzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ushauri wangu kwenye Kitengo cha Kupambana na Maafa katika Jeshi letu la Ulinzi na Usalama. Duniani kote leo, suala la maafa linapewa kipaumbele kikubwa kwani katika majanga yatokanayo na vitendo vinavyofanywa na binadamu ni mengi kuliko yale yanayotokana na asilia ya uumbaji wa Mungu *(Acts of God).*

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha *Risk Management* ni kwa ajili ya kupambana na majanga yanapotokea. Watanzania walio wengi hawana elimu ya kupambana na majanga na hasa athari zake. Jeshi letu linao uwezo mkubwa wa kutoa elimu hii kwa Watanzania. Jeshi letu likitumika vizuri hasa likiwezeshwa kiutendaji, nidhamu waliyonayo wanaweza sana kuokoa maisha ya Watanzania na mali majanga yanapotokea.

Mheshimiwa Spika, aidha, napendekeza Makambi ya Jeshi yaliyo karibu au katikati ya Makazi ya Raia yanaweza kuhamishwa kutokana na umuhimu wa kazi yao na malengo ya ulinzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pia napendekeza uwepo umuhimu wa makusudi kabisa wa kuimarisha Hospitali ya Rufaa ya Lugalo kwa maslahi ya pamoja ya Taifa letu.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kuanza mpango wa kupeleka vijana kuanza Mafunzo ya JKT. Serikali imeahidi kupeleka vijana 20,000 kila awamu kwa awamu mbili kwa mwaka. Nashauri Serikali izingatie uamuzi wake wa awamu mbili na kila mwaka itenge fedha za kutosha. Sheria irekebishwe iwe ni *compulsory* kwa kila kijana anayemaliza *‘A’ Level,* Chuo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, JKT itafundisha na kurekebisha vijana wetu ambao maadili yanaporomoka.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ulinzi wa Taifa *(NDC)* ni cha umuhimu kwa Watanzania. Nashauri Chuo hiki kiwe *managed* vizuri, kichukue wanafunzi hata kutoka nchi nyingine. Yafundishwe mafunzo ya kumuunda Kiongozi yeyote wa Serikali na hata *Private Enterprises*. Chuo kiwafanye Viongozi wawe Wazalendo na Utaifa urudi.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Akiba (Mgambo), wapewe motisha. Serikali iweke utaratibu Kampuni yoyote ya ulinzi nchini isiajiri walinzi ambao hawajapitia mgambo. Kukaa kwao katika ajira kutawapa elimu zaidi au ustadi zaidi na motisha. Bahati mbaya kukitokea vita, watafanya kazi ya kulinda nchi zaidi. Nashauri Serikali iweke utaratibu, Mshauri wa Mgambo Wilaya azitake Kampuni za Ulinzi katika eneo lake kufanya *parade* na kukumbusha zile *skills* za Kijeshi ili kuwafanya wasisahau.

Mheshimiwa Spika, Kampuni za Madini na nyinginezo za nje ya nchi, wanaajiri walinzi kutoka Nepal, South Africa na kadhalika. Kampuni hizi kwa mfano, *Resolute Ltd.* wa Nzega na Barrick na nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wanajeshi wastaafu wenye sifa nzuri wapewe majukumu ya kusimamia Vitengo hivyo. Jeshi Makao Makuu wanaweza kuwatolea *recommendation* nzuri, badala ya kutoa vibali vya ajira kwa walinzi kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Pamoja na hayo, naomba kushauri yafuatayo:-

Wanajeshi waliostaafu kwa ujumla wanaishi katika mazingira magumu, hasa wanaokabiliwa na ugumu wa maisha ni wale wa mwanzo. Nashauri wapewe fedha za kutosha za kujikimu.

Harusi za Kiraia zinazofanyika ndani ya Kambi za Jeshi, nashauri ziwe nje ya Kambi za Jeshi.

Wapishi wanaopikia Wanajeshi ambao wanatoka uraiani siyo *vetted*, hawaeleweki, wanapewa *tender.*

Mheshimiwa Spika, nauliza ikiwa vita vitatokea usalama wa nchi yetu utakuwaje?

Mheshimiwa Spika, nitashukuru nikipata majibu.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Spika, Kamanda wa Mgambo wa Meatu hana usafiri, naomba Wizara angalau iwapatie pikipiki ili kuwarahisishia shughuli zao.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. SALVATORY M. MACHEMLI:** Mheshimiwa Spika, naitaka Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ielekeze nguvu zaidi maeneo ya Maziwa na Bahari Kuu ili kuimarisha ulinzi katika mipaka yetu, kwani wakimbizi na maharamia wanapitia maeneo ya Maziwa Makuu

na Bahari kuingia bila vibali maeneo ya fukwe za Maziwa na Bahari zetu.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kuoa au Kuolewa ya Kijana anayeajiriwa na JWTZ ya kuwa muda wa miaka sita ndiyo anaruhusiwa kuoa au kuolewa ni muda mrefu; hivyo, ninaishauri Serikali ipunguze muda wa miaka sita na mapendekezo iwe miaka mitatu.

Mheshimiwa Spika, wastaafu wa JWTZ hali zao za maisha ni mbaya sana, ninaishauri Serikali iangalie upya pensheni hizo za wastaafu.

Mheshimiwa Spika, Siku ya Mashujaa ambayo huadhimishwa kila mwaka ni jambo jema lakini Serikali imewasahau Wajane na Watoto wa Mashujaa waliouwawa kwenye Vita vya Kagera mwaka 1978/1979 na kule Msumbiji ambapo kwa upande wa Kagera, Mnara wa Mashujaa upo Kaboya na kule Naliendele Mtwara, kwa mashujaa waliouwawa Msumbiji. Ushauri wangu kwa Serikali ifanye uhakiki wa wajane na watoto wa familia za mashujaa kuweza kuwapatia fedha za kukabilina na ukali wa maisha.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo ambalo ni vyema Serikali ikaangalia namna ya kurudisha alama za mipaka *Beacons,* sehemu ambazo zimeondolewa hasa mpaka kati ya Tanzania na Kenya katika Vijiji vya eneo la Tarime (TRM) na Migori Kenya katika Vijiji vya Nyamhunda, Panyakodi, Rouche, Ikoma na Kerongwe. Mpaka wa Tanzania na Zambia Tunduma, baadhi ya alama zimeondolewa na nyumba zipo katikati ya

mpaka wa nchi mbili.  Ushauri wangu, Serikali iandae utaratibu wa kushirikisha Wizara ya Ardhi na Mambo ya Nje za Nchi husika.

Mheshimiwa Spika, Mpaka wa Tanzania na Burundi umekuwa na uvamizi wa mifugo kuingia Tanzania toka Burundi na alama za mpaka zimeondolewa katika eneo la Mabamba.

Mheshimiwa Spika, suala la uajiri lina matatizo Visiwani hivyo liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT.KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Spika, kuhusu migogoro ya ardhi na wananchi:-

(a) Kwa nini kuwe na mwanya wa watu binafsi kuingilia maeneo ya Jeshi wakati kuna Viongozi wa Jeshi katika maeneo husika?

(b) Maeneo yaliyo katika Halmashauri kama Wilaya ya Serengeti, Kata ya Kisaka, Kijiji cha Bongega (Mung'we), utaratibu wa kupewa eneo hilo kwa mazoezi ya shabaha ni jambo zuri, lakini utaratibu wa kutaka kulichukua kinyemela ni kandamizi kwa Wanakata ya Kisaka.

Mheshimiwa Spika, Kambi za Jeshi zijengwe mbali na makazi ya raia na kuwa na *buffer zone*.

Mheshimiwa Spika, Wanajeshi wasiishi na Wananchi uraiani. Hii inasababisha kufahamiana na

watu wenye nia mbaya na kuwarubuni askari wanaoishi uraiani na hatimaye kujiingiza katika vitendo na matukio maovu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii, kwanza, kuwapongeza Waziri, Mkuu wa Majeshi na Mkuu wa JKT, kwa kazi nzuri wanazofanya katika kulinda mipaka yetu na kusaidia jamii. Lipo tatizo katika Kikosi cha Jeshi 95KJ na inawezekana pia katika Vikosi vingine vya Jeshi, kwa askari kutopewa pesa za chakula na pia mzabuni wa chakula wanachokula ukiangalia na gharama wanayokatwa askari haviendani (haikidhi). Naomba sana uchunguzi ufanyike ili kuondoa dosari hii katika Kikosi 95 KJ na Vikosi vingine kama lipo tatizo kama hili.

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kufahamu ni lini mafao ya Askari Alpius Mtatiro Keraryo, mwenye Na. UD 5235, ambaye alifariki mwaka 1996 akiwa Makao Makuu ya Jeshi kama kituo chake cha mwisho yatalipwa? Mjane wa Marehemu amefuatilia sana bila mafanikio. Naomba maelezo ya kina juu ya suala hili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo letu la Siha, naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha (MB), Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa Hotuba nzuri na yenye uchambuzi wa

kutosha, ambayo ameitoa asubuhi ya leo. Hongera sana Mheshimwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, naomba nilipongeze Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania, kwa kazi nzuri linalofanya ya kulinda mipaka ya nchi yetu. Mimi natoka mpakani mwa nchi jirani ya Kenya na Tanzania, kwa hiyo, naelewa umuhimu wa Jeshi letu. Hongera JWTZ na Mungu awabariki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, mimi ningependa kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hakuna kitu kinachoshangaza kama wimbi la Wakimbizi wa Kisomali na wengine ambao wanaingia humu nchini kwa njia za panya, huku Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama vikiwepo na vinaangalia usalama wa nchi yetu kutoka kila kona. Tatizo la wageni wazamiaji kutoka Somalia ni vyema liendelee kudhibitiwa na ifikie mahala watu au wageni hawa kutoka Somalia na maeneo mengine wasiingie kabisa humu nchini kupitia milango ya panya.

Mheshimiwa Spika, afadhali Mafunzo ya JKT sasa yarejeshwe, yatawafundisha vijana wetu uzalendo na kuipenda nchi yao, uwajibikaji mahala pa kazi, nidhamu, upendo, ukakamavu na kufanya kazi kwa

bidii. Enzi za zamani ni tofauti kabisa na sasa hivi, kwani vijana wa sasa hivi wamepoteza hivyo vyote nilivyovitaja hapo juu na ndiyo maana ufanisi wa kazi umepungua na matokeo yake ndiyo migomo na vurugu mbalimbali mahali na sehemu mbalimbali za kazi. Muda wa kwenda JKT urudishwe kama mwanzo kipindi cha mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi wanaofanya kazi au kuajiriwa katika kampuni binafsi za ulinzi hapa nchini wanalalamika kwamba hawalipwi vizuri kulingana na kazi wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, Walinzi wa Makampuni mbalimbali waliniletea hoja zao niziwasilishe hapa Bungeni wakati wa kusomwa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Walinzi hawa ambao wameajiriwa na makampuni binafsi ya ulinzi, wanaiomba Wizara au Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kuwasaidia kuyapitia maslahi na stahiki zao mbalimbali ili haki itendeke kwani wanachopata kwa sasa hakilingani na kazi wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nafasi za kujinga na JKT zitolewe *equally* kwenye Wilaya zote.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, namshukuru Mungu, kwa kunipa afya ya akili na ya kiwiliwili na kuweza kuchangia Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa mchango wangu, napenda nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Amiri Jeshi Mkuu, Raisi wetu mpendwa, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete (*Colonel* Mstaafu), kwa juhudi yake ya kuiongoza nchi katika misingi ya amani na utulivu wa kweli.

Napenda nimpongeze pia kwa kusimamia kwa umahiri mkubwa uanzishwaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa kule Zanzibar. Kwa kutekelezeka hilo, Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010 hasa kule Zanzibar ulifanyika *smoothly,* bila vitisho wala mikwaruzo yoyote; ni hatua nzuri, ya kizalendo na ya kidemokrasia.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zinazofanywa na Jeshi letu katika ulinzi wa nchi yetu, kuna haja kwa Serikali kuzithamini juhudi hizi li kuimarisha juhudi za Jeshi letu.

Mheshimiwa Spika, Kamandi ya Wanamaji inahitaji kuimarishwa hasa kwa ulimwengu huu wa utandawazi na uharamia. Kuimarisha Kamandi hii kutasaidia sana kuokoa rasilimali zetu za baharini zisiibiwe kiholela. Kwenye Bahari zetu Kuu kuna utajiri mkubwa ambao kama tukiulinda, utaimarisha kuinua uchumi wetu kwa kuongeza Pato la Taifa, kwa zaidi ya asilima sita. Hiki ni kiwango kikubwa, ni lazima kilindwe ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ni budi sasa kumaliza mizozo na mivutano baina ya Jeshi letu na Wananchi wetu. Jeshi ni muhimu kwa kuilinda nchi yetu na Wananchi ni muhimu pia ambao ndiyo nchi yenyewe, kwani nchi bila ya Wananchi siyo nchi?

Mheshimiwa Spika, JKT ni Sera nzuri kuirudisha kwa madhumuni yaliyokusudiwa. Ushauri wangu ni kuwa, Vijana na Wazee tukiwemo sisi Wabunge ambao watajiunga na Jeshi hilo, wapatiwe mafunzo stahiki kulingana na wakati tulionao na isiwe kuwatesa vijana hao kwa njaa na adhabu kali ambazo zitapelekea vijana kuchukia kujiunga na Jeshi hilo.

Mheshimiwa Spika, ni fahari kwa nchi yetu kushiriki kulinda amani sehemu nyingi Duniani na kuongoza Vikosi hivyo. Ni budi fahari hii tuidumishe kwa kuongeza demokrasia katika nchi yetu ili Jeshi liwe la Wananchi kama jina lake lilivyo.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kuwasilisha.

**MHE. LOLESIA J. M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa Hotuba nzuri. Hotuba imezungumzia mambo muhimu sana kwa ajili ya ulinzi na ustawi wa nchi yetu kwa ujumla. Mimi ningependa kuongelea kipengele kinachohusu ustawi wa maslahi ya Wanajeshi. Katika Bajeti ya Mwaka 2011/2012, mishahara ya askari iliongezeka na posho iliongezeka hadi kufikia shilingi 7,500. Kutokana na kazi kubwa wanayofanya Wanajeshi ni kwamba, hawana muda wa kufanya mambo mengine kwa ajili ya kuingiza kipato cha familia zao. Kwa sababu ya unyeti wa kazi zao, ninapendekeza posho zao ziongezeke kutoka shilingi 7,500 hadi kufikia shilingi 10,000 ili angalau ziwasaidie katika kumudu hali ya kimaisha.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni nyumba wanazoishi, kweli hazipo katika hadhi inyotakiwa. Naiomba Serikali ijitahidi kukarabati nyumba za Wanajeshi angalau ziwe katika hali nzuri. Wale Wanajeshi waishio uraiani, Serikali iweke utaratibu mzuri wa kuwawezesha ili wapate fedha za kupanga.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa mafunzo ya Vijana JKT ni muhimu sana kwa ustawi wa Taifa letu; kwanza, wanajifunza uzalendo, moyo wa utaifa, ukakamavu na pia wanapata mafunzo ya stadi za kazi katika Vyuo vya Ufundi, jambo ambalo linamsaidia kijana huyu kujitegemea kwa kujiajiri kutokana na ujuzi alioupata. Idadi ya vijana kwa mwaka wanaopata nafasi hizi za JKT ni wachache sana ikilinganishwa na idadi ya vijana wetu wanaohitimu Kidato cha Nne.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iongeze Bajeti Wizara ya Ulinzi hasa katika mafunzo ya Vijana JKT ili tuongeze vijana wengi zaidi kuliko hivi sasa. Hivi sasa vijana wengi wanamaliza sekondari bila ujuzi na kwa kupitia JKT, vijana wengi watapata ufundi na ujuzi utakaowasaidia kuboresha maisha ya vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni suala la Wanajeshi waliopigana Vita ya Iddi Amini, ninaomba wafikiriwe na Serikali iwajali, wanaishi maisha duni sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mola kwa kuniweka salama hadi siku hii. Pia nampongeza Waziri

wa Wizara pamoja na jopo lake lote lililotayarisha bajeti. Bajeti ni nzuri yenye kuleta matumaini mema. Napenda kukiri kwamba kazi ya Ulinzi ni kazi ngumu na ambayo inahitaji ushirikiano na wananchi kwa ujumla. Miongozo ni mizuri ila watendaji baadhi yao hutumia madaraka yao kinyume na utaratibu kama kuwatisha raia pale wanapokuta raia ambao labda wanawakuta katika mazingira yasiyo ya kawaida, kama wagomvi, walevi au wahalifu. Baada ya kufuata sheria na utaratibu mzuri au kuwaelekeza katika njia ya haki, wao huchukua hatua ya kuwatisha na kuwatoa chochote kwa manufaa binafsi.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Mgambo, hawa pamoja na mafunzo ya miezi mitatu hasa vijijini huwa hawatumiki ipasavyo kwa kuwa baada ya kumaliza mafunzo, ni baadhi tu ambao wanatumika na kupewa posho kama vile kuna vizuizi vya mazao vijijini au vya Maliasili hawa wabakio huona hakuna faida na kufanya wengine walio bado kupata mafunzo hayo kutothamini. Badala yake huwasaka wauza gongo na kuwatoza fedha na kujinufaisha kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya JKT yanapotolewa matangazo ili vijana kutuma maombi. Mara nyingi baadhi ya viongozi hutoa nafasi hizo kwa rushwa pamoja na baadhi ya viongozi husika huchukua vijana kutoka makwao (ndugu) badala ya wazawa wa maeneo husika. Naomba Wizara ione umuhimu wa kufuata taratibu za kuwapata waombaji na walengwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara ihakikishe walinzi walindao sehemu, licha ya sehemu za Serikali iwe

pamoja na sehemu za watu binafsi kwamba wawekwe walinzi wenye elimu ya ulinzi na wawe na silaha za ulinzi. Maana baadhi ya matajiri huweka mahotelini, madukani, katika mashamba makubwa na kadhalika. Walinzi wasio na silaha na kupelekea kuuawa na majambazi kwa kukwepa malipo ya kisheria.

**MHE. NAOMI M. KAIHULA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kuwa na afya njema na kuniwezesha kuchangia hotuba hii muhimu sana kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, hotuba katika maandishi ni nzuri, tatizo tu kubwa ni katika utekelezaji wake na upatikanaji wa fedha za kuiwezesha bajeti hii ifanikiwe. Nasaha zangu ni kuiomba Serikali ijitahidi kuipa fedha Wizara hii kwani nafikiri hii ni mmoja ya vipaumbele vya Serikali, kwani Wizara hii ikitumiwa vema katika Kilimo ita–*support* vizuri dhana ya Kilimo Kwanza na Viwanda na Biashara. Hivyo kuwa Jeshi la Ukombozi kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwingine ni kwamba Jeshi la Kujenga Taifa likiongozwa vema, litaweza kutoa msaada wa haraka kwa masuala mengine yanayoikabili nchi hii, kwa mfano, kutumia vijana hawa katika kuboresha elimu kwa njia ya kutumika kufundisha Elimu ya Watu Wazima, kusoma na kuandika.  Pia kupunguza mzigo wa walimu mashuleni kwa kuwatumia kuziba mianya ya upungufu wa walimu. Sio hivyo tu bali pia wanaweza kusaidia katika kutoa huduma muhimu kama vile afya, ujenzi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Wanajeshi wanaweza pia kutumika katika kunusuru mazingira kama vile kupanda miti na kustawisha misitu katika maeneo makubwa ya nchi yetu ambayo yanaletea kuifanya nchi yetu jangwa.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Akiba ni muhimu sana kwa shughuli nyingi zinazohitaji huduma lakini inashindikana kutokana na ukosefu wa watendaji *(manpower)*.

Mheshimiwa Spika, inawezekana kabisa kutekeleza mambo makubwa sana ili mradi Serikali ijitahidi kuwapatia vifaa vya msingi vya kazi katika shughuli zake.

Mheshimiwa Spika,ahsante na naomba kuwasilisha.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na Timu yake kwa hotuba nzuri iliyo na matumaini kwa Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kurudisha tena utaratibu wa JKT kwa vijana, lakini natoa rai yangu kuwa idadi na kasi ya *enrolment* vijana haitoshi ukilinganisha na miaka ya 1970 na 1980, kipindi hicho *camps* zote hapa nchini zilijaa vijana waliomaliza vyuo, shule na hata wafanyakazi. Hii ilipelekea wananchi kuwa wakakamavu na walinzi wazuri wa nchi. Kutokana na mafunzo yaliyotolewa wakati huo kwenye makambi yalipelekea vijana kujiajiri

wenyewe katika kilimo, ufugaji, useremala, biashara mbalimbali na kadhalika. Hivyo ni vizuri Wizara ikasimamia *enrolment* ya vijana na wafanyakazi katika kambi zetu.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya Magambo yangefutwa ili wote wanaoshiriki mafunzo ya Mgambo waweze kujiunga na JKT ili wanufaike zaidi.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru wakulima wa Mkoa wa Rukwa ambao wamekuwa mstari wa mbele kwa kuzalisha kwa wingi mahindi na kulisha nchi hii. Wakulima hawa wamekuwa wakitumia makasia (ng'ombe), lakini sasa hebu tuangalie bei ya matrekta na vifaa (vipuri) vya matrekta hayo ya SUMA JKT bei hizo zishuke ili wakulima hawa waweze kununua na waongeze kiasi cha uzalishaji ili kuinua uchumi wao.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Wizara kupitia maeneo yote na kukagua vifaa vyake ili kuzuia milipuko ambayo huacha uharibifu mkubwa kwa makazi ya watu yaliyo jirani na maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA ANDREW CLEMENT:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara pamoja na Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa kuweza kuweka hali ya amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iangalie sana suala la kambi zetu pamoja na nyumba za makazi ya askari zilizopo Ubago Zanzibar zifanyiwe ukarabati

kwani kambi hiyo na nyumba ziko katika hali mbaya sana ya uchakavu.

Mheshimiwa Spika, Jeshi limekubali kuwapatia wastaafu pensheni zao kila baada ya miezi mitatu na pensheni hizo kuwafuata katika mikoa yao, lakini naiomba Serikali ilitazame kwa huruma wastaafu hao waongezewe kutokana na hali ya maisha.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kuteuliwa na Rais kuongoza Wizara hii nyeti. Nampongeza Mkuu wa Majeshi *General* Mwamnyange na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri ya kuongoza Jeshi letu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumekuwa na matukio ya kutisha ya wananchi wasio na hatia kufa kwa milipuko ya mabomu katika Mkoa wa Dar es Salaam. Mpaka sasa Serikali haijasema chanzo cha milipuko hiyo na bado Serikali haijawahakikishia wananchi kwamba matukio kama haya hayatajirudia tena. Wananchi hatujajua kwamba ni hujuma zilizofanyika au ni nini? Naomba majibu ili Watanzania wanaoishi karibu na Kambi za Jeshi waendelee kuishi kwa amani.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kurudisha Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), lianze mara moja kwa kuwachukua vijana kama Serikali ilivyoahidi.

Swali langu, vijana watakaochukuliwa kujiunga na JKT. Je, ni wale wahitimu wa mwaka huu wa fedha au watachukuliwa ambao walihitimu miaka ya nyuma, lakini hawakupata nafasi ya kujiunga na JKT. Hata hivyo vijana 5000 tu ni wachache mno. Serikali itafakari.

Mheshimiwa Spika, naishauri badala ya kuwaacha vijana wanaomaliza kidato cha nne na kukosa nafasi ya kuendelea kidato cha tano na wale wanao maliza kidato cha sita na kukosa nafasi ya kuendelea na vyuo vikuu wachukuliwe na JKT kwa mujibu wa sheria badala ya kuwaacha wakizagaa mitaani bila kazi maalum.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni Wizara nyeti sana katika Taifa letu. Ni vizuri Wizara hii ikatengewa fedha za kutosha kwa ajili ya Ulinzi wa Taifa letu. Sioni sababu ya Hazina kuchelewa kupeleka fedha katika Wizara hii wakati wanajua umuhimu wa Wizara ya Ulinzi. Naiomba Serikali kuhakikisha kuwa Wizara ya Ulinzi inapata fedha za bajeti kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Wanajeshi hustaafu kufuatana na vyeo vyao. Wengine hustaafu wangali na nguvu zao na ujuzi mbalimbali wa kuweza kulitumikia Taifa hili. Kwa nini wanajeshi hao wasitumike kwa namna nyingine alimradi bado wana uwezo wa kulitumikia

Taifa. Wengi wao wako mitaani wakiwa na ujuzi mkubwa bila kazi maalum kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa ulinzi madhubuti wa Taifa, naishauri Serikali kuendelea kutoa mafunzo ya kisasa kwa Jeshi letu ili tuwe na Jeshi madhubuti na lenye silaha za kisasa. Nalipongeza Jeshi letu kwa ulinzi madhubuti pamoja na mapungufu yanayojitokeza kutokana na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. CHARLES J.P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuchangia bajeti hii kwa njia ya maandishi. Nalipongeza Jeshi kwa kupandisha daraja Hospital ya Lugalo na kuwa Hospital ya Rufaa. Pamoja na mahitaji ya kusambaza aina hii ya hospitali nchi nzima, ninao ushauri kwa Serikali, kupitia Jeshi iwaandae vijana wenye sifa za kusomea fani ya udaktari na tiba vijana hawa wapewe mafunzo ya Jeshi na mafunzo hayo. Hawa watakuwa ni wanajeshi, hivyo uadilifu na utiifu kwa Taifa utakuwa mkubwa sana. Kwa usalama wa Taifa letu sekta nyeti sasa lazima zitawaliwe na vijana walioandaliwa vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, nitoe mchango wangu kuhusu tatizo la mipaka ya Jeshi na Wananchi. Kambi ya Jeshi Kaboya ipo katika Jimbo langu la Muleba Kaskazini. Mimi kama Mbunge na mwananchi naunga mkono kuwepo Jeshi na zaidi kuwa na Kambi Mkoani Kagera. Tatizo hapa ni kuwa mipaka haiko wazi. Tunaishauri Serikali kwa kupitia Wizara ya Ulinzi na ile ya

Ardhi watuwekee mipaka ili tuishi kwa ushirikiano kama ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Spika, nichangie kuhusu nafasi ya Jeshi katika kujenga uchumi hasa kupitia sekta ya kilimo. Nashauri vijana watakaojiunga JKT hasa wale *voluntary*, wafundishwe kwa kina fani ya kilimo. Wakiwa na ujuzi vijana hawa wapewe zana na kuanzisha vituo vya kilimo katika sehemu mbalimbali za nchi. Hawa watasaidia wananchi hasa vijana kufungua mashamba na kuyaendesha katika hatua za mwanzo sambamba na njia hii. Nashauri utaratibu wa sasa wa Jeshi kuuza zana za kilimo upitiwe upya. Kwanza Jeshi litumie mtandao wake kuuza zana hizi badala ya Mawakala. Gawio linalobaki kwa Mawakala lingekuwa punguzo kwa mkulima na mnunuzi au kwa pato au faida ya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, naomba nishauri Serikali juu ya suala la usalama wa nchi na watu wake. Jeshi la Wananchi wanafanyakazi na vyombo washirika ambao kwa pamoja wanahakikisha amani na usalama vinashauri washirika wa Jeshi la Wananchi ni pamoja na Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Usalama wa Taifa na Mgambo. Ni busara kuwa katika kutimiza lengo letu wote inapotokea mmoja wa washirika hao ameshindwa au kuelemewa ni mategemeo kuwa moja ya washirika hao au wote watamsaidia.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu hapa ni kuwa Jeshi la Polisi limeshindwa kudhibiti majambazi wanaoendesha shughuli zao katika sehemu nyingi za nchi hasa Kagera, Geita, Kigoma, Shinyanga na

Tabora. Hawa si majambazi kimsingi ni wanajeshi ambao wametoroka toka katika nchi zao. Wanatumia silaha za kivita, wamejenga kambi katika misitu ya hifadhi na wanaendesha shughuli zao kwa kupora na kupeleka mali kwenye nchi walizotokea.

Mheshimiwa Spika, kwanza nashauri Serikali itumie Majeshi yake yote yakiongozwa na Jeshi la Wananchi kufagia watu hawa. Pili Serikali ifuatilie kwa kina nguvu nyuma ya makundi haya kwani kuna madai kuwa baadhi ya mikono ya waasi toka nchi jirani wengine wanatumiwa na mamlaka ya nchi watokazo hasa wale ambao pamoja na ujambazi wanajihusisha na uchungaji wa mifugo ya ng'ombe kwa makundi makubwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho nishauri Serikali kurejea utaratibu wake wa zamani wa kutumia Jeshi kuboresha na kuendeleza michezo. Michezo kwa mapana yake ina mchango mkubwa katika maendeleo na ustawi wa Taifa. Hivyo, naomba Jeshi la Mwananchi na hasa JKT pamoja na majukumu mengine wasaidie kuibua na kuendeleza vipaji vya mchezo.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kulipongeza Jeshi letu la Ulinzi na Taifa letu. Pamoja na shukrani hizo kuna mambo madogo madogo ambayo Jeshi letu halina budi kurekebisha.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri ya SUMA JKT, lakini tabia ya kutolipa madeni raia wake haifai kuvumiliwa. Mfano ni Kampuni ya *Millenium Express*

*Company Limited*, imekuwa ikiidai malipo ya kiasi cha shilingi 194,718,000/= baada ya kazi waliowafanyia. Baada ya juhudi za madai hayo kushindwa, wadai waliamua kwenda Mahakamani ambako kesi namba 138/2010, hukumu ilitolewa na kuamuru *TAKOPA* ilipe Kampuni ya *Millenium Express Company Limited*. Cha kushangaza mpaka sasa SUMA wameshindwa kulipa?

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri anipe majibu ya kina ni lini *Company* hii italipa hasa ikizingatiwa kuwa Mahakama imewasilisha malipo yafanyike? Pale walipojaribu kuchukua mali kwa nguvu kwa kutumia madalali, Jeshi limetumia mabavu kuzuia utekelezaji wa aina hiyo.

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara hii kwa kazi nzuri inayofanywa licha ya kuwepo dosari za hapa na pale. Naomba wakati wa majumuisho Mheshimiwa Waziri atoe maelezo ya kina juu ya mambo muhimu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi yapata miaka minne sasa tangu JWTZ kutoka Mwanza walipovamia ardhi ya wananchi wa Kijiji cha Bunere Jimbo la Mwibara, Wilaya ya Bunda, Mkoa wa Mara. Eneo lililovamiwa liko katikati ya kijiji hicho na limefanywa kuwa eneo la kufanyia mazoezi ya kivita kitendo ambacho kimesababisha wananchi wakose mahali pa kulima. Aidha, ardhi yenye mgogoro ninaouzungumzia hapa hautokani hata kidogo na aina ya migogoro iliyobainishwa na Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ukurasa wa 29 ambapo migogoro

hiyo itashughulikiwa na kikosi kazi atachokiunda. Naomba nipate maelezo ni lini Jeshi litaachia ardhi ya wananchi hao? Suala hili nimelisemea sana humu ndani katika maswali na hotuba, lipatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, SUMA JKT, dhana ya kilimo kwanza ndani ya ukopeshaji na uuzaji wa matrekta haujaweza kuwa na tija ya kuridhisha. Asilimia kubwa ya wakulima nchini wako vijijini na kipato chao ni kidogo na hawana mali ya kuweka kama dhamana kukopa trekta au fedha za kumiliki trekta. Hata kama bei ya matrekta itashushwa kama ilivyoshushwa hata kama *down payment* itapunguzwa kiasi gani bado wananchi wa kawaida vijijini hawatamudu kukopa matrekta haya, hivyo, yataendelea kukaa yadi kama yalivyo hapa Dodoma.

Naishauri SUMA JKT, kwa vile wana utaalam, zana hasa haya matrekta na wale vijana wanaojitolea miaka mitatu JKT waingie ubia wa mfumo wa *PPP* na wananchi wenye ardhi nzuri mabondeni ili wazalishe chakula kwa wingi. Njia hii ndiyo itatafsiri dhana ya Kilimo Kwanza kwa wananchi vijijini. Kwa mfano, Bonde la Ziwa Victoria ambalo wanaweza kuingia ubia na wananchi kwa mfumo wa *PPP* ni ardhi nzuri iliyoko kandokando ya Ziwa Victoria Jimbo la Mwibara katika Vijiji vya Buzimbwe, Bulamba, Kabainja, Kamkekere, Muranda, Namhula, Bulandabufwe, Nasimo na Kisonya. Naomba nipate majibu juu ya ushauri huu.

Mheshimiwa Spika, pensheni kwa Wanajeshi Wastaafu. Kumekuwa na wastaafu wengi ambao hawapati pensheni zao kwa wakati na hivyo

kusababisha waishi maisha magumu sana na wengine kulazimika kufanya kazi ya ulinzi kwa watu binafsi naomba kuwe na ufuatiliaji maalum wa Wizara kule Hazina.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Ulinzi na JKT Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara hii muhimu. Nawapongeza kwa dhati Viongozi na Watendaji Wakuu wa Wizara JWTZ na JKT kwa kazi nzuri wanayofanya kutekeleza Sera na Sheria za Ulinzi wa Taifa na Malezi ya Vijana.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara na Jeshi la Ulinzi na JKT kwa kutekeleza kwa vitendo Sera ya kujitegemea kwa kufanya utafiti na kutekeleza matokeo ya utafiti huo. Nalipongeza sana Shirika la Nyumba kwa kuendelea kutengeneza baadhi ya zana za ulinzi hapa nchini. Hata hivyo, nimefuatilia na kudhani kuwa sehemu kubwa ya silaha zinazouzwa kwenye maduka ya shirika zinaagizwa toka nje ya nchi. Nashauri kuwa shirika lijiimarishe zaidi kwa kutengeneza zana hizo kupitia ushirikiano na wawekezaji binafsi.

Mheshimiwa Spika, JKT linamiliki mashamba makubwa sana maeneo mbalimbali ikiwemo Ruvu. Sehemu kubwa ya maeneo haya hayatumiki ipasavyo *(efficient utilisation*), nashauri kuwa Jeshi liangalie uwezekano wa kuwekeza kuendeleza maeneo hayo ikibidi kupitia ubia ili kuongeza uzalishaji wa chakula nchini.

Mheshimiwa Spika, maslahi ya Wanajeshi, kwa maoni yangu posho inayolipwa wanajeshi haitoshi kwa kuzingatia mazingira wanayofanyia kazi. Ili kuwaepusha na vishawishi nashauri kuwa posho iongezwe angalau ifikie shilingi 15,000 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nyumba kwa ajili ya wanajeshi, nawapongeza sana viongozi wa Wizara JWTZ na JKT kwa kubuni mpango mkakati wa kuwezesha wanajeshi kupata nyumba za kuishi vikosini. Kwa kuzingatia uzoefu kwa wanajeshi wengi kupata tabu ya makazi baada ya kustaafu kwani wengi hustaafu bila ya kuwa na nyumba za kuishi na kutumia pensheni yao kujenga nyumba. Nashauri kuwa Wizara iandae utaratibu utakaowezesha maafisa na askari kupatiwa mikopo ili wajenge au kununua nyumba na hivyo wanapostaafu waishi maisha mazuri pasipo usumbufu. Ikiwezekana JWTZ ishirikiane na *NHC* kuandaa na kutekeleza mpango mkakati wa kuwapatia wanajeshi nyumba za kuishi baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi baina ya Jeshi na wananchi, mwaka 1984 Serikali ilihamisha wananchi wa Kijiji cha Oldonyosamba, Wilayani Arumeru ili kupisha uanzishaji wa Anga. Tokea JWTZ kukabidhiwa ardhi hiyo wamekuwa wakitumia kujipatia fedha kwa kuwakodisha wananchi hao hao walionyang'anywa ardhi bila fidia ya ardhi mbadala kama ilivyoahidiwa. Je, kama JWTZ ilikabidhiwa ardhi ambayo haihitaji kwa kuzingatia majukumu ya kikosi hicho kwa nini Wizara isifanye uhakiki wa mahitaji halisi na ardhi ya ziada irejeshwe kwa wamiliki wa awali? Vile

vile wanajeshi wamekuwa wakiruhusu uchimbaji wa mchanga kwenye vilima vilivyo kwenye eneo hilo na hivyo kusababisha uharibifu wa mazingirra.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa uamuzi iliyouchukua kupitia SUMAJKT kuagiza na kusambaza matrekta kwa wakulima nchini. Kwa maoni yangu, motisha iliyotolewa kwa wateja watakaonunua matrekta 50 au zaidi ya kulipa 15% ya malipo ya awali huenda ikanufaisha wafanyabiashara wakubwa ambao watanunua na kuhodhi ili wayauze baadaye kwa bei ya juu.

Mheshimiwa Spika, nashauri yafuatayo:-

(a) Motisha hiyo itolewe kwa watakaonunua matrekta 20; na

(b) Motisha hiyo itolewe kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimpongeze Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Naibu Waziri wake na Makamanda wote kwa kazi yao nzuri ya kulinda mipaka ya nchi yetu kwa umahiri mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, mie napenda nizungumzie kuhusu athari tuliyoipata wakati wa milipuko iliyotokea Mbagala na Gongolamboto, hivyo basi naishauri

Serikali iweke Ulinzi mkali kwenye maghala ya silaha. Kila baada ya muda kuwe na ukaguzi katika maghala haya ili isije ikatokea milipuko kama iliyoathiri wananchi kwa kupoteza maisha yao pamoja na kuwa na ulemavu na kuharibu mali na makazi yao. Jambo hili lililotokea katika nchi yetu, ni jambo ambalo limeacha kovu kubwa sana na haitosahaulika maisha. Serikali iimarishe na kukarabati maghala ya silaha ili hali hii isije ikatokea tena.

Mheshimiwa Spika, napenda nizungumzie kuhusu Hospitali ya Jeshi iliyopo katika kambi ya Jeshi ya Ali-Khamis *Camp* ya Wawi, Chake Chake, Pemba. Hospitali hii inatumika kwa familia za wanajeshi waliopo katika kambi hizi pamoja wananchi takribani wengi wanaoishi katika eneo jirani na kambi hii. Hivyo basi, naishauri Serikali iongeze madawa pamoja na vifaa vya maabara ili iendelee kuwa na ufanisi katika kuwasaidia wananchi hawa wanaoishi karibu na kambi hii.

Mheshimiwa Spika, hali ya Wanajeshi wetu mara tu wanapostaafu Jeshi, basi wanakuwa na hali mbaya sana ya maisha. Askari Jeshi hawa wastaafu wanalipwa fedha ndogo sana ya pensheni ambayo haitoshi kukidhi hali zao za maisha, mara nyingi wanajeshi wastaafu wanakuwa walinzi wa majumbani au madukani wakati wa usiku. Hii ni aibu kubwa kwa Jeshi letu na pia inadhalilisha sana taasisi muhimu sana. Hivyo, naiomba Serikali izingatie maslahi ya wanajeshi wetu hasa pale wanapostaafu ili iwasaidie kuendeleza maisha yao. Hawa wanajeshi wastaafu wameshafanya kazi kubwa ya kuilindia na kuijengea heshima kubwa

nchi yetu. Hivyo basi, Serikali ifikirie kuwasaidia hawa wanajeshi wastaafu.

**MHE. KOMBO KHAMISI KOMBO:** Mheshimiwa Spika, suala la sifa za mtu kuruhusiwa kujiunga na JWTZ linapaswa kuangaliwa upya na kwa usahihi unaofaa ili kuwatendea haki watu wote. Sifa zinazotakiwa ni pamoja na mtu awe raia wa Tanzania, awe na elimu ya kidato cha nne na kuendelea na awe amefaulu, awe hajaoa au kuolewa, awe na tabia na mwenendo mzuri, awe na umri kuanzia miaka 18 hadi 25, awe na akili timamu na afya nzuri.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kuoa au kuolewa inapaswa iondolewe kwani haina tija wala manufaa yoyote katika ujenzi wa Jeshi imara. Ifahamike kuwa kwa mujibu wa sheria za ndoa za Tanzania mtoto wa kike anaruhusiwa kuolewa hata akiwa na umri wa miaka 14 kwa ridhaa ya wazazi. Kwa mantiki hii inawezekana mtoto wa kike akahitimu darasa la saba na kuolewa, lakini baadae akapata fursa ya kujiendeleza hadi kidato ch nne au zaidi na kufaulu. Mtu huyu kama ana nia au upendeleo wa kujiunga na Jeshi kigezo hiki cha kuwa awe hajaoa na kuolewa itakuwa haijamtendea haki.

Mheshimiwa Spika, inawezekana pia akawa ameoa au ameolewa, lakini hajafunga ndoa na hivyo si rahisi kujulikana hasa kwa sababu haiko kimaandishi (vyeti vya ndoa havipo) mwanya huu unaruhusu ubaguzi kwani wale ambao wameoa lakini hawatajulikana wataingia Jeshini wakati wale waliooa

kihalali watakosa haki yao ya msingi kuingia pale wanapotaka.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kigezo hiki kibadilishwe kwani hata dunia na mifumo mbalimbali kwa sasa vinabadilika sana. Kuendelea kushikilia msimamo au baadhi ya mambo ni uhafidhina ambao hautaleta tija kwa Taifa letu.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono kwa dhati bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Naomba Serikali ihakikishe kuwa kila mwaka bajeti ya Wizara hii iwe inaongezwa hasa bajeti ya Maendeleo ili kulifanya Jeshi letu liwe linakwenda na wakati kwa kuwa na zana na vifaa vya kisasa.

Mheshimiwa Spika, Ulinzi wa Taifa lolote dunia liwe dogo au Taifa kubwa unategemea kwa kiwango kikubwa kuwepo kwa Majeshi ya kisasa na yenye weledi wa hali ya juu. Nafurahi kuona kwamba Serikali imeamua kulipatia Jeshi letu bajeti angalau inayoweza kuliwezesha Jeshi letu kutekeleza mipango yake ya maendeleo ikiwemo ununuzi wa zana na vifaa vya kijeshi vya kisasa zaidi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kukubali kuanzisha upya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT). Hatua ya Serikali ya kuanza hatua kwa hatua kwa kuanza na vijana wapatao 5,000. Hatua hii inastahili pongezi kwani kwa kuwa Jeshi la Kujenga Taifa linayo malengo ya kuwafundisha vijana mbinu mbalimbali za

Ulinzi, uzalishaji mali pamoja na kujenga uzalendo na umoja miongoni mwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Jeshi letu Jeshi la Ulinzi na Kujenga Taifa lina wajibu mkubwa wa kulinda mipaka ya nchi yetu. Jeshi letu limeonesha uwezo mkubwa katika kutekeleza majukumu yake pale liliposhiriki kikamilifu katika ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika. Jeshi letu lilishiriki kikamilifu katika kumwondoa Nduli Idd Amini Dada wa Uganda pale alipolivamia Taifa letu mwaka 1978. Jeshi letu limeshiriki kikamilifu katika operesheni mbalimbali za Kimataifa katika Lebanoni, Darfu Sudan, Comoro na kwingineko na kwa hakika askari wetu wamefanya kazi zenye kutukuka, narudi kulipongeza Jeshi letu kwa namna linavyoendelea kulinda mipaka yetu na Mataifa ya Jirani.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali iendelee kulijengea uwezo Taifa letu kwa kulipatia nyenzo na zana za kisasa pamoja na fedha za maendeleo katika mashirika yake ya Mzinga, Nyumbu na SUMA JKT.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa Watanzania hapa Wazalendo wa kutokuyatumia maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya vikosi vya majeshi ya nchi zetu. Tunahitaji Jeshi lenye nguvu na lenye weledi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ishughulikie mpaka kati ya Tanzania na Malawi haraka. Malawi wao wanaonesha kuwa mpaka upo ufukweni mwa Tanzania. Hii

inaonesha matendo yao katika uvuvi na mambo mengine. Jambo hili lishughulikiwe haraka maana likiachwa muda mrefu linaweza kuleta madhara makubwa sana kati ya nchi mbili hizi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iharakishe kuanzisha upya mpango wa vijana toka vyuoni kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria tabia za vijana wengi wa sasa haziendani na maadili ya Kitanzania na ni Jeshi hilo tu ambalo linaweza kurejesha maadili mema ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kutoa pongezi kwa Waziri, Makamanda wote wa vyombo vya Jeshi letu la Ulinzi na Usalama kwa kazi kubwa ya utekelezaji wa majukumu ya Ulinzi wa mipaka ya nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naiomba Serikali kushughulikia mgogoro uliojitokeza katika mpaka wa Malawi na Tanzania katika Ziwa Nyasa haraka na yamkini bila kujiingiza katika matumizi ya silaha pale patakapowezekana.

Mheshimiwa Spika, nalipongeza pia Shirika la SUMAJKT katika kuongeza kazi ya kusambaza matrekta kwa kupunguza masharti ya mikopo na kuwahusisha Wakuu wa Mikoa. Kwa kuwa kasi ya mauzo ya matreta hayo ni ndogo na hii itaathiri ulipaji wa mikopo hiyo ambayo Serikali huenda ikaishia hasara au faida kidogo hivi kuathiri mzunguko endelevu wa mikopo hiyo kwa ajili ya uwezeshaji na Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kupitia SUMAJKT kuangalia mbinu zaidi za kibiashara na usambazaji ili kuongeza mauzo ya matrekta haya ikiwamo kuwahusisha Halmashauri moja kwa moja badala ya Serikali za mikoa ambapo wakulima binafsi wadogo wadogo wapewe matrekta. Serikali isipoongeza mauzo ya matekta haya yanaweza kusababisha mkopo huu kwa Serikali kuishia katika hasara.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa imedaiwa kwamba, Serikali itadahili (*recruit)* vijana 20,000 kwa wakati mmoja katika JKT ambapo ni karibu 50% ya vijana wanaomaliza elimu ya kidato cha sita. Hii inasababishwa na changamoto na rasilimali fedha. Naishauri Serikali kurejea masharti kuwa idahili wale (vijana) wanaomaliza elimu ya shahada au stashahada badala ya kidato cha sita.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, nianze kabisa kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuleta hotuba nzuri ya bajeti katika Bunge letu. Vile vile naomba niipongeze Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kulinda Taifa letu na kuleta amani kwa nchi yetu. Hadi leo hii tunapoongea tuna uhakika mipaka ya nchi yetu ni salama na wananchi wanaishi kwa raha tupu! Hongera sana Majeshi yetu ya Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Kagera hasa Wilaya ya Karagwe iko mipakani mwa nchi za Rwanda, Burundi na Uganda na mipaka yetu ni mipana sana kiasi kwamba Ulinzi wa eneo hili unahitaji nguvu ya pekee sana kutoka Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa. Wilaya ya Karagwe tunayo maeneo makubwa na mazuri kwa ajili ya kufungua Kambi za JKT kwa ajili ya kilimo na uzalishaji mbalimbali mfano Kata ya Nyakakika, Kata ya Nyakasimbi, Kata ya Bweranyange, Kata ya Rugera na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lengo kubwa hasa liwe kuimarisha ulinzi katika mipaka ya nchi yetu dhidi ya majirani zetu wa Uganda, Rwanda na Burundi.

Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Serikali kuanzisha na kurudisha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria. Uamuzi huu ni wa busara na utasaidia kuleta uzalendo wa vijana wetu na kuongeza ukakamavu.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi bajeti ya Wizara zetu nyingi zimekuwa hazitoshi, napenda kutoa angalizo kwa Serikali ihakikishe bajeti ya Wizara hii inatosheleza mahitaji na inatolewa kwa wakati na yote bila ya visingizio vyovyote. Kwani kutofanya hivyo ni hatari sana kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Kambi nyingi za Jeshi la Wananchi wa Tanzania ziko kwenye maeneo ya makazi ya watu, mfano, Kambi ya Jeshi iliyopo Ubungo Kibangu Dar es Salaam; Kambi ya Jeshi la Lugalo; Kambi ya Jeshi la Gongolamboto na kadhalika. Makambi haya wakati yanajengwa yalikuwa mbali na

makazi ya watu, lakini kutokana na uhaba wa ardhi na mipango miji mibovu, wananchi wamejenga kuzunguka makambi haya na hivyo Kambi za Jeshi kujikuta zinazingirwa na makazi ya watu. Ili kuepukana na matukio ya milipuko ya mabomu kama yale ya Mbagala na Gongolamboto, nashauri maeneo ya Kambi yahamishwe na maeneo mbadala yatafutwe haraka.

Mheshimiwa Spika, vyeo vya maaskari wetu vitolewe kwa wakati na bila ya upendeleo wowote.

Mheshimiwa Spika, majengo ya Wanajeshi wetu ni muhimu ili kuwaweka wanajeshi mahali pamoja kambini. Vile vile mishahara na marupurupu (motisha) itolewe kwa wanajeshi wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa mstari wa mbele katika kushirikiana na nchi nyingine duniani kudumisha amani. *Operation* ambazo zimekuwa zinaongozwa na Umoja wa Mataifa katika nchi zenye mgogoro. Licha ya kazi nzuri ambayo inafanywa na Jeshi letu, kumekuwa na malalamiko hususani kutoka kwa askari wetu. Wanafanya kazi za kulinda amani Darfur- Sudan. Askari hawa wamekuwa wakilalamikia mapunjo ya stahiki za malipo yao, pia pesa za kujikimu. Kwa hali ilivyo inaonekana kuna sintofahamu nyingi juu ya mkataba wa kazi kwa vijana wetu na malipo halali wanayostahili kulipwa kutokana na mkataba husika kutokuwekwa wazi kwao.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa malalamiko toka kwa vijana wetu wanaofanya kazi ngumu ni busara Mheshimiwa Waziri akalielezea Bunge hili Tukufu. Askari wanaolinda amani katika nchi zenye migogoro maslahi yao ni yapi na kwa kiwango gani? Kiwango gani kinabaki Serikalini na kiwango gani ni stahiki ya wanajeshi husika.

Mheshimiwa Spika, kama Mbunge wa Jimbo la Kawe, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa hatua iliyochukuliwa na Wizara yako katika kutatua mgogoro wa ardhi baina ya Jeshi na wananchi katika eneo la Kunduchi Mtongani. Hatua ambayo ilipelekea kutengenezwa mipaka mipya ambayo iliwatambua wananchi waliokuwa wamejenga nyumba zao ndani ya lililokuwa eneo la Jeshi. Ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mpaka mpya haujazijumuisha nyumba zisizozidi kumi ambazo zilikuwa sehemu ya mapendekezo ya awali ya Kamati ya Wananchi wa Kamati ya Jeshi, hali ambayo imepelekea mfadhaiko mkubwa sana miongoni mwa wananchi hao ambao wengine ni wajane na wastaafu na ambao kuvunjwa kwa nyumba zao ni kuwamaliza kabisa kimaisha.

Mheshimiwa Spika, uhai wa wananchi hawa unategemea sana busara na huruma ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi. Kwa mchango huu naiomba Wizara yako iliangalie hili suala kwa jicho la huruma kwani inahusisha sehemu ndogo tu.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika kumekuwa na malalamiko pia toka kwa wanajeshi kupewa shilingi 7500 tu kwa siku kwa matumizi ya chakula wakati gharama za maisha zimepanda. Nini kauli ya Serikali kuhusiana na lalamiko hilo na kama kuna mpango wowote wa kuongeza kiasi husika ili kuendana na gharama za sasa za maisha.

Mheshimiwa Spika, Wanajeshi wastaafu (Jeshi la Akiba) nao wamekuwa wakiishi katika mazingira magumu na ya kifukara sana. Kutokana na kulipwa pensheni hafifu na duni. Pia kwa nyakati tofauti wastaafu hewa, wamekuwa wakiomba nyongeza ya pensheni husika iweze kuendana na hali ya sasa ya maisha au kulingana na wanajeshi wenzao wanaostaafu sasa kwa vyeo vile vile ambao wanajeshi hawa wastaafu walikuwa navyo wakati wanastaafu.

Mheshimiwa Spika, naomba kauli ya Serikali juu ya mustakabali wa kundi hili muhimu.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Timu yake ya Wataalam na hasa Makamanda wa Jeshi kwa kulinda mipaka ya nchi yetu kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, kwa muda mrefu nchi yetu iko katika hali ya utulivu na amani tangu wakati wa vita vya Iddi Amini 1978/1979. Hivyo ni muhimu kwa Serikali kuyafanya majeshi yetu kushiriki katika harakati za maendeleo ya uchumi wetu kwa mfano Jeshi lina ma-*engineer* wa aina mbalimbali,

*Civil, Mechanical, Chemical* na kadhalika. Wanajeshi wanaweza kushiriki katika ujenzi wa miundombinu kama barabara madaraja na kadhalika. Tusipowawezesha kuwa busy wanaweza kujiingiza katika mambo ambayo hayafai *an idle mind is the devils paradise,* naipongeza Serikali kwa kurudisha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana wetu. Siku zote naamini kwamba mafunzo ya kijeshi yanasaidia sana kujenga ukakamavu wa vijana wetu na pia kuwajengea nidhamu na uzalendo.

Mheshimiwa Spika, kipindi kirefu cha kutokuwa na mafunzo ya aina hii kimedhihirisha kuwa ni kipindi ambapo vijana wetu wamepoteza uzalendo, uadilifu na nidhamu. Naiomba Serikal iongeze bajeti katika eneo hili la mafunzo ili vijana wengi zaidi waweze kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa. Mpakani mwa Burundi na Tanzania sio shwari, Jeshi limeweka wanajeshi katika mipaka. Pia naipongeza Serikali kwa kupanga kutoa mafunzo ya Kijeshi kwa Wabunge vijana. Naamini mafunzo haya yatasaidia kuleta mabadiliko katika nidhamu ya Wabunge Vijana.

Mheshimiwa Spika, hali ya mpaka wa Tanzania na Burundi siyo shwari, Wilaya yangu ya Ngara inapakana na nchi mbili za Rwanda na Burundi. Mpaka wa Rwanda, Tanzania ni shwari sana lakini mpaka wa Tanzania na Burundi siyo shwari. Vyama vya Upinzani vya Burundi vina wanajeshi wake ambao wameingia misituni karibu na mpaka wa Tanzania na wanaendeleza mapambano dhidi ya Serikali ya Nkurunziza- Rais wa Burundi. Majambazi kutoka Burundi wamekuwa wakiwatupia mabomu wananchi wangu

(Watanzania ) wa Ngara. Pia Wilaya yangu ya Ngara inakabiliwa na Wahamiaji haramu ambao wamewawekea wananchi wangu mabomu ya majambazi wa kutoka Burundi yamewaua wananchi wanne katika Wilaya ya Ngara.

Mheshimiwa Spika, katika kumuenzi Baba wa Taifa ni muhimu kwa Serikali kuhakikisha shirika la Nyumbu linaendelea kustawi na kuimarika katika kutengeneza magari ya kivita kama lilivyokuwa likifanya wakati wa Serikali wa awamu ya kwanza ya Baba wa Taifa. Nyumbu ilikuwa ni wazo au ndoto ya Mwalimu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, je, katika hali ya usalama wa kikanda na kutokana na Tanzania kuwa mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na *SADC* kuna haja ya kuwa na Jeshi kubwa sana kiidadi ya wanajeshi au tunahitaji Jeshi dogo, lakini lenye zana za kisasa *highly mechanized*.

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Spika, madaraka makubwa katika Jeshi la Kujenga Taifa na Ulinzi (Mkuu wa Majeshi) tangu Uhuru na pia Muungano umeendelea kuegemea upande mmoja wa Muungano yaani Tanzania Bara. Jambo hili si jema sana kwa afya na uimara wa Muungano wetu ambao ni wa pekee duniani. Baada ya Muungano wafuatao ndio walioshika madaraka katika Jeshi letu. *General* Msh. Sarakikya (mstaafu) 1964- 1974; Hayati *General* A. Twalipo (Mstaafu) 1974- 1980; *General* D.B. Msuguri (Mstaafu) 1980- 1988; General E.M. Kiaro (Mstaafu) 1988- 1994; *General* R.P. Mboma (Mstaafu) 1994 – 2001;

*General* G.M. Waitara (Mstaafu) 2001- 2007 na General D.A. Mwamunyange 2007- hadi sasa.

Mheshimiwa Spika, ifike mahali uteuzi wa viongozi wakuu katika Jeshi letu la Muungano uzingatie sana suala la pande zote mbili ili kuepuka malalamiko yasiyo ya lazima kutoka upande mmoja ambao umetengwa.

Mheshimiwa Spika, inawezekana hili ni jambo moja tu kati ya mengi ambayo yanahitaji kuangaliwa upya hasa uteuzi unaojali pande zote mbili. Hivyo nahitimisha kwa kuitaka Serikali iwe makini sana katika masuala yote yanayohusu Muungano ili hatimaye tuwe na Muungano imara na thabiti.

**MHE. ASAA OTHMAN HAMAD:** Mheshimiwa Spika, baada ya kumshukuru Muumba *(Subhanah Wataala)* nakushukuru wewe kwa kuendesha vyema Bunge hili. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni chombo cha Muungano, hivyo kina dhima ya wingi wa mipaka yote ya nchi ikiwemo Tanzania Zanzibar. Kwa mantiki hiyo mbona inaonekana chombo hiki hakina taswira ya Muungano? Kwani kwa upande wa ajira kwa upande wa Zanzibar hasa Pemba vijana wa kisiwa hiki kamwe hawapewi ajira ndani ya Jeshi hili kama vile wao ni wageni ama ni jamii isiyostahiki kupewa ajira ya Jeshi la Ulinzi wa nchi yao waliyozaliwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri kwa kuwa yeye ni Mzanzibar na Mheshimiwa Rais kampa Wizara hii, mtu ambaye anaelewa, anatambua na ana uwezo mkubwa wa kuirekebisha hali hii, na ibakie kuwa ni historia. Mheshimiwa Waziri majibu yake juu ya suala hili

ni muhimu sana kwani Wapemba kwa sasa wanajiona kutengwa kwenye ajira ya chombo hiki. Halidhalika kuna fununu kuwa wale wanaopenya na kupata ajira ya chombo hicho ni wale tu ambao wazazi wao ni viongozi wa Chama Tawala (CCM) au Serikalini. Je, Mheshimiwa Waziri unasemaje juu ya jambo hili nyeti?

Mheshimiwa Spika, huoni kuwagawa wananchi wa nchi moja kwa maeneo yao wanayotoka asili ya wazazi wao na vyama vya kisiasa walivyokuwa wanachama wazazi wao au jamaa wa vijana hao, jambo hilo linakwenda kinyume na misingi ya haki za binadamu, haki za ajira na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ni mikakati ipi Mheshimiwa Waziri ameandaa ili wananchi wa Tanzania warejeshe imani, matumaini na upendo wa Jeshi lao kama ilivyokuwa miaka ya sabini.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa Vyama Vingi nchini ni maamuzi sahihi ya kikatiba yanapaswa kulindwa na kuheshimiwa ipasavyo. Hivyo basi, una kila sababu ya taratibu za pekee uzijengee na zitekelezwe na Wizara yako kwa lengo la kujenga umoja na upendo na mshikamano wa Watanzania bila ubaguzi wa aina yoyote. Kwa upande wa Zanzibar ajira hasa za ulinzi zinatawaliwa na usiasa zaidi kuliko vigezo na sifa za ajira yenyewe kutokana na mfumo mbovu wa kuwapata vijana watakaoajiriwa na Jeshi hilo kupitia Masheha wa Sheria wanazoishi.

Mheshimiwa Spika, Masheha hao wanawabagua vijana wetu kwa nyanja tofauti, jambo ambalo si jema

hata kidogo kuigwa nchini mwetu. Ni matumaini yangu kwake Mheshimiwa Waziri kuwa, jambo hili atalipa umuhimu wake na kulikomesha kabisa.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni ya Watanzania wote na kamwe si ya kundi fulani ndani ya nchi, au vijana ambao wazee wao ni kima fulani kimadaraka ya Serikali au Chama Tawala.

Mheshimiwa Spika, Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Afrika na Uwabariki Watanzania. Amina.

**MHE. JADDY SIMAI JADDY:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo hii kuhudhuria katika kikao hiki ambacho miongoni mwa mambo kadhaa yaliyopangwa kufanywa kwa siku hii ya leo pia kitatoa fursa ya kujadili na kupitisha bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu katika Wizara hii nitauelekeza katika kujadili hali mbaya ya miundombinu hususan ya kikazi yaliyopo katika makambi mengi ya Jeshi letu na hususan katika kambi ya Jeshi hii iliyopo katika Jimbo langu la Mkwajuni.

Mheshimiwa Spika, katika mojawapo ya vikao vya Bunge hapa Bungeni niliwahi kuwasilisha hoja ya hali mbaya ya miundombinu iliyopo katika kambi ya Potoa ambayo inafanya maaskari waliopo katika kambi hiyo kushindwa kutekeleza majukumu yao ya kazi kutokana na kukosa sehemu ya kuridhisha ya utekelezaji wa kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, majengo yaliyopo katika kambi hii ni chakavu mno kiasi cha kufanya maaskari hawa kuwa wanahama hama hasa wakati wa msimu wa mvua za masika.

Mheshimiwa Spika, nilipowasilisha hoja hii kwa Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii aliyekuwepo wakati ule ambapo niliiwasilisha kwa njia ya swali, nilijibiwa kwamba, mipango tayari imeshapangwa ya kukarabati miundombinu hiyo. Aidha, Waziri aliongeza kwamba kiasi cha shilingi milioni mia moja na tisa, zilishatengwa kwa kazi hiyo, hivyo namwomba Waziri atakapofanya majumuisho ya Wizara yake kutoa kauli thabiti ya kumthibitishia iwapo katika bajeti hii fungu hilo la kukarabati miundombinu si tu ya majengo ya ofisi za maaskari wetu bali pia na nyumba wanazoishi maaskari hao, yamezingatiwa katika bajeti yake hii, hususan kambi ya Potoa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na suala la miundombinu ya majengo ya maaskari, lakini pia lipo tatizo iwapo kama hakutochukuliwa hatua muafaka linaweza kusababisha madhara makubwa hapo baadaye katika jamii zetu hasa hasa jamii zile zinazoishi karibu na makambi ya Jeshi. Tatizo hili ni migogoro ya ardhi inayoendelea kati ya wanajeshi na raia wanaoishi karibu na kambi hizo.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa katika kambi ya Potoa kuna mgogoro mkubwa wa mpaka wa ardhi unaohusisha raia na maaskari wa kambi hiyo. Mgogoro huu kila kukicha unaendelea kukua na tayari suala hili

nilishaliwasilisha kwa Waziri na kuniahidi kwamba, binafsi angetafuta muda muafaka wa kutembelea kambi hiyo yeye na mimi ili kuweza kutathmini mgogoro huo na kuupatia ufumbuzi. Jambo ambalo hadi hivi sasa halijatekelezwa. Hivyo namwomba Waziri anipe maelezo kamili ni lini sasa safari hiyo ataifanya ili kutatua tatizo lililopo kwa kuwa siku ziendavyo ndivyo tatizo linavyoongezeka.

**MHE. MOZA ABEID SAIDY:** Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani kwa Serikali na Jeshi kwa ujumla kudumisha ulinzi na usalama wa nchi yetu. Tanzania ni nchi inayosifika kwa ulinzi wa mipaka na amani na utulivu kwani watu wake huwa wako huru na hufanya yale yote ya ujenzi wa Taifa kwa amani na usalama.

Mheshimiwa Spika, kwa makusudi ya dhati kuna watu hawaitakii mema nchi yetu kwa namna moja ama nyingine kwani haki haitafutwi kwa kulazimisha au kutumia nguvu. Napenda Mheshimiwa Waziri akija kuwasilisha majumuisho ya Wizara, aniambie ni lini Serikali itaona amani inaanza kutoweka taratibu na kuanza kudhihirika wazi kuwa kuna makusudi ya dhati ya kuichafua nchi kwa namna moja ama nyingine kwa kutolinda mipaka ya nchi na usalama. Kwa kuwa silaha zinatoka nje na kuingia nchini bila kujua na wakimbizi kuingia bila utaratibu na kufanya ongezeko la wahamiaji wasio halali kuongezeka. Je, Wizara ina wahakikishia nini wananchi wa Tanzania wenye kuanza kuwa na mashaka?

Mheshimiwa Spika, Serikali itambue amani hupatikana kwa mahitaji muhimu ya kimsingi na kuishi

kwa heshima, nchi ikitawalika kwa haki, sheria na usawa na mgawanyo wa rasilimali za nchi kwa faida ya wananchi wake wote.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Jeshi linafanya kazi katika mazingira magumu kwani vyombo vya Ulinzi na Usalama kulinda na kudumisha amani ni kazi ngumu zaidi katika nchi. Pia kuwalinda watu wasio na amani mioyoni mwao kukosa haki za msingi itakuja ilazimu Serikali kutafuta amani au kuirudisha amani. Pale panapokuwa na upendeleo wa utoaji wa ajira kwa Jeshi, kupendelea sehemu moja huleta manung'uniko kwa wananchi na kupoteza amani taratibu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie bajeti ya Wizara kwani haileti taswira nzuri ya utendaji kazi kwani Wizara hii inafanya kazi nyingi na ni ngumu ila iangalie sana sana mipaka ya nchi kwa macho mawili kwani tumeshuhudia matukio mengi yanayojitokeza yakiwa yameshamiri ndani ya nchi kama vile silaha kukamatwa, wakimbizi na wahamiaji haramu. Hii pia ni kuiongezea nchi mzigo wa wafungwa na kusababisha msongamano Magerezani. Hivyo, naishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kutoleta msongamano wa wahamiaji haramu kufugwa nchini petu kwa kutoangalia mipaka kwa umakini.

Mheshimiwa Spika, nilipongeze Jeshi kwa ukakamavu wake kwa kuwaajiri vijana na kuwawekea ukakamavu na kuwafundisha kazi na ujasiri, ila naomba kusiwepo na urasimu kwenye ajira hizo au mafunzo, vijana wachukuliwe kutoka katika kila eneo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Mheshimiwa Waziri akifanya majumuisho yake awaambie Watanzania lori lililobeba watu waliokuja kutupwa eneo la Dodoma hapa linahisiwa lilitoka Ethiopia, wamefikaje huku na wamepitaje maeneo ya mpakani mpaka kufika hapa tulipo? Je, ni kusudi au ni uzembe? Ahsante.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, napongeza wazo la Wizara kuanzisha JKT, lakini zaidi kushirikisha Wabunge Vijana. Naomba changamoto zifuatazo na zitazamwe.

Mheshimiwa Spika, mipaka ya nchi yetu hasa yenye maji kama Ziwa Nyasa na Tanganyika bado shida kubwa kwa upande wa Ziwa Tanganyika hasa eneo la Tarafa ya Wampembe, Wilayani Nkasi kumekuwa na matukio ya ujambazi ya kupora mali za wananchi katika vijiji vya Mpasa na Msamba.

Mheshimiwa Spika, matukio ya uhalifu huo yamekuwa yakijirudia rudia katika Vijiji hivyo vya Mpasa na Msamba na kumesababisha mamilioni kuporwa kutoka kwa wananchi. Kijiji cha Mpasa kimevamiwa zaidi ya mara nne na vilevile Msamba imevamiwa zaidi ya mara nne na wavamizi wanadhaniwa kutoka eneo la Kongo. Ili kudhibiti uporaji huu ningeshauri, pawepo na kikosi (kiteule) ili kushibiti eneo hili. Naomba tamko la Serikali katika suala la usalama la Tarafa ya Wampembe.

Mheshimiwa Spika, pamekuwepo upendeleo katika ajira za Jeshini. Maeneo yamekuwa yakigawiwa

nafasi, lakini wakubwa huwapeleka vijana wao na kufanya eneo lililotengewa wenyeji kutokupata nafasi ambazo zimetengwa kwa ajili ya Wilaya husika na Mikoa husika. Naomba tamko kukomesha jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kwa hakika bila kuwa na chombo cha usafiri cha uhakika katika Ziwa Tanganyika itakuwa vigumu kabisa kukabiliana na matatizo ya kiusalama katika Ziwa Tanganyika ambalo lina eneo kubwa la mpaka wa Magharibi.

Mheshimiwa Spika, Makazi ya Wanajeshi yaboreshwe, hali siyo nzuri, nashauri jitihada ziongezwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya vijana wa JKT, naipongeza Serikali ya Tanzania inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi kwa kuamua kwa makusudi ya kurejesha mafunzo ya vijana ya JKT. Aidha, katika hili naishauri Serikali iweke mikakati maalum na kuhakikisha kwamba mafunzo hayo hayafanywi kwa ubaguzi na vijana wote wanaohitaji mafunzo wapewe. Aidha, Serikali iwakusanye vijana wanaozurura mijini na kuwapeleka JKT na zoezi hili lifanywe kila mkoa.

Mheshimiwa Spika, kambi ya Jeshi la Mwanyanya, Zanzibar kihistoria ilikuwa kambi ya Makomandoo, lakini baadaye Serikali ikaigeuza kuwa kambi ya Jeshi kama zilivyo kambi nyingine. Sasa tokea kuwa kambi,

kumekuwa na upungufu mkubwa wa ukosefu wa maji, vitendea kazi muhimu, la kusikitisha zaidi kambi hiyo haijawekewa uzio ambao utawezesha kudhibiti eneo hilo na ukichukulia kwamba kambi hiyo iko vijijini. Aidha, naiomba Wizara ya Ulinzi kuchukua hatua za makusudi za kuyaboresha au kuyafanyia matengenezo kwa majengo na mabanda wanayoishi wanajeshi wetu, kwani ili utendaji uwe mzuri basi na makazi yawe mazuri.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kutuwekea Hospitali katika Kambi ya Jeshi la Bububu, Zanzibar, ambayo ni nzuri na inatoa huduma nzuri kwa wananchi wa Zanzibar na hasa wa eneo la Jimbo la Bububu. Hata hivyo, Hospitali hiyo imekosa vifaa muhimu vya kufanyia kazi vikiwemo *X-ray*, vifaa vya vipimo kwa akinamama. Aidha, hivi sasa kuna baadhi ya vifaa vimeanza kuharibika, hivyo, nashauri Jeshi kuanza utaratibu wa matengenezo ya vifaa hivyo kabla havijazidi kuharibika zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uajiri wa JWTZ na kadhalika, ni muda mrefu Serikali imekuwa na utaratibu wa kuwaajiri vijana kila muda unapofika lakini cha kusikitisha ni jinsi uajiri unavyofanywa wa JWTZ kule Zanzibar, huwa wanachukuliwa na kupimwa lakini wakifika Tanzania Bara wanapimwa tena na baadaye wanaambiwa *unfit* na wanarejeshwa Zanzibar na idadi kubwa wanaorejeshwa ni vijana wa Zanzibar. Nauliza ni kwa nini? Tokea mchakato huo uanze ni vijana wangapi wameajiriwa na wangapi wamerejeshwa hasa kwa Wazanzibar?

**MHE. JUMA OTHMANI ALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono bajeti ya Wizara ya Ulinzi kwa 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, naishauri Wizara na Jeshi wakati linapotoa ajira ni vyema likagawa nafasi kila Jimbo ili kuweka uwiano mzuri wa ajira kwa vijana wetu wa Tanzania. Nashauri huu utakuwa ni utaratibu mzuri kwani wasimamizi watakuwa ni Wakuu wa Wilaya.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, ili kuandaa vijana na watumishi wa umma kwa ujumla ni vyema sasa vijana wetu kabla ya kuanza kazi, wakapitia mafunzo ya JKT ili wapate mafunzo yatakayowafanya kuwa waadilifu na Wazalendo wa Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Rukwa tulikuwa na kituo cha Mafunzo ya JKT Luwa. Tunaomba kituo hicho kirejeshwe na hasa ikizingatiwa kuwa Mkoa huo unazalisha chakula kwa wingi, kituo kinaweza kutumika katika kutoa mafunzo ya kilimo bora kwa vijana wetu pamoja na kutumia nyenzo bora katika kilimo na ufugaji.

MheshimiwaSpika,matrekta yapelekwe karibu na wakulima ili kuwapunguzia usumbufu wa kuyafuata mbali. Hivyo, naomba Mkoa wa Rukwa nao uwe na kituo cha kuuzia matrekta kwani mkoa huu ni maarufu

sana kwa kuzalisha chakula kingi na wakulima wake wanajituma sana.

**MHE. WARIDE BAKARI JABU:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri wa bajeti ya Wizara yake.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa wanajeshi wetu kwa jinsi wanavyoweza kulinda nchi yetu na kutuongezea ulinzi na usalama ndani na nje ya mipaka yetu. Hii imedhihirika hasa pale walipoweza kuwakamata maharamia ndani ya Bahari yetu ya Mtwara. Vile vile kuhakikisha usalama katika Maziwa Makuu na kuwarudisha wapiganaji wa nchi jirani wanaotaka kuharibu nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naishari Serikali kuanzisha Mfuko wa Bima ya Afya kwa hiari kwa wanajeshi. Hii itawasaidia wakati wa kustaafu na pia itawasaidia kujitibu katika hospitali ya uraiani kwa hiari zao. Washauriwe kwa watakaokubali.

Mheshimiwa Spika, nashauri uharakishaji wa uanzishaji wa kambi ya JKT, Kagera kule mpakani kwani eneo tayari lipo limetengwa na hii itatusaidia kwenye ulinzi na usalama ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nashauri idadi ya wanafunzi wa JKT wanaoingia mwaka huu 5,000 kuwe na usawa kati ya wanawake na wanaume.

Mheshimiwa Spika, nashauri kule Jimboni kwetu Kiembe Samaki kuna kambi ya Chukwani kwa ajili ya

mafunzo. Eneo hili lipo karibu na wananchi, hivyo, eneo hili lirudishwe Serikalini wagawiwe wananchi waliokosa maeneo au wanaoundolewa kwa ajili ya utanuzi wa Uwanja wa Ndege, Jeshi libakie kwenye Kambi ya Buyu.

Mheshimiwa Spika, kuna wananchi wangu ndani ya Jimbo la Chukwani na Buyu maeneo yao yamechukuliwa na Jeshi baada ya kupima, lakini cha kusikitisha mpaka leo wananchi hawa hawajalipwa na wanahangaika. Hivyo, naomba Wizara iwafikirie kuwalipa.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba kuchangia hoja hii juu ya hoja ya Serikali kupima ukubwa wa Jeshi letu ili bajeti itengwe kutosheleza mahitaji yake. Wanajeshi wetu wajengewe *barracks* za kutosha ili wote wakae huko badala ya kuzagaa uraiani.

Mheshimiwa Spika, tatu, uangaliwe uwezekano wa kuanza kuhamisha kwa awamu kambi zilizoko mijini ili zisogee mbali na maeneo ya mijini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA**: Mheshimiwa Spika, napendekeza uanzishwaji wa JKT, kambi moja iwepo Igalula kwa ajili ya kilimo cha

tumbaku, mpunga, karanga, mahindi na alizeti. Kilimo cha umwagiliaji na ufugaji nyuki kurina asali na nta, kutazalisha pesa za kutosha kuendesha kambi na fedha za ziada kupatikana na kuboresha uzalishaji na kuongeza thamani ya mazao na ajira kuongezeka kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, suala la kizuizi cha maji (*water weir*) katika mto wa kutoka Ziwa Tanganyika kilichobomolewa na Jeshi la DRC na kusababisha maji mengi kupungua Ziwa Tanganyika. Je, uchunguzi umefanywa na Jeshi la Wananchi na Wizara ya Maji na Umwagiliaji?

**MHE. DKT. ABDULLA JUMA ABDULLA SAADALLA**: Mheshimiwa Spika, napongeza jitihada za Serikali kuleta Umoja wa Ushirikiano kiulinzi Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, napendekeza tuwe waangalifu katika kujadiliana katika '*mutual-defense pact'* ili tulinde heshima yetu katika zoni (kanda) lakini pia uzoefu wetu wa kulinda amani.

Mheshimiwa Spika, tuwe waangalifu kujiunga na *Amisom* tusije tukaingia katika mkumbo wa Al-Shabab. Tutumie *geographical shield* na *political shield*, kwa uangalifu sana ili zahma isikaribie nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, *early warning na disaster* na *conflict management* ni muhimu na mazoezi yaendelee.

Mheshimiwa Spika, ulinzi nchini, ulinzi uwe unahusu pia uharamia ndani ya nchi kwa vile unakuwa kidogokidogo. Pia matumizi ya mitandao na *jamii forum* zinaweza kuleta mfarakano nchini. Pendekezo, kikosi maalum cha utafiti na kukabiliana na hii *soft copy crime* au '*cyber crime'* katika kuiteka nchi yetu kinadharia.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa, naunga mkono utekelezaji wa sheria hasa Wabunge kwenda JKT.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Ulinzi, Chuo hiki kichukuwe Watendaji wetu, Wakurugenzi mpaka Mawaziri. Pia kihusishe na kuwa *center of excelency* katika kanda. Mahusiano na vyuo vyengine duniani ni muhimu, kiwe ni chachu ya kuchukua wanafunzi *direct* kutoka shule kwa maandalizi.

Mheshimiwa Spika, maslahi ya ngome, Jeshi liingie mkataba na *National Housing* ili zijengwe nyumba, wapewe tangu wanaajiriwa wakatwe mshahara wao kidogokidogo kutokana na maelewano ili wakitoka Jeshini (kambini) wawe na sehemu za kuishi na familia zao.

Mheshimiwa Spika, ulinzi wa rasilimali sio mipaka tu. Kuna rehema kubwa Tanzania imepata migodi na gesi. Uimara wa ulinzi uendelee juu ya rasilimali hizi. Kikosi maalum cha ulinzi ki-*strategy* ki-uchumi na ki-uvamizi hasa baharini. Ulinzi wa *uranium exploration* pia ni muhimu. Tusijiingize kwenye sheria na sera tu lazima tujilinde na *illegal trafficking of uranium (brief case bomb).*

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Wizara kwa kazi nzuri ya ulinzi wa mipaka ya nchi yetu pamoja na kupunguza matukio ya uharamia katika bahari ya Hindi. Pia hongera kwa kuingiza mpango wa JKT katika bajeti ya mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuiomba Wizara katika zoezi hili izingatie sana suala la kuzuia unyanyasaji wa watoto wa kike (udhalilishaji wa kijinsia) ikiwezekana watoto wa kike wawekwe kambi moja na wafundishwe na walimu wa kike.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika zoezi la uandikishwaji wa vijana kutoka vijijini na kujiunga na JKT kwa miaka ya hivi karibuni inasemekana kuwa kuna vitendo vya rushwa. Naiomba Wizara ifanye ufuatiliaji na uchunguzi wa kina ili kuwabaini wanaofanya hivyo na kuwachukulia hatua ili kuweza kuzuia tabia hii isiendelee maana ni aibu kubwa.

Mheshimiwa Spika, pia idadi ya vijana waliotajwa kuwa watakuwa ni wa majaribio, ni wachache kiasi kwamba wale wote watakaobaki watanung'unika lakini pia ni vizuri Serikali ikazingatia kwamba vijana hawa watatakiwa kujiunga na Chuo Kikuu mwezi wa tisa ambapo shughuli za kutuma maombi ya kujiunga na Chuo pamoja na kuomba mikopo zinafanyika kwa kipindi ambacho watakuwa katika mafunzo ya JKT (March- Agosti). Maombi haya yanatakiwa yafanyike kwa njia ya mtandao. Je, Serikali imeandaa mazingira ya kuwawezesha vijana walioko JKT kufanya taratibu

za kujiunga na Chuo Kikuu bila kuchelewa? Naomba Serikali iwaandalie mazingira mazuri vijana ili waweze kufanya mawasiliano katika mtandao wa *internet* ili wasipoteze muda wa kujiunga na vyuo mbalimbali. Vijana wanaomaliza JKT na kukosa Chuo waajiriwe.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, Serikali izingatie ulipaji wa madeni hasa yale ya maji na umeme, madeni haya yanaathiri sana maendeleo ya taasisi au mamlaka husika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Spika, katika sehemu za mwambao eneo la Kala - Nkasi Kusini, wananchi wamelalamika Jeshi kwa kwenda Kala - Kilambo cha Molechi na sehemu zingine za Kala wakiwa na Bwana Afya kukusanya pesa akiwa na silaha. Mwanajeshi huyo ambapo huwataka watoe laki tatu kwa kila shamba na kwa baadhi ya watu bila risiti na kusingizia kuwa hawajafanya usafi katika mashamba yao ya zamani porini hivyo hunyanyasa wananchi hao ambao wamekosa imani na Serikali yao. Wahusika hao, Bwana Afya na Mwanajeshi huyo wanasema anatokea Nkasi.

Mheshimiwa Spika, naliomba Jeshi lako Tukufu kushika hatamu ya kuwaadabisha vijana walio wengi wanaoishi mijini bila kazi kwani kazi hii ya kiuchunguzi yawezekana na kuwatia adabu kwa kupitia Wanajeshi tu kwani mimi ninaimani kubwa sana na Jeshi hili. Kwani Kilimo Kwanza hatutafikia malengo ikiwa Jeshi halitaingilia kati kwani *operation* iliyofanyika Kigoma

miaka ya 1981 ya kuanzisha vijiji vipya, nakumbuka Jeshi ndio waliofanya kazi hiyo na kuanzisha vijiji vya Simbo na kadhalika, mpaka leo vijiji hivyo vipo.

Mheshimiwa Spika, sensa nzuri ya watu wasiofanya kazi yaweza kufanikiwa kwa njia hii tu ya Jeshi. Hivyo naomba Serikali itenge fungu la fedha kwa ajili ya zoezi hilo kwani haiwezekani wakulima 200 walaji 1000 vitu vikaacha kupanda bei. Jambo hili si lelemama lakini baadaye litaleta shida nchini.

Mheshimiwa Spika, niombe Serikali iwasaidie kupandisha mapato yao au mishahara kwani hawa ni watu tunaoishi nao mitaani tunaona wanavyoathirika na maisha na katika Majeshi makini ya kujivunia nchi hii ni Jeshi si vinginevyo. Tunaomba Serikali iwajali waungwana hawa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaj wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi, Mnadhimu Mkuu, Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa na Wakuu wa Kamandi zote.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Wizara kwa mara nyingine tena (nilishauri jambo hili tangu mwaka 2005) kuwa wakati wa amani, Jeshi letu liugawe muda wake ili sehemu ya muda huo itumike kufanya na kutekeleza miradi ya kiuchumi yenye tija kubwa hasa ujenzi wa barabara, madaraja na majengo muhimu. JKT (SUMA) wana kitengo hicho lakini ni vema jambo

hili likafanywa kwa kada pana zaidi ya Jeshi. Endapo Jeshi litajenga barabara, madaraja na majumba (mfano Vyuo Vikuu), siyo tu kwamba jambo hili litanoa vipaji walivyo navyo Wanajeshi wetu na kuimarisha utayari wao wakati wa vita bali pia litawatayarisha Wanajeshi wetu kustaafu vema, kwani itawawia rahisi kujiunga na sekta ya ujenzi ambayo kwa sasa inatija kubwa mara tu wakistaafu.

Mheshimiwa Spika, jambo hili litawapunguzia usumbufu Wanajeshi wanaostaafu kwa umri mdogo kwani hivi sasa wanapata taabu sana kuingia katika sekta binafsi ambayo hawajaizoea sana. Lakini zaidi sana jambo hili litaimarisha usalama wa nchi yetu kwani Askari aliyestaafu hatashawishika kirahisi kujiingiza katika vitendo vya uhalifu. Je, Wizara inalionaje jambo hili?

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEH:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutufikisha hapa Bungeni katika hali ya uzima.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hotuba hii kwa upande wa maslahi ya Wanajeshi. Kama kuna sekta muhimu nchini basi Jeshi ni mojawapo. Kama hivyo ndivyo maslahi yao bado hayajawekwa vizuri. Naomba waangaliwe sana Wanajeshi katika maslahi ili waweze kufanya kazi zao kwa uaminifu zaidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, Kongwa tunaomba kambi ya JWTZ. Huko wanakokataa kambi za Jeshi leteni Kongwa.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu na pili wananchi wa Babati Vijijini kunipa fursa ya kuja hapa leo kuchangia Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuendelea kuimarisha Jeshi letu la Ulinzi JWT na kuwa na mpango wa kurejesha mafunzo ya vijana JKT. Naishauri Serikali iendelee kuimarisha Jeshi letu la Ulinzi kwa kuwa la kisasa zaidi na kuendelea kutoa mafunzo kwa Askari wetu ili kwenda na wakati.

Mheshimiwa Spika, tunawapongeza (JWTZ), Wanajeshi wetu kuwa wastaarabu na kuwa wanyenyekevu kwa wananchi wa Tanzania. Tukilinganisha na nchi zetu za jirani tu wao ni tofauti sana. Tunaomba Serikali kuangalia namna ya wananchi na taasisi mbalimbali nchini waweze kutumia wataalamu wazoefu na waliobobea huko Jeshini kupata ushauri na utaalamu wao kunufaisha jamii kama wanavyofanya katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Spika, tunashauri wataalam wa Jeshi letu waweze kutumika katika ushauri wa ujenzi wa majengo, barabara, madaraja na kadhalika. Uchoraji wa ramani (*architecture*). Pia tunaomba Jeshi letu liendelee kutoa mafunzo kwa jamii ya huduma ya kwanza *(first aid)* na uokoaji wakati wa majanga. Mfano wakati wa moto, mafuriko, tetemeko ili

Watanzania wengi zaidi wafahamu masuala ya huduma ya kwanza na uokoaji. Tunaomba mafunzo ya kujiendeleza kielimu Jeshini yazingatiwe. Wanajeshi wetu wawe na fursa hiyo ili tuwe na Jeshi lenye nidhamu lililoendelea kielimu na lenye kuonesha mfano kwa kutoa huduma kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kuanzisha tena mafunzo ya JKT na vijana wengi watapata fursa kujiunga JKT na kupata mafunzo ili waweze kujiendeleza katika masuala ya ulinzi na kujifunza masuala mbalimbali ya ustadi wa kazi ili waweze kujiendeleza kimaisha watakapofika uraiani. Pia itawapa fursa Watanzania wengi kupata mafunzo ya ulinzi ili waweze kupata ajira katika makampuni ya ulinzi binafsi. Pia mafunzo ya JKT yatasaidia vijana wengi kupata ufahamu wa historia ya nchi yetu, kujenga uzalendo na kupata mafunzo ya uokoaji wa maisha na mali pindi madhara yatakapotokea wakati wa majanga ya kitaifa, huduma ya kwanza wakati wa ajali mbalimbali kwa nidhamu ya hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri Serikali na tunaamini kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha ataweza kutekeleza mapema sababu ya umakini wake katika uendelezaji wa JKT na kuiendeleza JKT kibiashara na hasa katika sekta ya kilimo na ufugaji.

Mheshimiwa Spika, tunashauri bei ya vifaa vya kilimo kama vile majembe, ma-*harrow*, planta, trela, powatila na vingine ili kumnufaisha mkulima na kilimo kwanza kifanikiwe. Pia tunashauri JKT (SUMA) na Serikali

kuangalia namna ya kuondoa wakala katika mradi ya JKT (SUMA), *commission* au faida na malipo ya wakala yangeweza kupunguza bei ya vifaa na kuongeza huduma kwa jamii. Lengo ni kuendesha bila hasara lakini sio kwa faida kubwa sawa na wafanyabiashara. JKT huko miaka ya nyuma ilikuwa inazalisha chakula kingi, walikuwa na ng'ombe bora wa maziwa mfano kule Oljoro walikuwa wanalima zabibu bora, Makutupora, Oljoro.

Mheshimiwa Spika, tunashauri wapate wataalamu wa kilimo, wazuri ili tuboreshe uzalishahji wa chakula, mbegu, matunda na pia kuwapa mafunzo ya uzalendo na ustadi wa kazi. JKT wanaweza kuwa mfano mzuri kwa jamii katika kilimo, ufugaji na uvuvi na ufugaji wa nyuki. Pia JKT ishirikiane na taasisi mbalimbali mfano SUA, vituo vya utafiti mbalimbali pamoja na taasisi ya kuzalisha mbegu asili ili kukuza sekta ya kilimo na tuweze kupata mbegu nyingi bora, kulinda mazingira, kutoa elimu ya matumizi ya vifaa na zana za kilimo, matrekta na vifaa vyake mfano powatila, uzalishaji wa mbegu au miche ya matunda.

Mheshimiwa Spika, mwisho JKT wanaweza kujipanga vizuri wakawa wanazalisha chakula cha kulisha Majeshi yote nchini. Tunalipongeza Jeshi letu JWTZ kuwa na nidhamu ya hali ya juu. Muendelee na moyo huohuo, mvumilie wananchi ambao wanasema vibaya Jeshi letu.

Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kuunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kuwakilisha bajeti yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze pia Askari wetu kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa ajili ya ulinzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Askari wetu wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Ni vema Wanajeshi wenye vyeo vya kawaida wangeangaliwa kuongezewa hata marupurupu. Ukiangalia bajeti hii, utaona ni ndogo sana ukilinganisha na matatizo waliyonayo. Sababu si vizuri Jeshi kuwa na madeni kutoka kwa raia, kwa mfano kuwa wadeni wanaodaiwa mpaka wanafikia kupelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, naomba kujua kama kambi zetu zote za Jeshi zina hati ya kumiliki ardhi? Kwa kuwa kuna migogoro mikubwa sana ya uvamizi wa ardhi sasa hatujui kama Majeshi yanawavamia raia au raia wanavamia makambi ya Jeshi. Naomba kwa hili nipate ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, pia mipaka yetu haijapewa kipaumbele katika ulinzi wa kutosha. Ni kwa nini kumekuwa na wimbi la usafirishaji wahamiaji haramu ambao wengine wanapitishwa katika nchi yetu na wanakwenda kushikwa katika nchi jirani, wengine wanafia katika magari wakati wanasafirishwa.

Mheshimiwa Spika, ni utaratibu gani unatumika kupata vijana wanaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa katika kila Mkoa? Kumekuwa na malalamiko makubwa sana kwamba ni mpaka umjue mtu? Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, ni lini utaratibu wa kurudisha mafunzo ya JKT kwa vijana wote waliohitimu masomo yao ya shule na vyuo kwa kuwa utaratibu ule uliwasaidia sana vijana wetu wengine kuwajengea uzalendo na ukakamavu. Katika makambi hayo vijana wangepata fursa ya kujifunza ujasiriamali na kuweza kujiajiri wenyewe kupunguza dhima ya vijana wengi kutokuwa na shughuli ya kufanya na kujiingiza katika makundi mabaya. Naomba nipatiwe majibu ni lini mpango huu utarudishwa tena au kama kuna mkakati wowote wa kurudisha mpango huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MAJALIWA K. MAJALIWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, naomba sana suala la mipaka ya ardhi kati ya maeneo ya Jeshi na Raia, ni vyema sasa yabainishwe ili kuondoa migogoro iliyopo mfano *Nachingwea Farm*.

Mheshimiwa Spika, suala la makazi ya Askari litiliwe maanani kwa kuendelea kuwaaacha Askari kukaa

makambini zaidi ili kuwatenganisha na shughuli za uraiani. Siasa jambo ambalo linaweza kuleta matatizo.

Mheshimiwa Spika, suala la malipo ya wastaafu litiliwe mkazo ili kuondoa migogoro iliyopo.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. SAIDI M. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Maofisa wetu wote wa Jeshi kwa kazi nzuri ya kulinda mipaka na usalama wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Serikali kwa kukubali kurejesha mafunzo ya uzalendo kwa vijana kwenda mafunzo ya JKT.

Mheshimiwa Spika, vitendo vya Askari kupiga raia, changamoto hii bado haijapatiwa suluhu. Bado wako Askari wasio waadilifu wanaochukua sheria mkono kwa kupiga raia.

Mheshimiwa Spika, nimeletewa maelezo ya malalamiko ya Capt. Kichawele ambaye amefungwa na Mahakama ya Jeshi lakini anasema kwa uonevu na Wanajeshi hawataki kutoa rufaa yake hivyo anasota gerezani kwa uonevu. Tafadhali jambo hili lichunguzwe na majibu tuyapate.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia na kutoa ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kambi ya JKT Kanembwa – Kibondo. Kambi hii ilianzishwa mwaka 2007 lakini bado Wanajeshi hawajalipwa posho mbalimbali ikiwemo mizigo lakini pia familia zao ziko mbali nao. Napenda kuishauri Wizara iwalipe madeni yao na kuhamishia familia zao Kibondo.

Pili, mgogoro wa kambi hii ya JKT na wananchi. Baada ya kambi hii kuanzishwa, wananchi wa vijiji vya Kilemba na Kazilamihunda wamekuwa na mgogoro wa ardhi na mpaka na Jeshi. Napenda kuishauri Serikali kutatua mgogoro huu haraka kwani ni wa muda mrefu.

Tatu, vijana wanaojiunga na JKT/JWTZ. Napenda kuishauri Serikali kwamba Wabunge wahusishwe kwenye mchakato wa kuchagua vijana wanaojiunga na JWTZ na JKT ili Jeshi liendelee kuwa na Wanajeshi wanaotoka maeneo yote ya nchi. Pia napenda kushauri mchakato wa sasa, baadhi ya maeneo, baadhi ya watu huita/hudahili watu kutoka maeneo mengine na kusababisha wazawa wa eneo husika kukosa nafasi kila mwaka. Pia nashauri Wabunge tuitwe kwenye vikao vya Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Nne, Wanajeshi wanaoishi mipakani Wilayani Kibondo. Wanajeshi hawa wanaishi kwenye maeneo duni na hata kwenye nyumba za nyasi na nyingine zinavuja na wengi wako mitaani. Napenda kuishauri Serikali iboreshe makazi yao.

Tano, kuwaondoa Wanajeshi mipakani hasa Kibondo – Kigoma. Napenda kuishauri Serikali isitishe

zoezi la kuwaondoa Wanajeshi walio mpakani kwani wanatusaidia sana kwani nchi za Burundi, Kongo, Rwanda na kadhalika bado kuna wahamiaji wengi haramu na Polisi ni wachache lakini pia watu wanavuka mpaka kinyemela kutoka nchi za jirani na kufanya ujambazi.

Sita, napenda kuishukuru Serikali kwa kuweka program ya mafunzo ya kijeshi kwa Wabunge Vijana na mimi kama Mbunge kijana nimepokea jambo hili vizuri na niko tayari kwa mafunzo. Napenda kutoa ushauri pia kwamba zoezi hili lifanyike kwa Madiwani vijana watakaopenda kujiunga ili tupate viongozi wakakamavu.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri pia kwamba katika vijana 5000 watakaojiunga na JKT, vijana waliohitimu vyuo hivi karibuni wahusishwe, wenye umri wa miaka 24, 25 na 26.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na kupewa majibu.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa hii ili nami niweze kutoa maoni yangu katika hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, nikiwa nakubaliana kabisa na hoja ya kurudishwa kwa Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa sheria, napenda Serikali itoe ufafanuzi juu ya mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kufutwa kwa Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa sheria, ilikuwa ni lazima kwa mtu yeyote kupitia mafunzo ya jeshi hili kabla ya kujiunga na elimu ya juu na kwa wakati huo chuo kikuu kilikuwa kimoja tu kinachomilikiwa na Serikali. Je, katika utaratibu mpya wa Jeshi la Kujenga Taifa unaotaka kurejeshwa, itawalazimu vijana kwenda jeshini kabla ya kujiunga na vyuo vikuu? Ikiwa hivyo ndivyo, utaratibu huo utavihusu vyuo vikuu vya binafsi?

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa ni muhimu sana hasa katika kujenga uzalendo na ukakamavu kwa vijana wetu. Makambi ya JKT yalikuwa ni maeneo ambapo kazi nyingi na ngumu zilifanyika hasa mashamba makubwa sana, uvuvi na shughuli yoyote kulingana na hali ya nchi ya eneo husika. Pamoja na JKT kujishughulisha kwa kiasi kikubwa na shughuli za uzalishaji mali, kazi hizi hazikuwa na manufaa sana kwa Taifa hasa kuinua uchumi kwani hakuna kambi ya JKT iliyokuwa inaingiza ziada ya chakula kinachozalishwa katika Hifadhi ya Taifa ya Chakula. Aidha, kazi ngumu na nyingi zilizofanywa na JKT hazikusaidia kuinua hali ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali inapofikiria kurudisha Jeshi la Kujenga Taifa ilifanye liwe la kisasa zaidi, liendane na mahitaji halisi ya nchi kwa wakati huu hasa katika kupunguza umaskini uliokithiri. Makambi ya Jeshi yatumike kuzalisha chakula kwa wingi kama tulivyokuwa tunafanya zamani lakini wakati huu tulenge katika kuongeza hifadhi ya chakula ya nchi ili tuondokane na njaa na siyo tu Makambi ya JKT yazalishe chakula kwa kulima mashamba makubwa

sana na kufanya kazi zingine nyingi na ngumu lakini bila kuwa na malengo yoyote ya uzalishaji huo.

Mheshimiwa Spika, ni lazima Jeshi la Kujenga Taifa la wakati huu liwe la kisasa zaidi na lifanye kazi kwa malengo na kulingana na mahitaji ya nchi, kielimu zaidi si tu kuangalia masuala ya ukakamavu na uzalendo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. LETICIA M. NYERERE**: Mheshimiwa Spika, naomba nichangie moja kwa moja kwenye shughuli za SUMA JKT.

Mheshimiwa Spika, uagizaji wa matrekta utawarahisishia wakulima wenye uwezo wa kununua matrekta hayo lakini wakulima wengi vijijini hawana uwezo wa kulipa hata ile asilimia 10. Kwa mfano, trekta linalouzwa shilingi milioni 16.5, mkulima atatakiwa kutoa malipo ya milioni 1.6 fedha ambazo ni nyingi sana kwa wakulima wadogo walioko vijijini. Nashauri wakulima wasiokuwa na uwezo wakopeshwe matrekta na SUMA JKT kwa kuwapa angalau trekta moja kwa kila kijiji bila kuwataka walipe asilimia yoyote ya bei ya trekta. SUMA JKT iweke utaratibu utakaowawezesha kutoa sehemu ya malipo baada ya mavuno kwa pamoja kwa wana kijiji wote watakaotumia trekta hilo. Mpango huu ni muhimu sana kwani utawawezesha vijana wengi wanaokimbilia mijini wabaki vijijini na kujihusisha na kilimo ambacho kitakuwa kimerahisishwa. Mpango huu hakika utaongeza pato la Taifa kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO**: Mheshimiwa Spika, ulinzi na usalama ni muhimu sana kwani bila usalama basi ni vurugu tupu.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kurudisha tena Jeshi la Kujenga Taifa ili vijana wetu wajenge uzalendo na utaifa kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Jeshi letu limekuwa likifanya kazi zake katika mazingira magumu na kukumbana na changamoto nyingi hususan za makazi, mwingiliano wa maeneo wanayoishi au kambi zao na makazi ya wananchi. Ni vema basi Serikali ione ni kwa jinsi gani wanaweza kuweka kambi na makazi ya Wanajeshi mbali na wananchi kwa lengo moja tu la kukuza mahusiano mazuri.

Mheshimiwa Spika, Jeshi letu pamoja na kutokuwa na vita kwa muda mrefu, ni vema Jeshi letu likashiriki katika taaluma mbalimbali za ujenzi wa nchi yetu mfano katika kilimo hasa tukitambua kuwa kilimo ndicho kinachokuza maendeleo ya uchumi wetu kwa kasi kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na uingiaji wa watu wasio Watanzania kupitia mipakani. Ni ukweli ulio wazi kuwa nchi yetu ni kubwa sana na hivyo mipaka yake ni mirefu sana. Mfano bahari ya Hindi kuanzia Tanga hadi Mtwara ni zaidi ya km 1500 huku tukiwa na maziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa. Mipaka hii imekuwa ikitumika na wahalifu kutokana na ukubwa uliopo, hivyo Jeshi letu kushindwa kuhimili au ku-*monitor.* Hii ni

kwa sababu Jeshi bado halina vifaa vya kisasa vya ku-*detect* na kuweza kuona wahalifu hao, pia hawana vifaa vya kisasa kama *helicopters* na *speed boats* zitakazofanya doria mara kwa mara.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kutoa maoni yangu kuhusu hotuba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha (Mb) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba vijana wetu wanaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa, ni vigezo gani au ni utaratibu gani unaofuatwa hivi sasa? Kwa miaka ya nyuma, vijana waliomaliza kidato cha sita walijiunga moja kwa moja na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa utaratibu wa vijana kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa moja kwa moja baada ya kumaliza kidato cha sita ulikuwa ni utaratibu mzuri sana kwani vijana wa kiume na kike walijengewa ukakamavu mkubwa, uzalendo na utaifa. Je, Serikali ina mpango wowote wa kurudisha tena utaratibu huo wa vijana kujiunga na JKT mara baada ya kumaliza kidato cha sita? Napenda kuipongeza JKT kwamba limeweza kukarabati majengo mbalimbali yatakayotumiwa na vijana wa kujitolea pia ukarabati umefanyika katika makambi mfano Mafinga, Makutupora, Oljoro na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni nchi yetu ilipata majanga ya mafuriko na milipuko ya mabomu Dar es

Salaam. Napendekeza JKT itumie ujuzi wake kujenga majengo ya gharama nafuu ili matatizo yanapotokea watu/waathirika wawekwe katika majengo hayo badala ya utaratibu ulioko hivi sasa wa kuwaweka waathirika katika mahema kwa muda mrefu. Majengo hayo yanaweza kutengenezwa kwa *material* ambayo ni rahisi na ambayo inawezekana kukunjwa na kuhamishwa kwa kuhifadhiwa.

Mheshimiwa Spika, katika Awamu ya Kwanza za viongozi wetu Hayati J.K. Nyerere au Rais Mstaafu Mwinyi, Jeshi la Wananchi liliweza kutengeneza magari aina ya Nyumbu. Ulikuwa ni uvumbuzi mzuri ulioiletea nchi yetu sifa na mwamko katika maendeleo ya viwanda, sayansi na teknolojia ya magari. Napenda kuihoji Serikali, ni kitu gani kilizuia au kukwamisha utengenezaji wa magari ya Nyumbu? Je, Serikali haioni kwamba magari hayo yangetumika sio tu kwa matumizi ya kijeshi lakini pia wananchi na hasa wakulima wangeuziwa kwa bei/gharama nafuu kwa ajili ya matumizi ya kuhamisha mazao kutoka shambani hadi sokoni? Hivi sasa malori yananunuliwa toka nje, ni gharama kubwa na ni wachache wanaoweza kununua. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa anipatie majibu ni kitu gani kiliupata mpango ule wa utengenezaji wa magari ya Nyumbu?

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa uzalishaji ng'ombe kwa chupa unaofanywa na JKT utangazwe vizuri kwa wananchi ili wengi zaidi wafaidike na ng'ombe hao bora ambao wanaweza kabisa kusaidia

kupunguza umaskini kwa wananchi wetu kufanya ufugaji mzuri wa kisasa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni muhimu zoezi la Kilimo Kwanza lifanikiwe, bei ya matrekta ipunguzwe, bado iko juu, kuna baadhi ya wakulima wameshindwa kumaliza deni la trekta kwa wakati kutokana na ukame uliotupata miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchangia kwenye hotuba ya Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kero za mipakani ni vema Wanajeshi wetu wawezeshwe na wawekewe mazingira mazuri ya mpakani ili wawe tayari kuishi huko na kuweza kudhibiti uhalifu ambao kama ulinzi ukikosekana tutaathirika.

Mheshimiwa Spika, ni vema sasa makumbusho ya mashujaa wa Msumbiji yaliyoko Mtwara yaenziwe na viongozi wa kitaifa na wananchi watembelee mara kwa mara na hii inaweza kuchangia kwenye utalili. Pia ni vyema Wanajeshi wanaolinda pale wawekewe *incentive* ili eneo lile liwe lipo kwa muda wote, wanafunzi wa shule zetu wafanye *study tour* kwenda kuwaona mashujaa wetu. Hivyo ni vema kituo kienziwe.

Mheshimiwa Spika, pia kuna tatizo la Jeshi kujiongezea maeneo na kuendeleza bila kulipa fidia,

kwa mfano maeneo ya Kigoma, eneo la Kibirizi, Buronge katika Manispaa ya Kigoma Ujiji. Je, ni lini wananchi wa maeneo haya watalipwa fidia zao?

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kutekuliwa na Mheshimiwa Rais kuiongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua ile ahadi ya Serikali ya kuanzisha kambi ya JKT, Wilaya ya Manyoni, eneo la Sanjaranda imefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, napenda kupata ufafanuzi ni kwa nini Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Tanga kuna Kambi mbilimbili za JKT wakati Mikoa mingine hakuna kambi hata moja? Ni vigezo gani vinatumika kuanzisha ama kuacha kuanzia kambi za JKT katika Mikoa ama Wilaya nchini?

Mheshimiwa Spika, aidha, naipongeza Serikali kwa kuanza kutumia Jeshi kwenye matukio ya majanga na hususan majanga ya kukabiliana na matukio ya njaa; kama vile kusomba na kusambaza tani za vyakula kwenda maeneo maalum ambapo chakula kinaweza kusambazwa kwa urahisi. Napendekeza Jeshi litumike katika kufikisha kabisa chakula kwenye maeneo ya njaa kwa kila Wilaya ili Serikali iondokane na urasimu wa tenda ya kusafirisha chakula kutoka Maghala ya Taifa kwenda Mawilayani na sehemu zenye njaa. Aidha, Jeshi lipewe jukumu la kunyunyuzia ndege waharibifu (*quelea quelea*) kwenye maeneo yanakolimwa mazao yanayostahimili ukame kama

Singida na Dodoma. Serikali inunue ndege ya kunyunyuzia dawa na kuikabidhi Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ifanye kazi hiyo kwa ufanisi zaidi na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kupatiwa maelezo juu ya maeneo yote hayo ili kuniepushia bugudha ya kusimama kwenye Kamati ya Matumizi.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Spika, kunapokuwepo na usalama mahali popote pale iwe ni ndani ya familia, jamii na hata taifa kwa ujumla wake, ndipo panapokuwa na baraka za uwepo wa maendeleo ya maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa hali ya usalama ina maana ni amani. Pia ieleweke kuwa amani si kutokuwepo vita tu katika nchi ila ni upatikanaji wa huduma muhimu za jamii za msingi kwa kadri taratibu za nchi zilivyowekwa, tofauti na hapo amani inawezatoweka na kusababisha machafuko; hivyo basi kunahitajika uhuru wa kutosha pasipo kuvunja sheria ili kufanya shughuli mbalimbali kwa ajili ya kujipatia mahitaji ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, ninatambua kazi kubwa inayofanywa na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama na ninavipongeza kwa kuwa vyombo hivyo vimetumika katika shughuli za uokoaji wananchi wanapozama majini, kusaidia kukabiliana na janga la njaa kwa kutoa na kusafirisha vyakula katika maeneo

husika sambamba na kukabiliana na maharamia, napongeza sana kwa juhudi hizo nzuri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri ambayo imekuwa ikifanywa na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama bado kumejitokeza matatizo ambayo yamesababishwa na vyombo hivyo. Wanajeshi hawa wamekuwa wakivamia maeneo, ardhi ya kijiji au ya wananchi na kuipora, kupiga watu lakini pia na kujihusisha na vitendo vingine vingi vya kihalifu. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri akishirikiana na watendaji wake kuhakikisha mambo haya yanarekebishwa na hatimaye kuwa na jeshi lenye nidhamu zaidi.

Mheshimiwa Spika, pia kumekuwepo na madai ya Askari ambao walipigana vita katika baadhi ya maeneo ambayo Tanzania ilihusika mfano vita vya Kagera. Wanajeshi hao wengine wamekuwa walemavu na bado wanadai haki zao. Namwomba Waziri na Watendaji wake kulishughulikia hilo kama wapo ambao hawakupata stahiki zao sahihi basi wapewe au waelezwe ukweli kuliko nenda rudi ya kila siku isiyo na ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kutokana na umahiri mkubwa wa kazi aliouonesha kwa kipindi kifupi tokea uteuzi wake. Kutokana na hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia 100. Naomba kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa sana na mafanikio yaliyopatikana kutokana na shughuli za JKT. Hata hivyo, naomba Wizara iangalie uwezekano wa kubadilishana uzoefu na JKU kule Zanzibar ambalo lengo lake ni sawa na JKT. Kuna utaalamu ambao JKU wataweza kujifunza katika JKT na JKT wataweza kujifunza kutoka JKU.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kambi ya Jeshi Mazizini, naomba Wizara ielezee juu ya hadhari inazozichukua kutokana na uwepo wa kambi hii pale na yaliyotokea kutokana na milipuko ya Mbagala. Kambi ya Jeshi ya Mazizini kwa sasa imezungukwa na makazi ya watu na ikizingatiwa makazi ya viongozi wengi pamoja na taasisi za Serikali zinaendelea kujengwa karibu na kambi hiyo. Naomba Wizara ielezee tahadhari inazozichukua kutokana na ongezeko hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vikundi vya ulinzi binafsi, Wizara ielezee imejipanga vipi na udhibiti wa vikundi hivyo ili kudhibiti silaha ambazo vinazimiliki na ili kuepuka uasi na ujambazi unaotokana na wafanyakazi wa vikundi hivyo. Imeonekana kuwa kuna vikundi vingi sana ambavyo havijasajiliwa rasmi na hii inahatarisha sio tu mapato lakini pia usalama wa nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina migogoro mikubwa ya mpaka ya ardhi kati ya wananchi na Jeshi. Migogoro mingi imedumu kwa muda mrefu, ifike wakati sasa Wizara ya Ardhi ishirikiane na Wizara hii ili kuondoa kabisa tatizo hili.

Aidha, busara itumike kutoa fidia ya ardhi kwa wananchi au jeshi pale itakapokuwa lazima kufanya hivyo. Haipendezi walinzi wa nchi kugombea ardhi na wananchi wanaoshindwa. Lakini vilevile tutapunguza maafa yaliyowahi kutokea kwa majeshi kuwa karibu na makazi ya wananchi wa Gongo la Mboto na Mbagala.

Mheshimiwa Spika, ulinzi wa mipaka yetu hasa Magharibi. Suala hili limeainishwa wazi katika hotuba hii ukurasa wa nane. Ulinzi uongezeke kwani eneo hili la ukanda wa Ziwa Tanganyika si shwari sana, matukio ya uvamizi hutokea mara kwa mara na maisha hasa ya wavuvi na mali zao hupotea kila mwaka katika matukio ya uvamizi yanayotokea mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile bajeti yao iongezwe, wawe na *special fund* kwani matukio yanayotokea ni mengi mno hali inayopelekea wavuvi kuchangishwa petroli wakati wao wenyewe maisha yao ni duni na wengi wamepoteza mali zao kwa matukio ya ujambazi.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Kigoma Vijijini na ile ya Manispaa, nayo hulazimika kuchangia petroli hali inayopelekea kupata maswali mengi kwenye hoja za ukaguzi kwani hawana bajeti hiyo ila hulazimika pindi itokeapo dharura. Mfano mwezi June ilihitajika lita 300 za petroli ilibidi kila Halmashauri ichangie lita 100 na wakakopa na kuomba wafanyabishara wenye vituo vya mafuta kukopesha na kuchangia lita 100 iliyotakiwa na lita moja Kigoma ni kati ya Sh.2500 - 2800.

Mheshimiwa Spika, rada iliyopo Kigoma inaendeshwa kwa *generator,* mara nyingi mafuta ya kuwashia ile jenereta huisha matokeo yake wanashindwa kuitumia kiulinzi maana rada hiyo inazima. Hii ni hatari kwa usalama wa nchi yetu, hatua za haraka zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo limetokea hivi karibuni kutaka kupunguza ulinzi kwenye maeneo ya mipakani, ziwani kwa kuwa fedha zinazotolewa hazitoshelezi, mfano Kagunga, kwa kuwa vita ya Burundi imekwisha, ikaonekana pako shwari hivyo wahamishiwe eneo la Sibwesa, wananchi wanasema pako shwari katika mipaka yetu kwa sababu tu Wanajeshi wapo, wakiondoka hali ya uvamizi itarejea. Hivyo ulinzi uimarishwe zaidi na zaidi, kila siku ili amani iendelee kuwepo.

Mheshimiwa Spika, vilevile tatizo la Wanajeshi kutolipwa posho zao hasa wale wanaolinda mipaka yetu. Mfano mzuri ni kikosi 44 KJ hawajalipwa posho zao kwa muda mrefu sana. Kwa kutowalipa mnawapunguzia morali ya kufanyakazi hivyo kushindwa kuendesha maisha yao na familia zao na wategemezi wao. Walipeni, msiwashawishi kupokea rushwa au kushiriki vitendo vya kijambazi.

Mheshimiwa Spika, SUMA JKT wamefanyakazi nzuri lakini vitu vyao vinavyotengenezwa na viwanda vyao bado ni vichache. Waendelee kuitangaza ili wapate soko kubwa ili wazalishe zaidi mfano waanze na kuiuzia Serikali samani katika ofisi zote za Serikali nchini. Ili kupunguza gharama ya kuagiza samani zisizodumu, za

kichina lakini Serikali inasaidia ajira ya nchi zingine zinazouza samani kama China badala ya kuongeza ajira nchini na kukuza viwanda vyetu hasa vya SUMA JKT.

Mheshimiwa Spika, matrekta ya SUMA JKT bado ni ghali, yapunguzwe bei lakini vilevile wakopeshwe wakulima ili yatumike kuliko ilivyo sasa yanakaa juani pale Dodoma na Mwenge Dar es Salaam. Vilevile wawakopeshe Magereza yote yanayojishughulisha na kilimo mfano Kwitange Kigoma na mengine mengi ili uzalishaji uongezeke, Magereza yajilishe na yauze ziada kwa raia.

**MHE. ABDUL J. MAROMBWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja hii hasa ukizingatia kuwa mambo mengi ya msingi yametajwa na kupewa fedha ingawa sio za kumalizia matatizo makubwa yanayoikabili Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii, bado Wizara ina changamoto nyingi ambazo zinahitaji kushughulikiwa na Serikali. Miongoni mwa changamoto hizo ni posho kwa Askari. Naiomba Serikali iangalie upya posho za Askari ili waweze kufanya kazi kwa bidii zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni changamoto inayohusu uimarishaji wa huduma za tiba kwa Askari na wananchi wanaozunguka kambi za jeshi. Katika kikosi cha Mzinga - Morogoro, kuna majengo ya hospitali ambayo hadi sasa hayajakamilika. Ujenzi huu tangu uanze, umeshachukua zaidi ya miaka kumi jambo

ambalo linafanya majengo haya yawe kama magofu wakati ni imara na hayana mpasuko wowote. Naiomba Serikali kutafuta fedha popote pale ili majengo haya ya hospitali yakamilike.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni kuhusu matrekta ya SUMA JKT. Nalipongeza Jeshi la Kujenga Taifa kwa ubunifu huu uliofanywa wa kuuza matrekta kwa wingi katika nchi yetu na kwa bei rahisi ukilinganisha na yale yanayouzwa na kampuni mbalimbali hapa nchini. Pamoja na ubunifu huo, kuna haja ya Jeshi hili kufanya mambo makubwa mawili. Jambo la kwanza ni kutengeneza vivuli kwa matrekta hayo ambayo yapo juani siku zote kwa zaidi ya miaka miwili sasa. Kwa kufanya hivyo, yatasababisha matreka hayo kuwa imara.

Jambo la pili ni kulazimisha kukopesha matrekta katika taasisi za Serikali, *SACCOS* na hata kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wana uhakika wa kutosha wa kulipa fedha hizo. Kwa sasa baadhi ya taasisi kama vile Magereza -Kibiti yenye ardhi ya zaidi hekta elfu kumi (10,000) ambazo zinafaa sana kwa kilimo, wanahitaji trekta ili kuongeza uzalishaji wa chakula. Ni vizuri viongozi wa SUMA wakaenda kwenye Gereza hili na mengineyo ya kilimo na kuona uwezekano wa kuwakopesha matrekta.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wabunge, nashauri ile "*down payment*" iondolewe na badala yake wajaze mikataba ambayo endapo hawatalipa katika kipindi cha miaka mitatu, basi makato yote yafanyike katika kiinua mgongo chake cha mwisho.

Kwa kufanya hivi, idadi ya matrekta yatakayobaki yatakuwa machache. Naamimi Wabunge wakipatiwa matrekta hayo yatasaidia sana kuinua “Kilimo Kwanza” hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Jenerali Davis Mwanyange, Luteni Jenerali Shimbo, Meja Jenerali Ndomba, Brigedia Jenerali Dkt. Muzanila na Kanali Bahati, pamoja na wakuu wote wa idara na vitengo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara kupitia SUMA JKT kwa kukubali kupunguza bei ya matrekta kwa ajili ya kuinua kilimo nchini mwetu. Nawapongeza na kushukuru kwa niaba ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo napenda kulichangia ni suala la ulinzi wa amani katika nchi mbalimbali. Tumekuwa tukishuhudia nchi yetu, kupitia Majeshi yetu yakishirikiana na nchi nyingine ili kudumisha amani duniani. Tumeshiriki katika operesheni mbalimbali za kulinda amani zinazoongozwa na UN katika nchi zenye migogoro. Tumeelezwa kwamba Wanajeshi 1,081 wanashiriki operesheni za ulinzi wa amani katika nchi za DRC na kwingineko.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, natambua kwamba ziko fursa mbalimbali ambazo nchi

zinazopeleka Wanajeshi wake katika operesheni za ulinzi na amani hupata, kama vile kulipwa fedha kwa kila Mwanajeshi inayompeleka. Napenda Waziri alieleze Bunge ni kwa nini hatupeleki Wanajeshi wa kutosha, wenye uzoefu ili nchi ipate uzoefu, ijitangaze, mapato na pia kuongozea ajira kwa watu wake? Napenda kujua nchi ina mkakati gani kuhakikisha tunaongeza Idadi ya Wanajeshi wanaoenda kuiwakilisha nchi katika *peace keeping operations*.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara, nikiwa Mbunge wa wafanyakazi, kwa jitihada inazozifanya katika kulipa madeni ya Wanajeshi, posho mbalimbali na madeni mengine ya watumishi. Aidha, nashukuru sana kwa niaba yao kwa mipango ya ujenzi wa nyumba za makazi.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu sasa JKT iongezewe uwezo wa kibajeti ili waweze kuzalisha zaidi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA ABDULLAH AMOUR:** Mheshimiwa Spika, naamini ni jukumu la Jeshi kulinda mipaka ya nchi yetu. Nichukue nafasi hii niwapongeze kwa kazi yao nzuri walioifanya kwa muda mrefu na walikuwa wakifanya kwa ufanisi tu lakini la kusikitisha sana ni hivi karibuni tu yameanza kutokea mambo ambayo yameanza kutushtusha sana sisi raia na mambo haya ni kama yafuatayo; kuvamiwa kwa mipaka ya Kagera na kuingia kwa kundi kubwa la Wasomali na Waburundi na kuwatesa wavuvi kwa kuwapiga vibaya tu. Lingine limetokea hivi karibuni la kuokotwa kwa

wakimbizi kutoka Ethiopia ambao wametupwa huku Dodoma ambao ni maiti, cha kujiuliza, je, hawa wamepitia mpaka gani? Je, mipaka yetu siku hizi hailindwi tena?

Je, Askari ambao wapo barabarani wanafanya kazi gani na vituo vingapi hili kontena limekaguliwa? Je, hawana vifaa vya kisasa vya kubaini mizigo iliyokuwepo kwenye makontena na kama hawana, wana mkakati gani wa kuhakikisha vyombo hivi vinapatikana kwani ni hatari tupu kwani kontena hili lingekuwa limebeba silaha na baadhi ya wahalifu na wakafanikiwa kuingia Dodoma kama walivyofanikiwa kuingia na maiti Dodoma na wakati huohuo Serikali nzima ipo hapa Dodoma, ingekuwaje, Mungu aepushe jambo hili lisitokee. Ni lazima tuwe na mifumo ya kisasa kwa kuwa na teknolojia za kisasa katika kulinda mipaka yetu. Pia katika ulizi wa mipaka tuwashirikishe wananchi na tuombe bajeti ya hao wananchi ambao tutawashirikisha. Tukiwa na teknolojia ya kisasa kazi itakayofanywa na watu mia moja itafanywa na watu kumi tu na tunaweza kubaini maovu yote.

Mheshimiwa Spika, makazi ya Maaskari ambayo wanaishi Askari wetu yamechakaa sana. Hawa watu lazima tuwajali tena sana kuliko hata Madaktari, kwani hawa wanalinda maisha yetu pamoja na nchi yetu na mali zetu. Ni vizuri tuhakikishe kuwa watu hawa wanaishi kwenye makazi mazuri ili wawe na moyo wa kutulinda kwani kazi hii ni nzito sana. Wanajeshi waondokane na kukaa mitaani, watafutiwe sehemu na mipangomiji wajengewe makazi yao na haya yaendane na kupewa mafao mazuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SUBIRA K. MGALU**: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na afya njema inaniwezesha kushiriki kikamilifu katika shughuli za Bunge hili la Bajeti.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Viongozi wote na Vyombo vya Ulinzi na Usalama na Watendaji Wakuu wa Wizara hii kwa maandalizi mazuri ya hotuba hii ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu katika hotuba ya bajeti hii utajielekeza kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu shughuli za Shirika la SUMA JKT, naipongeza Serikali kupitia Shirika la SUMA JKT kwa utekelezaji wa Sera ya Kilimo Kwanza kupitia usambazaji wa zana za kilimo hasa matrekta. Naipongeza JKT SUMA kwa kuuza matrekta 786, kufungua vituo vya kuuzia matrekta katika Mikoa ya Dodoma, Mbeya, Mwanza na Arusha.

Mheshimiwa Spika, katika uongezaji wa vituo vya kuuzia matrekta, nashauri SUMA JKT waone uwezekano wa kufungua kituo cha kuuzia matrekta katika eneo la Segera, Wilaya ya Handeni, Mkoa wa Tanga ili kutoa fursa zaidi kwa wananchi wa maeneo ya Mikoa ya Tanga na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, nashauri Shirika la SUMA JKT kupitia wakala wa uuzaji wa matrekta hayo kushirikiana na Chuo cha Kilimo (MATI) Mlingano kilichopo Muheza-Tanga ambacho ni chuo pekee kinachotoa kozi ngazi ya Diploma inayohusiana na matengenezo ya dhana za kilimo ikiwemo matrekta. Ni wazi ongezeko la matumizi ya zana za kilimo hasa matrekta hapa nchini kwetu linahitaji wataalamu wengi wa zana hizo.

Mheshimiwa Spika, pia niipongeze Serikali kwa kupunguza bei za matrekta aina zote pamoja na kupunguza malipo ya awali/*down payment* kutoka asilimia 59 ya bei ya trekta hadi asilimia 30. Ni wazi jitihada hizi zitaleta mapinduzi makubwa katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu migogoro ya ardhi baina ya Jeshi na wananchi, hapa naomba nizungumzie mgogoro uliokuwepo baina ya Jeshi la Wananchi kupitia SUMA JKT na wananchi wa Kata ya Songa, Wilaya ya Muheza-Tanga, kijiji cha Kilongo. Eneo hili lina zaidi ya hekta 3,000 na wananchi walikuwa wanalima kwenye maeneo hayo. Hata hivyo, wakati wananchi wamepanda mazao yao, uongozi wa juu wa Jeshi ulitoa amri kwa wananchi hao ndani ya saa 48 waondoke ili kupisha SUMA JKT waweze kuendeleza shamba hilo.

Mheshimiwa Spika, suala hili limeleta mgogoro sana na kwa maoni ya wananchi, amri hiyo haikuzingatia ubinadamu kwa vile wananchi hao walishapanda mazao hivyo walihitaji muda kwa ajili ya

maandalizi ya kuondoka katika eneo hilo ambalo liliachwa muda mrefu bila kuendelezwa.

Mheshimiwa Spika, naomba uongozi wa Jeshi kupitia SUMA JKT ukutane na uongozi wa Wilaya ya Muheza pamoja na wananchi wa Kijiji cha Kilongo/Kitopeni, Kata ya Songa Muheza ili kuupatia ufumbuzi mgogoro huu wenye dalili ya kuhatarisha amani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Makamanda wote kwa kuandaa bajeti nzuri ya kisanyansi iliyowasilishwa kitaalamu. Ni mategemeo yetu kuwa bajeti hii itaenda sanjari na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, aidha, naipongeza kwa dhati Serikali kwa kupunguza bei ya matrekta kutoka shilingi milioni 25.6 kuwa shilingi milioni 16.5 kwa matrekta yenye "*horse power*" 50, na kwa matrekta yenye *horse power*" 70 toka shilingi milioni 45.8 kuwa shilingi milioni 38.8. Punguzo hili litainua azma ya Serikali ya Kilimo Kwanza kwa kuwawezesha wakulima kununua matrekta mengi zaidi na hivyo kuinua kipato chao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wanajeshi wetu wanafanya kazi nzuri ya ulinzi wa mipaka yetu, ni dhahiri kuwa wanahitaji utulivu katika maeneo wanayoishi. Hata hivyo hali halisi si hivyo. Kwa msingi

huo, naiomba Serikali ihakikishe kuwa Wanajeshi wanajengewa nyumba bora za kuishi. Inasikitisha kuona Wanajeshi wetu wengi wakiwa hawana makazi maalum hivyo kupanga katika nyumba ambazo nyingi hazina ubora na ni mbali sana na sehemu za kazi. Tatizo hili la ukosefu wa nyumba husababisha tatizo lingine la usafiri.

Mheshimiwa Spika, Serikali ifikirie kupandisha mishahara ya Wanajeshi ambayo ni midogo. Ongezeko la mishahara na kulipa madeni yao kwa wakati, kutaongeza *morale* ya utendaji kazi wao hasa ikizingatiwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**SPIKA:** Ahsante. Asubuhi nilikuwa nimewatambulisha wageni wa Mheshimiwa Daktari Festus Limbu, hawakuwepo, sasa wapo. Yupo Bwana Velantine Meherine na Micher Hoding, ni vijana kutoka Ujerumani wako kwenye Kituo cha Miyuji *Cheshaya Home* ambayo iko chini ya Kanisa Katoliki chini ya *Caritas.* Kwa hiyo, tunawakaribisha na mjisikie mko nyumbani. Nitamwita Mwanasheria Mkuu, yeye nitampa dakika ishirini.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nimeomba kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa ili niweke baadhi ya kumbukumbu sawa sawa, lakini kabla ya kufanya hivyo, naomba kwanza kusema kuwa naunga mkono hoja, na kama ilivyo kawaida, nina-*declare*

*interest* kuwa na mimi pia ni mlinzi wa akiba nikiwa nina namba ya kutumikia Jeshi la Kujenga Taifa Na. 5010 *Operation* Usafi, na ninafahamu wengi pia ni kama mimi humu ndani *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nawaomba Waheshimiwa Wabunge waidhinishe makadirio haya kusudi wenzetu waweze kufanya kazi zilizo mbele yao. Pili, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa jinsi ambavyo amewasilisha hotuba yake na pia Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, pamoja na Mchungaji Israeli Natse Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara hii. Ninajielekeza katika mambo mawili muhimu, kwanza, ni hili suala la watu wanaodaiwa kuwa waliuawa na askari wa Jeshi la Ulinzi, lakini pia nitazungumza kama nitapata muda suala ambalo linaonekana kama ni mgogoro baina yetu na majirani zetu, ndugu zetu wa Malawi.

Mheshimiwa Spika, hili suala la watu watatu wanaodaiwa kupoteza maisha kutokana na kupigwa risasi na Wanajeshi wa Jeshi la Ulinzi, ni tukio na siyo asili. Eneo ambalo Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani alisema, tayari Askari hawa pamoja na baadhi ya wanavijiji wameshitakiwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Morogoro, na bado uchunguzi au upelelezi wa suala hili unaendelea. Nami niseme kuwa ninaishia hapo kwa sababu vyombo vya dola vinashughulikia suala hilo.

Mahusiano baina ya Jeshi letu na raia kwa ujumla ukilinganisha na nchi nyingine ni mahusiano mazuri. Nafikiri wote tunakubaliana kwenye hili. Matukio

machache yanayotokea ya Askari na raia kuhasimiana hayawezi kuchukuliwa kama ndiyo hulka ya Jeshi kama Taasisi. Nafikiri hilo pia tukubaliane, kwa sababu kuna wakati fulani pia tunapata taarifa kwamba raia wameumiza Askari, na haya ni matukio, siyo hulka kama ilivyowasilishwa, yaani kwa maana kwamba, ni *isolated incidences,* hatuwezi kuyafanya matukio haya kama ndiyo tabia ya Jeshi letu.

Mheshimiwa Spika, naomba kila tukio linalotokea lishughulikiwe kipekee kuliko kuyajumuisha yote. Baba Mchungaji, ninathubutu kusema kwamba haya matukio ambayo tunayarejea, hayawezi kuwa ni ushahidi kwamba Serikali imekosa sifa ya kumiliki nguvu za dola, kama unavyosema kwenye ukurasa wa nane, Mchungaji huyu ni mlezi wa roho, na roho yangu inafurahi nikimwona na ninathubutu kusema kuwa dola ya Tanzania ni imara sana na vyombo vyake ni imara sana Baba Mchungaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ila tumeanza kuona matukio ya Wanasiasa ambayo yanataka kuvidhalilisha au kuvinyong'onyeza vyombo hivi vya dola. Sisi ambao tunakaa kimya kwa sababu tunatafakari, tunaona kwamba, kwa mfano, kuna watu wamejitokeza, wamesema wanataka kuuawa na Maafisa Usalama wa Taifa na wakataja majina. Wengine wanasema *AG,* kwa nini usichukue hatua? Kutafakari kwingi kunaweza kuwa na matatizo! Lakini leo, nitasema maneno kidogo hapa. Tumeona jinsi ambavyo Idara, mhimili wa dola (Mahakama) ulivyodhalilishwa na hapa hapa Bungeni tumeona tena leo kwenye

maneno haya, Jeshi la Ulinzi la Tanzania na Jeshi la Wananchi.

Mheshimiwa Spika, mimi na nyinyi wale ambao tulibahatika kwenda *National Service* tunajua kuwa Jeshi letu baada ya mwaka 1964 lilipoundwa upya, *concept* ilikuwa ni kwamba Wanajeshi ni samaki na sisi raia ni maji na maji na samaki haviwezi kuachana. Wale wenzangu, *Operation* Chakaza na Usafi kwa waliokuwa *National Service* na wale Wanamgambo, kuna wenzangu walikuwa wanaambiwa huendi vitani, wanalia, wanataka kutembea kwa mguu waende kule kwa Wahangaza, kwa sababu Wahangaza watani zangu ni waoga, waandikishwe kule ili waende Uganda; na ndugu zangu wengine Wahaya, kwa sababu wanasema tutapigana pamoja na sisi, wengine tulikuwa Shule na Mheshimiwa Mayunga anakuja kuhamasisha anatuambia wewe baba yako anakuja analia kuwa mama yako amechukuliwa na mwanaume mwingine, wewe unasema unasoma! Unasoma nini? Sasa angalia *effect* yake kwa wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, lakini ninashangaa maneno yanayotoka kinywani kwa baadhi yetu. Sikutegemea kabisa kuwa tunaweza kudhalilisha vyombo hivi. Baadhi ya kauli zetu sisi viongozi zinaelekea kwenye uchochezi. Nitasema leo kidogo. Tunayo Sheria ya Kanuni ya Adhabu *(penal code,)*naomba Waheshimiwa Wabunge tuisome kwa sababu sisi wote ni viongozi, tunaweza kupotoka, lakini tukielekezana tutarudi kwenye mstari.

Ukienda kwenye kundi ambalo linafanya fujo na katika kundi hilo kukatokea mauaji, Mheshimiwa ukisoma kifungu cha 23 cha Kanuni ya Adhabu, unaweza kuwa na wewe umo. Tuepuke haya mambo. Ukisoma kifungu kile cha 55 kinaonyesha vitendo ambavyo ni vya kichochezi, someni tuelewane, kazi yangu ni kulinda viongozi wa pande zote. Mimi sina Chama na mnafahamu, na sioni aibu kusema hivyo, ila kadi yangu ya zamani ninayo sandukuni kama *souvenir,* ninasema wazi. *(Vicheko)*

Mheshimiwa Spika, nyinyi wote ni viongozi na kazi yangu ni kuwalinda viongozi, ninapoambiwa nimkamate kiongozi wakati fulani nasita, lakini sasa nitaanza kutumia ile kalamu yangu ya *magenta*. Ombi langu ni kwamba Waheshimiwa Wabunge someni Sheria ya Usalama wa Taifa, someni Sheria ya *Penal code* ili twende pamoja, sitaki kurudia tukio la Singida juzi, lakini Serikali na vyombo vyote vya Upelelezi vinafanya kazi na tayari watu sita wameshakamatwa na wawili wanatafutwa ili waandikishe maelezo. Nawaomba wale ambao wataombwa, watoe ushirikiano wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nasema hivi, bila kumwelekeza mtu yoyote, lakini kama kuna Mbunge ambaye ataombwa, tunaomba mtoe ushirikiano wa kutosha na kama utapata uoga, njoo uniambie, tutakwenda wote.

Mheshimiwa Spika, kuna suala linaloonekana kama mgogoro baina yetu sisi na wenzetu wa Malawi. Historia ya jambo hili lina umri, kama nchi yetu na kama

Malawi limeanza siku nyingi sana. Wanahistoria wale ambao wanajua *Scramble of Africa,* wanajua jinsi Wazungu walivyogawana Afrika hii tarehe 23 Februari, 1890 Wajerumani walikuwa wanatawala Tanganyika, waliwekeana sahihi na Waingereza waliokuwa Malawi kuhusu mipaka. Lakini wale waliosoma zamani, wanajua, pia Mheshimiwa Profesa Kahigi utanisahihisha kama nitakosea, wakati Wazungu hawa wanagawana Bara la Afrika walipokuwa wanafika kwenye maziwa walikuwa hawaweki mipaka.

Kwenye maziwa hapakuwa na mipaka, kwa hiyo, Waingereza na Ujerumani wakawekeana Mkataba kwamba katika kifungu kimoja wanasema mpaka kati ya Ziwa Nyasa, yaani Malawi na Tanganyika wakati huo utawekwa baadaye, lakini Waingereza na Wareno wakaweka mpaka ule chini ya Ziwa upande ule wa Ziwa unaitwa NIASA, lakini hii Nyasa ya kawaida ya kwetu kulikuwa hakuna mpaka. Baadaye Wajerumani wakafukuzwa baada ya vita ya Kwanza ya Dunia. Kwa hiyo, mazungumzo kati ya Mwingereza na Mjerumani hayakumalizika na ule mpaka haukumalizwa, lakini *practice* ni kwamba Wajerumani walikuwa wanakaa kwenye Visiwa katika Ziwa Nyasa na walikuwa wanaendesha meli katika Ziwa Nyasa na Waingereza hawakupinga.

Mheshimiwa Spika, katika mazungumzo, tunasema kwamba haya mambo tunaelewana, baadaye kuna historia ndefu kidogo hata humu katika Bunge mwaka 1960/1961 kuna matamshi yalitolewa kuhusiana na mpaka wetu huu, Serikali ya Tanzania na Malawi wameunda *Taskforce,* wataalam na kwetu sisi

tunaratibiwa na Wizara ya Ardhi kwa ajili ya kuzungumzia mpaka huu. Sina wasiwasi kwamba tutafikia muafaka kwa sababu kuna vitu vingi ambavyo tunajiegemea sisi kwanza ni huo mkataba, lakini pia desturi katika Sheria za Kimataifa kwamba mnapo-*share* maji, mipaka ya maji huwa inakuwa katikati. Kuna wakati fulani nilikuwa nafundisha Malawi, kwa muda mfupi waliniomba katika Mahakama ya Biashara, nasema kwamba sisi hatudai ziwa Malawi kwa sababu sisi tuna letu linaitwa Ziwa Nyasa.

Upande wa kwetu huu unaitwa Nyasa na upande wa Malawi unaitwa Malawi, na ziwa lile ukienda katikati utaona maji mengine yanakwenda Malawi na mengine yanakuja Tanzania na kule chini ukienda kuna Msumbiji na Malawi. Kwa hiyo, hili jambo tutaelewana tu.

Kitu kingine ni ile Sheria ya *Law of the Sea,* Mkataba wa *Law of the Sea* unatuwezesha sisi kusema kwamba sisi tunadhani tuna haki kubwa kuliko ambavyo mwenzetu anavyosema kuwa ziwa lote ni lake, na tusingependa watu wa Ndumbi, watu wa *Mbambabay* kwamba wakitaka kwenda kuchota maji ziwani, wanaomba ruhusa wakitaka kuvua samaki wanaomba ruhusa, hiyo sidhani kama ndugu yetu ndiyo nia yake. Tutazungumza na tutaelewana. Tusipoelewana hatutapigana vita kwa sababu bado kuna *International Court of Justice,*na tunadhani tuna sababu kubwa sana, lakini pia tunategemea *reports,* vitabu vya *crown agents* vya Serikali ya Malawi 1928, 1927, 1938, na 1937 ambavyo vinaonyesha hivyo na kuna kitabu vingine pia tulichopewa na Baba wa Taifa,

kile kinakaa kwa *AG* Mheshimiwa Chenge, alimpa Mheshimiwa Mwanyika na Mheshimiwa Mwanyika alinipa mimi, tunapokezana, kwasababu Mwalimu alisema kwamba kukitokea shida, someni kitabu hiki. Kwa hiyo, tuko sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona nichangie kuhusu mambo hayo, lakini kubwa mimi ningeomba Waheshimiwa Wabunge kama viongozi, ningeomba tuwe waangalifu sana tunapotoa matamko yetu ndani ya vyombo hivi, au nje ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na ninamshukuru Mungu pia kwa kuniruhusu niseme, ahsanteni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu cha kwanza nilichosema ni kuunga mkono hoja, ninarudia tena ninaunga mkono hoja hii. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita mtoa hoja, muda wako ni saa moja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliopata fursa ya kuchangia katika hotuba yangu ya Makadirio na Mapato ya Matumizi. Waheshimiwa Wabunge waliopata nafasi ya kuchangia hoja hii ni 106. Kati yao Wabunge nane walichangia kwa kuzungumza na waliobaki wamechangia kwa maandishi. Naomba kuwataja Waheshimiwa Wabunge hawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Felix F. Mkosamali, Mheshimiwa Christina L. Mugwai, Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Rebecca M. Mngodo, Mheshimiwa Sabreena H. Sungura, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Philipa G. Mturano, Mheshimiwa David Z. Kafulila, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Abdul J. Marombwa, Mheshimiwa Dkt. Charles J. Tizeba, Mheshimiwa Angellah J. Kairuki, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Subira K. Mgalu, Mheshimiwa Zabein M. Mhita, Mheshimiwa Saidi M. Mtanda, Mheshimiwa Said A. Arfi, Mheshimiwa Moshi S. Kakoso, Mheshimiwa Capt. George H. Mkuchika, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Henry D. Shekifu, Mheshimiwa Eng. Omary R. Nundu, Mheshimiwa Ester A. Bulaya, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Salome D. Mwambu, Mheshimiwa Lazaro S. Nyalandu, na Mheshimiwa Fatuma A. Mikidadi. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, Mheshimiwa John J. Mnyika, Mheshimiwa Vincent J. Nyerere, Mheshimiwa Nyambari C. M. Nyangwine, Mheshimiwa Nassib Suleiman Omar, Mheshimiwa William M. Ngeleja, Mheshimiwa Prof. Peter M. Msolla, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Clara D. Mwatuka, Mheshimiwa Naomi M. Kaihula, Mheshimiwa Rosweeter F. Kasikila, Mheshimiwa Amina A. Clement, Mheshimiwa Felister A. Bura, Mheshimiwa Saada M. Salum, Mheshimiwa Charles J. P. Mwijage, Mheshimiwa Peter S. Msigwa, Mheshimiwa Alphaxard K. N. Lugola, Mheshimiwa Goodluck J. Ole-Medeye, Mheshimiwa

Kheir Ali Khamis, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Augustino M. Masele, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Thuwayba Idrisa Muhamed, Mheshimiwa Dkt. Hadji H. Mponda, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Halima J. Mdee, Mheshimiwa Deogratius A. Ntukamazina na Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Asha Athuman Hamad, Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy, Mheshimiwa Moza Abedi Saidy, Mheshimiwa Desderius J. Mipata, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Juma Othman Ali, Mheshimiwa Ignas A. Malocha, Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mheshimiwa Othmani R. Mfutakamba, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mheshimiwa Anastazia J. Wambura, Mheshimiwa Abia M. Nyabakari, Mheshimiwa Dkt. Cyril A. Chami, Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh, Mheshimiwa Job Y. Ndugai, Mheshimiwa Jitu V. Soni, Mheshimiwa Ritta E. Kabati, Mheshimiwa Majaliwa K. Majaliwa, Mheshimiwa Lolesia J. M. Bukwimba, Mheshimiwa Mendrad L. Kigola na Mheshimiwa Hawa A. Ghasia. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Sylveter Massele Mabumba, Mheshimiwa Janet Z. Mbene, Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu, Mheshimiwa Assumpter N. Mshama, Mheshimiwa Cecilia D. Paresso, Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mheshimiwa Salum H. Barwany, Mheshimiwa Profesa Kulikoyela K. Kahigi, Mheshimiwa Faki Haji Makame, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Pereira Ame Silima, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Muhammad

Ibrahim Sanya, mheshimiwa Amina N. Makilagi, Mheshimiwa Moses J. Machali, Mheshimiwa Zaynab M. Vullu, Mheshimiwa Christowaja G. Mtinda, Mheshimiwa Mathias M. Chikawe, Mheshimiwa Dunstan D. Mkapa, Mheshimiwa Dkt. Abdallah O. Kigoda, Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Mheshimiwa Meshack J. Opulukwa, na Mheshimiwa Betty E. Machangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Dkt. Augustine L. Mrema, Mheshimiwa Salvatory N. Machemli, Mheshimiwa James F. Mbatia, Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mheshimiwa Iddi M. Azzan, Mheshimiwa Dkt. Kebwe S. Kebwe, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge waliopata nafasi ya kuchangia hoja hii kwa kuzungumza ni hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis, Mheshimiwa Deo K. Sanga, Mheshimiwa Christowaja G. Mtinda, Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mheshimiwa Jaddy Simai Jaddy, Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mheshimiwa Dkt. Kebwe S. Kebwe na Mheshimiwa Jaji Fredrick Werema - Mwanasheria Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri majina haya hatuyajumuishi katika muda wako uliopewa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa hoja zilizotolewa ni nyingi sana na kutokana na muda kuwa

kidogo, sitaweza kuzitolea ufafanuzi na kuzitolea majibu zote, nitatoa majibu ya baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge na majibu ya hoja zitakazobaki, nitatoa kwa njia ya maandishi na kuyawasilisha kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa maelezo ya ufafanuzi wa hoja mbalimbali, napenda kusema maneno ya jumla mawili. Kwanza, nawashukuru sana Wabunge wote waliopata nafasi ya kuchangia, wametoa michango mizuri sana, wametupa mapendekezo na ushauri mzuri sana, sisi katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa tutaufanyia kazi ushauri na mapendekezo waliyotupa. Lakini pili, tunafarijika sana na kauli za Wabunge wote wa Kambi ya Upinzani na Wabunge wa Chama Tawala, sote kwa ujumla tunakubaliana kwamba Serikali inao wajibu wa msingi wa kuwekeza fedha za kutosha kwa ajili ya kuliimarisha Jeshi la Ulinzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali ina wajibu wa msingi wa kuhakikisha kwamba Jeshi la Wananchi wa Tanzania linatengewa fedha za kutosha ili liweze kutekeleza jukumu lake la kulinda mipaka ya nchi yetu na usalama wa nchi yetu kwa ujumla. Kazi hii haiwezi kufanywa na mtu mwingine. Hapana shaka hakuna Taifa au hakuna mtu anayeweza kufanya kazi hii tofauti na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, maendeleo na mafanikio ya Jeshi hususan wakati wa amani na wakati wa vita hutegemea sana umoja wa Jeshi, wananchi

na Serikali yao, ni muhimu basi suala hili likalindwa wakati wote. Mwanafalsafa mmoja wa zamani wa China, Bwana **Tsung** aliyeishi karne ya 500 B.C., aliwahi kusema kwamba ili kupata mafanikio katika vita, hatua zifuatazo ni muhimu kutekelezwa dhidi ya adui kabla ya kuanza vita hivyo. Hatua ni kama zifuatazo:-

Kwanza ni kuhakikisha unaitenganisha Serikali unayotaka kupambana nayo na wananchi wake; jambo la pili, ni kuhakikisha unatenganisha Serikali na Jeshi lake; na hatua ya tatu, ni kuhakikisha unatenganisha Jeshi na wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, nimeona ni vema niyanukuu maneno haya ya Mwanafalsafa wa Kichina kwa sababu zinaanza kujitokeza dalili na wakati mwingine za kutisha za kuyafanya au kudhihirisha yale ambayo Mwanafalsafa wa Kichina aliyasema karne nyingi zilizopita. Tumeanza kuwasikia baadhi ya wanasiasa ndani ya Bunge na nje ya Bunge wakianza kuonyesha dalili za kukosa imani na usalama wa Taifa. Baadhi yao wanakosa imani na Polisi, na baadhi yao wanaonesha kukosa imani na Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Jambo hili ni jambo la hatari sana.

Mheshimiwa Spika, watu makini na wenye akili timamu wanaposikia na kuona dalili hizi tatu alizozizungumza Mwanafalsafa wa Kichina wakiziona hawapaswi kukaa kimya. Ni jambo la hatari sana tukiziachia ziendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maslahi ya amani na usalama wa Jamhuri ya Tanzania, nawasihi,

nawashauri wanasiasa nikiwemo na mimi mwenyewe kupima na kuchagua maneno tunayotumia, hasa wakati tunapovizungumza vyombo vya ulinzi na usalama, vyombo ambavyo tumevikabidhi dhamana ya kutulinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina sababu ya kuwaziba watu midomo kukosoa pale panapostahili kutoa kasoro zinazojitokeza katika vyombo hivyo, lakini ni busara tu kuwa na uchaguzi mzuri wa maneno.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu, kuna migogoro mingi ya ardhi, inayolihusisha Jeshi la Wananchi wa Tanzania na wananchi kwa upande mwingine. Migogoro hii ipo mingi na sitaweza kuitaja yote hapa, nina hakika migogoro yote hii tunaielewa. Wapo baadhi ya Wabunge na wananchi wanaamini kwamba Jeshi la Wananchi wa Tanzania linavamia maeneo ya wananchi. Mimi sikubaliani na kauli hii.

Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba Jeshi la Wananchi lina utaratibu wa kuvamia maeneo ya wananchi. Kwanza, Jeshi la Wananchi wa Tanzania linapewa maeneo na Serikali kwa ajili ya ulinzi wa nchi yetu. Inawezekana wakati Jeshi la Wananchi linapokabidhiwa maeneo hayo, inawezekana sana ama, maeneo hayo hayajapimwa vizuri na kutolewa hati, ama inawezekana yametolewa hati lakini wananchi hawajalipwa fidia. Naomba niwahakikishie Wabunge kwamba tutalifanyia kazi jambo hili pale ambapo wananchi wenye haki na wanaostahili, maana ni jukumu la Serikali pale ambapo chombo cha

Serikali kimechukua eneo la wananchi kwa ajili ya shughuli za umma, basi kwa mujibu wa taratibu zetu, chombo hicho au mtu huyo anapaswa kufidiwa. Kwa hiyo, tutafanya jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia ukweli upo kwamba, wapo baadhi ya wananchi wanaoingiwa na tamaa, wamekuwa wakivamia maeneo ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Hata kwenye michango ya baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, wamesema Jeshi la Wananchi lina maeneo makubwa. Ndiyo, Jeshi la Wananchi lina maeneo makubwa, lakini tukiamua maeneo haya kuyatoa, siku moja tunaweza kujuta kwa uamuzi huo. Kwa sababu kama nilivyosema kwenye hotuba yangu kwamba Jeshi lipo kwa sababu Wananchi wa Tanzania wapo. Tunalihitaji sana kwa ajili ya shughuli za ulinzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Jeshi linakabidhiwa maeneo makubwa, lakini shughuli zao za ulinzi zinahitaji matumizi makubwa ya ardhi. Kwa sababu kuna wakati wanahitaji kufanya mazoezi na mazoezi haya siyo ya kupigana ngumi, mazoezi haya ni kutumia silaha na silaha zinaua, na kwa maana hiyo, inabidi maeneo ambayo wananchi wanaishi yanatakiwa kutengwa na Jeshi. Lakini kama mnavyojua, Jeshi hili lina silaha, silaha hizi nyingine ni za hatari. Tumeona katika baadhi ya maeneo zikilipuka zinaleta maafa kwa raia, ndiyo maana Serikali na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa tumekuwa tukiwasihi sana wananchi wasipende kuishi karibu na maeneo ya Jeshi kwa sababu hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini wapo baadhi ya wananchi wakiona eneo la Jeshi lina vichaka hivi, na miti na magugu makubwa, basi wao hupenda kupeleka ng'ombe wao. Jambo hili ni hatari. Vichaka vile, magugu haya, ni maficho, tunayahitaji. Sasa ni vizuri mambo haya wananchi wakaelewa. Lakini kwa kuwa tunatambua kwamba Jeshi la Wananchi wa Tanzania lipo kwa ajili ya Wananchi wa Tanzania, na jina hili la Jeshi la Wananchi wa Tanzania halikutokea kwa bahati mbaya, Waasisi wa Taifa hili akiwemo Mwalimu Nyerere alikusudia kwamba hili Jeshi lipo kwa ajili ya maslahi ya wananchi wa Tanzania kulinda Uhuru wa wananchi wa Tanzania. Kwa maana hiyo, wakati mwingine tunapoona kuna migogoro kati yetu na wananchi hasa inayohusiana na mipaka, tumekuwa hatusiti kuitatua migogoro hiyo kwa njia ya amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mifano ya maeneo ambayo Jeshi la Wananchi wa Tanzania tumebadilisha mipaka yetu ili tuwasaidie wananchi waendelee kutumia ardhi katika maeneo yenye migogoro. Eneo la Kunduchi katika Jimbo la Mheshimiwa Halima Mdee, kulikuwa na tatizo la mipaka kati ya wananchi, tumebadilisha mipaka na kuwasaidia wananchi; eneo la Chukwani kulikuwa na tatizo hilo, *Tanganyika Packers* Arusha kulikuwa na tatizo hilo tumebadilisha mipaka, *Lugalo Barracks* tumefanya hivyo, eneo la Gongo la Mboto pia tumefanya hivyo. Kwa ujumla niseme kwamba tutaendelea kushirikiana na wananchi, lakini ni wito wetu kuwaomba wananchi wa Tanzania na wao waendelee kuheshimu maeneo ya Jeshi ili tuendelee

kujenga mahusiano mema kati ya raia na Jeshi la Wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa migogoro hii ya mara kwa mara iliyokuwa ikitokea, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali za Mikoa na Halmashauri za Wilaya itaendelea kuyapitia maeneo yote yenye migogoro ya ardhi kama nilivyosema awali, kwa lengo la ama kufufua mipaka ya Makambi yaliyokwishapimwa na kuyapatia hati rasmi ama maeneo ambayo hayajapimwa yapimwe rasmi na wale wananchi ambao wataathirika katika maeneo ambao wanayo haki, tutaendelea kutoa fidia kama nilivyosema hapo awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mchango wake Mheshimiwa Kebwe alisema baadhi ya Kambi za Jeshi la Wananchi wa Tanzania ziko katikati ya Mji. Ni kweli. Niliwahi kumsikia mtu mmoja akisema mawazo yanayofanana na hoja aliyoeleza Mheshimiwa hapa, amesema Mheshimiwa Waziri kwa nini Jeshi la Wananchi wa Tanzania haliondoki kwenye maeneo ya Dar es Salaam na kuhamia porini? Mimi nilimpa hoja tu nikamwambia, kama askari amepewa jukumu la kulinda jengo la Bunge na akaamua kukaa katika uwanja wa Shehe Amri Abeid, atakuwa analinda Bunge au analinda Uwanja wa Shehe Amri Abeid? Akanitazama. *(Makofi)*

Sasa ninachokusudia kusema ni kwamba Jeshi la Wananchi wa Tanzania pale Dar es Salaam unapowaona Mjini wanayo kazi ya kulinda ule Mji wa Dar es Salaam, utakapowaondoa kuwapeleka porini

wanakuwa hawafanyi tena kazi ya kulinda Mji wa Dar es Salaam watakuwa wanalinda pori na wanyamapori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu hoja ya vijana kwa mujibu wa sheria, nakiri kwamba, ni kweli idadi ya vijana ambao tumeamua kuwachukua mwaka huu wa fedha 5,000 ni ndogo sana ikilinganishwa na idadi ya vijana wanaostahili kujiunga na JKT kwa mujibu wa sheria. Lakini hali hii imesababishwa na ufinyu wa bajeti. Laiti tungekuwa na uwezo mkubwa, basi tungeweza kuchukua zaidi ya vijana 20,000 kwa mara moja. Lakini gharama ya kuwachukua vijana 20,000 kwa kipindi cha miezi sita tu, ni karibu Shilingi bilioni 140. Bila shaka tutaona kwamba hiki ni kiasi kikubwa sana fedha. Lengo la Serikali ni kuwachukua vijana wote wanaostahili kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria pale tutakapokuwa na uwezo. Hata hivyo, lengo hilo hatutaweza kulitekeleza kwa mwaka huu kama nilivyosema.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana pia na hoja ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu kuongezwa kwa muda wa mafunzo kutoka wiki tatu hadi wiki nne au sita hivi. Muda huu tukubaliane na hoja hiyo, lakini jambo la msingi la kufikiria hapa iwapo tutaongeza muda kutoka wiki tatu za awali kama tulivyosema na kutoa mafunzo ama kwa wiki sita ama miezi mitatu. Bila shaka muda huu utakuwa unaingiliana na muda wa Bunge. Sina hakika kama Waheshimiwa Wabunge hao baadaye hawatatoa visingizio vya kutaka kurudi katika majimbo yao hasa mambo yanapopamba moto katika mafunzo. Sina hakika! Lakini kwa kuwa mmelitaka

wenyewe la miezi mitatu tutalifanyia kazi na bila shaka tunakubali wazo hilo. Aidha, tunaukubali ushauri, Waheshimiwa Wabunge ambao siyo vijana wanaopenda kujiunga na mafunzo haya tunawakaribisha tu waanze kujiorodhesha majina yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine iliyowasilishwa hapa, Serikali iweke utaratibu wa kushughulikia madeni binafsi ya wanajeshi na kuepuka kuongezeka kwa madeni yasiyolipika. Napenda kutoa maelezo yafuatayo, mapendekezo na maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama tumeyapokea na tutayafanyia kazi. Aidha, kwa sasa madeni yote ya Wanajeshi pamoja na Wazabuni yamewasilishwa Hazina kwa ajili ya kuombewa fedha za kulipia madeni. Jumla ya madeni yote hayo ni karibu Shilingi bilioni 44.4.

Kuhusu kasi ya kukamilisha mapitio ya Sheria ya Ulinzi wa Taifa Sura 192 na ile ya Jeshi la Kujenga Taifa sura ya 533, mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Ulinzi wa Taifa Cap. 192 unaendelea. Halmashauri ya Majeshi ya Ulinzi ilishapitisha marekebisho hayo. Wadau mbalimbali akiwemo Mwanasheria Mkuu wa Serikali walipelekewa mapendekezo ili watoe maoni yao. Mwanasheria Mkuu wa Serikali alitoa mchango mkubwa na kushauri kuwa kwanza ipitishwe Sera ya Ulinzi wa Taifa kwanza, halafu baadaye ndiyo marekebisho ya Sera ya Ulinzi wa Taifa yapelekwe katika Baraza la Mawaziri. Hata hivyo, Sheria hii hivi sasa inasubiri maoni ya Sera ya Taifa ya Ulinzi kutoka Zanzibar ambayo tulimkabidhi Mheshimiwa Waziri wa

Nchi, Ofisi ya Rais anayeshughulikia Vikosi vya SMZ tarehe 8 Juni, 2012. Kwa hiyo, maoni hayo yatakapokuwa tayari, tutayafanyia kazi ili hatimaye tukamilishe utayarishaji wa sera na hatimaye tuangalie marekebisho ya Sheria.

Hoja ya tatu ya Kamati hiyo, Serikali iweke fedha za kutosha kwa ajili ya Chuo cha Ulinzi wa Taifa, yaani *National Defence College* za kuendesha mafunzo kwa watu wanaokusudiwa na kutolewa kwa wakati. Serikali itatenga fedha za kutosha za kuendesha mafunzo haya za Chuo hicho cha Ulinzi wa Taifa kwa kuzingatia hali halisi ya Bajeti ya Serikali. Gharama za kuendesha mafunzo katika Chuo hiki ni kubwa. Hata hivyo, wanafunzi watakaoanza mafunzo kwa mwaka huu wa fedha 2012/2013 gharama za mafunzo zitalipwa na Wizara, Idara na Taasisi zitakazowapeleka wanafunzi katika Chuo hicho. Chuo hiki kimetangazwa na kuanzishwa rasmi *(The Defence Forces Establishment of the National Defence College Order, 2012 GN 75)* ya tarehe 9 Machi, 2012.

Ushauri wa nne, Serikali ijipange kuongeza idadi ya vijana watakaojiunga na mafunzo ya JKT kwa mujibu wa Sheria kutoka idadi itakayoanza na vijana 5000. Mapendekezo pamoja na ushauri huu uliotolewa na Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama tumeyapokea kwa moyo mkunjufu na tutayafanyia kazi.

Wazo la tano, ni Makampuni ya kigeni yasiruhusiwe kuweka walinzi wao ili kudhibiti kuzagaa na matumizi mabaya ya silaha. Hakuna Kampuni

yoyote ya kigeni ambayo imeingia au imeruhusiwa kufanya shughuli za ulinzi katika bahari yetu ikiwa na silaha nzito. Kama kuna taarifa hizo, tunaomba Waheshimiwa Wabunge watuwasilishie taarifa hizo ili tuweze kuzifanyia kazi na hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani ametoa hoja ifuatayo: Anasema iwapo matrekta 1846 yaliyotolewa bandarini yametolewa kwa gharama ya Sh. 4,048,025,331/=. Gharama ya kuondoa trekta moja kwa maana hiyo ni Shilingi ngapi, na gharama hizi ni za kitu gani? Napenda kumjibu Mheshimiwa Natse kama ifuatavyo:-

Shirika la Suma JKT lilipokea shehena ya makontena 454 yaliyokuwa na vipande vya matrekta ambayo havikuunganishwa pamoja na zana zake, pampu za kusukuma maji, vipuri na vifaa vya karakana. Kwa maana hiyo, halikuletwa trekta moja moja. Kiasi hicho cha fedha nilichokitaja hakikuhusishwa na utoaji wa matrekta peke yake au makontena hayo 450 kama nilivyosema awali, bali kilitumika kwa utoaji wa mizigo yote iliyokuwemo kwenye makontena hayo. Gharama hizo zilikuwa ni za mambo yafuatayo:-

Kwanza, kodi za msingi, bandari na kwa wakala wa meli; pili, gharama ya uhifadhi wa makontena kwa makampuni ya bandari ya nchi kavu; tatu, gharama za adhabu ya kuchelewesha makontena kwa makampuni ya wakala wa meli ambayo ni

*Mediterranean Shipping Company* na *Safmarine* na *Sea Trade.*

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Kwa nini JWTZ limechelewa kununua meli za kivita kwa ajili ya Kamandi ya Wanamaji? Ni kweli, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imechukua muda mrefu kununua meli za kivita, lakini naomba kuwafahamisha Waheshimiwa Wajumbe kwamba iko tofauti kati ya kununua shati mnadani na kununua meli za kivita.

Mheshimiwa Spika, ununuzi wa meli za vita una mchakato unaohitaji umakini wa hali juu sana. Kwa maana hiyo basi, tulilazimika kuwapeleka China Watalaam wetu wa masuala ya meli za kivita ili waweze kuziona meli hizo tunazotarajia kuzinunua China. Mkuu wa Kamandi ya Wanamaji Meja Jenerali S. S. Omar mwishoni mwa mwezi uliopita alikwenda China kwa ajili ya kazi hiyo ili kuangalia.

Sasa baada ya hatua hiyo, tunatarajia mchakato huu wa kupata meli za kivita utakamilika mwezi Septemba, mwaka 2012. Lakini katika hatua tu ya kulipa, maana huwezi kulipa halafu kesho ukaweza kuipata hii meli. Inaweza kuchukua muda kati ya mwaka mmoja mpaka mwaka mmoja na nusu. Sasa mwezi Septemba, tunatarajia kukamilisha taratibu za malipo kwa sababu baadhi ya fedha, tayari zimeshatengwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tunatarajia ifikapo Desemba mwaka huu, 2012 Serikali ya Watu wa China

itatupa msaada wa meli moja ya kivita. Tunategemea kwamba meli hiyo itakapofika, inaweza kutoa mchango na msaada mkubwa sana. *(Makofi)*

Pia Jeshi la China, kwa kupitia Kampuni moja ya Kichina inatarajia kutupatia meli nyingine ambazo zimeshatumika, lakini hazikutumika muda mrefu. Tunatarajia meli hizo baada ya kufanyiwa matengenezo na zikawa katika hali nzuri kufika katika kipindi kati ya miezi sita. Kwa hiyo, kwa ujumla, hizo ndizo hatua ambazo sisi Wizara ya Ulinzi tunazichukua ili kuhakikisha kwamba tunapata meli za uhakika ambazo zitasaidia sana katika kufanya doria.

Hoja ya tatu, kulikuwa na hoja kwamba: Je, Serikali inawezekana kuzipiga marufuku Kampuni za ulinzi binafsi zinazotoa ulinzi kwa Makampuni ya gesi na mafuta hivi sasa? Napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Makampuni haya binafsi ya Ulinzi yameingia Mkataba wa Ulinzi na Makampuni ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia na wameingia makubaliano hayo na Makampuni yenye meli za utafiti baada ya kuona kwamba Kamandi ya Jeshi la Wanamaji halikuwa na vyombo vingi kama walivyotarajia wao.

Kwa kawaida, wanapenda Kampuni ambazo zinachimba na kutafuta mafuta, wanapenda sana kuwe na meli ambayo inakaa pale pale kuangalia uchimbaji wa mafuta bila kuondoka. Sasa sisi kutonana na uchache wa vifaa vyetu, mara nyingi haviwezi

kutumika katika utaratibu huo. Vifaa vyetu vinakuwa vinafanya kazi ya doria.

Jeshi la Wananchi wa Tanzania linashirikishwa pale Kampuni hizi zinapopewa leseni au vibali vya kufanya kazi hiyo. Jeshi hivi sasa linatumia muda huu wa kipindi cha mpito, hiki kipindi ambacho nimesema tunatarajia tunaweza kupata meli za kivita, tutatumia muda huu kujiimarisha na hatimaye kuchukua hatamu ya ulinzi katika eneo hilo.

Aidha, jeshi linajiandaa kufanya makubaliano na Makampuni hayo kupitia Shirika la Maendeleo *(TPDC)* ili kutekeleza jukumu hilo la ulinzi kikamilifu.

Kutokana na sababu nilizoziainisha hapo juu, kwa sasa hatuwezi kuzipiga marufuku mara moja Kampuni za Ulinzi binafsi mpaka hapo tutakapohakikisha kwamba Mikataba yao isichukue muda mrefu. Yale Makampuni ambayo mikataba yao itamalizika katika kipindi cha karibuni, tutaishauri basi wasiingie katika Mikataba mingine mipya wakati Jeshi la Wananchi wa Tanzania likijiandaa katika kuchukua hatua hiyo.

Mheshimiwa Spika, hoja ya nne iliyotolewa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani: Jeshi la Wananchi wa Tanzania linachukua hatua gani kulinda usalama wa maeneo ya Ziwa Victoria na Ziwa Nyasa?

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi ndilo lililokabidhiwa jukumu la kushughulikia vitendo vya ujambazi vinavyotokea katika Ziwa Victoria na maeneo mengine. Hata hivyo, kutokana na

kuongezeka kwa vitendo vya ujambazi katika eneo la Ziwa Nyasa, Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeshaagizwa na Serikali kuchukua hatua za kuidhibiti hali hiyo. Hivi sasa Mkoa wa Mwanza, kwa mfano, umelipatia Jeshi la Wananchi wa Tanzania, eneo kwa ajili ya kuweka Gati ya Meli za Kivita katika Ziwa Victoria ili kuimarisha ulinzi na usalama katika eneo hilo. Kama mnavyojua, zamani Jeshi la Wananchi wa Tanzania lilikuwa likilinda eneo la Ziwa Nyasa lakini baadaye liliamuliwa kuondoka, mwaka 1973 baada ya Serikali kubaini kuwa, hakukuwa na tishio kubwa la usalama. Hivi sasa Jeshi la Wananchi wa Tanzania linakamilisha mpango mahususi wa kurejesha ulinzi katika eneo hilo la Ziwa Nyasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpango huu unatarajiwa kuanza katika Mwaka huu wa Fedha wa 2012/13 na hatua hii itahusisha kufunguliwa kwa viteule vya Jeshi la Nchi Kavu *(Detachment).* Jechi la Wanamaji na Jechi la Anga pia litakuwa na Viteule vyake kwenye eneo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya tano, sababu za kusitisha mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria zimekwisha? Ili utaratibu huu wa kuwachukua vijana kwa mujibu wa Sheria uwe endelevu, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Kama tunavyojua, katika kipindi cha mwaka 1990, nchi yetu kama ilivyo nchi nyingine za dunia ya tatu, ilikumbwa na matatizo makubwa sana ya kuichumi. Kwa mantiki hiyo basi, Serikali ililazimika sana

kupunguza matumizi yake katika baadhi ya maeneo na kwa mnasaba huo, Jeshi la Kujenga Taifa liliathirika na halikuweza kuchukua vijana wa kujiunga na mafunzo hayo kama nilivyosema. Hata hivyo, Serikali yenu imebaini kuwa kusitishwa kwa zoezi la kuchukua vijana kwa mujibu wa Sheria, kumesababisha mmomonyoko mkubwa wa maadili miongoni mwa Vijana wa Kitanzania. Aidha, Serikali imebaini kuwa vijana wengi hivi sasa ambao wanakosa mafunzo ya kuwapatia uzalendo, wanakosa mafunzo ya uvumilivu, nidhamu na ubunifu. Kwa hiyo, Serikali sasa imelazimika kurejesha utaratibu huu kuanzia Mwaka huu wa Fedha wa 2012/13 ili kuwajenga tena vijana kuwa na moyo wa uzalendo na ubunifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja ya sita, Jeshi la Wananchi wa Tanzania lina mkakati gani wa kuwaendeleza Wataalam wa Sekta ya Kilimo, Madawa na Mifugo? Jeshi la Wananchi wa Tanzania limekuwa na kawaida ya kuwapeleka askari na maafisa wake katika vyuo mbalimbali ili kujifunza taaluma mbalimbali. Kwa mfano, hivi sasa Jeshi la Wananchi wa Tanzania lina wanafunzi wanaosoma kada hizo katika Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, Vyuo vya Uyole na Tengeru ili kujipatia maarifa mbalimbali ya shughuli za kilimo. Jeshi la Wananchi wa Tanzania pia limewapeleka vijana wake wengi nje ya nchi kujifunza shughuli mbalimbali katika taaluma ya sayansi.

Mheshimiwa Spika, hoja ya saba, JKT inachukua hatua gani za dharura ili kuijengea taswira njema ya SUMA JKT kutokana na vitendo vya ubadhirifu? Sina hakika kama Taasisi ya Umma, Afisa wake mmoja au

mfanyakazi anapofanya vitendo vya ubadhirifu kama taasisi nzima inahukumiwa kwa kitendo hicho. Sina hakika, na kama huu ndiyo utaratibu, basi ya Uongozi utakuwa mgumu sana, maana leo itakuwa Taasisi ya Serikali, siku moja itakuwa Chama cha Siasa, akitokea mwizi mmoja kwenye Chama cha Siasa, kinapoteza haki na imani mbele ya jamii. *(Makofi)*

Hata uongozi katika familia, mtu mmoja akimnyonga mtu mwingine, familia nzima inawajibika kwa kufanya kosa hilo. Mimi nilidhani mfanyakazi wa taasisi fulani anapofanya kosa la kuvunja Sheria, vyombo vinavyohusika vinapaswa kuchukua hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme jambo moja; kazi ya Kiongozi si kuwazuia watu kufanya makosa, hatuna uwezo huo. Watu wanapofanya makosa, zichukuliwe hatua pale pale, hiyo ndiyo kazi ya Uongozi. *(Makofi*)

Suala la tuhuma za Watendaji wa SUMA JKT kwa sasa lipo Mahakamani na nina hakika Mahakama itatumia weledi wake kuwahukumu wale wenye hatia, wataingizwa kwenye hatia na wasio na hatia wataachiwa huru. Hata hivyo, Wizara yangu ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, tayari imeshachukua hatua kadhaa na nitazitaja; kwanza, wiki iliyopita nimemteua Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la SUMA JKT, Brigedia Jenerali Kilo;ni mtu makini, nina hakika anao uwezo wa kusimamia kazi hiyo. Nimekuwa nikitafakari sana juu ya jambo hili maana utendaji wa SUMA JKT umekuwa ukinisononesha sana, siridhiki. Naomba niseme ukweli

siridhiki na ndiyo maana nikaona nichukue hatua mapema za kutafuta Kiongozi ambaye anaweza kusimamia kazi hii. Naomba tumpe moyo na nguvu. Endapo baada ya mwaka mmoja au miwili atakuwa hamudu kazi, sisi tunao vijana wengi katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kazi hiyo tutamtafuta mtu mwingine na kama nae atakuwa hamudu na tunadhani yuko Mtanzania nje ya chombo chetu au nje ya Wizara anao uwezo wa kufanya kazi hii kwa uaminifu na uadilifu, tunaweza kumfikiria wakati huo ukifika.

Jambo la pili ambalo tumechukua hatua na nimetangaza kupitia Bunge lako Tukufu kwamba, kama kuna Mtanzania yeyote ambaye ni raia, hafanyi kazi katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania, anao uwezo wa kuwa Mkurugenzi wa Vitega Uchumi, anao uweledi, utaalamu, siyo utaalamu wa kwenye makaratasi, ameshafanya biashara, anafahamu vizuri uwekezaji, maana nahitaji mtu makini.  Kwa nini nalizungumza jambo hili? Nimefanya utafiti katika muda ambao nimekuwa katika Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, nimeona tunao uwezo mkubwa sana kama tutautumia vizuri.  Hivi sasa nimeanzisha mashamba kama matano hivi ambayo tukiwa na uwezo, tunaweza kuwekeza fedha, kama hatuna uwezo na teknolojia tunaweza kumtafuta mtu makini mwenye uwezo tushirikiane nae. Kwa mfano, tunalo eneo la Ruvu lina maji ya kutosha na ardhi nzuri; tunalo eneo la Chita, ardhi nzuri, ina rutuba na ina maji ya kutosha, tuna eneo hapa Makutupora ni zuri kwa ajili ya kilimo cha zabibu; tunalo eneo Oljoro linaweza kutumika kwa mazao mbalimbali ikiwemo maharage; tunalo eneo

lingine Mafinga. Ndiyo maana nasema tunamhitaji mtu makini, mwenye uzoefu, mwenye uweledi katika masuala ya biashara na uwekezaji, atusaidie kuainisha wawekezaji walio makini, wenye mitaji tunayohitaji ili washirikiane nasi katika kuiendeleza SUMA JKT.

Waheshimiwa Wabunge wamesema, wanahitaji sana kuiona SUMA JKT kiwe ni chombo chenye uwezo wa kufanya shughuli za kilimo na biashara. Sasa naomba niwahakikishie kwamba, mimi ninayo dhamira hiyo ya kuibadilisha SUMA JKT liwe ni Shirika ambalo linafanya kazi kwa tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyasemi haya kwa sababu nataka kupendezesha tu masikio yenu hapana, nalizungumza kwa uchungu mkubwa kwa sababu jambo linanigusa. Wale wanaonifahamu, nikisema natenda na wakati mwingine sipendi sana kuzungumza lakini hupenda kutenda ili watu waone. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, naomba mshirikiane nami katika kutekeleza dhamira hiyo; uwezo tunao na sababu ya kufanya hivyo tunayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo imeelezwa na Waheshimiwa Wabunge wengi waliopata nafasi ya kuchangia wanasema hivi; sasa Jeshi la Wananchi wa Tanzania linakabiriwa na uhaba mkubwa sana wa nyumba kwa Maafisa na Askari na kutokana na hali hiyo, Wanajeshi wapatao kama 10,000 na ushee hivi, hivi sasa wanaishi nje ya Makambi. Jambo hili ni kweli, lakini naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba,

Serikali yenu inalitambua tatizo hili na wala hatukufunga mikono tu hivi hivi, tumeanza kuchukua hatua. Hatua ya kwanza kama nilivyoeleza katika Hotuba yangu ya Bajeti; tayari tumeshasaini mkopo wa fedha zipatazo Dola milioni 285 kutoka Exim Bank ya China na mkataba huu au mkopo huu ulitiwa saini tarehe 20 mwezi uliopita. Gharama yote ya ujenzi wa nyumba hizi za Askari wapatao 10,000 ni Dola za Kimarekani milioni tatu. Tukifanya hesabu, kuna upungufu wa kama Dola milioni 15.

Sasa hizi Dola milioni 15 ni mchango wa Serikali na tayari Serikali imeshaanza kutenga kama Dola milioni tano kwenye Bajeti hii ya Mwaka wa 2012/2013, lakini tumeziweka kwa thamani ya shilingi. Kwa hiyo, utaona kuna bilioni kama nane. Kwa hiyo, tutaifanya kazi hiyo katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka huu. Sasa Waheshimiwa Wabunge wale wanaodhani kwamba Serikali haitoi majibu; hivi tunahitaji majibu gani zaidi ya haya?

Mheshimiwa Spika, wazo lingine ambalo limetolewa na Waheshimiwa Wabunge wanasema, Maafisa na Askari wengi hivi sasa wana tatizo la nyumba, kwa hiyo, Serikali iwasaidie ili watakapostaafu waweze kupata nyumba bora na kwa mkopo nafuu. Naomba nitoe maelezo kama ifuatavyo:-

Hivi sasa Jeshi la Wananchi wa Tanzania tayari limeshafanya mazungumzo na kampuni mbili za ujenzi wa nyumba nafuu. Kampuni ya kwanza kufanya nayo mazungumzo na imeonesha dalili njema ya kutekeleza jambo hili ni *Msagara Investment Company*, ambayo

ina viwanja 2000 huko Bagamoyo. Kampuni ya pili ambayo imefanya mazungumzo na Jeshi la Wananchi wa Tanzania ni kampuni ambayo inaitwa *EVIK Company* ya China, ambayo ina viwanja vipatavyo 5000 huko Kigamboni.

Kampuni hizi zitakapoanza shughuli za ujenzi, basi nyumba hizo zikikamilika zitakabidhiwa kwa Maafisa hao na Maafisa hao watakatwa fedha kwa ajili ya kulipia mkopo huo kutoka kwenye mishahara yao. Kama nilivyosema awali, sitaweza kuzijibu hoja zote, hoja zilizobaki kwa kuwa sikupata nafasi za kutolea ufafanuzi na maelezo, nitatoa maelezo kwa maandishi na hatimaye nitawakabidhi Waheshimiwa Wabunge wakati huo ukifika.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII**: Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

## KAMATI YA MATUMIZI

## MATUMIZI WA KAWAIDA

### Fungu 38 – Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania

**MWENYEKITI:** Wheshimiwa Wabunge, kama kawaida mshahara wa Waziri sio kineno cha kule kwako ni maneno ya Sera, kufuatana na Kanuni zinavyosema.

Kif. 1001 - *Defence Force Head Quarters' Command* ...................................................... . Sh.511,936,765,000

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nipo hapo hapo *Defence Force Headquarters' Command, Items* 210500 na 220700. Nikianzia kwenye 210500, gharama hizi…

**MWENYEKITI**: Moja tu sio viwili.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya nakwenda hapo hapo, moja tu 210500, gharama hizi za kodi za pango, umeme ya *Personal Allowances- In-Kind.*

**MWENYEKITI**: Rudia tena Kifungu gani?

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, 210500 - *Personal Allowances- In-Kind.*

**MWENYEKITI**: *Personal Allowances- In- Kind* ndiyo chenyewe hicho?

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *yes*?

**MWENYEKITI**: Si ndiyo hicho unachosema *Personal Allowances-In-Kind;* sio hicho?

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, 210500, hiyo ni *Sub-Vote 1001*, *Defence Force Headquarters' Command.*

**MWENYEKITI**: Sawa, Kifungu kidogo kipi?

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti*, Sub-Vote* 210500.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Item 210500* hiyo ni *Sub Vote 1001*, *Defence Forces Headquarters' Command.*

**MWENYEKITI:** Kifungu Kidogo kipi?

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Item 210500.*

**MWENYEKITI:** Haya, inaitwa *Personal Allowances – In – Kind.*

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawasawa.

**MWENYEKITI:** Sasa endelea.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kufahamu, kwa kuwa kuna mabadiliko ya kila wakati ya kodi za pango na kupanda kwa gharama za umeme na mambo mengine ni kwa nini imejitokeza hakuna badiliko lolote kati ya mwaka 2011/2012 na 2012/2013? Naomba maelezo.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema, lakini Waswahili wanasema, unakata nguo kwa mujibu wa ukubwa wa mwili wako. Sasa sisi tulichopewa ndicho hiki, kwa hiyo, tunapanga kwa mujibu wa kile tulichopewa. Kama kuna ziada, mimi kama Waziri wa Ulinzi, nitapenda sana ipatikane hiyo ziada.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo kwenye *Defence Forces Headquarters' Command. Item 220400 - Medical Supplies and Services.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana hawakupata kitu ni *zero* na mwaka huu ni *zero;* hivi tuseme hawa Askari hawaumwi? Nataka nipate maelezo hapo.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba, Askari kwa sababu wao ni wanadamu wanaumwa kama tunavyoumwa sisi Waheshimiwa Wabunge. Matumizi yao angalia mwisho huku kwenye kifungu cha mwisho kinachohusiana na Hospitali za Jeshi, ndiko yalikowekwa.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitasimama wakati wa Mshahara wa Waziri.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1007 - *Land Forces Command ........................* Sh. 8,077,061,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1008 - *Air Defence Command ........................*Sh. 6,210,402,000

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *Air Defence Command,* kwa ufupi, nataka nielewe tu kwa sababu hii *figure* nzima kutoka *Item* ya mwanzo *210300* mpaka mwisho *411000,* Mafungu yaliyotengwa mwaka jana na mwaka huu ni *item* mbili tu zilizotofautiana, zote zipo sawasawa ki-*figure.* Ilikwendaje hata zikawa sawasawa ikawa hakuna *minus or plus* katika hizi *figures?*

**MWENYEKITI:** Katika Kamati ya Matumizi, hatuendi hivyo, utueleze ni kitu gani unataka kuuliza hapa. Wewe unatuuliza bonge la *Vote* hapa, uliza unachotaka kuuliza! *(Kicheko)*

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Spika, inanitia wasiwasi kwamba, utengenezaji wa Bajeti katika Matumizi ya Wizara yoyote huwa ama kunakuwa na fedha zimeongezeka au zimepungua;

lakini hapa ukiangalia kwenye *Office and General Supplies and Services - 220100* na kwenye *Acquisition of Office and General Equipment,* ndiyo sehemu mbili tu ambazo zina tofauti, nayo ni tofauti ndogo tu, lakini *item* zote zilizobakia zipo sawasawa. Ni kweli kwamba, matumizi ya mwaka jana na mwaka huu hayatofautiani Kisera au katika hizo sehemu ambazo wao wamehitaji kwamba watengewe hizo fedha?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika busara na akili ya kawaida, kama umeomba fedha nyingi katika kutekeleza majukumu yako hukuzipata, basi busara inakutuma ili uweze ku-*maintain* kile ambacho ulikifanya mwaka jana ukifanye mwaka huu mpaka pale utakapotengeneza uwezo mwaka unaokuja.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuzungumzia Kasma 410600, ambayo tayari imeshatolewa ufafanuzi.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni *Command* ya Anga ya *Defence Command* na nipo katika *Item 220800*.

Mheshimiwa Waziri, anakumbuka kwamba, wengi wa Wataalamu wetu katika *Command* hii wanastaafu na pia ukikumbuka maelezo ambayo umetupatia kwamba, utakuwa na mbadala wa kuweza kuwaandaa vijana wapya kutoa mafunzo katika *Command* ya Anga, kwa mambo yetu ya ulinzi.

Sasa pamoja na kwamba unasema unachopewa ndiyo unachochukua, lakini hebu nithibitishie maelezo yako ya kawaida ya kwetu yale kwamba, utaandaa mazingira ya kutoa mafunzo kwa vijana wapya wa Komandi ya Anga, kutokana na wale wanaostaafu; kwa nini mabadiliko haya hayatokei?

**MWENYEKITI:** Hayatokei wapi sasa? Mheshimiwa Waziri, hebu tulia kwanza aweke vizuri swali lake. Sisi tupo kwenye Kamati ya Matumizi, yanatokea wapi sasa?

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ninachotaka kumwambia Mheshimiwa Waziri ni kwamba, Komandi ya Anga, *Air Defence Command,* ukiangalia kwenye *Item 220800,* yaani hayo mafunzo ya ndani ambayo inaendana sambamba katika mafunzo hayo na badiliko kutokana na wale ambao wanastaafu, Wataalamu wetu wa zamani na kupatikana kwa vijana wapya ambao atawapa mafunzo. Kwa mujibu wa maelezo ambayo sisi ametupatia mwenyewe, ambayo tunayafahamu kwamba, anaandaa mazingira ya kupata vijana wapya ambao watatoa hayo mafunzo na alisema kutakuwa na ongezeko fulani fulani lakini katika maelezo yake anasema kwamba, fedha iliyobakia ni ile ile shilingi 174,787,000.

Naomba maelezo ya ufafanuzi juu ya hili.

**MWENYEKITI:** Kwamba, hela hizi zitatosha hayo maandalizi; basi ndiyo swali.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema, fedha hizi hazitoshi. Namwomba aangalie kwenye Fungu la Utawala; Ngome, kuna bilioni 1.2 kwa ajili ya shughuli hiyo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1009 - *Navy Command* .............................Sh. 2,611,237,000

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kasma 220100 - *Office and General Supplies and Services.* Naomba maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwa nini Mwaka huu wa Fedha *amount* hii imekuwa karibu mara mbili ukilinganisha na miaka mingine ya fedha; mwaka uliokwisha na ule mwingine?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa naanza sasa kuchanganyikiwa, maana fedha zikitengwa kidogo inakuwa mgogoro, zikitolewa nyingi maneno, sasa tunataka tufuate msimamo upi! Hapa tumetekeleza hoja waliyoisema Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tupo katika kutengeneza mazingira tu ya Mheshimiwa Waziri apate fedha kwa wakati na zinazotosha, asiwe na wasiwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *Navy Command,* kwenye *Clothing, Bedding, Footwear and Services.*

**MWENYEKITI:** Sema Kifungu Kidogo ndiyo utueleze.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu Kidogo 250600, ambacho kimetengewa shilingi 805,000 kwa mambo yote hayo; *Clothing, Bedding, Footwear and Services.* Mbona pesa ni ndogo sana? *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwamba, watu hawatapewa *uniforms* tena?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Sanya kwamba, fedha ni kidogo, lakini hizi za kushikia Kifungu tu, fedha zipo katika Fungu la Utawala, Ngome.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwenye *Item 220800 – Training – Domestic.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba yake Mheshimiwa Waziri, kuna fedha ambazo zimetengwa kununua Meli za Vita kwenye *Command* hii ya *Navy.* Pia, mbali ya kununua hizi Meli za Vita, lakini ni dhahiri kwamba, meli zetu mda mwingi zinaharibika kwa sababu ya kukosa ama uwezo wa mafuta, lakini pia namna ya kuweza kupatikana kwa mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anieleze kuna tatizo gani zaidi ambalo

limejitokeza na mkakati wake wa kupambana na maharamia na fedha za mafunzo ambazo zimewekwa; ananunua meli, anataka kupambana na maharamia, lakini kiwango cha fedha ndiyo hicho na huku unataka kununua meli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba univumilie kwa hili, atueleze vizuri.

**MWENYEKITI:** Hapana bwana, hizi ni *training.* Wewe uliza, hizi *training* ni za watu gani; maharamia tena wa nini?

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba maelezo.

**MWENYEKITI:** Kwamba hizi fedha zitatumika kwa ajili ya *training* ya hawa watu watakaoendesha meli mlizosema mnanunua?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema, fedha za mafunzo katika *Command* zote, zitaonekana katika Fungu la Ngome, Fungu la Utawala, *Headquarters',* ndiko ambako fedha hizo zipo. Naomba Mheshimiwa Mbunge, aangalie huko.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi*
*bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1010 - *Military Hospitals* ................................ Sh. 2,480,753,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi*
*bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 39 – Jeshi la Kujenga Taifa**

Kif. 1001 – *The National Service Force* ………….. Sh. 131,197,222,000

**MWENYEKITI:** Kuna *Addendum,* mtaiona.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *Sub Vote, 1001, Item 220800 - Training Domestic.*

Namwomba Mheshimiwa Waziri atueleze hii *training* ni kwa ajili ya watu gani na kwa nini imepoungua kwa zaidi ya shilingi milioni 200 ukilinganisha na ya mwaka jana?

**MWENYEKITI:** Ahsante, hio ndiyo swali. Mheshimiwa Waziri si umeona? Hii *training* hapa ni ya watu gani kwa sababu imeshapungua kiwango?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna mabadiliko hayo, lakini katika huo mwaka wa kwanza, tulikuwa kwenye maandalizi. Sasa hivi, tayari tupo kwenye utekelezaji. Kwa hiyo, kwa hakika zinahitajika fedha zaidi katika kuetekeleza programu hiyo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi*
*Pamoja na mabadiliko yake)*

**Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

Kif. 1001 - *Administration and HR Management...*

**MWENYEKITI:** Aah, kaeni wote. Utaratibu hauendi namna hiyo. Utaratibu ni kwamba, Katibu atasoma Kifungu na kiwango cha fedha ndiyo mtasimama. Haya, endelea.
Kif. 1001 - *Adminstration and HR Management.....* Sh. 13,690,500,000

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa Sera ni kupeleka Vituo vya Kijeshi katika kila Wilaya; na kwa kuwa katika Wilaya ya Misenyi tayari tumeshatenga eneo; ni lini Kikosi kitaweza kwenda kuanza kuchukua sehemu ile?

**MWENYEKITI:** Kwani Sera hiyo ikoje ya kupeleka Vituo kila mahali? Mheshimiwa Waziri, huzungumzii mahali fulani ni kwa ujumla wake; Sera ya kupeleka Vituo vya Jeshi sijui wapi sasa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunao mpango wa kuanzisha Viteule katika maeneo mbalimbali. Sasa katika hilo, sehemu ambayo anaizungumzia Mheshimiwa Mbunge, baada ya kumaliza shughuli hizi za Bunge, tutalitembelea eneo hilo tuone kama kuna haja ya kufanya hivyo, basi Wizara ya Ulinzi na Jeshi la

Kujenga Taifa itachukua hatua. Kama hakuna haja ya kufungua Kituo, tutachukua hatua nyingine kwa mujibu wa mazingira yatakavyoonesha.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Wakati nachangia kwa njia ya maandishi, niliishauri Serikali kuamua na kulitumia Jeshi la Wananchi kama Jeshi Kiongozi likiongoza Majeshi mengine ya Ulinzi kama Jeshi la Polisi na Magereza, kuwakabili watu wanaotoka nchi za nje, wakiwateka wananchi na kuwavua nguo na kuwanyang'anya mali zao hasa katika Mikoa ya Magharibi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa, Mheshimiwa Waziri, rafiki yangu, hakunijibu. Ningependa majibu.

**MWENYEKITI:** Yaani Sera ya Ulinzi wa Mipakani eeh? Waziri, hajakupata vizuri.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sauti yenyewe *panasonic,* halafu husikii. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi, nilielezea haja ya Serikali yangu kuitumia Wizara ya Ulinzi kama Kikosi, kama Jeshi Kiongozi, likiongoza Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Jeshi la Mgambo la Intelijensia, kuwakabili watu wanaotoka nchi za nje, wakiwavamia Watanzania, wakiwazuia kutembea usiku na kuwapiga na kuwanyang'anya na wengine wakienda kufanya

ujambazi kwenye nchi nyingine, ambaye ni rafiki yangu lazima nikiri hakunijibu.

**MWENYEKITI:** Halafu ndiyo anakujibu, Waziri wa Ulinzi, Sera ya Ulinzi ya Mipakani.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye maelezo yangu ya ufafanuzi wa hoja mbalimbali, tunayo mipango na dhamira ya kuanzisha Viteule mbalimbali katika maeneo mbalimbali ili tuweze kusogeza huduma za Jeshi la Wananchi wa Watanzania katika maeneo ya mipakani. *(Makofi)*

Katika suala la ushirikiano kati ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Vyombo vingine vya Dola, kwa muda mrefu tumekuwa na utaratibu huo. Vyombo vyote vya Ulinzi chini ya Uenyekiti wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania, tumekuwa na utaratibu huo wa kufanya operesheni hizo za pamoja. Kama Mheshimiwa Mbunge anadhani hatua hiyo haitoshelezi, basi tutajitahidi kuchukua hatua zinazostahiki ili tuhakikishe kwamba, usalama wa wananchi wa mipakani unalindwa. *(Makofi)*

**MHE. ALPHAXARD K. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu nilizungumzia Sera ya Uwekezaji ndani ya utaratibu wa *PPP*; yaani kwamba, Serikali iingie ubia na watu binafsi kwa kutumia Shirika hili la SUMA JKT na nikaeleza kwamba kuhakikisha hii Kaulimbiu ya KILIMO KWANZA badala ya matrekta haya kukaa kwenye *yard* muda mrefu wakati wananchi wanaohitaji wana uwezo

mdogo wa kukopa. Kwa nini Jeshi la Kujenga Taifa ndani ya SUMA JKT wasiende kwenye maeneo mbalimbali katika nchi yetu ambapo kuna mabonde, mito na maziwa na nikataja kule Ziwa Victoria, kuna Vijiji kama Kabainja na Kalukekere kuna maeneo ili matrekta haya badala ya kukaa huko waingie kwenye hiyo Sera ya Uwekezaji ndani ya *PPP*. Nataka maelezo Serikali inasema nini juu ya hiyo Sera ndani ya SUMA JKT. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa Mheshimiwa Mbunge siyo mbaya ni mzuri, lakini kwa maoni yangu jambo hili tunahitaji kulifanya kwa umakini na kwa hatua. Kama nilivyosema kwenye maelezo yangu, tayari sasa hivi Shirika la SUMA JKT, limeainisha maeneo matano ambayo tunataka kushirikiana na wawekezaji wenye mtaji wa kutosha, walio makini na wenye teknolojia ili tuingie nao ubia tuendeleze maeneo matano ya kilimo. *(Makofi)*

Kabla jambo hili hatujalikamilisha tunaanza kufanya jambo lingine, wasiwasi wangu ni kwamba, wananchi wanasema mpanda farasi wawili huchanika msamba. *(Kicheko)*

Namwomba Mheshimiwa Mbunge atupe muda tuanze na hili la kwanza, halafu tukilikamilisha vizuri tuingie hatua ya pili ya kwenda kwenye maeneo mbalimbali na kuingia ubia na wananchi mbalimbali. Kama wasiwasi wake ni suala la matrekta, katika Hotuba yangu nilisema wazi kwamba, tunaziomba Halmashauri za Wilaya ziwadhamini wakulima wadogo

wadogo kwenye maeneo yao. Wakikubali kufanya hivyo, tutaretemsha kiwango cha kuweka malipo ya awali kutoka asilimia 30 hadi asilimia kumi. Je, Mheshimiwa Mbunge haioni nia na dhamira njema ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa juu ya jambo hili?

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimekuwa nikipata malalamiko mbalimbali kutoka kwa vijana wenzangu katika mikoa mbalimbali, wakilalamikia utaratibu mzima ambao unatumika kwa ajili ya kuwapata vijana wanaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa. Waheshimiwa Wabunge pia wamekuwa wakilalamika humu ndani kwamba kunakuwa na upendeleo fulani, wale ambao wana *refer* ndiyo wamekuwa wakichuliwa hata kama hawana sifa na kuwaacha vijana wengine ambao wana hamu ya kutoa mchango katika Jeshi lao. Je, Wizara ina taarifa hii; na kama ina taarifa imechukua hatua gani ili kuhakikisha kunakuwa na usawa na vijana wote wanapata fursa ya kulitumikia Jeshi lao?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bulaya, kama ifuatavyo:-

Mimi sina taarifa ya jambo hilo analolizungumza kwamba, vijana wanaojiunga na Jeshi la Kujenga Taifa wanachukuliwa kwa njia za upendeleo na wale ambao wana watu wakubwa wanaoweza kuwatetea ndiyo ambao wanapata fursa hiyo. Sisi tunachukua vijana hawa kwa sifa maalum; sifa ya kwanza ni Utanzania wao; sifa ya pili ni kuwa na afya nzuri,

iliyoimarika; na sifa ya tatu ni elimu. Kwa kawaida kuna wakati hata vijana wa Darasa la Saba, lakini inaonekana sasa vijana wa Darasa la Kumi na Mbili wamekuwa wengi sana.

Sasa Mheshimiwa Mbunge anaposema vijana ambao hawana sifa, mimi sijalibaini jambo hilo, lakini kama anao ushahidi kwamba kuna vijana angalau kijana mmoja aniambie fulani, kwenye Kambi fulani amechukuliwa na yeye hana sifa zinazotakiwa. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, akinipa ushahidi wa kutosheleza, tutachukua hatua zinazostahiki.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi, nilimkumbusha Mheshimiwa Waziri kwamba, Sera ya Taifa kuhusu UKIMWI inasema UKIMWI ni Janga la Kila Mtu. Nikamwomba anipe ufafanuzi katika Jeshi lake la Ulinzi anawasaidiaje vijana wanaojiunga na Jeshi hilo kwani sheria yake inasema kijana akiajiriwa anatumikia miaka sita ndipo anaoa ama kuolewa. Je, hao vijana wataishi vipi miaka sita na watajikinga vipi kupitia Sheria hiyo? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Chilolo, kama ifuatavyo:-

Kwanza, Askari na Wanajeshi kwa ujumla kama ilivyo kwa raia wengine wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wanapewa elimu kuhusiana na masuala ya

UKIMWI hasa kujizuia na tamaa za mwili ili waweze kujikinga na maradhi ya UKIMWI. *(Makofi)*

Utaratibu huu na falsafa hii ya kuwataka vijana wakae kwa muda wa miaka sita kabla ya kuoa si uamuzi ambao umefanywa hivi hivi tu, umefanyiwa utafiti wa kutosha, ikabainika kwamba kwa kawaida kazi za ulinzi kama hizi kuna wakati kijana atahitaji kwenda kwenye mapigano au zoezi la kudumisha amani. Sasa fikiria tu kijana ambaye ametoka *honey moon* jana anaambiwa meli ipo tayari ingia uende Darfur, fakiria unyonge anaoupata, ndiyo maana watu ambao wameasisi vyombo hivi wakaweka utaratibu angalau kijana akae miaka sita ajenge uzoefu na alijue jeshi vizuri ili hatimaye baada ya miaka sita ikitokea zoezi hilo atakuwa na uzoefu wa kutosha na fikira za kutosha.

Pia kipindi hiki cha miaka sita tunampa nafasi kijana ajitayarishe, ajenge maisha, angalau aweze kujijengea nyumba ya kuishi ili hatimaye ukifika wakati wa kustaafu, tusitoe malalamiko kama haya tunayoyatoa wakati ambapo mlikuwa mkichangia bajeti yangu. Kwa sababu vijana wamepata muda wa kujitayarisha vizuri, kama tunataka tuendeleze utamaduni wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania ambao umejengwa kwa miaka mingi, naomba tusiingize siasa, tuendeleze tu tutaweza kuwa na Jeshi imara, linalofuata taratibu. Kama wanasiasa kila mmoja ataingiza la kwake, mimi nafikiri kidogo hatutafanya vizuri. Nashukuru. (*Makofi)*

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nauliza Sera ya Uanzishaji wa Kambi Mpya za JKT kwa sababu kuna Kambi ambazo zimekuwa zikianzishwa na watu wanakaa kule muda mrefu bila kupelekewa familia zao; yaani wake zao na pia wanachelewa kulipwa kwa muda mrefu. Kambi hizi ni nyingi mfano Kambi ya JKT Kanembo. Sasa Serikali inachukua muda gani kuwahamishia familia na kuwalipa posho zao mbalimbali kama za mizigo?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA:** Serikali inao wajibu huo wa kuhakikisha kwamba, Wanajeshi kama walivyo Wafanyakazi wengine wa Serikali, wawe karibu na familia zao. Kwa mnasaba huo, tutajitahidi kadiri inavyowezekana, vijana hao, maafisa na askari wa kawaida, waweze kupewa posho zao hizo ili hatimaye wazitumie na kuzisogeza familia zao karibu nao. *(Makofi)*

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya maeneo muhimu katika Sera ya Ulinzi ni ulinzi katika mipaka. Sasa ningependa kusikia kutoka kwa Mheshimiwa Waziri; kuna umaalum gani ambao maafisa ambao wako mpakani hususan mpaka wa Kigoma wanapewa na naisema hivyo kwa sababu nazingatia kwamba kule Kigoma imefika mahala kwenye mpaka wa Ziwa wavuvi ndiyo wanachanga pesa ya mafuta kwa askari waweze kufanya *patrol* Ukanda mzima wa Ziwa. Kwa hiyo, ningependa kujua ni umaalum kiasi gani ambao ninyi mnautoa kama Wizara kuhakikisha Wanajeshi ambao wapo mpakani hususan mpaka wa Kigoma wanapata vitendea kazi

na wanapata huduma za kutosha ili waweze kulinda mpaka ule ambao ni mrefu na upo wazi kwa muda mrefu?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nia na dhamira ya Serikali kuhakikisha kwamba, Wanajeshi na Wafanyakazi wengine wa Serikali, wanapewa huduma zinazostahiki waweze kutekeleza majukumu yao. Kwa maana hiyo basi, tunao wajibu huo wa msingi, tumekuwa tukifanya hivyo na tutaendelea kufanya hivyo, pale ambapo kuna kasoro hawapati huduma kama wanavyostahiki, tutajitahidi kutumia bajeti ambayo tumepewa ili tuweze kuwasaidia kwa kadiri inavyowezekana ili hatimaye Viteule hivyo ambavyo kama nilivyosema kwenye maelezo yangu hapa tumesema, tunao mpango maalum wa kuanza au kuanzisha Kiteule Maalum katika eneo la Kigoma. Kwa namna hiyo, tunadhani pengine matumizi haya ya mafuta yanaweza kupungua sana.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Katika mchango wangu wa maandishi, niliomba ufafanuzi wa Kisera kuhusu utaratibu wa kuhudumia Vijana wa JKT, ambao kwa bahati mbaya inatokea wanaumia kwenye Kambi za Mafunzo. Sasa kwa kuwa mwezi Machi, 2013 vijana zaidi ya 5000 waliohitimu Kidato cha Sita wataingia Kambini, ningependa ufafanuzi kutoka kwa Serikali kuhusiana na utaratibu huu wa kuhudumia vijana wanaoumia kambini.

**MWENYEKITI:** Eeh, ikiwemo na ninyi mkienda huko.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida vijana na askari wanapokuwa kwenye mafunzo kunakuwa na madaktari maalum na wanapoathirika kwa namna moja au nyingine, madaktari hao wamekuwa wakitoa huduma. Pia tunazo hospitali zetu, kwa mfano, Hospitali ya Rufaa ya Lugalo, kama kutakuwa na kijana ambaye ameumia anahitaji matibabu zaidi, basi utaratibu upo wa kupelekwa kwenye hospitali hiyo kupata matibabu.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kati ya makundi ambayo yanaishi katika mazingira magumu sana ni Wanajeshi Wastaafu ambao ni askari wa akiba. Katika mchango wangu nilitaka nipate ufafanuzi kama Serikali ina mpango wowote wa maboresho ya pensheni kwa ajili ya askari wetu ambao wengi wanaishi katika mazingira magumu na wengi wanalipwa pensheni ambayo imepitwa na wakati kabisa na haiendani na maisha ya sasa.

Mwaka jana aliyekuwa Waziri alisema kwamba ataliangalia. Nataka nijue Waziri kama kuna mipango yoyote ya muda mfupi kwa sababu hali za Wanajeshi wetu ni mbaya sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri au Waziri mwingine anaweza kusaidia; mfano, Waziri wa Utumishi hapo. *Okay,* wana utaratibu wao.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa wastaafu kupata pensheni zao hauna tofauti sana na watumishi wengine wa Serikali. Nami kama Waziri wa Ulinzi, najua mchango wa askari hawa wastaafu katika ulinzi wa Taifa letu. Kweli wengine wanaishi kwenye mazingira magumu wanastahiki kupata malipo yaliyo bora, lakini uamuzi huo hautakuwa wa Wizara ya Ulinzi peke yake, ni uamuzi ambao unapaswa kuzingatiwa na Serikali kwa ujumla. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo amesikia na Mheshimiwa Waziri wa Fedha yupo. Sasa mimi kama Balozi wao nitajenga hoja na Serikali, kama nina hoja za msingi Serikali itapima na hatimaye kuchukua hatua zinazostahiki. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Suala la jinsia ni mtambuka na Serikali na *NGOs* zimekuwa zikipigania sana usawa wa jinsia katika ngazi zote. Hata leo wakati ukitaja Maafisa waliokuwa hapa juu, nadhani wote walikuwa wanaume. Naomba kujua wana mkakati gani kuhakikisha kwamba hata wanawake wanakuwa katika nyadhifa hizo kwa sababu naamini wanawake tunaweza? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, nadhani umelipata hilo swali?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa Maafisa mbalimbali kupandishwa vyeo unategemea mambo mawili; kwanza, unategemea kiwango cha elimu ambacho wakati wa kuandikishwa ananzia nacho au

weledi wa kazi hiyo anayoifanya. Kwa maana hiyo basi, mpango wetu tunawasajili akina mama na hasa ambao wanahisi kwamba wana taaluma za hali ya juu sana, waje wajiunge na Jeshi; nina hakika kwamba, wataweza kupanda haraka haraka.

Mpaka sasa pengine kama alivyosema, ni wachache sana waliopo; wapo Maafisa wa Jeshi wenye vyeo vya u-Brigadia Jenerali wawili, watatu, lakini pengine kwa maoni yake kama hawatoshi basi yeye na mimi tushirikiane ili tusajili akina mama wengi zaidi wenye taaluma waweze kujiunga na jeshi na kunufaika na mpango huu.

**MBUNGE FULANI:** Hakuna Viti Maalum?

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu, nilihoji kuhusu gari aina ya nyumbu kwa kuwa ni katika awamu ya kwanza kuingia...

**MWENYEKITI:** Sikusikii umesema? Mheshimiwa Mngodo, ngojea kwanza hatukusikii vizuri sijui ina-*vibrate*, hebu anza tena.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Katika mchango wangu wa maandishi, nilihoji kuhusu gari aina ya nyumbu; kwa kuwa katika Uongozi wa Awamu ya Kwanza kuingia Awamu ya Pili, Jeshi letu lilipiga hatua kubwa katika utengenezaji wa gari aina ya nyumbu; magari ambayo yangeweza kutumika si kwa shughuli za kijeshi lakini kuboreshwa na hivyo kutumika kwa wananchi katika kukabiliana na changamoto za usafiri

wa mazao yao kutoka mashambani kupeleka sokoni. Ningependa kujua ni kwa nini hakuna kiwango chochote cha fedha ambacho kimetengwa kwa nyumbu ili waweze kujiendesha?

**MWENYEKITI:** Wewe unauliza huo Mradi wa Nyumbu umeachwa maana hapa tupo kwenye *development* kwamba Mradi wa Nyumbu sasa umeachwa?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ina dhamira ya dhati ya kuliendeleza Shirika la Nyumbu, liweze kutekeleza wajibu wake kikamilifu na limetengewa fedha. Namwomba Mheshimiwa Mbunge aangalie kwenye Kasma 270802, Shirika hilo limetengewa shilingi bilioni 3.4.

**MWENYEKITI:** Kwenye *development* au wapi? Mheshimiwa Dokta Kebwe.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nilichangia kwa maandishi kwamba ili kuimarisha ulinzi katika nchi yetu na pia kuimarisha ulinzi katika mbuga zetu za wanyama ikiwemo Mbuga ya Serengeti na hata kudhibiti mauaji kama yaliyotokea mwezi uliopita kwenye Mbuga ya Serengeti.

Kwa nini Jeshi letu liwe la kisasa, wapate ndege ambayo inaweza ikaimarisha ulinzi kwa kupiga picha hata katika mawingu au nyakati za usiku? Ahsante.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mheshimiwa Dkt. Kebwe, kama ifuatavyo:-

Jeshi la Wananchi wa Tanzania tayari inazo ndege ambazo zina uwezo wa kupiga picha na kama haamini jambo hilo, naomba baada ya kumaliza Bunge hili aje nikamwoneshe ndege hizo. Sitaweza kusema hadharani ni ngapi lakini napenda nimwoneshe kwa sababu *seen is believing.*

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii.

Katika mchango wangu wa maandishi, nilizungumzia juu ya umuhimu wa vitendea kazi vya Jeshi la Ulinzi hasa katika Ukanda wa Ziwa Tanganyika, ambapo sasa hivi kumekuwa na maharamia wanaoingia kwenye mpaka wetu kupitia Ziwa Tanganyika na Wanajeshi wa *DRC* wanaokuwa katika mapigano wanapozidiwa wanakuja na kuingiza silaha katika Ukanda huo. Je, Serikali kupitia Wizara ya Ulinzi imejipanga vipi kuboresha vitendea kazi ikiwa ni pamoja na kuwapatia meli za kivita katika Ukanda huo wa Ziwa Tanganyika au Bodi za Kisasa ambazo zinaweza zikakabiliana na uharamia huo?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Ulinzi, litachukua hatua mbili ili kutekeleza hatua hiyo.

Kwanza, kuendelea na utaratibu wa kuanzisha Viteule kwenye Maeneo Maalum yenye mahitaji hayo.

Pili, kwenye maelezo yangu ya bajeti nilisema kwamba, tutanunua meli za kivita pamoja na boti ziendazo haraka sana kwa ajili ya kufanya doria katika Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria na Ziwa Nyasa.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Sera ya Taasisi au Shirika la Nyumba ilikuwa ni kukuza teknolojia kwa ajili ya Jeshi la Wananchi na pia kuwa ni chemchemi ya teknolojia.

Je, Sera hii mpaka sasa imetekelezwa vipi na imeleta manufaa yapi kwa Watanzania?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika letu la Nyumbu limepata mafanikio kama ifuatavyo:-

Kwanza, tumetafiti utengenezaji wa gari ambayo inaitwa Nyumbu na gari hiyo inafahamika na imeshaonekana. Pili, tumekuwa tukitafiti vifaa mbalimbali vinavyotumika katika shughuli za kilimo, lakini utafiti zaidi unaendelea ili tufikie hatua zaidi nyingine ya angalau kutengeneza matrekta madogo madogo, tupo katika hatua ya utafiti lakini *Inshallah* tukiendelea kuunganisha nguvu zetu, nina hakika kwamba tutaweza kuifanikisha kazi hiyo si muda mrefu ujao.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Katika mchango wangu wa maandishi nilichangia nafasi ambazo zinatolewa na Jeshi la Wananchi kwa

upande wa Zanzibar. Nafasi hii tulilalamika kipindi cha bajeti cha mwaka jana, lakini tumeletewa nafasi za kutosha kwa upande wa Muungano za kuja Zanzibar, nafasi hizi hazikuwafikia walengwa. Je, Mheshimiwa Waziri atahakikishaje hizi nafasi ambazo zinatolewa Tanzania Bara zinawafikia walengwa?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli Mheshimiwa Mbunge anasema nafasi hizi zilizotolewa Zanzibar hazikuwafikia walengwa, tutajitahidi ziwafikie walengwa, kwa sababu mimi nilidhani nafasi hizi kwa kuwa zilipelekwa Zanzibar zimetumiwa na Wazanzibari. Tutalifanyia kazi jambo hilo na kuwachukulia hatua zinazostahiki ili kipindi kinachokuja ziweze kuwafikia walengwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Katika mchango wangu wa maandishi nilimwuliza Waziri kuhusiana na deni la Kampuni ya *Meriniam Express* ambayo wanai SUMA JKT, walijenga Barabara ya Bagamoyo - Msata na kwa kusema hivi simaanishi kulidhalilisha Jeshi kwa sababu sote tunaliamini kama wengine wanavyotaka kupotosha. Ni vipi hili deni ambalo kesi iliamuliwa SUMA JKT wailipe kampuni hii na walijaribu kuwapa *scrap* ya kuchanganya zege ili ifidie lakini wakashindwa kuiuza. Baadaye dalali alipotaka kwenda kukamata mali ili wafidie deni la shilingi milioni mia moja tisini na zaidi, Jeshi lilitumia mabavu kwamba hilo ni eneo la ulinzi wachukue vitu vyao.

Katika kujenga dhana ya Utawala Bora; Waziri anasema nini ili watu hawa watu waweze kupewa haki yao tuishi kwa amani kama Taifa?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachosema Mheshimiwa Msigwa ni kwamba, kama maamuzi ya Mahakama yameshatolewa, sisi Serikali tunaheshimu Utawala wa Sheria. Kama hilo ni kweli, basi tutalifanyia kazi na kama kuna mtu anastahiki kupewa haki yake kwa mujibu wa Sheria, tutafanya hivyo. Hili suala la kwamba ni kweli Jeshi ni eneo la ulinzi, mtu hawezi kuingia kwenye eneo la Kambi.

Jeshi hili lina Viongozi wao na mmojawapo ni Waziri ambaye ni Mwanasiasa mwenzenu. Huyo mwenye deni au anayekidai chombo hicho, namwomba aniletee nyaraka tuzipitie na tukibaini kwamba anayo haki, bila shaka atapatiwa haki hiyo kwa mujibu wa Sheria.

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Kujenga Taifa linadaiwa madeni sugu ya ulipaji wa maji na umeme; na kwa kuwa Bunge hili linapitisha kila wakati bajeti ya kulipa bili ya umeme na maji: Je, Serikali sasa haioni kuwa ni wakati mwafaka wa kuwalipa *allowance* Wanajeshi hao kwenye mishahara yao ili walipe hizo bili za maji wenyewe badala ya kupita kwenye mikono mingine ambayo wanatafuta hizo fedha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri; una maelezo?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunayo madeni na ni kweli pia tumekuwa tukitengewa fedha, lakini nyote ni mashahidi kwamba, fedha hizi tunazotengewa kiwango chake ni kidogo sana ukilinganisha na madeni tuliyonayo. Utaratibu huu alioupendekeza Mheshimiwa Mbunge ni mzuri lakini atupe muda tuutafakari na kuufanyia kazi.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi na kuongea nilielezea kwa kirefu sana kuhusu maduka ya Jeshi na nia nzuri ya Serikali ya kuwafanya watu wetu waweze kupata bidhaa na vifaa vingine kwa bei nafuu na hivyo kutoa msamaha wa kodi katika maduka hayo ya Jeshi.

Katika majumuisho, Waziri hakugusia chochote, lakini nataka ufafanuzi kujua ni kigezo gani kinatumika cha kuwafanya wawekezaji wa maduka hayo ambayo niliyasema, wawekezaji ni wenye asili ya Kiasia, kuuza bidhaa na vifaa vingine kwa bei ya juu kuliko hata bei nyingine zinazouzwa na maduka mengine ya mitaani ilhali wao wana *tax exemption.* Kwa nini Wizara imekaa kimya kuangalia ni kwa kiasi gani maduka haya yameendelea kuwanyonya Wanajeshi badala ya kuwafanya waishi katika maisha ambayo walikusudiwa na Serikali? Naomba kujua ni kigezo gani kinatumika kuwafanya wawekezaji hawa wauze kwa bei kubwa?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda niseme jambo hili ambalo analieleza Mheshimiwa Mbunge na sisi Wizara tunalifahamu, lakini Viongozi wa Wizara hawawezi kuamka tu wakaanza kupiga makelele kwa jambo ambalo hawakuulizwa. Huo siyo utaratibu wa Uongozi.

Sisi tulipolisikia jambo hili tulikaa Wizara tukalifanyia kazi na uamuzi tulioutoa ni kwamba, ni kweli baadhi ya wafanyabiashara hawa wamekuwa biashara yao haiwanufaishi Wanajeshi. Kwa hiyo, tumesema mikataba ambayo hivi sasa inaendelea ikimalizika basi ifungwe isiendelee tena na kazi hii tumeamua kuipa kampuni yetu ya Mzinga ifanye upembuzi yakinifu, watuoneshe kama wana uwezo wa kuifanya.

Shirika la pili ambalo tutalifikiria ni SUMA JKT, nalo watuoneshe kama wana uwezo wa kutekeleza jambo hili na kama wana uwezo basi tutawapa biashara hiyo waisimamie.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Opulukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Washauri wa Mgambo karibu nchi nzima wana matatizo makubwa sana ya vyombo vya usafiri na hivyo kuwafanya washindwe kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Je, Wizara itakuwa tayari sasa kuwasaidia Washauri wa Mgambo ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu ya kutokuwa na vyombo vya usafiri waweze kufanya kazi zao jinsi inavyotakiwa?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa Mheshimiwa Opulukwa ni mzuri sana, tutauchukua na kuufanyia kazi.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nimeeleza kwamba, hali ya mpaka kati ya Burundi na Tanzania kwa upande wa Ngara siyo shwari, kwa sababu Wanajeshi wanaoipinga Serikali ya Nkurunzinza, Rais wa Burundi, wameweka makao yao karibu na vijiji mbalimbali vya Ngara, kiasi kwamba kati ya mwaka jana na mwaka huu, wananchi wanne wameuawa kwa mabomu katika Kijiji cha Wendo. Pia Mji Mdogo wa Kabanga, ambao Mheshimiwa Waziri ameutembelea, unasumbuliwa sana na majambazi wenye silaha kutoka Burundi. Hatuna shida na mpaka wa upande wa Rwanda; je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba Wananchi wa Ngara hawaendelei kuishi katika hali ya wasiwasi? Wananchi wengi wamehama vijiji vyao vya mpakani mwa Burundi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kunakuwa na Vikao Maalum vya Mawaziri wa Ulinzi kwa upande mmoja, lakini na Wakuu wa Majeshi wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki hukutana. Kwa maana hiyo basi, sisi Mawaziri kwa upande wetu tutalichukua jambo hilo tulizungumze na kutafuta njia stahiki za kumaliza tatizo hili.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nilikuwa naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri kwamba, wakati nachangia kwa maandishi niliuliza Serikali iliweka mpango mzuri kupitia SUMA JKT wa kuleta matrekta na zana za kilimo zisaidie katika Sekta ya Kilimo. Serikali iliweza kupunguza bei za matrekta na tunaipongeza kwa hilo. Je, katika zana zilizobaki kwa mfano majembe, matrela, *harrow, planter* na vifaa vinginevyo ambavyo havijateremshwa bei; Serikali ina mpango gani kuteremsha bei ili wakulima waweze kunufaika na hilo?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa Mheshimiwa Mbunge ni wa maana sana, tutauchukua na tutautafakari, tukihisi kwamba tuna uwezo wa kufanya hivyo, bila shaka hatutasita kuchukua hatua hiyo ili tuwasaidie wakulima wadogo wadogo katika kutekeleza Sera ya KILIMO KWANZA.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 104(1), naongeza dakika 30 ili tuweze kumaliza kazi iliyobaki. Mheshimiwa Kigola.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali.

Katika Tanzania kuna Watanzania wengi sana walishiriki Vita Kuu ya Pili ya Dunia ya Mwaka 1939 - 1945 na Watanzania hao sasa hivi ni wazee, wapo ambao walishiriki katika Jeshi lile na hawalipwi kitu chochote. Je, Serikali ina mpango gani wa

kuwatambua na kuanza kuwalipa kama wastaafu wengine?

**MWENYEKITI:** Swali hilo linafanana na alilouliza Mheshimiwa Halima Mdee. Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilichukue suala hili na tulifanyie kazi ili tuweze kupata orodha sahihi ya wazee ambao walishiriki katika Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia, tuwe na takwimu sahihi na kutafuta njia ya kuwasaidia.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mchango wangu wa maandishi nilitaka kufahamu kupitia Hotuba ya Waziri katika ukurasa wa 17 kwamba, nchi yetu inashiriki katika ulinzi wa amani katika nchi mbalimbali za Afrika kama Darfur, DRC na nchi nyingine. Wakati huo huo huko nyuma katika miaka ya 70, nchi yetu ilishiriki katika Ukombozi wa Kusini mwa Bara la Afrika mpaka nchi hizo sasa hivi zimejitawala kwa juhudi za Serikali yetu ya Tanzania. Serikali ya Tanzania pamoja na hayo yote ambayo tumeyafanya; athari kubwa imepatikana na watu wetu wamepoteza maisha, uchumi umeathirika na maeneo mengine katika nchi yetu uchumi wake uko nyuma kwa sababu ya ushiriki wetu katika vita hivyo vya Kusini mwa Bara la Afrika. Je, Serikali inapata ahueni yoyote katika nchi hizo ambazo nchi yetu ilishiriki katika kuwapatia Uhuru na kuendeleza amani katika nchi zao?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi wa kuzisaidia nchi za mstari wa mbele katika ukombozi haukuwa wa hivi hivi tu. Mwalimu alisema Tanzania haiwezi kuwa huru kama Mataifa mengine ya Afrika hayakuwa huru. Kwa hiyo, tuliamini wale tuliowasaidia ambao tunapakana nao amani katika nchi zao zikivurugika, amani ya Tanzania haitakuwa salama. Ndiyo, tuliuchukua uamuzi huo kwa kuamini kwamba tukifanya hivyo na Tanzania itafaidika.

Katika hali ya kawaida hata Mheshimiwa Barwany hivi wale unaowasaidia wote unategemea siku moja wakurudishie? Kuna wakati mwingine unamsaidia mtu tu kwa fikra na mawazo ya kibinadamu, maana binadamu ana wajibu wa kuwasaidia watu wengine wenye shida.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kilio cha askari walioshiriki Vita vya Kagera ni kikubwa, hali zao ningesema hawana viungo, miguu na wengine hawana mikono, lakini familia za wale ambao walifariki au waliuawa kwenye Vita ni mbaya zaidi. Pia walioshiriki Vita vya Msumbiji na kuzikwa kule Naliendere Mtwara, nao familia zao ni mbaya sana na wamenituma niseme hivi; mnasubiri mpaka wafe ndiyo muwaenzi? Ni utaratibu gani wa Sera ambao umepangwa kuhakikisha kwamba wale walio hai na familia za waliokufa walikufa wanaandaliwa utaratibu wa kuwasaidia kimaisha?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina jibu na uamuzi wa haraka haraka hapa, lakini labda niseme tu kwamba, tukichukua uzoefu wa wenzetu wa Afrika Kusini, Wizara yao ya Ulinzi inashughulikia Maveterani ambao wameshiriki kwenye vita na kutafuta utaratibu wa kuwahudumia. Nafikiri jambo hili si vibaya tukajifunza kwa watu ambao wamefanya vizuri. Kwa maana hiyo, nasema sisi kama Serikali, nisitoe jibu na kueleza *commitment* za Serikali moja kwa moja, lakini nadhani utaratibu huo mzuri sisi Wizara ya Ulinzi tutajenga hoja kwa Serikali ili hatimaye tuone njia ya kuwasaidia watu hawa.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jibu zuri la Mheshimiwa Waziri kuhusu namna gani anaweza akashughulikia matatizo ya ardhi, lakini tatizo la ardhi limekuwa kubwa kiasi ambacho idadi ya watu inavyoongezeka, Wizara inadai au wenye Kambi wanadai kwamba, wananchi na raia wanavamia maeneo yao. Wakati huo huo na raia nao wanasema maeneo yao yanazidi kuchukuliwa na Kambi au Wizara husika.

Kwa bahati nzuri, mwaka huu Mheshimiwa Tibaijuka, aliliweka bayana suala hili na kutoa ufafanuzi kwamba zile Wizara au Taasisi zote zitakazokuwa na matatizo ya ardhi, atashirikiana nazo ili kuondosha tatizo hilo. Wakati huo huo Jeshi la Ulinzi ni Chombo cha Muungano, matatizo haya yako pande zote mbili; upande wa Tanzania Bara na upande wa Tanzania Zanzibar na Mheshimiwa ametuhakikishia kwamba,

atalishughulikia na kufuatilia kuona wale watakaokuwa wanadai au kuwa na haki ya kulipwa fidia kwa mujibu wa hali ilivyo watalipwa fidia hiyo. Wakati huo huo anasema kwamba, ataishona nguo yake kwa mujibu wa kitambaa alichopewa, ina maana fedha hizo hazitakuwepo.

Je, Waziri anaweza akatufafanulia angalau kwa kuanza tukajua maeneo ambayo yanaweza yakafanyiwa hiyo kazi na wananchi wakaangaliwa na kupewa fidia yao kwa bajeti ya mwakani au inawezekana kwa mwaka huu kuifanya kazi hiyo kwa pande zote mbili za Muungano; yaani Tanzania Bara na Zanzibar? (*Makofi*)

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna sababu ya kutoukubali ushauri ambao una nia ya kusaidia kutatua tatizo la Wizara yangu kuhusiana na migogoro ya ardhi. Kwa maana hiyo, nitafanya kila linalowezekana kuhakikisha ninashirikiana na Waziri, Mheshimiwa Profesa Tibaijuka, katika kuhakikisha tunatafuta ufumbuzi wa jambo hili na maeneo gani kwa upande wa Zanzibar tunahitaji kuyafanyia kazi kwa haraka. Tutajitahidi pia kutafuta taarifa na hatimaye tutaona tutaweza kuchukua hatua gani katika kutatua tatizo hili. (*Makofi*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts*……...………………Sh. 235,792,999

Kif. 1003 - *Policy and Planning* ..............................Sh. 408,630,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1004 - *Internal Audit Unit*...............................Sh. 153,877,000

**MHE. ESTHER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda nipate ufafanuzi kwenye *Sub Vote 1004,* Kasma 220800, kuhusiana na *Training – Domestic.* Mwaka huu haijatengewa fedha kabisa. Sasa sijui hawatatoa mafunzo ndani ya nchi?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za mafunzo hayo anayoyazungumzia Mheshimiwa Mbunge, zitaonekana katika vifungu ambavyo vipo kwenye Utawala.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1005 - *Procurement Management Unit*..............Sh. 107,059,000
Kif. 1006 - *Legal Services Unit* .................................Sh. 46,532,000
Kif. 1007 - *Government Communication Unit* .........Sh. 134,721,000
Kif. 1008 - *Military Tender Board Unit*......................Sh. 0

Kif. 1009 - *Independent Telecommunication Network*
...............................................................................Sh. 88,334,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 – *Industries, Construction and Agriculture* ...Sh. 680,244,000
Kif. 2002 - *Military Research and Development*.........Sh. 201,599,000
Kif. 2003 - *Building Consulting Unit* ......... ...................Sh. 57,539,000
Kif. 2004 - *Estate Management and Development Unit*
.....................................................................................Sh. 45,225,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## MIPANGO YA MAENDELEO

### Fungu 38 – Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania

Kif. 1001 - *Defence Forces Headquarters' Command* ........................................................ Sh. 14,000,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na mabadiliko yake)*

**Fungu 39 – Jeshi la Kujenga Taifa**

Kif. 1001 - *The National Service Force* ................Sh. 5,000,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

Kif. 1003 - *Policy and Planning* .................................Sh. 100,000,000
Kif. 1009 - *Independent Telecommunication Network* ............................................................... .Sh. 3,300,000,000
Kif. 2001 - *Industries, Construction and Agricultur* .Sh. 52,900,000,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 - *Military Research and Development*.... Sh. 332,886,566,000

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kifungu hiki kimeongezeka kutoka shilingi bilioni 128 mpaka bilioni 332, sina tatizo na nyongeza ya fedha kwenye kifungu hicho, ila kwenye mchango wangu wa maandishi nilizungumzia Kasma 6103 ambayo ni ya kifungu, kinachohusiana na *Military Research and Development*. Niliomba ufafanuzi iwapo matumizi ya kifungu hiki cha utafiti na maendeleo

kama yatahusisha Jeshi letu vilevile kufanya utafiti kwenye masuala ya mafuta na gesi, kwa sababu naelewa Jeshi linafanya utafiti kwenye masuala ya teknolojia, kama litahusika pia na masuala ya mafuta na gesi kwa sababu ni Sekta ambazo ni nyeti kwa usalama wa nchi na ni vizuri Jeshi letu likajiingiza kwenye masuala siyo tu utafutaji wa mafuta na gesi, bali utafiti juu ya *role* ya Kijeshi katika masuala ya kiusalama kwenye tasnia ya mafuta na gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata ufafanuzi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utafikiri Mheshimiwa John Mnyika ameingia kwenye akili yangu, kwa sababu wiki iliyopita nilizungumza na Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Profesa Muhongo na kumwambia kwamba, nafikiri sasa wakati umefika Jeshi la Wananchi wa Tanzania lishirikishwe kikamilifu katika utafiti na uchimbaji wa *Uranium*, kwa sababu ni madini ambayo ni ya hatari. Pili, katika masuala ya gesi na mafuta, Jeshi la Wananchi wa Tanzania ni lazima lishirikishwe kikamilifu katika jambo hilo. Tumekubaliana kwamba, nimwandikie barua rasmi, nitafanya kazi hiyo wiki hii ili hatimaye hatua ziweze kuchukuliwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Fedha hizi haziko huko au zipo huko?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za kutekeleza kazi hiyo hazitoki hapa, zitatokana na fedha zitakazopatikana

kwenye masuala mengine ya utawala na nyingine kutoka Makao Makuu ya Ngome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba, sehemu kubwa ya fedha hizi itatumika katika kulipia madeni ya zana na vifaa ambavyo tayari tumeshavinunua na tunavitumia, tuna jukumu hilo la kulipa madeni hayo.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi pia nipo kwenye *Vote* hiyo hiyo 2002, kifungu kidogo cha 6103, hapa tunazungumzia masuala ya *research and development*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, azma ya Serikali yetu ni kuleta kilimo chenye tija. Hivi karibuni tumeona wakulima wengi na hasa wale wa Mikoa ya Kusini, wakipata shida sana kupata mbegu bora za kisasa na hasa katika mazao ya mahindi ili kuongeza uzalishaji wa chakula. Wakati tunapitisha Bajeti ya Serikali, tuliona kwamba, Serikali ina azma ya kuongeza uzalishaji wa chakula na hasa kwenye Zao la Mpunga, lakini lipo tatizo kubwa sana la mbegu hizo bora na za kisasa. Tulisema pia kwamba, Majeshi yetu haya na hasa hizi Kambi za JKT zitumike katika kuondoa kabisa tatizo la kuagiza mbegu kutoka nje ya nchi na hivyo tujitosheleze kwa mbegu ndani ya nchi, mbegu ambazo zinaendana na hali halisi ya mazingira ya nchi yetu, hali ya hewa na kila kitu kinachofanana ndani ya nchi yetu.

Sasa nataka kuwa na uhakika iwapo fungu hili lililotengwa sasa hivi hapa kwenye masuala ya *research* litatekeleza kiu na azma ya Watanzania na hasa wale Wakulima wa Mazao ya Chakula kuhakikisha wanapata mbegu bora na za kisasa, ambazo zitazalishwa ndani ya nchi yetu, badala ya kutegemea mbegu kutoka nje ya nchi ya Tanzania? *(Makofi)*

**SPIKA:** Je, hili fungu ndiyo kazi yake?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki hakitahusika na suala la kuendeleza uzalishaji wa mbegu kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, lakini akiangalia Fungu la *Policy and Planning* kwenye *Sub Vote 1003,* ataona fedha ambazo zitashughulikia jambo hilo ambalo amelieleza. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Wakati *Sergeant-at-Arms* anaweka hiyo Siwa, mnatakiwa kukaa kimya na siyo kunong'ona nong'ona kama nilivyowasikia wengine.

Mheshimiwa mtoa hoja, taarifa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naomba radhi sana, wakati nilipokuwa nikifanya majumuisho nilimsahau Mheshimiwa Faith Mitambo. Kwa hiyo, naomba kumtaja kama mmoja wa watu ambao wamechangia hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati imepitia Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Fungu 38 - Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa na Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, kifungu kwa kifungu pamoja na marekebisho yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka 2012/2013 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nichukue nafasi hii, kwanza kabisa, kumpongeza Waziri kwani ingawa amekaa Wizarani pale muda wa miezi michache, bado ameweza kufanya kazi nzuri. Naamini ni kwa sababu ya ushirikiano mzuri ambao amekuwa

nao na Wasaidizi wake wote kuanzia wale wa Majeshi yote pamoja na wale alionao Wizarani. Tunawaombea waendelee kufanya kazi kwa ukamilifu katika kipindi kijacho. Naamini kabisa kama walivyosema wenzangu hapa, Majeshi yote ndiyo kinga yetu sisi, hata tufanye mambo yetu yote lakini Majeshi yetu ndiyo yanayotufanya tulale usingizi. Kwa hiyo, tunawapongeza kwa kazi nzuri iliyofanywa na Majeshi haya na tunawaomba waendelee kufanya kazi vizuri zaidi katika siku zijazo kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo dogo tu hapa kwamba, kulikuwa na mchezo wa kirafiki ambao ulifanyika kati ya *Bunge Sports Club* na Timu ya *Albino United* kutoka Dar es Salaam. Mchezo huu ulifanyika Siku ya Jumamosi na matokeo ni kwamba, timu zote zilitoka sare ya magoli mawili. Wanasema mchezo ulikuwa mzuri na nyota wa mchezo huo alikuwa Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mbunge wa Ziwani. *(Makofi)*

Jumamosi ijayo kutakuwa na mchezo mwingine na Timu ya *CRDB Bank*. Wachezaji wote mnaombwa kuhudhuria mazoezi kila siku asubuhi na kufanya mazoezi ya nguvu kujiandaa na mchezo huo. Pia ifahamike kwamba, Jumamosi zote zijazo kutakuwa na michezo ya kirafiki. Kwa hiyo, jamani mfanye mazoezi ili mtuletee ushindi. Nina tangazo lingine linahusu kikao ambacho Waheshimiwa Wabunge wanaotoka mikoa inayolima pamba walikuwa wakutane mchana. Hawakukamilisha hoja yao, kwa hiyo, wataleta siku inayofuata. Wabunge wanaotoka mikoa ambayo inalima pamba walikuwa wakutane mchana huu, kwa

hiyo, wanaendelea kufanya kazi yao nadhani mengine tutaendelea kuwasikiliza.

Waheshimiwa Wabunge, kesho tunaingia Wizara ya Mambo ya Ndani, katika mpangilio wetu wa ratiba ya kazi ilikuwa iwasilishe Bajeti yake kwa siku moja, lakini kufuatana na orodha tuliyonayo inakuwa ngumu sana. Kwa hiyo, tutaangalia kama itabidi kufanya marekebisho, tutawaeleza kesho asubuhi, lakini kwa sasa wale watakaokuwa wamejiandaa waendelee kujiandaa. *(Makofi)*

Sina matangazo mengine, nawashukuru sana kwa kazi nzuri mliyofanya siku ya leo.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Baada ya Spika kusimama hakuna Mwongozo. Sasa ninachosema ni kwamba, nawashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya siku ya leo. Naona wengi mnaendelea kuzifahamu Kanuni hasa kwenye Kamati ya Matumizi na hivyo tunaweza kumaliza vitabu vyote. Naomba mwendelee kusoma Kanuzi zetu kwa makini, usichukulie uzoefu tu kwamba fulani alisimama akasema hivi na wewe unataka kusimama hivyo hivyo. Sisi tunaendelea kuingia ndani kwenye Kanuni ili tuweze kurudisha nidhamu katika Bunge letu.

Waheshimiwa Wabunge, ninaahirisha kikao mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.00 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,*
*Tarehe 17 Julai, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*